

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 1 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA FEDHA:**

Taarifa ya Mwaka ya *The National Microfinance Bank Limited* kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 31 Desemba, 2003 (*The Annual Report of the National Microfinance Bank Limited for the Year ended 31<sup>st</sup> December, 2003*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Accounts of the Capital Markets and Securities Authority for the Year 2002/2003*).

Taarifa ya Mwaka ya *The Insurance Market Performance* kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31 Desemba, 2002 (*The Annual Report of the Insurance Market Performance for the Year Ended, 31<sup>st</sup> December, 2002*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.158

**Mashamba yaliyotelekezwa Wilayani Arumeru**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa Mwaka 1987 Mheshimiwa Rais alifuta Hati Miliki kwa baadhi ya mashamba yaliyotelekezwa Wilayani Arumeru kwa nia njema ya kusaidia wananchi wasio na ardhi ya kulima na kwa kuwa wananchi wengi waliogawiwa mashamba hayo wameshindwa kulipa fidia ya Sh.172,000/= kwa ekari moja. Je, Serikali haioni kuwa ni

vyema wananchi hao wasio na uwezo wakaruhusiwa kudhaminiwa na Serikali za Vijiji vyao waweze kulipia mashamba hayo kwa muda ili kutatua tatizo hilo la muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mwaka 1987 Mheshimiwa Rais, alifuta Hati Miliki za baadhi ya mashamba katika Wilaya ya Arumeru. Mashamba hayo ni *Tanzania Plantation Limited* na *Umoja Sisal Estate*. Kufuatia hatua hiyo, shamba ambalo limekuwa tayari kugawiwa ni shamba la *Umoja Sisal Estate* lenye ukubwa wa ekari 2,398.87 ambalo baada ya kufanyiwa uthamini na Serikali ilionesha thamani ya shamba hilo ni Sh.349,326,900/= inayojumuisha thamani ya ardhi, majengo na mazao.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru iliingia makubaliano na mmilikaji wa awali kuhusu namna ya ulipaji fidia wa shamba hilo. Makubaliano yaliyopo ni kulipwa kwa awamu tatu kutokana na wananchi kulipia Sh.172,000/= kwa ekari. Katika utekelezaji, Baraza la Madiwani katika Kikao chake cha tarehe 4 Oktoba, 2002 liliamua kugawa shamba hilo kupitia Kata. Kata zilizoteuliwa kupewa ardhi ni kumi nazo ni Nduruma, Mashono, Sikon II, Bwawani, Maji ya Chai, Olturoto, Kikwe, Akheri, Nkoarisamba na Moivo. Katika kipindi cha mwaka mmoja Kata hizo zimeweza kulipia ekari 102 tu zenye thamani ya Sh.17,544,000/=, nazo ni Nduruma ekari 46, Mashono ekari 30, Sokon II ekari 10, Bwawani ekari saba, Maji ya Chai ekari sita, Olturoto ekari tatu. Kutokana na hali hiyo, Baraza la Madiwani lilikutana tarehe 12 Novemba, 2003 na kufanya marejeo ya maamuzi yake ya awali na kuamua wananchi wa Arumeru kwa ujumla wajitokeze kununua mashamba ili kulipia fidia bila kujali utaratibu wa Kata kama ilivyoamuliwa awali kwa kuwa kipindi cha makubaliano cha kuanza kulipia fidia hiyo bila tozo ya faida kilishapita.

Mheshimiwa Spika, baada ya kipindi cha miezi sita ya Azimio la tarehe 12 Novemba, 2003, Halmashauri imeweza kuuza jumla ya ekari 763 zenye thamani ya Sh.131,236,000/=. Aidha, imegawa kiasi cha ekari 400 kwa wananchi wa Oljoro waliokosa mashamba mwaka 1997. Mpaka sasa Halmashauri imebakiwa na ekari 1,151.87 ambazo zipo wazi kununuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kuvipa Vijiji uwezo wa kuwadhamini wananchi ili walipie mashamba hayo kwa muda mrefu haliwezekani. Hii ni kwa sababu kwanza, Vijiji hivi havina uwezo kifedha na pili, Sheria na Kaununi za kulipa fidia zinataka fidia ilipwe yote katika kipindi cha miezi sita tangu uthamini ufanyike. Endapo fidia haitalipwa katika kipindi hicho, basi mlipwa fidia itabidi alipwe riba mpaka hapo fidia itakapokamilishwa. Aidha, uwezo wa Halmashauri wa kuvidhamini Vijiji haupo kutokana na uwezo finyu wa mapato.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize swali moja. Kwa kuwa nia ya Mheshimiwa Rais kufuta Hati Miliki ya mashamba haya ilikuwa inalenga wale wananchi wasio na uwezo na wasio na ardhi ya kulima; na kwa kuwa maombi haya leo yamekataliwa rasmi; na kwa kuwa katika Wilaya ya Arumeru kuna shamba la Serikali la *Themi Holding Ground* ambalo Serikali hailitumii ipasavyo na haina fidia kubwa; je, Serikali itakubali maombi ya wananchi wa Arumeru kupewa shamba hili ili wale ambao wamekosa kwa ajili ya bei hii kubwa waweze kupata mashamba hapo? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wameonesha nia ya kupata hii ardhi, wameweza kutekeleza masharti bila matatizo yoyote. Kwa hiyo, bado rai ya Serikali iko pale pale. Kwa eneo lililobaki wananchi ambao wanataka hiyo ardhi wajitokeze ili waweze kupata hiyo ardhi. Lakini kuhusu hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelileta, kwa upande mmoja ni jambo jipya kwa sababu hatukulifanyia utafiti wa kutosha, lakini tunachoweza kusema tu ni kwamba, hii ardhi anayoizungumzia kwa sasa ni mali ya Serikali na itaendelea kutumika kwa madhumuni yaliyowekwa na Serikali mpaka hapo Serikali itakapoona vinginevyo. (*Makofi*)

Na.159

### **Kituo cha Afya Bukundi**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Bukundi kilichoko Wilayani Meatu hakipatiwi huduma kama Kituo cha Afya kwa kipindi kisichopungua miaka sita sasa:-

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia huduma kama vile gari, dawa na wataalam wanaohusika na kituo hicho kama Kituo cha Afya?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutokutoa huduma zinazostahili katika Kituo hicho ni kuwanyima wananchi haki ya huduma za msingi na hatimaye kusababisha vifo vinavyoweza kuepukwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya na kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya inayosimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inatoa huduma ya madawa na vifaa muhimu vya matibabu kwa Vituo vyote vya kutolea huduma kupitia mpango unaoandaliwa kila mwaka na Halmashauri zote nchini. Kwa upande wa

gari la wagonjwa, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo hili sugu karibu katika Vituo vya Afya vingi hapa nchini zikiwemo Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la magari ya kubebea wagonjwa, Ofisi yangu imekuwa ikiwasiliana na Hazina juu ya uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa ya Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya kwa vipindi viwili mfululizo lakini imeshindikana kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, Halmashauri inashauriwa kuendeleza juhudi za ununuzi wa gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Bukundi kupitia bajeti yake na tunayo mifano mizuri kama vile Kilwa ambao wameweza kufanya hivyo kupitia bajeti yake kwa kununua magari manne ya wagonjwa. Lakini vile vile Halmashauri inashauriwa kufanya juhudi za kujaribu kuwasiliana na Wahisani mbalimbali kama njia nyingine ya uwezekano wa kupata usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wataalam, Kituo kinapaswa kuwa na watumishi 30 ambapo waliopo kwa sasa ni saba tu. Ili kukabiliana na upungufu huu, Halmashauri iliomba kibali cha kuajiri watumishi zaidi. Kibali kimekwishapatikana cha kuajiri watumishi sita kwa mwaka 2004/2005 ambao ni pamoja na *Assistant Medical Officer* mmoja, *Clinical Officer* mmoja, *Nursing Officer* mmoja, *Laboratory Assistant* mmoja, *Dental Therapist* mmoja na *Nurse Assistant* mmoja. Jitihada zaidi zinafanyika ili kuhakikisha Kituo hiki kinapatiwa vifaa na watumishi zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la swali (a) kuwa kwa kutambua haki ya kila mwananchi kupatiwa huduma za msingi, Serikali inaendelea kutoa huduma za Afya katika Kituo cha Bukundi kupitia Programu ya Mfuko wa pamoja wa Afya. Aidha, ili kurahisisha mawasiliano kati ya Vituo vya Afya na Hospitali ya Wilaya, Serikali imekwishaweka *network* ya mawasiliano ya *Radio Call* kati ya Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya Bukundi na Hospitali nyingine katika Mkoa wa Shinyanga ikiwemo Hospitali ya Mkoa. Hivyo, kwa mazigira haya ni dhahiri kuwa hatua zimekwishachukuliwa kukabiliana na matukio ya dharura ambayo yanaweza kutokea katika Vituo vya Afya Wilayani humo. (Makofi)

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa bahati nzuri mwenyewe amekiri kwamba kweli kuna upungufu wa watumishi na Kituo cha Afya kinatakiwa kiwe na idadi ya watumishi wasiopungua 30, sasa walioko kwenye Kituo cha Bukundi ni tisa na wakati huo huo tena wamepata kibali cha kuweza kuajiri watumishi sita tu.

Je, Serikali haioni kwamba katika kupeleka watumishi wachache hivyo ni kuweza kupeleka Kituo hicho kutokufanya kazi vizuri na kuathiri afya za watu kwa sababu Kituo hicho kinahudumia idadi ya watu zaidi ya laki moja, kiasi cha Tarafa nzima; je, Serikali haioni kwamba ingefaa ipeleke watumishi wanaoweza kukidhi idadi ya watumishi au ikama ya watumishi katika Kituo hiki cha Bukundi? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tu nimpe changamoto Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, kama hao sita atawapata nitafurahi sana kusikia kwamba ameweza kufanikisha. Mara zote tunasema tatizo ni upatikanaji wa hawa wataalam na juzi Mheshimiwa Dr. Gama alijaribu kui-*challenge* Serikali kwamba, wako wengi mitaani na sisi tukasema hebu watafuteni hao waje watuone ili tuweze kuwapa kazi kwa sababu nafasi ni nyingi sana hazina wataalamu. Tatizo kubwa ni watu wenyewe hawatoshi, lakini Wizara ya Afya inaendeleza juhudi zake za kuendelea ku-*train* watu hawa lakini lazima tukumbuke kwamba, tatizo ni kubwa sana na tusitegemee kwamba litamalizika katika kipindi kifupi kijacho.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu Kituo cha Afya cha Bukundi kipo mpakani kabisa mwa Wilaya ya Meatu na Iramba Mashariki na kwa kuwa kinatoa huduma pande zote mbili, ni kwenye Vijiji vya Nyahaa, Nyadundu, Endasiku na Mitominane, je, Serikali haioni kwamba Vituo vya Afya kama hivi kuna umuhimu wa kuviongezea nguvu mapema kwa sababu vinahudumia watu zaidi ya idadi iliyokadiriwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Kituo hiki kiko mpakani na kinatoa huduma kwa wananchi wengi. Lakini nilitaka nimkumbushe vile vile kwamba, upatikanaji wa madawa kwa ajili ya Kituo hiki na vifaa vingine vinavyohitajika kwa ajili ya Kituo hiki, vinategemea matokeo ya takwimu za utoaji wa tiba katika Kituo hicho. Kwa hiyo, haiwezekani ukatoa madawa ya watu kumi wakati kinahudumia watu laki moja. Hizi takwimu ndio zinazoisaidia Wizara ya Afya pamoja na sisi kuweza kupeleka madawa ya kutosheleza. Kwa hiyo, ningependa nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa maana hiyo, Kituo hiki kitakuwa kinapata huduma zote zinazohitajika. Lakini rai yake nyinginetunaikubali kwamba kama kuna mapungufu ya namna yoyote, tutajaribu kulitazama tena na Sekta ya Afya tuone kama kuna mapungufu tuweze kuyarekebisha.

**SPIKA:** Maswali kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Semindu Pawa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, swali hili nilikuwa nimelipeleka Wizara ya Utawala Bora, lakini kwa shingo upande naomba swali hili lijibiwe. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa nini kwa shingo upande? (*Kicheko*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Katika kumbukumbu zangu hapa ninaandika Wizara niliyopeleka, nililipeleka Utawala Bora, sasa leo anajibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji! Kwa sababu Muhimbili haibinafsishwi wala *TANESCO* haibinafsishwi, kwa hiyo, nilikuwa nauliza Utawala Bora. Ahsante nashukuru.

**SPIKA:** Serikali ni moja kwa hiyo, Waziri yeyote anaweza kujibu.

Na.160

### **Ubinafsishaji wa Mashirika Mbalimbali**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inatambulika duniani kote kwa ustaarabu wake na imefanya mageuzi mengi yanayojali maslahi ya umma katika Sekta zote kama vile Maji, Afya, Barabara, Umeme, Elimu, Ulinzi, Kilimo, Ushirika na Masoko, Mifugo, Reli, Simu na kadhalika na kwa kuwa mafanikio hayo na mageuzi yameletwa na Watanzania wenyewe:-

(a) Je, kwa nini baadhi ya Mashirika ambayo hata hayajabinafishwa yanawekwa/yanatolewa kwa viongozi wa ngazi za juu wa kigeni?

(b) Kwa kufanya hivyo na kwamba madaraka makubwa ndani ya Makampuni/Mashirika au Taasisi kama vile *TANESCO* na Muhimbili ni Utawala Bora au ni utawala mbadala na unakusudia nini katika kipato, tija na ufanisi au uzalishaji mali?

(c) Je, pale inapotokea kuwa utawala huo wa kigeni ndani ya baadhi ya Mashirika hayo, kwa mfano, Muhimbili unapofikia hatua ya kutamka bei ya juu ya tiba kinyume cha sera za nchi bila kuishirikisha Wizara au Bodi husika, Watanzania tueleweje hali hiyo na Serikali inasema nini katika hali kama hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (k.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Semindu Pawa, asiwe na wasi wasi tutajibu kwa Utawala Bora vilevile. (*Kicheko*)

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inapoamua kuweka uongozi wa kigeni katika Mashirika yake, ni kwa nia ya kuleta mabadiliko na kuboresha tija na ufanisi wa huduma za Mashirika hayo. Mashirika yanawekwa chini ya uongozi wa kigeni kutokana na mwenendo wa uzalishaji ama huduma wa mwaka hadi mwaka, kutokuwa na ufanisi na tija ya kuwezesha Shirika kuwa na huduma bora kwa wananchi. Ili kutekeleza uamuzi huo, Serikali hutangaza zabuni zenye ushindani wa wazi kwenye vyombo vya habari na kuwataka watu au Kampuni za Watanzania na wageni kuleta maombi kufanya kazi inayokusudiwa. Wale tu wanaokidhi malengo ya Serikali ndio wanaochaguliwa kwa utaratibu wa zabuni kwa mikataba maalum kwa Mashirika ambayo hayajabinafishwa.

(b) Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuwepo viongozi wa kigeni wa ngazi ya juu katika kuendesha Mashirika au Makampuni au Taasisi za Umma ni kuwa na utawala mbadala wenye lengo la kuongeza uzalishaji na tija kwa Mashirika yanayozalisha bidhaa na kuboresha huduma na tija kwa Mashirika yanayotoa huduma. Mara hali itakapokuwa ya kawaida na mara atakapopatikana Mtanzania atakayeonyesha uwezo wa kuendesha Mashirika hayo, Serikali haitasita kumwachia uongozi na kwa utaratibu unaokubalika. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa sababu hata mfumo wa swali lenyewe kwa mpango wa Serikali, lilipelekwa Mipango halafu anajibu Waziri wa Utumishi. Kwa hiyo, nao huu sio Utawala Bora.

**SPIKA:** Nimeshakueleza kwamba, Serikali ni moja na wewe unaiuliza Serikali, kwa hiyo, yeyote anayejibu, anajibu kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, uliza maswali yako ya nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa nini Muhimbili ilikuwa na mafanikio makubwa sana wakati wa utawala wa Mheshimiwa Prof. Phillemon Sarungi na kwa nini sasa wasitafute humu humu nchini Tanzania, wanayo habari kwamba Watanzania hawataki utawala mbadala kama alivyokuwa ametamka Waziri katika jibu lake?

(b) Kwa kuwa Muhimbili na *TANESCO* hazibinafsishwi ila Muhimbili ni Hospitali ya Taifa na *TANESCO* itakodishwa, je, kwa utaratibu huo utawala uliopo hivi sasa muda wao ukipita Watanzania wakiwa tayari wataondoka? Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Semindu Pawa kwamba, tutamjibu maswali yake kama vile ambavyo angejibu yule ambaye alimtarajia.

Mheshimiwa Spika, Muhimbili ilikuwa inafanya kazi kwa ufanisi chini ya Mheshimiwa Prof. Phillemon Sarungi wakati akiwa Mkuu wa Shirika la Muhimbili, nampongeza sana. Wakati hali ya huduma ilipohitaji mabadiliko Muhimbili, tulitangaza Watanzania na wageni wakaomba ile nafasi na ikaonekana kuwa kwa huduma na ufanisi unaotakiwa yule aliyechaguliwa ndiye anayefaa. Kwa upande mmoja tunalinda ajira za Watanzania, lakini kwa upande mwingine lazima tulinde haki ya Watanzania kupata huduma bora. Kwa hiyo, yule ambaye atatoa huduma bora ndiye ambaye atachaguliwa kushika nafasi ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la pili, ni kweli kabisa kwamba, si kweli kwamba daima hakutakuwa na Mtanzania atakayekuwa na uwezo. Pale tutakapotangaza na Mkataba wa huyu utakapokwisha, Serikali haitasita endapo tutakapotangaza

atajitokeza Mtanzania mwenye uwezo na atakeyewahakikishia Watanzania huduma bora Muhimbili na *TANESCO*.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Hutokea mara nyingi sana Mashirika yanayofanya vizuri na baadaye kubinafsishwa, lakini matokeo yake ni kwamba wafanyakazi wake hawalipwi maslahi yao. Kwa mfano, *TTCL*, *Polyster*, ni nini kinachotokea? Ni kwa sababu gani inafikia hatua tunatangaza inafanya kwa faida, lakini tunapobinafsisha wafanyakazi hawalipwi, ni nini kinatokea, kwa mfano *Polyster*? (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwangu ni swali jipya, lakini Mheshimiwa Waziri kama una majibu unaweza kuendelea kuyatoa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) :** Mheshimiwa Spika, Mashirika yanapobinafsishwa si kwa sababu yanafanya vibaya, ni kwa sababu ya sera ya msingi ya Serikali kwamba, Serikali itafanya kazi zile za msingi na kazi za uzalishaji na kutoa huduma zifanywe na wadau wengine hususan sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kila mara tunapobinafsisha wafanyakazi huwa wanalipwa pale ambapo Shirika lile lina uwezo wa kuwalipa. Lakini hata pale ambapo Shirika halina uwezo, yale malipo ya msingi ya wafanyakazi huwa yanalipwa. Ila pale tu wanapotaka mkono wa kheri au wa kwaheri wakati Shirika halina ufanisi na halina ziada, basi haiyumkiniki Watanzania wengine kuwachangia kwa kupitia kodi na kuacha sehemu nyingine ya kutoa huduma ili kuwalipa watumishi wa sehemu hizo ambazo Mashirika yao yanabinafsishwa. (*Makofi*)

Na.161

### **Uboreshaji wa Elimu Nchini**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA (k.n.y. MHE. JOHN L. MWAKIPESILE)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inastahili pongezi kubwa na za dhati kwa juhudi zake za kuongeza, kuboresha na kuendeleza Elimu ya Msingi na ya Sekondari nchini kote:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kuongeza kujenga *High Schools* ili wanafunzi wengi zaidi waingie Vidato vya Tano na Sita?

(b) Je, ni wanafunzi wangapi walifaulu vizuri mitihani ya Kidato cha Nne katika mwaka 2000 - 2003 lakini wakashindwa kuingia Kidato cha Tano kwa kukosa nafasi au ada?

(c) Je, Serikali iko tayari kupokea ombi la Wananchi wa Kyela la kujenga *High School* itakayoendeshwa na Serikali na je, sera inasemaje juu ya jambo hilo?



**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuongeza idadi ya wanafunzi wa Sekondari wa Kidato cha Tano na Sita kama inavyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004 - 2009. Katika mpango huo, baadhi ya Shule za Sekondari ya Juu yaani za *A-Level* zilizopo zitaongezwa na hili linaanza katika Bajeti hii ili kuchukua wanafunzi wengi zaidi na shule mpya zitajengwa hasa katika Wilaya zile zisizo na Shule za Sekondari ya Juu.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali katika *SEDEP* ni kuwa na Sekondari ya aina hiyo katika kila Makao Makuu ya kila Wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, wanafunzi waliokuwa na sifa ya kuchaguliwa kungia Kidato cha Tano lakini hawakuchaguliwa katika Shule za Serikali kwa kukosa nafasi ni kama ifuatavyo: Mwaka 2000 waliokuwa na sifa ni 14,083, waliopangwa katika Shule za Serikali ni 8,705, waliokosa nafasi ni 5,378. Mwaka 2001 waliokuwa na Sifa ni 13,448, waliopata nafasi ni 9,223 na waliokosa nafasi ni 4,225. Mwaka 2002 aliokuwa na sifa ni 16,571, waliopata nafasi ni 10,158 na waliokosa nafasi ni 6,413. Mwaka 2003 waolikuwa na sifa ni 22,001, waliopata nafasi ni 13,383 na waliokosa nafasi ni 8,618.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanafunzi waliokosa nafasi za Kidato cha Tano katika Shule za Serikali wanategemewa kupata nafasi hiyo katika Shule zisizo za Serikali na baadhi yao katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Ufundi. Aidha, wapo wanafunzi waliochaguliwa kuingia Kidato cha Tano katika Shule za Serikali, lakini kwa hiari yao, waliamua kujiunga na Shule zisizo za Serikali. Kwa hiyo, nafasi zao hujazwa na wale waliopo katika orodha ya akiba. Wizara haina taarifa ya mwanafunzi aliyeacha kuingia Kidato cha Tano kutokana na kukosa ada.

(c) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuwa na Shule ya Sekondari ya Juu kama nilivyosema katika Makao Makuu ya kila Wilaya. Hivi sasa Wizara yangu inafanya uchambuzi ili kuainisha Shule zitakazoongezewa nafasi kwa ajili ya Sekondari ya Juu peke yake na nyingine kuwa za mchanganyiko wa Sekondari ya kawaida na ya Juu katika Mikoa na Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Kyela.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa inaonekana idadi kubwa sana ya vijana wetu hawakwenda Elimu ya Juu, je, Serikali haioni ni vizuri sasa tuongeze idadi katika hizo Sekondari inazopanga kuzijenga katika Wilaya mbalimbali angalau iwe mara mbili ili iweze kukidhi haja hii ambayo kwa kweli vijana sasa wanakosa nafasi ambayo ni ya msingi zaidi?

Pili, kwa kuwa na Wilaya yangu ya Mbozi ni mojawapo pamoja na wazee wenzangu, ambayo haina Sekondari ya Juu ya Serikali, je, anaweza kunihakikishia kwamba Mbozi itapewa kipaumbele vile vile? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kama tungeongeza angalau mara mbili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwamba, katika *SEDEP* lengo ni kuongeza nafasi za Sekondari mara tano. Tumelenga mara tano. (*Makofi*)

Kuhusu swali la pili kwamba, Mbozi ipewe umuhimu, nakubali kabisa kwa sababu kama nilivyosema, lengo la Serikali ni kwamba, angalau kila Makao Makuu ya Wilaya tuwe na Sekondari ya *A-level* ya *Boarder* ili iweze kupokea wanafunzi katika Sekondari hizi nyingi ambazo tunatarajia kuziongeza katika nchi nzima. Kwa hiyo, nitashukuru sana kama Mheshimiwa Eliachim Simpasa, atanza kuandaa mapendekezo, Sekondari ya pale Mbozi ijengwe wapi au tuongeze Daraja A pale itakapokuwepo.

Naomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane katika jambo hili, ni kuangalia ile Sekondari iliyokaa mahali pazuri au pale ambapo Makao Makuu ya Wilaya haipo Sekondari ya namna hiyo, basi ni kuangalia nafasi nzuri panapofaa kujenga Sekondari hiyo. Lengo ni kwamba, iwe inachukua wanafunzi wa *A - Level* watupu na iwe ya *Boarder* kwa sababu ya wanafunzi wanaotoka katika sehemu mbalimbali za Wilaya hiyo. Kwa hiyo, tukishirikiana hivyo, naamini tutakwenda upesi. Hili pia nitalifafanua zaidi katika hotuba yangu ya Bajeti. (*Makofi*)

Na. 162

### **Ujerumani Kufadhili Miradi ya Maji Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Litumbakuhamba na Kata za Ngumbo, Ntipwili, Chiwanda, Mbaha na Kingirikiti wananchi hawana kabisa maji safi na salama, lakini katika barua ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo yenye Kumb. Na. 179/344/01 ya tarehe 2 Agosti, 2002 akijibu mchango wangu niliochangia wakati wa Bajeti ya mwaka 2002/2003 alielezea kuwa Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (*KfW*) wameonyesha nia ya kufadhili miradi ya Maji Mkoa wa Ruvuma ikiwemo Wilaya ya Mbinga.

Je, mazungumzo kati ya Serikali yetu na Shirika hilo la Maendeleo la Ujerumani yamefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (*KfW*), wamekuwa wakitusaidia kufadhili miradi ya maji kwa kipindi kirefu hadi sasa, hususan katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Mwaka 2000 Wizara yangu ilianzisha mazungumzo na *KfW* yenye lengo la kuwaomba waelekeze msaada wao pia katika Mikoa ya Kusini mwa nchi yetu, ukiwemo Mkoa wa Ruvuma. Mazungumzo hayo yalizia matunda baada ya *KfW* kukubali kupanua miradi ya maji katika Miji ya Mbeya, Iringa na Songea. Huu ni mwelekeo mzuri wa wafadhili hawa muhimu kuelekeza ufadhili wao katika Mikoa ya Kusini. Pamoja na kufikia hatua hiyo, Wizara yangu bado inaendeleza mazungumzo na wafadhili hao ili waweze kusaidia kufadhili miradi mingi zaidi ya maji hususan Wilayani na Vijijini ikiwemo Wilaya ya Mbinga na Vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, jitihada zaidi zinazoendelea sasa ni kuingiza Wilaya zote katika mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unaofadhiliwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia, ambapo miradi ya maji itaelekezwa kulingana na mipango ya Wilaya husika. Wilaya ya Mbinga inakusudiwa kuingizwa kwenye awamu ya mwisho ya programu hiyo inayotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2004.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yanayoleta matumaini yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa mazungumzo kati ya Serikali na Shirika la *KfW* bado kukamilika, kwa hiyo, miradi hiyo bado haitaweza kukamilika mapema. Je, Serikali haiwezi kutumia bajeti yake walau ikakamilisha mradi mmoja kati ya hiyo niliyoiomba? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri naelewa umuhimu ambao Serikali inauweka katika kuhakikisha kwamba, maji safi na salama yanawafikia wananchi wote hapa nchini na pia nafahamu shauku aliyonayo Mheshimiwa Mbunge, hasa matatizo yaliyopo katika Jimbo lake na ndiyo sababu kwa kushirikiana naye katika mipango yetu ya Serikali, moja ya mpango ambao nimeueleza ni huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao utafikisha miradi ya maji katika maeneo yote ya Wilaya ya Mbinga ambako wananchi pamoja na viongozi watakuwa wamechagua miradi hiyo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, ili kuwa katika haraka au katika njia bora zaidi ya kutuletea miradi ipi inayohusika ashirikiane na uongozi wa Wilaya ili miradi hiyo iweze kutufikia mapema ili programu ikianza tu tuweze kuingiza miradi hiyo katika programu yetu.

Na. 163

### **Maeneo kwa ajili ya Wafugaji**

**MHE. BENSON M. MPESYA (k.n.y. MHE. NJELU E. M. KASAKA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetoa maelekezo kwa Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ili kutenganisha shughuli za kilimo na ufugaji:-

(a) Je, Serikali imetenga bajeti ya kuwezesha Halmashauri kufikisha huduma muhimu hasa maji katika maeneo yanayotengwa kwa ajili ya wafugaji ambayo mara nyingi huwa ni mapya?

(b) Je, Serikali iko tayari kuufufua mradi wa kuangamiza Mbung'o Wilayani Chunya ili kupanua maeneo yanayofaa kwa ufugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Meshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Meshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 2002, imeziagiza Halmashauri za Wilaya, kuandaa maelezo na miongozo rahisi ya kuelimisha wananchi na Serikali zao za vijiji kuhusu haki na wajibu wa kisheria kuhusu matumizi ya ardhi kwa lengo la kuepusha migongano miongoni mwa watumiaji wa raslimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu hutenga bajeti kwa ajili ya kuchangia juhudi za Halmashauri za Wilaya ili ziweze kufikisha huduma muhimu hasa maji katika maeneo yanayotengwa kwa ufugaji. Bajeti hii huwa ni ya uwiano wa Serikali kuchangia asilimia 50, Halmashauri ya Wilaya asilimia 30 na kijiji husika asilimia 20 kwa kila mradi wa maji tunaoupeleka. Kuanzia mwaka 2001/2002 hadi sasa, Serikali imekwisha changia uchimbaji wa malambo 294 kwa gharama ya shilingi 727 milioni na katika idadi hiyo jumla ya malambo 174 yamekwisha chimbwa yakiwemo malambo manne yaliyopo Wilayani Chunya na maeneo ya Mbugani, Mapogoro, Mbangala na Upendo Mashariki.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, palikuwa na mradi wa kuangamiza mbung'o Wilayani Chunya ulioteklezwa katika eneo la Mbangala karibu na Ziwa Rukwa kuanzia mwaka 1988 hadi mwaka 1991 kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*). Mradi huo ulikuwa na lengo la kufanya jaribio la kuangamiza mbung'o kwa kutumia vitambaa vilivyopakaliwa dawa katika mazingira ya Tanzania, baada ya kuonyesha mafanikio nchini Zimbabwe. Wakati huo huo mradi ulilenga kuwanufaisha wafugaji wahamiaji waliokuwa wanahamia Mkoani Mbeya kutoka Mikoja ya Mwanza, Shinyanga na Tabora. Licha ya mafanikio yaliyopatikana, mradi haukuwa endelevu kwa sababu wafugaji wahamiaji wengi wao hawakuweka makazi ya kudumu katika eneo la mradi na badala yake walihamia maeneo mengine. Kwa wakati huu, wapo wafugaji wachache wenye mifugo ipatayo 20,000 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mradi huu ulimaliza muda wake katika maeneo niliyoyataja ikiwemo Chunya, Wizara yangu inatekeleza mpango wa kutokomeza mbung'o hapa nchini kwa kuwafundisha mabwana mifugo wasaidizi juu ya mbinu shirikishi za kudhibiti mbung'o. Wataalam hawa wanatumika katika Halmashauri zao kuwahamasisha, kuwafundisha na kuwashirikisha wafugaji ili waweze kutumia na

kuchangia mbinu hizo ili utekelezaji uwe endelevu. Mbinu hizo mpya na za kisasa ni rahisi kutumiwa na wananchi na ni salama kwa mazingira.

Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya katika vijiji 30 vya Mkoa wa Kigoma na vijiji 10 Mkoa wa Tabora. Kadhalika Shirika Msalaba Mwekundu na lile la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wakimbizi (*UNHCR*), yanasaidia kufadhili mpango huu katika maeneo ya makambi ya wakimbizi na baadhi ya vijiji vinavyozunguka makambi hayo katika mikoa hiyo kwa kusambaza mitego ya kuua mbung'o. Mpango kama huu unaendelea kutumika katika mbuga za Serengeti ambako mwaka 2000/2001 ulionyesha mafanikio makubwa ya kudhibiti matukio ya ugonjwa wa malale.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa Wilaya ya Chunya ni kati ya Wilaya ambazo zimepokea wafugaji wengi kutoka katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na kwa sababu kumekuwa na migongano na wakulima, je, Serikali haioni sasa kwa kuufufua tena mradi huo tutakuwa tumewasaidia wenzetu hawa ambao tungependa tuishi nao vizuri? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wafugaji wengi wamehamia maeneo hayo na siyo maeneo hayo tu, wafugaji wengi sasa hivi wanaendelea kuhamia maeneo mengine na kuna wengi pia wameingia mpaka sehemu za Zambia. Lakini tunachotafuta kwa mpango huo kuwa endelevu ni kwa wafugaji kukakaa kwenye maeneo kwa muda mrefu sehemu moja. Lakini mpaka hivi sasa walikuwa wana-*move* sana, wanatoka Nyanda za Juu wanakwenda sehemu nyingine kwenye mabonde. Kwa hiyo, unakuta kwamba tuna matatizo ya kuweza kutekeleza programu hii kwa utaratibu ambao unakubalika.

Kwa hiyo, *stability* hiyo tunaitegemea kwamba baada ya muda mfupi ujao na wakati huo huo tunatafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza huu mpango, nina hakika kwamba tutafanikiwa tukisaidiana na uongozi wa Wilaya husika.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hili zoezi la kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu ndani ya Bunge na katika hotuba mbalimbali na hata katika Maazimio mbalimbali, lakini limeonyesha kwamba halina mafanikio kwa sababu kazi hii imekuwa ikiachiwa kwenye Halmashauri na wananchi.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuainisha Wilaya zile ambazo zina mifugo mingi ili kwa kuanzia tuwe na kianzio kama ilivyo Wilaya ya Mbarali na Wilaya zingine zenye mifugo mingi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mpango huu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na wakulima umekuwa ukizungumzwa kwa muda mrefu. Lakini pia ni kweli kwamba, tuna tatizo moja, tunapozungumzia wafugaji na wakulima unakuta kwamba tunaweka *assumption* ya kudhania kwamba, watu hao ni tofauti. Mfano, wafugaji na wakulima wanaotoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora, utakuta wanafanya shughuli zote mbili. Wanafanya ufugaji na wanafanya na ukulima. Sasa kuwatenga inakuwa ni vigumu sana utenge vipi. Cha msingi tunaomba Wilaya husika kama kunatokea matatizo ya mgongano ni kuchunguza vizuri kuona mgongano huu unatokana na nini.

Kwa sababu nimeona maeneo mengi mgongano wa wakulima na wafugaji mara chache sana unahusisha shughuli wanazozifanya. Lakini mara kwa mara utakuta kwamba, unahusisha mahusiano mengine ya kijamii, kuoana na matatizo mengine badala ya matatizo husika hasa ya ufugaji na ukulima ambao ndiyo chanzo cha mgongano. *(Makofi)*

Na. 164

### **Vyama vya Ushirika**

**MHE.STEPHEN M. KAHUMBI (k.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa zipo Wilaya mpya zilizoanzishwa nchini na vipo Vyama vya Ushirika ambavyo mpaka sasa vinashirikisha Wilaya mbili yaani viko ndani ya Wilaya mbili tofauti:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu wowote wa kuziruhusu Wilaya mpya au Wilaya zile zinazoshirikisha Vyama vya Ushirika kuanzisha vyama vyao Kiwilaya ili kuendeleza juhudi za kukuza uchumi kiwilaya?

(b) Kama Wilaya hizo zinaruhusiwa kugawanya Vyama vya Ushirika vinavyomilikiwa na Wilaya mbili, je, ni nani atakuwa msimamizi wa mgao wa mali na raslimali za vyama hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika ni vyombo vya kiuchumi vinavyoundwa kwa hiari na wanachama wenyewe ili kuimarisha uwezo wao wa kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii kwa kushirikiana. Dhana ya kushirikiana huimarishwa kwa wanachama kuyakabili matatizo yao kwa pamoja bila kuzuiwa na mipaka ya kiutawala ya Kiserikali na huweza kubadilika kutokana na mahitaji ya wakati. Hivyo basi, eneo linalohudumiwa na chama cha ushirika kilichoandikishwa hufuata eneo ambamo

wanachama wanaokiunda wamekubali kushirikiana bila ulazima wa kufuata mipaka ya kiutawala ya Serikali. Kigezo muhimu kinachozingatiwa ni uhai wa kiuchumi wa chama kinachohusika. Kutokana na hali hii, Vyama vya Ushirika, wakati mwignine huwa na eneo linalogusa Wilaya zaidi ya moja na kwingine Mikoa zaidi ya mmoja kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo, Serikali haizuii Vyama vinavyohitaji kugawanyika kuweza kufanya hivyo ili mradi chimbuko la kugawanyika kwa chama ni uamuzi wa wanachama wenyewe kupitia Mikutano Mkuu ambayo mahudhurio yake hayapungui theluthi mbili ya wanachama wote. Katika Mkutano Mkuu huo, Halmashauri ya Chama kinachogawanyika huwasilisha mapendekezo yenye uchambuzi wa kina kuhusu uhai wa kiuchumi wa vyama vipya vinavyopendekezwa, mgawanyo wa mali na madeni baina ya vyama vipya na maeneo mapya yatakayohudumiwa na vyama hivyo.

Maamuzi ya Mkutano Mkuu kuhusu kujigawa kwa chama hupelekwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika, ambaye baada ya kujiridhisha juu ya uhai wa kiuchumi wa vyama vipya vitakavyotokana na mgawanyiko huo kwa wakati huu na miaka ya usoni kwa kuweka maanani ushindani wa biashara unaotokana na utandawazi na soko huria, huweza kuidhinisha maombi ya mgawanyiko na kuandikisha vyama hivyo vipya.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri ambalo linazingatia Kanuni za Ushirika zilizoanzishwa kule *Rochi Dam*. Sasa ninataka kumwuliza kidogo kwamba, je, viongozi kwa faida zao wanaotaka kugawa vyama kwa kufuata mipaka ya kiutawala, si wanapiga vita ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli kwamba, vyama hivi vya ushirika vinapoanzishwa vinatakiwa vianzishwe kwa kuzingatia *demand driven*. Kusema kweli kwamba, wanachama wanaohitaji kuanzisha chama hicho waonyeshe mahitaji bila kujali mipaka ya kiutawala ya Kiserikali. Kwa hiyo, endapo kutatokea mahali ambapo viongozi wa namna nyingine wanajaribu kuanzisha Vyama vya Ushirika kufuata mipaka ya Kiserikali bila kujali ile *demand driven* wanakiuka utaratibu. Kwa hiyo, naomba tushirikiane kutoa maelekezo hayo na ushauri ili Vyama vya Ushirika vianzishwe katika misingi inayostahili.

Na. 165

### **Uandikishaji wa Vizazi na Vifo**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa uandikishaji wa vizazi na vifo ni mambo ya lazima na ya kisheria na kwa kuwa wananchi sasa wanaelewa umuhimu wake kwao wenyewe na kwa Taifa:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba huduma hiyo inawafikia wananchi wote wanaohitaji na kwa wakati unaofaa?

(b) Je, Serikali za Vijiji ambazo kuanzia mwezi Julai, 2003 zitakuwa na Maafisa Watendaji watakaoajiriwa au walioajiriwa na Serikali hawawezi kutengenezewa Regista Maalum za kuandikisha Vizazi na Vifo ambazo zitatumika baadaye kutoa vyeti mahsusi?

(c) Je, katika Jimbo la Bumbuli ni vizazi na vifo vingapi vimeandikishwa tangu 1996 hadi Desemba, 2002?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kawaida usajili wa vizazi na vifo ulikuwa ukifanyika katika ngazi ya Wilaya tu, lakini kwa kutambua umuhimu wa kusajili vizazi na vifo, usajili ambao unafanyika chini ya Sheria ya Usajili ya Vizazi na Vifo (*Registration of Births and Deaths Ordinance Cap. 108*), Serikali imeanzisha mikakati ya kuifikisha huduma hii muhimu kwa wananchi wote na kwa wakati unaofaa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha Mradi Maalum wa kuandikisha vizazi na vifo (*Civil Registration Programme*), ambapo usajili unafanyika wa watoto wote waliozaliwa na vifo vyote vinavyotokea katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Mradi huo hadi sasa umekwisha enezwa katika Wilaya 82, Lushoto ikiwa ni mojawapo.

Mkakati mwingine ni kuanzisha usajili wa vizazi na vifo katika ngazi ya vijiji ambapo Maafisa Watendaji wa Vijiji watakuwa na Rejesta Maalum za kuandikisha vizazi na vifo ambazo zitatumika baadaye kutoa vyeti. Hata hivyo, usajili huo umeanza kutumika hivi karibuni tu na bado uko katika maeneo machache. Baadhi ya maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Mbeya na Morogoro.

Mkakati mwingine ni kuifanya Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu kuwa Wakala wa Serikali ili iweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuboresha utaratibu wa kuandikisha vizazi na vifo nchini. Maandalizi ya kuifanya Idara kuwa Wakala yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mikakati hiyo, Wizara yangu kupitia Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu, ina mikakati ya kuendelea kutoa mafunzo kupitia vyombo vya habari kwa kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili la usajili wa vizazi na vifo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza katika jibu la kipengele (a), hivi sasa Maafisa Watendaji wa Vijiji, wanasajili vizazi na vifo kwa kutumia Rejesta Maalum. Hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa William Shellukindo kwamba, utaratibu



anaoupendekeza unawezekana na tayari umeanza kutekelezwa katika baadhi ya mikoa hapa nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, hivi sasa utaratibu tulionao ni wa kuweka takwimu kiwilaya na baadaye kuziwasilisha kwa Msajili Mkuu. Hivyo, hatuna takwimu za vizazi na vifo mahsusi kwa Jimbo la Bumbuli. Tunazo takwimu za Wilaya yote ya Lushoto ambazo tunaweza kumpatia Mheshimiwa Mbunge, baada ya kujibu swali hili.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya watoto, ingawa nina maswali madogo ya nyongeza. Je katika uandikishaji wa vifo na vizazi kuna gharama zozote na kama zipo, si vyema zikaondolewa ili wananchi wajitokeze kwa wingi kuandikisha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, usajili wa vizazi una gharama zake. Kwa mtoto aliyesajiliwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu toka azaliwe gharama yake ni Sh.3,500/= kwa cheti ili mradi tu atakapokwenda kusajili awe ana taarifa ya kizazi ambayo inatolewa katika zahanati na vituo vya afya kama nilivyosema. Kwa mtoto aliyesajiliwa ndani ya kipindi cha miezi minne na kuendelea ada yake ni Sh.4,000/=. Lakini kwa yule ambaye amesajiliwa katika kipindi cha kuanzia miaka 10 toka azaliwe ada yake ni Sh.10,000/=. Lakini kwa ada ya cheti cha kifo ni 3,500/=.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia utaona kwamba, gharama hizi si kubwa sana endapo usajili utafanyika muda mfupi baada ya mtoto kuzaliwa. Lakini pia labda nikumbushe, kwa kuwa ninajibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, aliwahi kusema katika Bunge hili Tukufu kwamba, kila shughuli ina gharama zake. Kwa hiyo, pale unapozalisha mali kuna gharama zake na ukizaa pia kuna gharama zake. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi vijijini hawaelewi utaratibu huu wa kusajili na kwa kuwa ili kurahisisha Daftari la Wapiga Kura ni lazima uwe na cheti cha kuzaliwa.

Ni kwa nini Serikali isielekeze hospitali au sehemu wanako jifungulia akina mama kwamba wapewe vyeti, vyeti vile vikae pale hospitalini pindi anapojifungua anapewa cheti pale pale, kwa nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba, katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali, kunakuwa na fomu maalum ambazo ni za kuwaarifu uzazi. Kwa hiyo, inaitwa Taarifa ya Uzazi. Cheti hiki ndicho kinachomfanya baadaye yule anayeandikisha aweze kupata cheti cha kuzaliwa. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa sheria ya uandikishaji wa vizazi na vifo. Sheria hii inataka kuwepo na taarifa ya kuzaliwa na baadaye taarifa hizo hukusanywa na

kupelekwa kwa Msajili wa Wilaya, kwa hiyo, huo ndiyo msimamo wa kisheria hivi sasa. (Makofi)

Lakini tunafahamu kwamba, pia wapo wanawake wengi sana katika nchi yetu ambao wanajifungua nje ya vituo vya afya na huu utaratibu wa kuwawezesha Watendaji wa Vijiji kuandikisha ni namna mojawapo ya kuharakisha zoezi zima la uandikishaji.

Lakini pamoja na hayo, niseme kwamba, Serikali imewahi pia kupokea rai kwamba, utaratibu uharakishwe na uletwe karibu zaidi na wananchi na hivi sasa Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu, inatazama uwezekano wa kuwa takwimu hizi zinakusanywa kwenye ngazi ya chini kabisa na pia kurahisisha usajili lakini sharti la muhimu ni kuangalia kwanza sheria yenyewe ambayo inataka usajili ufanyike kwenye ngazi hii ya Wilaya. (Makofi)

Na. 166

### **Mawasiliano ya Simu**

**MHE. KHALID S. SURU (k.n.y. MHE. DAMAS P. NAKEDI)** aliuliza:-

Kwa kuwa miundombinu ya mawasiliano ya simu ni nyenzo mojawapo muhimu katika uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ukweli kwamba gharama za simu hapa Tanzania ziko juu kuliko ilivyo kwa nchi jirani zetu na Ulaya?

(b) Je, gharama hizo za simu ni ghali kwa kiasi gani ikilinganishwa na gharama za nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za Ulaya Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, gharama za simu hapa nchini ni za juu kulinganisha na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(a) Gharama za uwekezaji katika mitandao (*Network Investment Costs*) ni za juu kwa Tanzania. Hii inachangiwa na ukubwa wa nchi kijiografia ukilinganisha na Kenya, Uganda na nchi nyingi za Ulaya Magharibi.

(b) Kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi yetu dhidi ya dola ya Kimarekani na sarafu nyingine zitumikazo kwenye biashara za kimataifa.

(c) Ukuaji mdogo wa soko la huduma za simu unaotokana na kukua polepole kwa Watanzania wenye uwezo wa kutumia huduma hizo.

(d) Uchache wa miundombinu mwambata, kama umeme na barabara inachangia ongezeko kubwa la gharama za uendeshaji.

(e) Kodi mbalimbali zinazotowazwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

(f) Gharama za maingiliano ya simu baina ya mitandao.

Kwa wastani gharama za simu za kulipia kabla (*Prepaid*) kwa simu za ndani kwa dakika (katika Shilingi za Kitanzania) ni kama zifuatavyo:-

	<i>United Kingdom</i>	<i>Uganda (VAT 17%)</i>	<i>Kenya (VAT 16%)</i>	<i>Tanzania (VAT 20%)</i>
<i>Peak</i>	210	257	320	430
<i>Off-Peak</i>	210	193	320	430

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Serikali kuwa, mwelekeo wa bei za simu nchini utazidi kushuka kadri ushindani wa utoaji wa huduma ya simu unavyoongezeka nchini.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza na pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mawasiliano ya simu ni muhimu sana kwa sababu yanachochea maendeleo huko vijijini na kwa sababu simu hizi ni ghali sana, sasa kwa nini Serikali isikubali kuchangia ruzuku ili wananchi wetu waweze kuweka simu na waweze kununua kwa bei nafuu ili waweze kupata simu, kwa sababu simu sasa hivi siyo anasa tena ni maendeleo?

Pili, Serikali imekuwa ikitoa ahadi za kueneza simu vijijini nchini kote pamoja na kule Kondo katika maeneo ya Tarafa za Pahi, Bereko, Kolo, Goima, Kwamtoro, Farukwa na Mondo. Je, Serikali ina mpango gani kwenda kumaliza hiyo ahadi yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama unavikumbuka vijiji vilivyotajwa? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, nia ya Serikali kupeleka simu vijijini bado ipo na tutaendelea. Kimsingi tulikubaliana tunaanza kwenye Mikoa, Wilaya halafu kwenye vijiji. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni hivi karibuni tu tumepata nafasi ya kupeleka simu Kondo. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, anisaidie mtambo ule una watu 1,000 lakini mpaka sasa hivi kuna watu 320 tu.

Ili huduma ziende vizuri, watumiaji wakitumia mzunguko ule hela ile inatumika kufanya shughuli nyingine na kuwekeza sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nikijibu huko nyuma kwamba, kutakuwa na mpango maalum wa simu vijijini na mpango huu uko njiani kukamilishwa. Shughuli hizi zikimalizika, nina hakika vijiji vyote alivyovitaja Mheshimiwa Khalid Suru, vitanufaika.

Na. 167

### **Leseni ya Kusafirisha Mizigo Tanzania**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y. MHE DR. LAWRENCE M. GAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa leseni za kusafirisha mizigo Tanzania (*TBL*) inatolewa Mjini Dar es Salaam tu na hivyo kuleta usumbufu na gharama kubwa wahasika. Je, ni sababu gani zinazofanya leseni hizo zisitolewe Mikoani au Wilayani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mikoa na Wilaya hazitoi leseni za Kitaifa za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa sababu hazina mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na.1 ya mwaka 1973, Mamlaka Kuu ya Leseni (*Central Transport Licensing Authority*), chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ndio taasisi pekee iliyoruhusiwa kutoa huduma hiyo. Makao Makuu ya Mamlaka yako Dar es Salaam. Mamlaka hufanya Ziara Mikoani ambapo leseni hizo hutolewa. Aidha, ziara hizi husaidia Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine kutatua kero za wateja na pia kudhibiti leseni zisigushiwe.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapunguzia usumbufu na gharama kubwa wahasika, Mamlaka Kuu ya Leseni hutoa ratiba ya ziara zake Mikoani na kuwaarifu wahasika mapema kupitia magazeti na Mamlaka za Leseni za Usafirishaji za Mikoani ili waweze kujiandaa kupokea huduma hizo.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alitangaza kuondoa ukiritimba katika masuala ya biashara na kwa kuwa moja kati ya kero kubwa sana ni hii ya Wizara kuhodhi masuala yote ya kutoa

leseni pamoja na sheria, je, haoni kwamba sasa huu ni wakati muafaka wa kubadilisha sheria hiyo ili wananchi na wafanyabiashara waweze kunufaika katika masuala ya usafirishaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba, ni lengo la Serikali kuondoa matatizo kama hayo ambayo ameyazungumzia ili kuwapa nafuu wananchi kupata huduma kwa urahisi zaidi. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nia na lengo la ku-centralize mambo haya ni kuondosha kasoro mbalimbali ambazo zimejitokeza za kughushi leseni. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuanzia Julai, 2003 mpaka leo 2004 leseni zilizoghushiwa ni 2,183 lakini huko Mikoani leseni za Mikoa kwa magari ya Mikoani zinatolewa katika Mikoa yote.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wake umekwisha, sasa tunaendelea kama kawaida na matangazo ya vikao vya leo. Kuna matangazo mawili la kwanza ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Athumani Janguo, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane katika kikao maalum cha Kamati hiyo baada ya kipindi hiki cha maswali katika ukumbi Na.231, lakini vile vile anawakaribisha Wabunge wote wa Mkoa wa Pwani, wahudhurie kikao hicho, nafikiri kuna masuala maalum yanazungumzwa.

Kamati nyingine ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa tano kwenye ukumbi na.227, ghorofa ya pili.

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 - Wizara ya Ujenzi**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kwa kukamilisha kazi ya kupitia, kujadili na kutoa ushauri kuhusu Bajeti ya Wizara yangu na hatimaye kuidhinisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005. Wizara yangu imejitahidi kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu katika Bajeti hii na tutaendelea kuyafanyia kazi maelekezo ya Kamati yaliyobaki na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole zangu nyingi kwa kifo cha Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, ambaye alikuwa Mjumbe wa

Kamati ya Miundombinu. Wakati wa uhai wake alitoa michango mizuri sana kwenye Kamati hii. Mungu aiweke roho ya marehemu mahali peponi, *amen*.

Dira ya Wizara ya Ujenzi ni kuendeleza Sekta ya Ujenzi ili iwe endelevu, yenye ufanisi na inayotoa huduma bora na nafuu katika mazingira ya ushindani ili kuchochea na kuleta ufanisi katika maendeleo ya jamii na kiuchumi na hivyo kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Aidha, katika kuendeleza Sekta ya Ujenzi, ili kutumia kikamilifu faida ya kijiografia iliyonayo Tanzania katika kuziunganisha nchi kadhaa tunazopakana nazo na Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Kigoma, Bukoba na Mtwara, Wizara yangu inaendelea kutekeleza ukarabati na ujenzi wa Barabara Kuu kwa kiwango cha lami katika Kanda Kuu Tisa za Usafirishaji kwa kadri hali ya uchumi wetu na bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika uanzishwaji wa Wakala wa Barabara (*TANROADS*) na Wakala wa Majengo (*TBA*), Taasisi hizi sasa ndizo zenye majukumu ya utekelezaji wa kazi za barabara na majengo na nyumba za Serikali. Kazi hizi zilikuwa zinafanywa na Wizara moja kwa moja hapo awali. Majukumu yaliyobaki yanayoendelea kutekelezwa na Wizara yanahusu:-

- Kuandaa Sera, kubuni Mikakati na kupanga Mipango inayolenga katika ukuzaji, uimarishaji na uendelezaji wa sekta ya ujenzi nchini katika muda mfupi, wa kati na mrefu;
- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi kwa kuzingatia mikakati iliyowekwa;
- Kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo pamoja na Wakala nyingine zinazotarajiwa kuundwa chini ya Wizara kama vile Wakala wa Ufundi na Umeme (*Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency - TEMESA*) na Wakala wa Bohari Kuu ya Serikali (*Government Stores Agency - GSA*);
- Kuratibu shughuli za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi ambazo ni Baraza la Taifa la Ujenzi na Bodi za Usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Usimamizi wa Vifaa;
- Kutafuta fedha za nje na za ndani za kugharamia miradi ya barabara, madaraja, vivuko na kadhalika;
- Kuandaa na kusimamia viwango vya ubora wa kazi za ujenzi, ukarabati pamoja na matengenezo ya barabara; ujenzi nyumba na majengo ya Serikali; vifaa vya kawaida vitumiwavyo na Serikali; mitambo; magari na vifaa vya umeme.
- Kusimamia shughuli za Usalama wa Barabara (*Road Safety*);

- Kusimamia shughuli za ununuzi, ukarabati na matengenezo ya magari, viyoyozi na vifaa vya elektroniki, kuendesha vivuko na ukodishaji wa magari, mitambo ya kokoto na mitambo ya barabara ambavyo ni mali ya Serikali; na
- Kusimamia Maendeleo ya Watumishi wa Wizara.

Aidha, majukumu mengine ya Wizara yanayotekelezwa kupitia Wakala, Baraza la Ujenzi, Bodi na Vituo/Vyuo vilivyo chini ya Wizara ni kama yalivyofafanuliwa kwa kirefu katika aya ya 38 hadi 69.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha majukumu yaliyotajwa hapo juu, Wizara imejiwekea mikakati ifuatayo:-

- Kutafuta vyanzo vya ziada vya fedha za Mfuko wa Barabara ili kukidhi mahitaji ya matengenezo ya mtandao mzima wa barabara;
- Kutoa kipaumbele katika ukarabati na ujenzi wa barabara kwa kufuata Kanda Kuu za Usafirishaji, Barabara za Mikoa na za Wilaya ambazo ni muhimu kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya kilimo na huduma nyingine muhimu za kitaifa;
- Ili kuimarisha mabadiliko yanayofanyika katika sekta ya Ujenzi, Wizara itaendelea kuboresha uwezo (*Capacity Building*) wa Wakala wa Barabara na Majengo ili kuongeza ufanisi zaidi katika matengenezo na ukarabati wa barabara, nyumba na majengo ya Serikali;
- Kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitambo ya ujenzi kwa kuimarisha karakana za Serikali na kuhamasisha watu binafsi kuanzisha kampuni za kukodisha mitambo;
- Kukaribisha Sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa miradi ya barabara na majengo ya Serikali. Aidha, Wizara yangu inakamilisha Mwongozo rasmi utakaoweka wazi utaratibu wa Ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za ujenzi wa barabara, majengo na madaraja;
- Kuendeleza mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa kizalendo ili wasimamie na kutekeleza vizuri mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara;
- Kusimamia Sheria ya Udhhibiti wa Uzito wa Magari na matumizi bora ya barabara kwa kuwashirikisha wadau wote;
- Kuimarisha huduma za vivuko nchini kwa kununua vivuko vingine vipya vyenye uwezo mkubwa na kuvifanyia ukarabati vivuko vilivyopo hivi sasa.
- Kuwaelimisha wananchi ili waweze kutambua mipaka ya maeneo ya barabara (*Road Reserve*) na kutayarisha ramani za barabara zitakazoonyesha mipaka ya miliki ya

barabara zote nchini. Aidha, uwekaji wa alama za kuonyesha mipaka ya maeneo ya barabara nao sasa umepewa umuhimu katika miradi yote inayotekelezwa.

- Kuendeleza teknolojia ya nguvu kazi ili kuwapa uwezo wananchi wengi zaidi kushiriki katika kazi za matengenezo ya barabara katika maeneo yao bila kusubiri msaada kutoka Serikalini;

- Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi, kuendesha mafunzo kwa Wafanyakazi wa Wizara ili kuwajengea uwezo wao wa kufanya kazi na kukamilisha uanzishwaji wa Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*) na Wakala wa Bohari Kuu ya Serikali (*GSA*).

Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) zimepanga kutekeleza miradi ya barabara katika Kanda tano. Miradi inayohusika ni ile iliyokubaliwa katika Mkutano wa mwaka 1998 na pia miradi mipya ambayo ilikubaliwa iongezwe kwenye mtandao wa miradi ya barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa mashauriano kati ya Wahisani na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 29 - 30 Aprili, 2003. Wahisani walikubaliana na utekelezaji wa miradi iliyokuwepo toka mwaka 1998 na miradi mipya iliyoongezwa. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kushirikiana na Sekretariati ya Jumuiya hiyo tunaendelea kuwasiliana na Wahisani kwa lengo la kufanikisha ahadi hiyo. Hali halisi ya maendeleo ya upatikanaji fedha ama utekelezaji wa kila mradi ni kama ilivyofafanuliwa katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2003 kilifanyika kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali za nchi za Mashariki mwa Afrika (*Eastern Africa Sub-region Summit*), Mjini Nairobi - Kenya. Pamoja na mambo mengine, Wakuu wa Nchi walikubaliana msisitizo uwekwe kwenye miradi ya barabara iliyoko kwenye kanda tano za barabara za Afrika Mashariki zilizokwisha ainishwa. Aidha, Wizara yangu imeainisha miradi ya barabara itakayoingizwa katika Mkakati Mpya wa Kuondoa Umaskini (*The New Partnership for Africa's Development - NEPAD*). Miradi hiyo ni pamoja na barabara zenye urefu wa kilomita 7,499 na Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji. Miradi hii inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani 2,414.4 milioni.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Programu ya uendelezaji wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara unaendelea kwa miradi mikubwa (*Anchor Projects*) mitatu. Hatua zilizofikiwa kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Mtwara - Masasi - Songea - *Mbamba Bay*, kazi ya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*) ilimalizika mwezi Januari, 2004. Kazi ya usanifu wa kilomita 200 kati ya Songea na Matemanga itafanyika katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa kugharamiwa na fedha zilizobaki baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu.

(ii) Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, zinaendelea. Serikali ya Japan imekubali kimsingi tangu mwezi Oktoba, 2003 kuwa itasaidia ujenzi wa daraja hili na imeahidi kuleta ujumbe Tanzania kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2004 ili kufanya uchunguzi wa kitaalam. Katika mwaka wa



fedha wa 2004/2005 Serikali ya Tanzania imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuanza kufanya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*).

(iii) Serikali imeendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wa Mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma - Katewaka, kwa lengo la kuhakikisha kuwa mradi utakapoteklezwa utakuwa na manufaa kwa uchumi wa nchi hususan sekta ya umeme. Serikali iliona ni vema kwanza ijiridhishe na matokeo ya awali ya utafiti uliofanywa na wawekezaji kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi, kiufundi, kifedha na pia masuala ya mazingira. Mnamo mwezi wa Mei, 2004 Serikali imewaelekeza NDC na Wizara ya Nishati na Madini kufanya majadiliano na wawekezaji wa mradi kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2004 ulifanyika mkutano huko Maputo - Msumbiji uliojumuishia nchi zinazotekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Kikanda (*Spatial Development Initiative*). Nchi zilizowakilishwa ni Msumbiji, Afrika ya Kusini, Zimbabwe, Malawi, Namibia, Angola na Tanzania. Kimsingi, mkutano ulisisitiza umuhimu wa kanda za maendeleo. Mkutano ujao wa pamoja kwa nchi hizi utafanyika Tanzania kabla ya mwisho wa mwaka 2004. Mkutano huu utasaidia kuutangaza Mpango wa Maendeleo na miradi iliyomo katika Ukanda wa Mtwara kwa wawekezaji wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mtandao wa barabara zetu hapa nchini umekuwa unakua mwaka hadi mwaka. Mwaka 1961 kulikuwa na barabara za lami zenye urefu wa km 1,300 na za changarawe/udongo km 29,500. Hadi kufikia mwaka huu 2004 kuna km 4,837 za lami na km. 80,063 za changarawe/udongo. Mategemeo ni kwamba mwishoni mwa mwaka 2005/06 tutakuwa na jumla ya km. 6,500 za lami na hii itatokana na kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Singida - Manyoni - Dodoma, Somanga - Nangurukuru - Lindi - Mingoyo, Mtukula - Muhutwe - Lusahunga, Shelui - Nzega, Ilula - Tinde/Isaka - Nzega, Makuyuni - Ngorongoro, Dar - Bagamoyo, Singida - Shelui, Barabara za Jiji la Mwanza na Barabara za Jiji la Dar es Salaam, Makutano - Butiama, Longai - Rombo, Dar es Salaam - Kibiti n.k kazi ambazo ziko kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, ikifika mwaka 2008/2009 tutakuwa na jumla ya km. 8,500 za barabara za lami hii itatokana na kukamilika kwa barabara ya Singida - Babati - Minjingu, Babati - Dodoma - Iringa, Tunduma - Sumbawanga - Kigoma - Nyakanazi, Tanga - Horohoro, Usagara - Geita - Kyamorwa/Biharamulo, Musoma-*Fort Ikoma*, Itigi - Igalula - Tabora - Ipole, Mbeya - Chunya - Makongolosi na 200 km za barabara ya Mtwara - Mbambabay na kadhalika. Pia kama mambo yataendelea hivi tunategemea ikifika mwaka 2012 barabara zote kuu zenye urefu wa km 10,300 ziwe zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, miradi ya barabara iliyokamilika, inayoendelea kutekelezwa na iliyopo katika maandalizi katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu (tangu mwaka 1995) ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Barabara iliyokamilika (1995 - 2004) ni ifuatavyo:-

- (i) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Dar es Salaam - Mlandizi (km. 55) kwa msaada wa *DANIDA* kwa gharama ya Sh. 33.6 bilioni.
- (ii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kawawa (km. 7.5) pamoja na barabara nyingine za Dar es Salaam (km. 15.18) kwa msaada wa Serikali ya Japan kwa gharama ya Sh. 22.75 bilioni.
- (iii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya *Wazo Hill* - Bagamoyo (km. 43) kwa msaada wa Serikali ya Italia kwa gharama ya Sh. 14.6 bilioni.
- (iv) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mwanza - Ilula (km. 101) kwa mkopo wa *IDA* kwa gharama ya Sh. 27 bilioni.
- (v) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Njenga - Masaniga (km.11) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 3.4 bilioni.
- (vi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mikumi - Kidatu (km. 36) kwa msaada wa *Swiss Development Cooperation (SDC)* kwa gharama ya Sh. 4.41 bilioni.
- (vii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kasumulo - Ibanda - Uyole (km. 103) kwa msaada wa *European Commission (EC)*, kwa gharama ya Sh. 6.2 bilioni.
- (viii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya *KCMC* - Mweka (km. 9) kwa msaada wa *NORAD* kwa gharama ya Sh. 829.5 milioni.
- (ix) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (km. 5.2) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 1.132 bilioni.
- (x) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara (km. 14) zierendazo kwenye Hoteli za Kitalii zilizopo kwenye Pwani ya Jangwani na Kunduchi Mkoani Dar es Salaam kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 4.028 bilioni.
- (xi) Ujenzi wa Daraja la Mto Rufiji (*Mkapa Bridge*) kwa mkopo wa *Kuwait Development Fund* na *OPEC/SAUDI ARABIA* kwa gharama ya Sh. 35 bilioni.
- (xii) Ujenzi wa madaraja 22 katika barabara ya Tanga - Horohoro, *TANZAM* na Tunduma - Sumbawanga kwa mkopo wa Benki ya Dunia kwa gharama ya Sh. 15.46 bilioni.
- (xiii) Ununuzi wa Vivuko vya Kilombero na Ukara kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 2.0 bilioni.
- (xiv) Ukarabati kwa kiwango cha lami (km. 104) barabara ya Himo - Arusha kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa gharama ya Sh. 12.22 bilioni.

(xv) Ujenzi kwa kiwango cha lami (km. 27.48) barabara ya Himo - Holili na Himo - Marangu kwa msaada kutoka Serikali ya Norway kwa gharama ya Sh. 5.231 bilioni.

(xvi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kobero - Nyakasanza (km. 59) kwa msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwa gharama ya Sh. 9.5 bilioni.

(xvii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Musoma - Sirari (km. 84) kwa msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwa gharama ya Sh. 18 bilioni.

(xviii) Ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Dar es Salaam Mkuranga (km. 60) kwa mkopo kutoka mifuko ya Kuwait na *OPEC* kwa gharama ya Sh. 9.12 bilioni.

(xix) Ukarabati kwa kiwango cha lami (km. 2.5) barabara ya Msamvu - Morogoro kwa msaada kutoka Serikali ya Uswisi kwa gharama ya Sh. 2.0 bilioni.

(xx) Ujenzi kwa kiwango cha lami (km. 14) barabara ya *Monduli Junction - TMA* - Monduli kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 860 milioni.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Barabara inayoendelea ni ifuatayo:-

(i) Ukarabati wa barabara ya lami ya Chalinze - Morogoro - Melela (km. 129) kwa msaada wa *DANIDA* kwa gharama ya Sh. 37 bilioni.

(ii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma - Manyoni (km. 127) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 65 bilioni.

(iii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Singida (km. 119) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 40 bilioni.

(iv) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Shelui - Nzega (km. 108) kwa mkopo wa *African Development Bank (ADB)* kwa gharama ya Sh. 24 bilioni.

(v) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nzega/Ilula - Tinde/Isaka (km. 168) kwa msaada wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) kwa gharama ya Sh. 59 bilioni.

(vi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kagoma - Muhutwe (km. 24) kwa mkopo wa *OPEC* kwa gharama ya Sh. 5.2 bilioni.

(vii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Muhutwe - Mutukula (km. 112) kwa mkopo wa *African Development Bank (ADB)* kwa gharama ya Sh. 19 bilioni.

(viii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Somanga - Masaniga/Matandu (km. 33) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 13.33 bilioni.

(ix) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nangurukuru - Mbwemkulu - Mingoyo (km. 190) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 92.8 bilioni.

- (x) Ukarabati wa barabara za Mwanza Mjini na Mwanza - Nyanguge (km. 58) kwa msaada wa *EU* kwa gharama ya Sh. 19 bilioni.
- (xi) Ukarabati wa barabara ya Tunduma - Songwe (km. 70) kwa msaada wa *NORAD* kwa gharama 12.23 bilioni.
- (xii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Makuyuni - Ngorongoro (km. 77) kwa msaada wa Serikali ya Japan kwa gharama ya Sh. 23.0 bilioni.
- (xiii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mkuranga - Kibiti (km. 79) kwa mkopo wa *KUWAIT* na *OPEC* kwa gharama ya Sh. 10.5 bilioni.
- (xiv) Matengenezo ya barabara ya *TANZAM* sehemu ya Mlima wa Kitonga (km. 7.64) kwa msaada wa Serikali ya Japan kwa gharama ya Sh. 7.15 bilioni.
- (xv) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Pugu - Kisarawe (km. 6) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 1.8 bilioni.
- (xvi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Halali - Ilembula (km. 5.2) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 427 milioni.
- (xvii) Ujenzi wa barabara (km. 923) kwa kiwango cha changarawe katika Mkoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kagera kwa mkopo wa (*African Development Bank - ADB*) kwa gharama ya Sh. 21.3 bilioni.
- (xviii) Upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa daraja la Furuu katika Mkoa wa Morogoro kwa msaada wa Serikali ya Japan kwa gharama ya Sh. 500 milioni.
- (xix) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Mwanza (Usagara) - Kyamyorwa/Biharamulo (km. 338) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 8.605 bilioni.
- (xx) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara ya Tunduma - Sumbawanga (km. 230) umekamilika mwezi Machi, 2004 kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa gharama ya Sh. 1.520 milioni.
- (xxi) Usanifu wa kina na usimamizi wa ujenzi wa barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai (km. 70) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 8.89 bilioni.
- (xxii) Upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa barabara ya Minjingu - Babati - Singida (km. 223) kwa kutumia fedha za ndani na wafadhili kwa gharama ya Sh. 984.4 milioni.
- (xxiii) Upembuzi yakinifu wa barabara ya Rujewa - Madibira - Mafinga (km. 153) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 240.8 milioni.

(xxiv) Usanifu wa awali na wa kina wa barabara ya Mbeya - Chunya - Makongolosi (km. 125 kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 1.08 bilioni.

(xxv) Usanifu wa kina wa barabara ya Msimba - Ikokoto - Mafinga (km. 167) kwa mkopo wa Benki ya Dunia wa Sh. 840 milioni.

(xxvi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kiabakari - Butiama (km. 12) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 2.4 bilioni.

(xxvii) Ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma - Morogoro (km. 256) kwa msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwa gharama ya Sh. 27.06 bilioni.

(xxviii) Ujenzi kwa kiwango cha changarawe barabara ya Uvinza - Malagarasi (km. 54) kwa kutumia fedha za ndani kwa gharama ya Sh. 1.7 bilioni.

(xxix) Usanifu wa daraja jipya la Mpiji umekamilika na tathimini ya zabuni za ujenzi imekamilishwa na Mjenzi ameteuliwa 2004. Serikali ya Tanzania inagharamia mradi huu kwa kutumia uwezo wake wa ndani. Gharama za usanifu na usimamizi na ujenzi ni Sh. 1.2 bilioni.

(xxx) Upembuzi yakinifu wa barabara ya Mtwara - Songea - *Mbamba Bay* (km. 833) kwa msaada wa *Kuwait Development Fund* kwa gharama ya Sh. 1 bilioni.

(xxxi) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kagoma - Biharamulo - Lusahunga (km. 154) kwa mkopo kutoka *ADB*. Zabuni za ujenzi zimeitishwa mwezi Aprili, 2004. Jumla ya Sh. 73.0 bilioni zinategmewa kutumika.

(xxxii) Usanifu wa kina wa barabara ya Arusha - Namanga (km. 105) hadi *Athi River* kwa mkopo kutoka *ADB*. Mkataba wa Usanifu wa kina umesainiwa tarehe 16 Aprili, 2004 kwa gharama ya *US\$ 951,289.74*. Mradi wote (usanifu na ujenzi) unategemewa kugharimu Sh. 40 bilioni.

(xxxiii) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Singida - Shelui (km. 110) kwa mkopo wa Benki ya Dunia. Taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi zinaendelea. Jumla ya Sh. 50.0 bilioni zimetengwa.

(xxxiv) Maandalizi ya ujenzi wa Barabara ya Kilwa, aidha, ukarabati wa Barabara ya Mandela (*Port Access*) (km. 17) kwa msaada wa *EU*. Zabuni za ujenzi zimetangazwa mwezi Machi, 2004. Miradi yote miwili itagharimu Sh. 26 bilioni.

(xxxv) Mkataba wa Usanifu wa kina wa barabara ya Ndundu - Somanga (km. 60) unatarajiwa kusainiwa mwezi Julai, 2004. Kazi ya usanifu itakamilika mwezi Machi, 2005 na kufuatiwa na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa mikopo kutoka Kuwait na *OPEC* kwa gharama ya Sh. 11 bilioni.

(xxxvi) Usanifu wa daraja jipya la Ruvu kwa kutumia fedha za ndani, mkataba wa usanifu wa kina umetiwa saina mwezi wa Aprili, 2004 na ujenzi unakadiriwa kugharimu Sh. 2 bilioni hivyo mradi wote utagharimu Sh. 2.52 bilioni.

(xxxvii) Daraja la Umoja Serikali ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji zimetia saina makubaliano ya awali (*Memorandum of Understanding*) kuhusu ujenzi wa Daraja la Umoja tangu tarehe 28 Machi, 2002.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizungumza na Serikali ya Japan alipokwenda kuhudhuria Mkutano wa *TICAD III* mwezi Oktoba, 2003. Katika mazungumzo hayo, Serikali ya Japan ilikubali kimsingi kuwa itasaidia ujenzi wa Daraja la Umoja. Serikali ya Japan imeahidi kuleta ujumbe Tanzania kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2004 ili kufanya uchunguzi wa kitaalamu. Wizara imetenga Sh. 800 milioni kwenye bajeti ya 2004/2005.

(xxxviii) Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ujenzi wa Daraja kuunganisha eneo la Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam, Serikali imekaribisha wawekezaji mbalimbali ili kushiriki katika ujenzi na uendeshaji wa daraja hilo. Ujenzi wa daraja hili la njia mbili (*Dual Carriageway*) unakisiwa kugharimu *US\$ 46 milioni* (Sh. 46 bilioni za Tanzania). Serikali na *NSSF* tumeingia katika mkataba wa maelewano ambapo, *NSSF* watahusika katika ujenzi wa daraja hili, maandalizi yako kwenye hatua nzuri.

(xxxix) Miradi ya Ujenzi - Zanzibar (*US\$ 23.376 Milioni*). Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ujenzi inayoendelea kwa upande wa Zanzibar ni kama ifuatavyo:-

- Ukarabati wa barabara ya Mkoani hadi Mtuwaliwa yenye urefu wa kilometa 5.5. Barabara hii inajengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa gharama ya *U.S. \$ 2.104 milioni*. Ujenzi uko katika hatua za mwisho kukamilika.

- Ukarabati wa barabara ya Mtuwaliwa hadi Chake yenye urefu kwa kilometa 23. Barabara hii pia inajengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa mkopo wa *U.S.\$ 3.584 milioni*. Mradi bado unaendelea.

- Barabara ya kiungo kuelekea uwanja wa ndege wa Pemba. Barabara ina urefu wa kilometa 6 ambayo pia inajengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa gharama ya *U.S.\$ 0.802 milioni*. Kazi bado zinaendelea.

- Barabara za Kati Unguja zenye jumla ya kilometa 30. Hizi zinajengwa kwa mkopo kutoka Mfuko wa *OPEC* na Kuwait.

- Ukarabati wa dharura wa uwanja wa ndege wa Zanzibar. Mkataba wa matengenezo hayo umetiwa saina mnamo mwezi Aprili, 2004. Ukarabati huu umewezekana kutokana na mkopo kutoka Benki ya Dunia *U.S. \$ 9,086*.

(xxxix) Miradi ya *RUSIRM* (Sh. 35 bilioni). Mradi wa *RUSIRM* ni wa muda wa miaka mitano ya matengenezo ya barabara kwa mikoa ya Iringa Kusini na Ruvuma.

Mradi ulianza rasmi Julai, 2000 na utaisha Juni, 2005. Mradi unagharamiwa kwa pamoja kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya *Euro* 34.17.

(xli) Matengenezo ya barabara chini ya *TANROADS* (Sh. 139.258 bilioni). Kupitia *TANROADS* jumla ya Sh. 27.413 bilioni (2001/2002), Sh. 31.063 bilioni (2002/2003), Sh. 35 bilioni (2003/2004), zilitengwa na kutumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja na Sh. 45,788 bilioni zimetengwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja. Fedha hizi zote zimetokana na fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*).

Miradi mingine ya barabara kuu, barabara za mikoa na vijiji zinazoshughulikiwa na Wizara ya Ujenzi zimetolewa maelezo kwenye Kitabu chetu cha Bajeti 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Barabara ifuatayo ipo kwenye maandalizi:-

(i) Babati - Dodoma - Iringa kazi za kuanza usanifu zimepangwa kuanza mwaka huu kwa kutumia fedha toka *IDA* na fedha za Serikali. Jumla ya Sh. 2.41 bilioni zimetengwa kutumika kwa kazi za maandalizi.

(ii) Tabora - Kaliua - Malagarasi - Uvinza - Kigoma, usanifu na uandaaji wa tenda za zabuni unaendelea.

(iii) Tunduma - Sumbawanga - Kigoma - Nyakanazi, usanifu na upembuzi yakinifu umepangwa kufanyika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005.

(iv) Musoma - Fort Ikoma, usanifu kwa kiwango cha lami umepangwa kuanza mwaka huu wa fedha.

(v) Korogwe - Handeni - Kilosa - Mikumi, usanifu/upembuzi yakinifu umepangwa kuanza mwaka huu wa fedha.

(vi) Mwandiga - Manyovu, ujenzi wa kiwango cha lami (*Otta Seal*) unanza mwaka huu wa fedha wa 2004/2005.

(vii) Bagamoyo - Saadani - Tanga, wawekezaji wa *BOT* na *B.O.O.T.* wanakaribishwa.

(viii) Ununuzi wa kivuko cha Kigongo - Busisi, Sh. 2.5 Bilioni. zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu wa 2004/2005.

(ix) Kibaha - Tumbi Hospital, Sh. 500 milioni zimepangwa kutumika, tenda za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami zimetangazwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Miradi yote ambayo imekuwa ikitekelezwa kwa kutumia misaada ya wafadhili, pia imekuwa ikichangiwa na Serikali kwa kupitia fidia (*compesation*), misamaha ya kodi na kadhalika. Aidha, kasi ya ujenzi wa barabara

imeongezeka baada ya Serikali kupitia Waraka Na. 5 (2001) kuamua kutenga fedha kila mwezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara mpya. Fedha zilizotengwa ni Sh. 11 bilioni (2001/2002), Sh. 22 bilioni (2002/2003), Sh. 32 bilioni (2003/2004) na Sh. 49.95 bilioni (2004/2005).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza, kuna miradi mingi ya barabara ambayo aidha imekamilika, inaendelea au iko kwenye maandalizi. Miradi hii yote haitakuwa na maana kwa Taifa kama eneo la hifadhi ya barabara. Litaendelea kuvamiwa, hadi sasa Wizara imekwishatumia zaidi ya Tshs. 6.8 bilioni kulipia fidia kwa mujibu wa sheria. Napenda kusisitiza, kuwa, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa eneo la hifadhi ya barabara linaendelea kuwa wazi ili miradi niliyoitaja iweze kutekelezeka na hivyo lengo letu la kuwa na barabara kuu zote za lami ifikapo 2012 likamilike, Wizara ilikwishatoa tangazo kwenye vyombo vya habari.

Napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, kwa ushirikiano mkubwa wanautoa katika kuondoa majengo na viziwi vingine vilivyo ndani ya Hifadhi ya Barabara, Napenda kusisitiza kuwa, Serikali itaendelea kuziwekea alama ya X na kuzibomoa shughuli zote zilizoendelezwa ndani ya Hifadhi ya barabara kinyume na sheria yakiwemo mabango.

Napenda kutoa rai kwa wale waliobaki ndani ya hifadhi hiyo na ambao mali zao ziko ndani ya eneo la hifadhi na hasa zilizokwisha wekewa alama ya X, kuwa waache kuyaendeleza maeneo hayo.

Hii inatokana na ukweli kuwa zoezi hili ni la kudumu wala halijaitishwa na pale muda utakapofika wa kulihitaji eneo husika (baada ya kupata fedha za ujenzi), itabidi mali hizo ziondoke. Hali kadhalika miradi inayoendelea kukamilika isivamiwe na ujenzi wa aina yeyote katika hifadhi ya barabara. Tunasisitiza nyumba zilizowekewa X na zile zitakazowekewa X alama hiyo isifutwe. Kwa maana hiyo, miradi iliyokamilika, inayoendelea na miradi iliyo kwenye maandalizi ya kujengwa kwa sasa kama nilivyoitaja hapo juu, ni lazima majengo yaliyo kwenye hifadhi ya barabara yaondolewe mapema ili miradi husika isikwame.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu Dira, Majukumu na Mikakati ya Wizara yangu na mtandao wa barabara zetu na hali yako, naomba sasa kulieleza Bunge lako Tukufu, hali ya utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 3,724,943,000.00 kupitia Idara zake zinazokusanya mapato ambazo ni Ufundi na Umeme, Ugavi na Huduma za Utawala. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2004, jumla ya shilingi 3,072,020,781.58 zilikusanywa ambazo ni asilimia 82.5 ya malengo yaliyowekwa. Mchanganuo wa mapato hayo kwa kila idara umeonyeshwa kwenye Kiambatanisho Na. 1 kilichoko ukurasa wa 85. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 59,689,799,900 za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi shilingi 45,156,999,600 zilikuwa fedha za Mfuko wa



Barabara na shilingi 14,522,800,300 zilikuwa za Matumizi Mengineyo na Mishahara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2004, jumla ya shilingi 11,381,802,114 za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimetumika ambazo ni sawa na asilimia 78.4 ya fedha zote zilizotengwa kwa mwaka huu. Pia hadi Mei, 2004 jumla ya shilingi milioni 43,940 za Mfuko wa Barabara sawa na asilimia 97 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka huu zilikuwa zimetolewa kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, matengenezo ya Barabara Kuu na zile za Mikoa yaliyopangwa yalilenga kuhudumia kilomita 16,274 na madaraja 1,809 kwa kutumia jumla ya shilingi 61,399,954,000 ambapo shilingi 40,234,901,000 ni kutoka Mfuko wa Barabara na shilingi 21,165,063,000 zilikuwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2004, kazi zilizokuwa zimeanza na zinaendelea kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara zinahusisha mikataba 705 ya makandarasi yenye thamani ya shilingi 31,024,700,000 na kazi zinazofanywa na *TANROADS* moja kwa moja (*Force Account*) zenye thamani ya shilingi 2,861,210,000. Aidha, hadi mwishoni mwa mwezi Mei, 2004, jumla ya barabara zenye kilomita 10,898 na madaraja 1,119 vilifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha Ukarabati na Matengenezo ya Barabara Kuu katika Kanda nne zenye urefu wa km. 2,643 zilizoharibiwa na mvua za *El Nino* za Mwaka 1997/98. Kazi zinazofanywa kwenye Barabara za Kanda hizi ni pamoja na ukarabati/matengenezo ya madaraja madogo na makalavati, kutengeneza matuta ya barabara na kuweka changarawe kwenye sehemu zilizoharibika.

Mheshimiwa Spika, urefu halisi unaohusika na Ukarabati/Matengenezo haya kwenye Kanda zote nne ni Km 845 ambazo zimegawanywa kama ifuatavyo:-

- Ukanda wa Ziwa (Mwanza na Mara) km. 128, barabara za Usagara - Katoro, Nyamswa - Ikoma na Nyanguge - Musoma. Sehemu kubwa ya matengenezo zaidi ya asilimia 90 imekamilika;
- Ukanda wa Kati -Magharibi (Tabora, Rukwa na Singida) km. 325, Barabara za Tabora-Nzega, Tabora-Ipole-Koga, Ipole-Rungwa, Manyoni-Rungwa na Mpanda-Koga. Kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2004;
- Ukanda wa Kusini (Iringa, Ruvuma na Mtwara) km 203, barabara za Songea-Masasi, Songea-Mbamba Bay na Itoni-Manda. Mkandarasi anaendelea na kazi; na
- Ukanda wa Magharibi (Kigoma na Rukwa) km 189, barabara za Sumbawanga-Kasesya, Mpanda-Uvinza, Uvinza-Kanyani na Mwandiga-Manyovu, mkandarasi anaendelea na kazi.

Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya jumla ya Shilingi bilioni 14.56 ambapo

*ADB* itoa kiasi cha Shilingi bilioni 13.08 na Serikali ya Tanzania itachangia kiasi cha shilingi bilioni 1.48.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *RUSIRM* ni wa muda wa miaka mitano ya matengenezo ya barabara kwa Mikoa ya Iringa Kusini na Ruvuma. Mradi ulibuniwa mwaka 1995 na kuanza rasmi Julai, 2000 na utaisha Juni, 2005.

Mradi unagharamiwa kwa pamoja kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya *Euro* 34.17 milioni. *EU* itachangia *Euro* 21.8 milioni na Serikali ya Tanzania *Euro* 12.37 milioni. Kwa sasa hivi (2003/2004), mradi uko mwaka wa nne wa utekelezaji. Hadi kufikia Machi, 2004, zaidi ya km. 600 kati ya km. 898 zimefanyiwa ukarabati mkubwa kwa Mikoa ya Iringa na Ruvuma. Aidha, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya kawaida (*Routine and Recurrent Maintenance*) yamekuwa yakiendelea kwa barabara zote chini ya mradi zenye jumla ya km. 2,716 na kufanya ziendelee kupitika bila matatizo kwa mwaka mzima. Mpaka sasa Serikali ya Tanzania imechangia *Euro* 7,455,410 na *EU* imechangia *Euro* 15,581,375.52.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi milioni 157,180.04 kwa Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi milioni 48,989.47 zilikuwa fedha za hapa na shilingi milioni 108,191.57 zilikuwa fedha za nje. Kati ya fedha za hapa shilingi milioni 4,470.47 zilikuwa fedha za Mfuko wa Barabara na shilingi milioni 44,519.00 zilikuwa fedha za Maendeleo kutoka Hazina. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2004, shilingi milioni 43,340.95 sawa na 97.4% ya fedha zote za Maendeleo kutoka Hazina na shilingi milioni 3,994 sawa na asilimia 89 ya fedha za Mfuko wa Barabara zilizopangwa kwa mwaka 2003/2004 zilikwishatolewa. Aidha, katika kipindi hiki, Bajeti ya Maendeleo ilipunguzwa kwa shilingi bilioni 1.178 ili kuchangia dharura za ununuzi na usambazaji wa chakula cha njaa na kusaidia gharama za uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2003/2004 ni kama ulivyofafanuliwa katika maelezo ya Taasisi husika katika aya ya 38 hadi 69.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wizara imepata mafanikio mengi katika utekelezaji wa mipango ya mwaka 2003/2004, kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa mradi. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

(i) Kukamilika na kufunguliwa rasmi kwa Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji tarehe 2 Agosti, 2003. Aidha, madaraja mengine 23 kati ya Tunduma - Sumbawanga, Tanga - Horohoro na barabara ya *TANZAM* yamekamilika.

(ii) Kuweka Mawe ya Msingi kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa kiwango cha lami wa barabara za Mbwemkulu-Mingoyo (km. 95), Dodoma-Manyoni-Singida (km. 246), Ilula-Tinde/Isaka-Nzega (km. 168) na Songwe - Tunduma (km. 70). Aidha, barabara

nyingi zinaendelea kukarabatiwa kwa kiwango cha lami na changarawe ili nchi yote iendelee kupitika. Pia, madaraja yanaendelea kutengenezwa katika barabara mbalimbali.

(iii) Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizungumza na Serikali ya Japani alipokwenda Japan kuhudhuria Mkutano wa *TICAD III* mwezi Oktoba, 2003. Katika mazungumzo hayo, Serikali ya Japan ilikubali kimsingi kuwa itasaidia ujenzi wa Daraja la Umoja. Serikali ya Japan imeahidi kuleta ujumbe Tanzania kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2004 ili kufanya uchunguzi wa kitaalamu. Pia, ili kuhakikisha kuwa Daraja hili linapata fedha za ujenzi, Serikali ya Tanzania imeamua kuanza kutenga fedha za ndani katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2004/2005 ili kuanza kufanya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*).

(iv) Katika mwaka huu 2004 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), wameonyesha nia ya kuwekeza katika Daraja la Kigamboni. Serikali na *NSSF* tumeingia katika Mkataba wa Maelewano ambapo katika kipindi cha miezi sita, *NSSF* watawasilisha Serikalini mpango wao madhubuti wa kujenga daraja hili. Baada ya hapo mapendekezo yao yakikubalika na Serikali kazi za ujenzi zitaanza.

(v) Kivuko cha Ukara kimeshanunuliwa na kazi ya kukifunga itakamilika mwezi Juni, 2004. Aidha, Kivuko cha Kilombero ambacho kilinunuliwa mwaka 2002/03 kinaendelea kufanya kazi vizuri.

(vi) Usajili wa magari kwa namba za Serikali:

Usajili wa magari ya Serikali na ya miradi uliendelea kufanyika ili kupunguza matumizi mabaya ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali. Kuanzia mwezi Januari, 2002 hadi kufikia Mei, 2004, usajili umefanyika kama ifuatavyo: Magari 3,204 yamesajiliwa kwa namba za ST, magari 2,834 kwa namba za SU, magari 477 kwa namba za SM, magari 4,301 kwa namba za *DFP* na magari 105 kwa namba za *PT*. Aidha, pikipiki 1,207 zilisajiliwa kwa namba za ST, 338 kwa namba za SU, 215 kwa namba za SM, 1,487 kwa namba za *DFP* na 3 kwa namba za *PT*. Halikadhalika ilisajiliwa mitambo 199 kwa namba za *CW*, 93 kwa namba za SU, 21 kwa namba za SM na 81 kwa namba za *DFP*. Hivyo, kwa kipindi hicho jumla ya magari 11,026, pikipiki 3,250 na mitambo 394 imesajiliwa kwa namba za Serikali na kufanya jumla ya vifaa vilivyosajiliwa tangu zoezi lianze kuwa 15,064.

(vii) Wakala wa Majengo umewauzia Watumishi wa Serikali na wa Mashirika ya Umma nyumba zipatazo 5,248 kuanzia mwaka 2002 hadi sasa na fedha zinazopatikana zinatumiwa kujenga nyumba nyingine. Jumla ya shilingi 41,567,805,337.00 zinatarajiwa kukusanywa kutokana na mauzo ya nyumba hizi. Katika nyumba 5,248 zilizouzwa, nyumba 4,234 wameuziwa Wafanyakazi wa Serikali na nyumba 1,188 zimeuzwa kwa Wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari (*THA*). Aidha, nyumba zipatazo 2,580 za Shirika la Reli (*TRC*) zitauzwa kwa Watumishi wanaoishi katika nyumba hizo.

Wakala pia umejenga nyumba 173 Dar es Salaam, Dodoma na Arusha na umetiliana Mkataba na Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza kujenga nyumba

nyingine 300 za Watumishi wa Serikali katika Manispaa ya Dodoma ili kuharakisha uhamishaji wa Makao Makuu kwenda Dodoma.

Aidha, Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hivi karibuni umekamilisha kuandaa mwongozo wa utaratibu wa kuingia ubia wa wawekezaji binafsi kwa ajili ya kuendeleza *Prime Areas* zilizo chini ya Wakala. Mwongozo huo utanza kutumika mwaka 2004/05.

(viii) Tatizo la kuzidisha uzito katika barabara zetu linaendelea kupungua ambapo mpaka sasa magari yanayozidisha uzito ni chini ya asilimia 10 ukilinganisha na asilimia 30 kwa mwaka 1998. Mafanikio haya yote yanatokana na Wizara kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuendesha kampeni za kuwaelimisha wadau wetu kuhusu suala la Usalama Barabarani kupitia vipindi vya Radio na Televisheni pia makala katika magazeti.
- Kufunga mizani ya kisasa na kununua mizani 18 inayohamishika (*mobile*).
- Kufukuza wafanyakazi 140 katika vituo vya mizani baada ya kutuhumiwa kujihusisha na rushwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo yaliyoathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2003/2004 ni pamoja na:-

- Ufanisi duni wa baadhi ya makandarasi katika kutekeleza kazi za barabara;
- Upungufu wa mitambo ya kuwawezesha makandarasi wazalendo kumudu utekelezaji wa kazi za barabara;
- Baadhi ya wahisani kuchelewa kutoa fedha kufuatana na ratiba iliyowekwa hivyo kuchelewesha miradi kuanza ama malipo kwa makandarasi kwa muda uliokubaliwa katika mikataba;
- Upungufu wa fedha kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo na kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara pamoja na ujenzi wa nyumba za kuwauzia wafanyakazi wa Serikali; na
- Utaratibu mrefu wa kutoa zabuni (hasa kwa miradi ya Wahisani) umechelewesha kuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka wa 2004/2005 ni kufanyia matengenezo Barabara Kuu na Barabara za Mikoa zenye urefu wa kilomita 13,333 na madaraja 1,692. Fedha zilizopangwa kutumika ni shilingi 56,784,146,000 ambapo shilingi 45,788,352,000 ni za Mfuko wa Barabara na shilingi 10,995,794,000 ni fedha za kigeni.

Mchanganuo kamili wa Mpango wa Matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa kwa mwaka 2004/2005 ni kama unavyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 7 kilichoko ukurasa wa 108 hadi 122.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inakadiria kutumia jumla ya shilingi milioni 89,606.6 fedha za ndani na shilingi milioni 129,623.4 fedha za kigeni katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya upembuzi yakinifu, usanifu, ukarabati na ujenzi wa Barabara Kuu na za Mikoa. Kati ya fedha za ndani, shilingi milioni 5,087.6 ni fedha za Mfuko wa Barabara na shilingi milioni 84,519 ni fedha za Maendeleo kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha za ndani kwa mwaka 2004/2005 umezingatia mambo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Mpango Maalum wa ujenzi wa barabara za Somanga-Lindi-Mingoyo na Dodoma-Manyoni-Singida kwa kutumia fedha za ndani, jumla ya Sh. 49,950,000,000.00 fedha za hapa zimetengwa kwa mradi huu.

(ii) Kuelekeza mgawanyo wa rasilimali kwenye miradi ya Barabara Kuu na za Mikoa inayoendelea. Jumla ya shilingi zipatazo 29,334,000,000.00 fedha za hapa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 5,087,600,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa miradi hii.

(iii) Kutenga rasilimali za kutosha kwenye miradi mipya yenye fedha za kigeni na miradi mipya ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara mbalimbali zinazotarajiwa kujengwa. Jumla ya shilingi zipatazo milioni 5,235,000,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

(iv) Muhtasari wa Mpango wa Ujenzi/Ukarabati wa Barabara Kuu umeonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 5 kilichoko ukurasa wa 94 hadi 101 na ule wa Barabara za Mikoa katika Kiambatanisho Na. 6 kilichoko ukurasa wa 102 hadi 107.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani ni tatizo kubwa hapa nchini. Tathmini ya hasara zitokanazo na ajali za barabarani inaonyesha kuwa ajali huchangia hasara ya kati ya asilimia 1 na 2 katika pato la Taifa kwa mwaka. Wizara ya Ujenzi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kupunguza ajali na uharibifu wa barabara. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kuanzisha mfumo wa kisasa wa uwekaji wa takwimu za ajali kwenye Kompyuta ili kurahisisha upatikanaji na uchambuzi wa takwimu, kufahamu sehemu sugu za ajali na kuzifanyia utafiti na kuzirekebisha ili kuondoa vyanzo vya ajali. Mafunzo yametolewa kwa Askari wa usalama barabarani na Wahandisi kuhusu uwekaji na uchambuzi wa Takwimu za ajali kwa kutumia Kompyuta. Aidha, tafiti za vyanzo vya ajali zinaendelea kufanyika na kuchukua hatua za kuzuia ajali;

- Kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) iliyoko chini ya Wizara ya Elimu tumeandaa mitaala kwa ajili ya somo la elimu ya usalama barabarani katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Walimu nchini. Majaribio ya kufundisha somo hili

katika baadhi ya Shule za Msingi na Sekondari katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro yanendelea. Aidha, tathimini ya somo hili inafanyika ili liweze kufundishwa katika shule nyingine;

- Kufanya Utafiti na kupendekeza mifumo bora ya ukaguzi wa magari, shule za udreva na utoaji wa leseni za udreva;
- Kutoa elimu ya usalama barabarani kwa njia ya redio, televisheni, magazeti, vipeperushi na kadhalika kwa watumiaji wa barabara wa aina zote;
- Kudhibiti uzito wa magari makubwa katika barabara zetu kwa kutumia mizani pamoja na kuwaelemisha wasafirishaji kuhusu ufungaji wa mizigo na athari za uzidishaji uzito. Aidha, mzani mmoja unaohamishika umenunuliwa, Ujenzi wa Mizani ya Mwendakulima (Shinyanga) na Mikumi (Morogoro) umekamilika na Mzani wa Mikese (Morogoro) uko katika hatua za mwisho kukamilika;
- Kuandaa mfumo wa usalama barabarani utakaozingatiwa katika kila hatua ya ujenzi wa barabara, yaani *Road Safety Audit System*;
- Kuandaa rasimu za kanuni za barabara, miongozo ya uendeshaji magari na ya kufundishia wakaguzi wa magari;
- Ili kuondoa tatizo la rushwa, Wizara kupitia Wakala wa Barabara imekuwa ikiwashirikisha wadau wote kuanzia wanaoagiza, wanaosafirisha mizigo, Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) ili kuhakikisha kwamba mizigo inayoagizwa na kusafirishwa katika barabara zetu inakuwa katika viwango vinavyoruhusiwa na hivyo kupunguza mianya ya rushwa. na
- Kukamilisha Mpango Kabambe kuhusu masuala ya usalama barabarani (*Road Safety Master Plan*) mnamo Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- Kuendelea kuwaelemisha Wananchi juu ya utumiaji salama wa barabara zetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari;
- Kujenga mzani wa kisasa katika eneo la Mpemba (Tunduma) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mizani mingine maeneo ya Nangurukuru na Mingoyo mkoani Lindi na mwigine mkoani Dodoma. Mizani hii itajengwa sambamba na ujenzi wa barabara unaoendelea kati ya Nangurukuru - Mingoyo na Dodoma - Manyoni;
- Kuendelea kudhibiti uzito wa magari katika barabara zetu;
- Kuendelea kuendesha mafunzo ya uwekaji wa takwimu za ajali kwenye kompyuta na uchambuzi wake; na

- Kuendelea na tathimini ya mpango wa kufundisha somo la elimu ya usalama barabarani katika Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025. Katika kutekeleza azma hii, Wizara yangu imeweza kuwaongezea wananchi kipato kwa kuwapatia ajira za matengenezo ya barabara kwa kutumia nguvu kazi ambapo sio tu wanapata kipato, bali pia huboresha barabara zetu kwa kuzikarabati na kuzitengeneza.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Wizara yangu imeendelea kuratibu na kutoa miongozo ya matumizi ya teknolojia hii, kufuatilia utendaji na kutathmini ubora wa kazi katika miradi ya barabara. Aidha, Wizara imeendelea kukiwezesha Chuo chake cha *Appropriate Technology Training Institute (ATTI)* - Mbeya kutoa mafunzo ya teknolojia sahihi ya nguvu kazi kwa kazi za barabara kwa mafundi wasimamizi wa kazi za barabara wapatao 85 kutoka Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini.

Katika kutoa umuhimu wa matumizi ya teknolojia hii, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, imeandaa na kukamilisha Mwongozo wa Kitaifa wa kuratibu shughuli zote zinazohusiana na matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi. Utekelezaji wa Mpango huu utanza mwaka wa fedha wa 2004/2005. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), iliandaa na kuwa mwenyeji wa semina ya kimataifa ya wadau wa nguvu kazi (*Labour Based Practitioners*), ambayo iliwashirikisha washiriki 210 kutoka nchi mbalimbali 24 duniani. Semina hii ilifanyika Arusha mnamo mwezi Oktoba, 2003 na ilitoa changamoto kubwa katika kuboresha na kudumisha matumizi ya nguvu kazi katika kazi za barabara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara yangu itatekeleza Mpango wa Kitaifa wa matumizi ya nguvukazi katika matengenezo ya barabara ambao utaratibu shughuli zote za matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi katika kazi za barabara nchini kwa kuzingatia ushirikishwaji wa sekta binafsi. Vilevile, Wizara itakiendeleza na kukipatia nyenzo, miundo mbinu na vitendea kazi Chuo cha *ATTI* - Mbeya ili kiweze kujitegemea na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara itaimarisha maktaba (*Labour Based Documentation Centre*), ambapo nyaraka mbalimbali za shughuli za teknolojia ya nguvu kazi na rejea mbalimbali zinazohusiana nayo zinahifadhiwa. Wizara itashiriki na kuratibu shughuli za utafiti kwa lengo la kutathimini ubora wa kazi za barabara zinazojengwa na kutunzwa kwa kutumia teknolojia hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kipindi cha 2003/2004, imeendelea kuhamasisha na kuelimisha wanawake na jamii kwa ujumla ili wanawake waweze kushiriki kwa wingi zaidi katika kazi za barabara. Ushirikishwaji huu unatofautiana mkoa kwa mkoa kulingana na mila na desturi, jitihada za wataalam walioko kwenye mikoa za kuhamasisha na kushirikisha na uelewa wa jamii husika. Wizara yangu imeendelea kuchapisha na kusambaza kwa wadau makala mbalimbali kama vile vipeperushi na mabegi yenye ujumbe wa uhamasishaji wa kuelimisha jamii, wadau, vikundi vya wanawake na wanaume ili washiriki katika shughuli za sekta ya ujenzi.

Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa ushirikishwaji wa wanawake katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Kagera, Mtwara na Pwani na ukusanyaji wa takwimu katika maeneo ambayo yanatekeleza mpango huu. Vilevile, Wizara imeshirikiana na Shirika la Maendeleo la Norway (*NORAD*) kuhamasisha shule zenye michepuo ya sayansi ili ziweze kuhamasisha wanafunzi wa kike kwenye shule zao kuyapenda masomo ya sayansi. Walimu 50 kutoka shule mbalimbali wamepatiwa mafunzo, na wanawake wataalam 25 wamepatiwa mafunzo ya uongozi na mabadiliko katika uongozi na wengine 12 wamepatiwa mafunzo ya juu ya *computer*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara imepanga kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha na kuendeleza vikundi vya wanawake vinavyofanya kazi za barabara ili vifikie ngazi ya kujiandikisha daraja la VII la Ukandarasi wa nguvu kazi au zaidi, kuendelea kuhamasisha wanafunzi na walimu wa shule za sekondari zenye michepuo ya sayansi ili kuongeza idadi ya wataalam wanawake wa uhandisi na teknolojia nyingine zinazohusiana na ujenzi;
- Kuandaa makala mbalimbali zitakazotumika kuelimisha jamii, washika dau, vikundi mbalimbali katika sekta ya ujenzi kuhusu ushirikishwaji wanawake na faida zake;
- Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara kwenye mikoa na miradi mbalimbali ya barabara; na
- Kutoa mafunzo na semina za masuala ya ushirikishwaji wanawake, uongozi na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ugavi na Huduma ina majukumu ya kusimamia Ununuzi, Utunzaji Usambazaji wa vifaa na upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa ajili ya shughuli za Serikali (*Procurement and Supply Management*). Aidha, Idara ya Ugavi na Huduma inasimamia Taratibu za Ugomboaji na usafirishaji wa shehena za Serikali (*Clearing and Forwarding Agent*), pamoja na shughuli za uendeshaji wa Bohari Kuu ya Serikali.

Takwimu kutoka vyanzo mbali mbali zinaonyesha kwamba kati ya asilimia 60 hadi 70 ya matumizi ya Serikali hutumika katika ununuzi wa vifaa, kazi na huduma (*Goods, Works and Services*). Serikali pia hutumia fedha nyingi katika kugomboo shehena zake kutoka nje ya nchi zinazoletwa kupitia bandari, viwanja vya ndege na mipakani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Idara ilipanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuongeza utoaji na usambazaji wa vifaa na huduma kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Bohari za Mikoa kufikia Shilingi bilioni 18;



- Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Maafisa Ugavi katika shughuli za ununuzi na utunzaji wa vifaa vya Serikali kwa kuwapa mafunzo ya muda mrefu na mfupi;na
- Kuongeza usimamizi wa ukaguzi wa vifaa na huduma kwa mikoa yote kwa kutembelea na kukagua vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo haya ni kama ifuatavyo:-

- Hadi Mei, 2004 bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 13.568 zimeuzwa kwa wateja;
- Wafanyakazi 28 walipelekwa kusoma Shahada ya juu ya Biashara inayohusu masuala ya Manunuzi. Aidha, wafanyakazi 37 walipelekwa kusomea kozi mbalimbali hapa nchini;
- Ukaguzi umefanyika Bohari 10 za Mikoa ya Tanga, Arusha, Moshi, Kigoma, Singida, Kagera, Mara, Shinyanga, Dodoma na Morogoro; na
- Bohari za Mikoa ya Mara, Kigoma, Morogoro na Singida zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2004/2005 ni:-

- Kuongeza vitendea kazi kama magari na *computer* kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu;
- Kuhakikisha kwamba taratibu zinaendelea kufanyika ili kukamilisha uanzishaji wa Wakala wa Bohari Kuu ya Serikali ifikapo Juni, 2006;
- Kuandaa orodha ya viwango vya vifaa ambavyo vinatumika Serikalini kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali;
- Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Ugavi Serikalini kuhusu sheria, kanuni na taratibu kama zilivyoainishwa na Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 3 ya mwaka 2001.
- Kuhakikisha kwamba Watumishi wa Ugavi Serikalini wanaendelea kupewa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika taaluma yao ili wafanye kazi zao kwa upeo mkubwa na ufanisi;
- Kuimarisha shughuli za Kitengo cha Wakala wa Ugomboaji na Usafirishaji wa Shehena za Serikali kwa kukiongezea vitendea kazi ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa gharama nafuu; na
- Kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kununua magari ya kusambaza vifaa mikoani.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ufundi na Umeme kwa kutumia vitengo vyake mbalimbali imeweza kutekeleza majukumu yake ya kuratibu, kutathmini, kusajili, kufuta, kukodisha na kufanya matengenezo ya magari na mitambo ya Serikali, uendeshaji wa Vivuko na Mitambo ya kusaga mawe, ushauri, usimamizi wa miradi, usimikaji na matengenezo ya mitambo ya umeme, mabarafu, viyoyozi na vifaa vya Electroniki. Aidha, Idara imeendelea na zoezi la kusajili magari, mitambo na pikipiki za Serikali kwa namba za Serikali kama nilivyokwishaeleza hapo awali

Katika kuboresha huduma kwa Wananchi, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004 imenunua kivuko kimoja cha Bugolora-Ukerewe Mkoani Mwanza kwa Shilingi 1,000,000,000 kitakachofanya kazi kati ya Mwanza na Ukerewe na hivyo kupunguza kero kubwa iliyokuwa inawakabili wananchi wa maeneo hayo.

Pia, mkataba wa ununuzi wa Boti mbili za uokoaji umesainiwa na boti hizo zinategemewa kupatikana mwishoni mwa mwezi Agosti, 2004 na zitatumika katika kivuko cha Magogoni Dar es Salaam na Kigongo - Busisi Mkoani Mwanza. Pia zimenunuliwa *Life Jackets* 345 kwa ajili ya matumizi ya Mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam.

Magari matano yamenunuliwa kwa ajili ya kuimarisha karakana katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mtwara, Manyara na Ruvuma. Aidha, katika kuimarisha kitengo cha ukodishaji wa magari ya Serikali (*G.T.A.*) magari mawili aina ya *Mercedes Benz* yamenunuliwa.

Pia, Idara imeendelea kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme. Miradi 17 kati ya 58 imekamilika na iliyobaki 41 inaendelea. Jumla ya Shilingi 110,000,000 zimepatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, malengo yafuatayo yamepangwa:-

- Kununua kivuko kipya cha Kigongo - Busisi mkoani Mwanza;
- Kununua kivuko kilichokuwa kinamilikiwa na *TAMOFA* katika mto Ruvuma eneo la Kilambo - Mtwara;
- Kununua *Vending Machine* ya kukatia tiketi katika Kivuko cha Magogoni kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato;
- Kukarabati vivuko vya Mv. Kigamboni, Mv. Rufiji, Mv. Sengerema, Mv. Pangani, Mv. Kilombero na kile cha Kyanyabasa kilichopo Mkoani Kagera;
- Kubadilisha mfumo wa uendeshaji kutoka uvutaji wa kamba unaofanywa na watu na badala yake kutumia winchi katika kivuko cha mto Ruhuhu Mkoa wa Ruvuma; na
- Kununua Boti mbili za uokoaji, magari matatu (*4WD*) na Vifaa vya karakana (*Workshop Tools*).

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuifanya Idara ya Ufundi na Umeme kuwa Wakala utakaojulikana kama *Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (TEMESA)*, zinaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 60. Inatarajiwa kuwa, Wakala utanza kufanya kazi rasmi mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Bodi ya Mfuko wa Barabara imezidi kujiimarisha kwa kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na usimamizi wa fedha za Mfuko wa Barabara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Bodi ilitarajia kukusanya shilingi milioni 64,510 kwa ajili ya kazi za barabara. Hadi Mei, 2004, shilingi milioni 61,616 (96%) ya lengo, zilikuwa zimekusanywa. Kati ya kiasi hicho Bodi ilipokea na kugawa jumla ya shilingi milioni 57,675 kama ifuatavyo: *TANROADS* shilingi milioni 39,946, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa shilingi milioni 17,117, Wizara ya Ujenzi shilingi milioni 3,944 na shilingi milioni 618 kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko. Mwelekeo unaonyesha kwamba, ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni, 2004, Bodi ya Mfuko itafikisha lengo lake la kukusanya shilingi 64,510 milioni.

Aidha, Bodi imeshiriki katika semina mbalimbali zinazoendeshwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*) na TAMISEMI kwa Watendaji wa Halmashauri na Makandarasi ili kutumia nafasi hiyo katika kuwaelimisha washiriki umuhimu wa matumizi bora ya fedha za Mfuko. Bodi ya Mfuko itaendeleza juhudi hizi katika mwaka ujao wa fedha.

Vilevile, Bodi kwa kutumia ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, imeendelea kufanya ukaguzi wa kawaida pamoja na ukaguzi maalum wa kuhakiki mapato yake kutoka kwa wakala wa ukusanyaji.

Katika juhudi za kuongeza mapato ya Mfuko, Bodi imeandaa mapendekezo ya kuongeza vyanzo vya mapato ambayo yanafanyiwa kazi na Serikali. Bodi imeweza pia kutoa mafunzo ya usimamizi wa Mfuko kwa watumishi na wajumbe wa Bodi. Pia Bodi imechapisha Kijarida kinachotoa mwongozo juu ya matumizi ya fedha za Mfuko ambacho kimegawiwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali inategemea kukusanya jumla ya shilingi 71,443 milioni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Kati ya fedha hizi shilingi 50.01 milioni (70%) zitapelekwa Wizara ya Ujenzi na shilingi 21.433 milioni (30%) zitapelekwa TAMISEMI.

Aidha, Mfuko unatarajia kupata kiasi cha shilingi 8,000 milioni kutoka Jumuiya ya Ulaya ikiwa ni msaada kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Katika fedha hizi, Wizara ya Ujenzi itapata Shilingi bilioni 5.6 na TAMISEMI Shilingi bilioni 2.4.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Bodi ya Mfuko wa Barabara inategemea kuendelea kuboresha makubaliano ya utendaji (*Performance Agreements*) na

taasisi zinazotekeleza kazi za barabara na kutoa ushauri wa kuboresha utendaji kwa kuzingatia uzoefu wa nchi nyingine ili kuhakikisha kwamba ubora wa kazi unalingana na fedha zinazotolewa. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, itaendelea kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Mfuko kutoka vyanzo mbalimbali na kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizo kwa kuimarisha ukaguzi wa ubora wa kazi na Fedha.

Katika kufanikisha malengo na majukumu yake, Bodi itaandaa Mpango wa muda mrefu (*Strategic Plan*) uwe dira ya kuiongoza na katika kuongeza ufanisi wa utunzaji wa kumbukumbu za fedha na itaanza kutumia mfumo mpya wa kompyuta wa kudhibiti matumizi ya fedha (*Computerized Financial Management System*).

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara una miaka minne tangu ulipoanzishwa. Katika kipindi hicho, umeendelea kutekeleza vizuri majukumu yake ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa zenye jumla ya kilometa 35,000. Aidha, muundo wa *TANROADS* umepitishwa rasmi na Ofisi za Kanda sasa zimeondolewa Mikoani na zimehamishiwa Makao Makuu ya Wakala. Katika kipindi hiki cha miaka minne Wakala umefanikiwa kuweka mifumo ya kisasa ya menejimenti na mawasiliano Makao Makuu na Ofisi zote za mikoa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuimarika kwa Wakala na ukweli kwamba fedha za matengenezo zimekuwa zinapatikana kwa wakati na kwa kiasi kilichopangwa, Wakala umejitahidi kuongeza ufanisi na kuongeza uzuri wa hali ya barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia *TANROADS* itaendelea kutunza barabara zetu kwa kusisitiza pamoja na mambo mengine masuala yafuatayo:-

- Wenye magari wanatakiwa kuwa waangalifu ili wasizigonge alama za barabarani. Baadhi ya wananchi wamekuwa waking'oa alama na samani nyingine za barabara. Ukosefu wa alama na samani unachangia kuwepo kwa ajali. Wananchi wanaombwa kulinda na kutunza alama za barabarani;
- Mwendo wa kasi ni kichocheo kikubwa cha ajali. Madreva na wenye magari wanatahadharishwa kuhusu jambo hili. Pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na alama za tahadhari barabarani, ukaguzi wa mwendo wa magari na ubora wa magari vitafanyika mara kwa mara;
- Shughuli ya upimaji wa uzito wa magari itaendelea kuboreshwa ili kuhakikisha magari yanazingatia sheria na taratibu zilizowekwa;
- Wananchi wanaojenga au wanaofanyia shughuli zao kando ya barabara katika eneo la mita 22.5 kila upande wa Barabara Kuu na zile za Mikoa, wanatakiwa kuzingatia sheria ya barabara inayowataka kuheshimu eneo hilo na kuliacha wazi. Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa hifadhi ya barabara, jukumu lao la kutunza barabara na itaendelea kuwachukulia hatua kali ikiwa ni pamoja na kubomoa

au kuwaondoa wote walio katika eneo la hifadhi ya barabara pindi maeneo hayo yatakapohitajika kwa miradi ya barabara; na

- Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Mkoa na Wilaya wanaombwa kutoa ushirikiano kwa Wizara/Wakala kwa kutoa ushauri na kujadili kwa makini taarifa za matengenezo na matumizi ya fedha wakati wa vikao vya Bodi za Barabara.

Aidha, ni vyema ieleweke kwamba kazi nyingi za matengenezo zinafanywa na makandarasi wazalendo hivyo zinachangia kutoa ajira kwa wananchi walio wengi na hivyo kuboresha hali zao za maisha.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*) umeanzishwa chini ya Sheria Na 30 ya mwaka 1997 ya Wakala wa Serikali na kuzinduliwa rasmi mwezi Mei, 2002. Madhumuni ya kuanzishwa Wakala huu ni pamoja na kuweka utaratibu na kanuni zitakazowawezesha wafanyakazi wa Serikali kumudu kugharamia makazi bora wakiwa bado kazini na baada ya kustaafu.

Kwa kuzingatia hayo, majukumu ya Wakala ni kujenga majengo ya Serikali kwa viwango vinavyotakiwa na kuyatunza, kutoa ushauri wa kitaalam na kusimamia miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali, kuuza nyumba za serikali kwa kuwakopesha wafanyakazi wa ngazi zote ili waweze kuzimiliki kabla ya kustaafu na kuendelea kujenga nyumba mpya na kuwauzia wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wakala ulipanga kufanya kazi zifuatazo: Kuzifanyia matengenezo nyumba za Serikali 262 katika mikoa yote ya Tanzania Bara, kuuza pamoja na kujenga nyumba 500 za gharama nafuu na kufanya kazi za ushauri zitakazoingiza kiasi cha Shilingi 372,086,700.

Hadi Aprili, 2004, jumla ya nyumba 177 zimefanyiwa matengenezo katika mikoa mbalimbali. Aidha, Wakala umeanza ujenzi wa nyumba 300 kwa ajili ya viongozi wa Serikali katika Manispaa ya Dodoma na zabuni ya ujenzi wa nyumba 10 za gharama nafuu mjini Babati Mkoani Manyara zimeshatangazwa. Jumla ya nyumba 5,248 zimeuzwa kwa watumishi wa Umma hadi sasa na kiasi cha fedha kilichokusanya kutokana na mauzo ya nyumba kwa mwaka 2003/2004 hadi kufikia mwezi Mei, 2004 ni Shilingi 3,511,318,753.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Wakala umepanga kukusanya jumla ya shilingi 9,284,134,361 kutokana na mauzo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali, upangishaji wa nyumba za kibiashara, huduma za ushauri na ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi. Mapato haya yataelekezwa kwanza katika kukamilisha nyumba 300, ambazo ujenzi wake unaendelea pamoja na kujenga nyumba nyingine. Aidha, Wakala utaendelea na matengenezo ya kawaida ya nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*Contractors Registration Board*), ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 17 ya mwaka 1997 na kupewa

majukumu ya kusajili makandarasi wa aina zote, kuratibu shughuli na mwenendo wa makandarasi wote na kujenga uwezo wa makandarasi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Bodi imetayarisha Dira ya Miaka Mitano ya 2004 - 2008 kwa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi. Dira hii inalenga katika maeneo makuu sita ambayo ni kuboresha uwezo, ujuzi na maadili ya Makandarasi, kuhakikisha kwamba makandarasi wa kizalendo wanatumika ndani na nje ya nchi, kuongeza ubora wa kazi za ujenzi, kuhakikisha kwamba afya na usalama kazini unazingatiwa na kuongeza ufanisi wa shughuli za Bodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Bodi imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kusajili jumla ya makandarasi 968. Hii inafanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa hadi Mei, 2004 kuwa 3,094.

(ii) Bodi imefuta usajili wa makandarasi 135 mwezi Januari 2004 kwa kushindwa kutimiza masharti ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi Na. 17 ya 1997 ikiwa ni pamoja na utendaji mbaya wa kazi. Hii imefanya jumla ya makandarasi waliofutwa tangu mwaka 1999 kufikia 1,448.

(iii) Bodi imefanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi 946 katika kipindi cha 1999 - Mei, 2004. Kati ya hiyo, miradi 414 ilikuwa na mapungufu mbali mbali ya uvunjaji wa sheria ambapo wahusika walichukuliwa hatua za kisheria. Hadi Mei, 2004 jumla ya kesi 25 zipo Polisi na kati ya hizo kesi 15 ziko mahakamani.

(iv) Hadi Mei, 2004, Bodi imeshaendesha kozi 12 chini ya Mpango Endelevu wa Mafunzo ya Makandarasi (*Sustainable Structured Training Program*), ambapo Makandarasi 300 walihudhuria. Tangu Mpango huu uzinduliwe mwaka 2001, jumla ya kozi 29 zimeshaendeshwa na kuhudhuriwa na makandarasi 900.

(v) Mfuko wa kusaidia Makandarasi (*Contractors Assistance Fund*) umeboreshwa kwa kuongeza fedha na sasa Mfuko huo una zaidi ya Shilingi milioni 600. Aidha, wanachama wa mfuko huo maalum wa kusaidia makandarasi kupata dhamana za malipo ya awali (*Advance Payment Guarantee*) na dhamana za zabuni (*Bid Bond*), waliongezeka hadi kufikia 251. Hadi Mei, 2004 jumla ya wanachama 198 wa Mfuko huo walikuwa wamefaidika. Mfuko unalenga kuwasaidia makandarasi wadogowadogo wazalendo.

(vi) Bodi ilifanya marekebisho ya sheria yake ndogo ili kuboresha mazingira katika sekta hii, na kutoa uwezo zaidi wa kuendeleza makandarasi wazalendo. Mabadiliko haya yanahusu: -

- Kuongeza thamani ya viwango vya juu vya kazi katika kila daraja la Ukandarasi kwa kuzingatia thamani ya fedha za Tanzania katika soko la dunia;

- Kuweka sifa za chini (*Minimum Qualifications*) za nafasi ya Mkurugenzi Mmiliki wa Kampuni ya Ukandarasi ili kuhakikisha kwamba biashara ya ukandarasi inafanywa na wenye fani zinazotakiwa; na

- Ili kuongeza nafasi za kazi kwa makandarasi wazalendo, Bodi imesajili Makandarasi wageni katika daraja la kwanza peke yake ili kuhakikisha kwamba ni wageni wenye uwezo mkubwa tu ndio wanaoruhusiwa kufanya kazi Tanzania. Aidha, Bodi imeweka utaratibu wa Makandarasi kusajili miradi na kupata nembo maalum kwa kila mradi wanaotekeleza ili kuondoa udanganyifu wa watu kununua majina ya makandarasi waliosajiliwa na kufanya kazi kinyume cha sheria. Vilevile hatua hii inalenga katika kuiwezesha Bodi kudhibiti ukiukwaji wa viwango vya kazi kwa kila daraja na kukusanya takwimu zinazotakiwa katika Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa yanayowakabili makandarasi nchini ni pamoja na mitaji midogo na masharti magumu ya kupata mikopo ya kufanyia kazi kutoka mabenki na taasisi zingine za fedha, udhaifu wa uendeshaji na usimamizi wa miradi miongoni mwa makandarasi na ukosefu wa vifaa na mitambo ya ujenzi kwa makandarasi wenyewe, hii ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kuimiliki, bei kubwa za kukodisha mitambo na uchache wa sehemu za kuikodisha.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2004/2005 ni pamoja na kuendelea na zoezi la kusajili makandarasi wa ngazi zote, kuendelea kusimamia Mfuko wa Kusaidia Makandarasi nchini, kutoa mafunzo chini ya Mpango Endelevu wa Mafunzo ya Makandarasi (*Sustainable Structured Training Program*), kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi katika sehemu mbali mbali na kuendelea na zoezi la usimamizi wa Sheria ya usajili wa makandarasi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (*National Board for Materials Management - NBMM*) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1981 kwa Sheria ya Bunge Na. 9. Bodi ina majukumu ya kusimamia, kuratibu na kuendeleza fani ya Ununuzi na Ugavi. Bodi pia huendesha mitihani, hudhibiti mienendo ya wanataaluma na husajili wataalamu.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Bodi imetekeleza yafuatayo:-

- Imesajili wataalamu 112 hivyo kufanya idadi ya wataalamu waliosajiliwa kufikia 1,609;

- Imetahini Wanataaluma 1,967 kwenye ngazi mbalimbali.

- Bodi imeweza kutembelea na kukagua sehemu za kazi mkoani Dodoma na kubaini watendaji wasio na sifa. Wafanyakazi 11 tu kati ya waliokaguliwa 58 ndio waliokuwa wamesajiliwa na kutambulika kisheria;

- Mafunzo endelevu (*Continued Professional Development*) yameendelea kutolewa ambapo warsha na semina 24 ziliendeshwa kwa watendaji wa ngazi zote za Serikali Kuu,

Wilaya, Miji, Manispaa na kadhalika. Mafunzo haya, yalihusu pia sheria ya Manunuzi ya Umma;

- Utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vitendo (*Internship*) yameanzishwa kwa wanataaluma wanaotoka vyuoni ili wapate uzoefu katika kazi;
- Bodi ikishirikiana na *Crown Agents - UK* iliendesha semina ya uhamasishaji kwenye Sheria Na.3 ya Ununuzi. Lengo la semina lilikuwa ni kuboresha mbinu za ufundishaji, uandaaji machapisho ya masomo (*manuals*) na pia utoaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu;
- Mafunzo mengine yaliyotolewa ni pamoja na namna ya kupambana na janga la UKIMWI, kuondoa kero za rushwa na kudumisha maadili ya kazi;
- Katika kuboresha mfumo wa mafunzo, Bodi imebadili mitaala ili ikidhi mabadiliko yanayoletwa na ukuaji wa utaalamu ulimwenguni, teknolojia na sheria za ununuzi; na
- Bodi imetoa ushauri wa kitaalamu kwenye Serikali na Asasi zake, pia imeandaa miongozo ya kazi (*Operations Manuals*), mfumo wa kazi na utunzaji wa kumbukumbu kwenye shughuli za ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo ambayo Bodi inakumbana nayo katika utekelezaji ni pamoja na upungufu wa vitendea kazi, nyenzo muhimu za kufanyia kazi na usafiri, uhaba wa fedha za kutoa elimu kwa vitendo na waajiri wengi kushindwa kuajiri wanataaluma wanaotoka vyuoni moja kwa moja kwa kuwa hawana uzoefu kazini kutokana na ama kutojua sheria ama kuidharau na kufanya utekelezaji kuwa mgumu hasa kuhusu suala la kuajiri wataalamu wasio na sifa. Ili kukabiliana na tatizo hili, Bodi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na Sheria Na.9 na hali hii itaondoa tatizo la uvamizi kwenye fani na pia kuongeza ajira kwa wahitimu wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Bodi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 ni pamoja na:-

- Kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya 1981;
- Kuongeza idadi na kiwango cha wanaofaulu mitihani toka wastani wa asilimia 39.5 ya sasa hadi kufikia asilimia 50;
- Kuboresha uwezo wa maktaba na kupata wakufunzi wenye upeo mkubwa zaidi na kuboresha mafunzo kwa wakufunzi;
- Kufungua vituo vya kutahini katika mikoa ambayo huduma za Bodi hazijafika;
- Kuimarisha usimamizi wa sheria Na.9 ili waajiri wengi waweze kuitii sheria na kupata fursa ya kutumia wataalamu waliopo ipasavyo;



- Bodi itoa huduma zaidi kwa njia ya warsha, semina na ushauri wa kitaalumu kama mbinu mbadala ya kuongeza kipato;

- Bodi itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine zikiwemo Bodi za kitaaluma na vyuo mbalimbali ili kuweza kupata ufumbuzi wa matizo yanayoathiri ukuaji wa taaluma. Kwa kushirikiana na vyombo husika, itakamilisha muswada wa marekebisho ya Sheria Na.9 na kuuwakilisha Bungeni; na

- Katika kuleta ufanisi zaidi na kukuza uwezo wao kitaaluma, Bodi itaendelea kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili ya Wahandisi ilianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 15 ya mwaka 1997 na imepewa madaraka ya kusimamia mienendo na shughuli za kihandisi zinazofanywa na wahandisi pamoja na kampuni za ushauri wa kihandisi.

Jukumu kubwa la bodi hii ni kulinda masilahi ya taifa na watumiaji wa huduma za kihandisi kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa au na makampuni ya ushauri wa kihandisi yaliyosajiliwa kwa kuzingatia viwango na maadili ya kihandisi ili kuhakikisha usalama wa maisha, mali na mazingira. Katika kutekeleza jukumu hili, bodi inafanya yafuatayo:-

- Kusajili wahandisi pamoja na makampuni yanayotoa ushauri wa kihandisi;

- Kupitia na kutoa maamuzi juu ya maombi ya kusajiliwa;

- Kuwaendeleza wahandisi kitaaluma, ikiwa pamoja na kusimamia programu ya mafunzo kwa wahandisi wahitimu (*Internship*);

- Kuratibu mienendo na shughuli za kihandisi za wahandisi na makampuni ya ushauri wa kihandisi;

- Kujenga uwezo (*Capacity Building*) wa wahandisi na makampuni ya ushauri wa kihandisi; na

- Kuandaa machapisho mbalimbali yanayohusu shughuli za Bodi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2004, Bodi imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kusajili Wahandisi - 909 ikiwa ni asilimia 152 ya lengo la mwaka;

- Kusajili Kampuni za Ushauri tisa, ni asilimia 81.8 ya lengo la mwaka;

- Ziara za kanda nne zimefanyika ikiwa ni asilimia 57.1 ya lengo la mwaka;

- Kuendesha mihadhara nne ikiwa ni asilimia 66.7 ya lengo la mwaka;
- Kuendesha kozi fupifupi nne ikiwa ni asilimia 200 ya lengo la mwaka;
- Kuandaa na kuendesha mtihani wa kitaaluma mmoja, ikiwa ni asilimia 50 ya lengo la mwaka;
- Kuendesha na kusimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi 250 ikiwa ni asilimia 48 ya lengo la mwaka; na
- Kuratibu Siku ya Wahandisi, ikiwa ni asilimia 100 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, Bodi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Ufinyu wa Bajeti, kwa kuwa shughuli za Bodi zimepanuka hivyo ada kama chanzo pekee cha mapato haiwezi kukidhi shughuli zote. Tatizo hili limesababisha kuahirishwa au kufutwa utekelezaji wa baadhi ya mipango yake;
- Ukosefu wa ajira kwa wahandisi wahitimu. Wahandisi wahitimu wazalendo hukosa ajira kwa kutokuwa na uzoefu wa kufanya kazi na hivyo kusababisha waajiri kuajiri wahandisi wa kigeni. Hata hivyo, tatizo hili linatazamiwa kupungua baada ya kuanzishwa kwa utaratibu wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu; na
- Idadi ndogo ya kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani.

Ni azma ya Bodi kuendelea kuyatafutia ufumbuzi matatizo haya ili kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya mwaka wa fedha 2004/2005, ni kutekeleza kazi zifuatazo: Usajili wa Wahandisi 1,030, usajili wa Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 15, kufanya ukaguzi mikoani kwa kutembelea kanda tano zenye mikoa 16, kuandaa mihadhara ya kitaalamu, mafunzo ya vitendo kwa Wahandisi wahitimu na kozi fupi, kuratibu Siku ya Wahandisi, Mtihani wa Kitaaluma, kushughulikia uanzishwaji wa Kampuni za Ushauri wa Kihandisi mikoani ili kusogeza huduma hii karibu na watumiaji na kukamilisha maandalizi ya programu ya mafunzo ya kujiendeleza kwa wahandisi.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Bodi imeanzisha utaratibu wa kusherehekea *Annual Engineers' Day*. Siku hii maalum ina lengo la kuwatambua wahandisi na makampuni ya kihandisi yaliyotoa michango mikubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini na kuwahamasisha Wahandisi kuwa wabunifu na hivyo kuharakisha maendeleo ya taifa. Sherehe kama hizi zitakuwa zinafanyika kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilianzishwa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 1997. Majukumu makubwa ya Bodi hii ni pamoja na: -

- Kusajili, kusimamia, kuangalia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na kampuni za kitaalamu na za ushauri zinazohusiana na kuhusika na fani hizo. Lengo la Bodi ni kuhakikisha kuwa wataalam hawa, wanatoa huduma za kitaalamu zinazokidhi mahitaji ya wananchi na mazingira yao;

- Kulinda utaalamu (*Professionalism*); na

- Kuhamasisha umma na wataalam, kushirikiana na wadau wengine kama vile Bodi mbalimbali chini ya Wizara;

Katika mwaka wa fedha wa 2003 /2004, Bodi ilifanikisha kutekeleza yafuatayo:-

- Kusajili Wabunifu na Wakadiriaji Majenzi wa ndani 22 na wa nje 5. Aidha, Bodi ilisajili kampuni za ndani 9 na za nje 2 na kufikisha jumla ya wataalam wa ndani na nje waliosajiliwa tangu Bodi ianze kuwa 293 na kampuni za ndani na za nje kuwa 123;

- Kutembelea na kukagua sehemu za majenzi katika mikoa 12 ya Tanzania. Sehemu 182 za majenzi zilikaguliwa na kufikisha jumla ya sehemu za majenzi zilizokaguliwa tangu Bodi kuanza kufanya kazi hiyo kufikia 1,841;

- Kukamilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Na. 16 ya mwaka 1997;

- Kuandaa na kuendesha makongamano mawili ya taaluma hizi mbili katika kuwanoa wana taaluma chini ya Mpango wa Taaluma ya Elimu Endelevu (*Continued Professional Development*);

- Kutayarisha na kutahini wana taaluma wanaoomba kusajiliwa na Bodi;

- Katika kuhakikisha Sheria Na. 16 ya 1997 na Sheria Ndogondogo (*GN No.168/2000*) za Bodi zinafuatwa, Bodi iliweza kutoa adhabu, maonyo na kuwapeleka mahakamani wale walioonekana kukaidi sheria;

- Kukamilisha matayarisho ya Rasimu ya Sheria ya Taifa ya Majengo (*National Building Control Act*) kwa kuwashirikisha wadau. Mapendekezo yake yaliwasilishwa kwenye vyombo vya juu kwa hatua zaidi;

- Kuzindua Mpango wa Mihadhara ya Kitaaluma yenye lengo la kutambua michango ya wana taaluma wa Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi, kuhamasisha kizazi kipya kujiunga na fani hizi mbili na kubadilishana uzoefu;

- Kutayarisha na kuwasilisha kwenye vyombo husika taarifa ya utendaji ya mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria Na. 16 ya 1997;
- Kutayarisha *Standard Documents* kwa ajili ya kurahisisha usimamiaji wa Sheria Na. 16 ya mwaka 1997 na Sheria Ndogondogo Namba 168 ya 2000 kwenye sehemu za majenzi; na
- Kuhusu mitihani ya Bodi, maombi 76 ya wataalam yalipokelewa. Wataalam 57 waliotimiza masharti waliruhusiwa kufanya mitihani na kati ya hao 17 walifaulu na 11 walisajiliwa na Bodi. Aidha, wataalam 4 na kampuni 3 za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zilifutiwa usajili kwa kukiuka Sheria Na.16 ya 1997 na kufanya jumla ya wataalam waliofutiwa usajili tangu Bodi ianze kuwa 272 na makampuni 8.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya Bodi ilikabiliana na changamoto zifuatazo: Upungufu wa fedha uliathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa malengo yaliyowekwa na Bodi, kutojitokeza kwa wana taaluma wa sifa za kati kutahiniwa kwa ajili ya usajili kunashusha idadi ya watahiniwa na hivyo kuathiri mpango wa usajili na mapato ni kidogo, hayakidhi mahitaji ya Bodi.

Kwa hiyo, Bodi inakabiliwa na matatizo ya upatikanaji wa vitendea kazi, utekelezaji wa mipango mizuri, kutoa elimu kwa umma na kadhalika. Hii inatokana na kutokuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Bodi inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kusajili wataalam 50, kuimarisha taratibu za usajili, kuimarisha sera na mfumo wa Sheria wa Bodi, kuendelea na ukaguzi wa sehemu za majenzi katika mikoa yenye shughuli nyingi za ujenzi ikiwemo Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro na Tanga na Bodi inaandaa mafunzo maalum ya vitendo kwa ajili ya kuwasaidia wahitimu wa taaluma husika ili waweze kutimiza masharti ya kuweza kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. Vilevile, Bodi itaendelea kupiga vita rushwa kwa kuwaelimisha wataalam wake kuhusu kufuata Sheria na imetayarisha *Practice Note* itakayowataka watekelezaji miradi yenye maslahi kitaifa km. hospitali, shule, nyumba za wageni, hoteli, nyumba za kupangisha na maofisi kuwatumia wataalam waliosajiliwa na wasimike mabango yanayoonyesha hivyo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi limeanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 20 ya mwaka 1979. Majukumu makuu ya Baraza ni pamoja na kusimamia na kuratibu maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini na kushauri kuhusu Sera, Mipango na mikakati ya kukuza sekta, kutoa ushauri wa kiufundi (*Technical Audit*), kutoa mafunzo kwa washauri wazalendo, ukusanyaji wa takwimu za ujenzi na kufanya utafiti, kuchapisha na kusambaza habari kuhusu shughuli za sekta na utoaji wa miongozo ya kiufundi ikiwa ni pamoja na kanuni za zabuni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Baraza lilipanga kutekeleza yafuatayo: Kutoa msukumo katika utekelezaji wa Sera ya Ujenzi, kutoa mafunzo kwa makandarasi, wahandisi washauri, watendaji wakuu hasa wa Serikali za Mitaa kuhusu

masuala mbalimbali ya sekta ikiwemo Sheria ya Manunuzi ya Umma (*Public Procurement Act No. 3 of 2001*), usimamizi wa mikataba ya ujenzi, kuboresha upatikanaji wa takwimu za shughuli za ujenzi, kutoa huduma za ushauri kuhusu ukaguzi wa miradi, ujenzi wa barabara, ukadiriaji wa gharama za ujenzi, kutoa mafunzo ya utekelezaji wa miradi ya miundo mbinu kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partnerships - PPPs*) na usuluhishi wa migogoro na kufuatilia kukamilishwa kwa uundwaji wa Mfuko wa Fedha wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2004 kazi zifuatazo zilitekelezwa: Baraza lilikamilisha utayarishaji wa Mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Ujenzi na kuisambaza kwa wadau mbalimbali ili kutolewa maoni. Mfuko wa Fedha wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*) una mtaji wa Shilingi bilioni 5 na utatoa mitaji ya kufanyia kazi kwa wadau wa sekta ya ujenzi kwa masharti nafuu kuliko benki. Mitaji hii ni pamoja na dhamana, mikopo ya kufanyia kazi (*Working Capital*) na mikopo ya kununulia vifaa na mitambo ya ujenzi.

Kwa kushirikiana na *Tanzania Investment Centre* na wadau wengine, Baraza limekuwa likishughulikia upatikanaji wa mapendekezo ya kuboresha mazingira bora ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kiuchumi kwa njia ya (*Public Private Partnerships - PPPs*). Baraza pia limeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Na. 20 iliyounda Baraza ambayo yanashughulikiwa na Serikali ili iendane na Sera ya Taifa ya Ujenzi ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Baraza litatoa msukumo wa utekelezaji wa Sera ya Ujenzi. Kipaumbele kitatolewa kwa malengo na mikakati inayolenga kuondoa matatizo makuu ya sekta ya ujenzi ambayo ni uwezo mdogo, tija ndogo na ubora hafifu wa kazi. Aidha, Baraza litaendelea kusimamia Mfuko wa *CIDF*, kutoa huduma za ushauri wa kiufundi kwa Wadau mbalimbali kuhusiana na tathmini za zabuni, uteuzi wa Washauri, utayarishaji wa makabrasha ya Zabuni, madai, usuluhishi wa migogoro, usimamizi wa miradi na uchapishaji wa majarida.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ujenzi - Morogoro kilianzishwa kwa lengo la kufundisha Mafundi Sanifu, Mchundo na Wahandisi wa Wizara ya Ujenzi na Halmashauri za wilaya. Kwa sasa, Chuo kinatoa pia mafunzo kwa mafundi Sanifu na Stadi wa fani mbalimbali wanaoshiriki kazi za ujenzi kwenye sekta za umma na binafsi. Katika mwaka wa fedha 2003/04, Chuo kilipanga kufundisha mafundi Sanifu 150 katika fani za matengenezo ya barabara, majengo na ufundi, mafundi stadi 60 katika stadi mbalimbali, madreva wapya 120 na kuendeleza madreva wa umma 90, kukarabati majengo mawili na kununua samani na pia kununua gari moja (*mini - bus*). Hadi kufikia Mei, 2004 Chuo kimefanikiwa kufundisha mafundi Sanifu 124 wa fani mbalimbali, madreva wapya 142, kuendesha mafunzo ya mafundi stadi mbalimbali 60 na kuendesha mafunzo kwa madreva wa umma 26.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, chuo kimepanga kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu 75, madreva mahiri 30, wanafunzi wa udreva wa awali 80 na mafundi stadi mbalimbali 60.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji Teknolojia kilianzishwa mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuimarisha/kuboresha sekta ya usafirishaji kwa kutumia mbinu ya usambazaji wa teknolojia kwa wadau wa sekta nzima ya usafirishaji.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kituo kilipanga kuimarisha na kuboresha huduma ya maktaba ya Kituo, kutekeleza kwa majaribio mradi wa *TRAC* katika Shule za Sekondari za Azania, Jangwani na Mzizima Jijini Dar es Salaam, kuandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau makala na majarida kuhusu Kituo, kuanzisha tovuti ya Kituo na takwimu mbalimbali. Aidha, kituo kilipanga kuandaa kozi nne na warsha mbili kwa wadau, kuendelea kutangaza/kunadi kwa wadau huduma zinazotolewa na Kituo ili kuongeza matumizi ya huduma zinazotolewa, na kushiriki katika mikutano ya kimataifa ya utafiti na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya barabara na usafirishaji kwa ujumla.

Hadi Mei, 2004 Kituo kilisambaza kwa wadau 668 makala na taarifa zinazoelezea teknolojia mbalimbali katika sekta ya usafirishaji. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Baraza la Taifa la Ujenzi, Taasisi ya Barabara ya Marekani (*US FHWA*) na *Tanzania Global Development Learning Centre*, Kituo kimeendesha warsha ya *Public-Private Partnerships in Transport Sector, Reforms, Development and Management*. Kituo, kimeshiriki katika makongamano matatu ya Kimataifa na kongamano, mikutano na semina 12 nchini ili kujifunza, kubadilishana uzoefu na kubaini teknolojia zinazofaa kutumika hapa nchini. Wadau 141 walitumia huduma ya Maktaba ya Kituo na kwa kushirikiana na taasisi nyingine 20 za wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi hapa nchini, kimeendelea kuratibu uandaaji wa mradi unaolenga kujenga uwezo wa sekta nzima ya ujenzi hapa nchini. Ripoti yenye mapendekezo ya mradi huo imekamilika na inafanyiwa kazi. Ili kuboresha utendaji wa kazi za Kituo, shughuli za utendaji zimehamishiwa kwa Wakala wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Kituo kwa mwaka 2004/2005, ni kuandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau makala na majarida kuhusu kituo, kuandaa na kuendesha kozi na warsha kwa wadau, kuendelea kutangaza/kunadi kwa wadau huduma zinazotolewa na kituo ili kuongeza matumizi ya huduma zinazotolewa na kushiriki katika mikutano ya kimataifa ya utafiti na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya barabara na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, watumishi wapya 38 walijiriwa, 1,412 wa kada mbali mbali walipandishwa vyeo na 138 walithibitishwa kazini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2003/2004, watumishi 26 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 935 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea ujuzi na ufanisi katika kazi zao. Wizara yangu itaendelea na juhudi za kuwapatia mafunzo zaidi wafanyakazi wake katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara ya Ujenzi, iliendelea kutekeleza Mpango wa Uboreshaji Utumishi wa Umma Serikalini. Mradi wa kuanzishwa Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi (*Performance Management System*) katika Wizara hii ulianzishwa Januari, 2003. Wizara imeshiriki hatua kwa hatua katika kutayarisha na kuandika Mpango Mkakati (*Strategic Plan*), kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006 na Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Aidha, utaratibu mpya wa kupima Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma umeanza kwa kuwahusisha kwanza Watendaji Wakuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara kupitia Kamati ya UKIMWI imeendesha Warsha za kuhamasisha Wafanyakazi wa ngazi zote kupambana na UKIMWI. Aidha, Warsha kama hizo zimeendeshwa kwa Wafanyakazi wa baadhi ya Miradi ya Ujenzi wa Barabara kama vile miradi ya barabara za Makuyuni-Ngorongoro, Chalinze-Melela na kadhalika.

Halikadhalika, Kamati ya ukimwi ya Wizara kwa kushirikiana na Mtaalam Mshauri (*Consultant*), imeandaa Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) ya utekelezaji wa shughuli za kupambana na UKIMWI Wizarani kwa kipindi cha kuanzia 2004 - 2007.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili, Wizara ya Ujenzi imeunda Kamati ya Maadili kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kamati hii itahakikisha inashirikiana na taasisi nyingine za Serikali kama vile PCB na Tume ya Uchunguzi katika utekelezaji wa kazi zake. Aidha, itafuatilia kwa karibu uwajibikaji wa watumishi wa wizara katika kutoa huduma kwa wananchi na katika kutekeleza majukumu yao kwa ujumla. Aidha, Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kupiga vita rushwa katika Sekta ya Ujenzi ambayo Wizara yangu inaendelea kutekeleza ni pamoja na kuendelea kutekeleza kikamilifu Sheria Na. 3 ya mwaka 2001 (*Public Procurement Act No. 3*), ambayo inapunguza sana mianya ya rushwa katika utoaji zabuni za ujenzi, ushauri na ununuzi wa vifaa. Vile vile katika kupunguza rushwa kwenye vituo vya mizani, Wizara inapunguza mizani ya kizamani na kuweka mipya ambayo inatumia kompyuta na imeongeza mizani inayohamishika (*Portable Weighbridges*). Aidha, Wizara imefukuza watumishi 140 Waliotuhumiwa kujihusisha na rushwa katika vituo vya mizani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 3,109,483,490.00 kutokana na vianzio vyake mbalimbali. Idara zinazokusanya maduhuli ni Utawala, Ugavi na Huduma pamoja na Ufundi na Umeme. Idara za Ufundi na Umeme pamoja na Ugavi na Huduma ziko chini ya *Retention Scheme* hivyo huruhusiwa kutumia kiasi fulani cha makusanyo yao kugharamia matumizi ya kawaida na kiasi kingine kinachobakia hupelekwa HAZINA. Muhtasari wa Makusanyo ya Mapato kwa mwaka 2004/2005 ni kama ulivyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 8 kilichoko ukurasa wa 123.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara ya Ujenzi imetengewa jumla ya shilingi 62,099,569,100.00 fedha za hapa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi zinajumuisha Mfuko wa Barabara Sh. 50,010,100,000.00, Mishahara ya Wizara Sh. 2,552,525,400.00, Mishahara ya Taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara Sh. 4,634,749,400.00, Ruzuku kwa Taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara Sh. 533,262,900.00, *Retention* Sh. 2,329,623,840.00 na Matumizi Mengineyo kwa Wizara Sh. 1,760,212,060.00.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa na muhimu wa Wahisani katika kufanikisha malengo ya sekta hii. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru wahisani wote kutoka nchi mbalimbali, kwa moyo wao wa kusaidia nchi hii. Wahisani hao ni pamoja na Serikali za nchi za Denmark, Finland, Italia, Japan, Marekani, Norway, Saudi Arabia, Switzerland na Uingereza ambazo kwa kiasi kikubwa zimeisaidia sana sekta ya Ujenzi. Pia nayashukuru mashirika ya kimataifa ya *ADB*, *EU*, *IDA* na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait na *OPEC* kwa kuendelea kusaidia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuishukuru kwa mara nyingine Kamati ya Bunge ya Miundo Mbinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, kwa ushauri mzuri waliotupa katika kuandaa bajeti hii. Nawashukuru pia viongozi wa ngazi mbalimbali katika Wizara ya Ujenzi ambao ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, Katibu Mkuu, *Engineer* John Kijazi, Wenyeviti wa Bodi za *RFB*, *NCC*, *CRB*, *ERB*, *AQSRB* na *NBMM*. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Wakala zote zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kuonyesha utendaji mzuri wa kazi na uwajibikaji. Vile vile napenda kuwashukuru Wwananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Biharamulo Mashariki, kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yaliyonikabili. Kwa pamoja ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa Miundombinu, hususan barabara katika kukuza uchumi. Lengo la Wizara yangu ni kuhakikisha Barabara Kuu zote Tanzania Bara zenye urefu wa kilomita 10,300 ziwe zimekamiliwa kujengwa kwa kiwango cha lami ifikapo mwaka 2012. Hivyo, hatua mbalimbali tunazochukua ndani ya Wizara ni katika kufanikisha lengo hili. Tunatambua tatizo la upatikanaji wa fedha lakini siku zote tutaendelea kujitahidi ili fedha kidogo inayopatikana itumike katika ujenzi wa barabara. Siku zote penye nia pana njia. Naamini lengo letu litafanikiwa kutokana na kasi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaoendelea sasa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2004/2005, naomba Bunge lako Tukufu liidhinisha bajeti ya jumla ya Shilingi 287,237,763,100 ambapo kati ya hizo, Shilingi 146,618,569,100 ni za hapa na Shilingi 140,619,194,000 ni za nje. Fedha za hapa zinajumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 62,099,569,100 na fedha za Maendeleo Shilingi 84,519,000,000. Fedha za nje zinajumuisha Shilingi 129,623,400,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya



Barabara Kuu na za Mikoa na Shilingi 10,995,794,000 za matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na. 81(1) ya mwaka 2003, napenda nitumie fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa ya Kamati ya Miundombinu inayohusu Wizara ya Ujenzi juu ya Mipango na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati kuhusu Fungu 47 la Wizara ya Ujenzi, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Miundombinu, kutoa pole kwa familia ya Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, pamoja na wapiga kura wake wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kuondokewa na mpendwa wao. Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati yangu, alikuwa ni mtu mwenye busara, hekima, upendo, aliyeshirikiana na kila mtu na asiye penda makuu. Kifo chake cha ghafla kimeacha pengo kwa wote waliokuwa wakimfahamu vizuri. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Danhi Beatus Makanga, kwa ushindi alioupata katika Jimbo lake la Bariadi Mashariki na kuwakilisha wananchi kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, karibu sana. Aidha, napenda pia kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika hasa Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hilo. Tuna matumaini makubwa kuwa yeye pamoja na timu yake watatuwakilisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Yasebasi Ng'wandu, Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu na Mhe Arcado Denis Ntagazwa, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuchaguliwa kwao kuongoza Taasisi za Kimataifa na Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *SADC Parliamentary Forum.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge, waliopata misukosuko mbalimbali katika kipindi hiki cha Bunge. Wabunge hao ni Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Mheshimiwa Parmukh Hoogan Singh na Mheshimiwa Dr. Lawrence Mtazama Gama, kwa kufiwa na watoto wao. Aidha, tunawapa pole Mhe.

Anne K. Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi wakiwa safarini, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mhe. Charles Makongoro Nyerere, kwa kupata ajali wakiwa safarini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 103B (1) ya Toleo la 2003. Majina ya Wajumbe wa Kamati hii ni Wafuatao:-

Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Zamda S. Bozzen, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Buriani, Mheshimiwa Robert J. Buzuka, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, Mheshimiwa Ally A. Karavina, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa, Mheshimiwa Mohammed H. Missanga, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame na Mheshimiwa Maria D. Watondoha.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, pamoja na mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa mwaka 2003. Kamati iliridhishwa na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Ujenzi kuhusu Mpango na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2004/2005. Pamoja na hayo, Wizara ilitoa maelezo kuhusu kazi zilizopangwa kufanywa katika kipindi cha 2004/2005 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu John Kijazi, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza maelekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka uliopita kwa kadiri ilivyoweza. Aidha, napenda kuipongeza Wizara kwa juhudi zilizofanywa katika utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2003/2004, yaliyohusu Dira ya Wizara, wataalam, ushirikishwaji wa wanawake katika ujenzi wa barabara, kubuni vyanzo vya mapato na kuboresha utendaji wa Wizara. Kamati inaishauri Wizara iendelee kuufanyia kazi ushauri na maagizo ya Kamati ambayo bado hayajapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa na Waziri wa Ujenzi kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Wizara kwa mwaka 2003/2004, ilionyesha kuwa katika kipindi hicho Wizara ilipata mafanikio na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2003/2004 kama ifuatavyo: -

Kukamilika na kufunguliwa kwa Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji, kuweka mawe ya msingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mbwemkulu - Mingoyo, Dodoma - Manyoni - Singida na Ilula - Tinde/Isaka - Nzega, Daraja la Umoja limefikia hatua nzuri ya kuanza kwa ujenzi baada ya kukamilisha maandalizi muhimu na wawekezaji wameonyesha nia ya kuwekeza, usajili wa magari kwa namba za Serikali, marekebisha ya Sheria za Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya ujenzi, kuboreka kwa utendaji wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa kuuza nyumba za Serikali na kuendelea kujenga nyumba nyingine na kupungua kwa tatizo la kuzidisha uzito wa magari katika barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipata changamoto katika miradi yake na kuathiri utekelezaji wa kazi za barabara kutokana na sababu zifuatazo: Ufanisi duni kwa baadhi ya wakandarasi katika kutekeleza kazi za ujenzi wa barabara, kutokuwa na mitambo ya kutosha kwa wakandarasi wazalendo kuwawezesha kumudu kazi za kujenga barabara, kucheleweshwa kwa ahadi za wafadhili katika miradi waliyoahidi kuisadia fedha au wakandarasi kucheleweshwa malipo yao kwa muda uliokubalika katika Mkataba, ukosefu wa fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa kulingana na mahitaji kwa kazi za ujenzi wa barabara na pamoja na ujenzi wa nyumba za kuwauzia wafanyakazi wa Serikali na urasimu uliopo katika kutoa zabuni hasa kwa miradi ya wahisani huchelewesha kuanza kwa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 3,109,483,490/= kutokana na vianzio mbalimbali. Idara zinazokusanya maduhuli ni Utawala, Ugavi na Huduma, Ufundi na Umeme.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka huu wa 2004/2005, ni kufanyia matengenezo barabara kuu na barabara za Mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 13,456.3 na kujenga madaraja 1,692.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuwa na mpango mzuri kwa mwaka 2004/2005, Kamati inashauri Wizara iboreshe utaratibu wake wa kuwasilisha taarifa. Mawasilisho yawe wazi na kila Idara iainishe majukumu yake na kuonyesha ni kiasi gani cha fedha kinachoombwa katika makisio na matumizi ya Wizara kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, Dira ya Wizara izingatie uwezekano wa kuendeleza uchumi wa kijiografia kwa kutumia nafasi tuliyonayo. Miundombinu ya barabara izingatie uchumi wa kijiografia ili kuvutia wawekezaji pamoja na soko la usafirishaji. Ujenzi wa barabara uende sambamba na reli na bandari ili kufungua njia za uchumi, kwa mfano, barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga ifike hadi bandari za Kasanga na Karema katika Ziwa Tanganyika na kwingineko nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa kwa vile njia zote za usafirishaji ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, ni vyema basi Serikali ikawekeza na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha njia za Reli na Bandari. Kamati

inashauri kuwa, Sheria ya Mfuko wa Barabara irekebishwe ili iweze kuhudumia pia ujenzi na maendeleo ya reli na bandari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazoendelea katika ujenzi wa barabara nchini, Serikali itoe kipaumbele pia kwa barabara za kuunganisha Mikoa kama vile barabara za Dodoma - Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma; Nzega - Tabora - Sikonge - Rungwe, Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Uvinza - Kigoma - Manyovu na barabara ya Mtwara - *Mbambabay*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa Wizara ifuatilie kwa karibu maendeleo ya ujenzi wa barabara zote ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilishwa kwa wakati kulingana na Mikataba na makubaliano yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosheleza katika kuendeleza miradi yake, Kamati inashauri kwamba, utaratibu wa *Build, Operate and Transfer (BOT)*, uendelee kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kutunga sheria itakayosimamia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa tamko rasmi kuhusu bomoa bomoa ya nyumba na majengo yaliyo katika hifadhi za barabara kwamba, zoezi hilo litakuwa likifanyika mara unapowadia muda wa ujenzi wenyewe. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa ni vyema alama za maeneo yatakayobomolewa ziendelee kuwekwa ili wahusika wajiandae na vilevile Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu zoezi hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa zoezi la uwekaji wa *beacons* katika hifadhi za barabara liendelee kwa kuwashirikisha zaidi wananchi kupitia kwa Halmashauri za Wilaya, ambako wananchi wataelimishwa na kuhamasishwa kulinda hifadhi hizo. Kamati inapendekeza wanavijiji washirikishwe na kuhamasishwa kulinda barabara zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza ulinzi na kuweka mikakati madhubuti katika kuhakikisha kuwa Daraja la Mkapa lililojengwa kwa fedha nyingi linalindwa dhidi ya hujuma na wizi wa vifaa. Kamati inashauri kuwa daraja hilo liwekewe ulinzi wa saa 24 au kufungiwa vifaa vya usalama ili kuhakikisha kuwa lipo katika hali ya amani. Utaratibu huo uwekwe pia katika sehemu nyingine nyeti ili kulinda mali za Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuipongeza Wizara kwa juhudi zake katika kupambana na rushwa. Kuhusu matatizo yanayojitokeza katika vituo vya mizani, Kamati inaishauri Serikali kutafuta mbinu za kuimarisha ulinzi katika vituo hivyo. Aidha, Serikali iwekeze katika mitambo (mizani) ya kisasa ili kuondoa kero na msongamano wa magari katika vituo hivyo kama vile Kibaha. Mizani iliyopo sasa imepitwa na wakati na haikidhi haja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza Bodi za Usajili wa Wakandarasi (*CRB*), Usajili wa Wahandisi (*ERB*) na Usajili na Wabunifu Majengo (*AQSRB*), kwa kuwasaidia wataalamu wazalendo, kuwa na mikakati madhubuti ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitimu masomo yao kupata ajira ili kuwapatia uzoefu. Pamoja na utaratibu huo mzuri, Kamati inasisitiza wataalam hao (Wahandisi na Wabunifu Majengo), wapewe nafasi za *internship* ili wapate uzoefu. Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha na kutoa mafunzo kwa Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakandarasi Wazalendo.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Makandarasi wa nje ambao wapo daraja la kwanza ni 3% ya Makandarasi wote waliosajiliwa na kwa kuwa Makandarasi Watanzania ni 97% ambapo thamani ya kazi za ujenzi wanazopewa Makandarasi wa nje ni zaidi ya 80%, Kamati baada ya kuangalia uwiano huo inashauri kuwa, Sheria ya Manunuzi ya Serikali irekebishwe ili kutoa kipaumbele (upendeleo wa makusudi), kwa Makandarasi na Washauri Wazalendo wenye uwezo. Hii itasaidia kuondoa umaskini kwani fedha zitabaki hapa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa wito kwa Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na Miji, ziwajibike katika uharibifu wa barabara unaosababishwa na mifugo. *Stock Routes* zifanyiwe kazi ili kulinda barabara zetu. Suala la usafirishaji wa makundi ya mifugo utafutiwe ufumbuzi ili kuimarisha hifadhi na utunzaji wa barabara. Magari yenye uzito mkubwa yadhibitwe kupita katika barabara zenye uwezo mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ujenzi wa nyumba za Serikali uzingatie mipango Miji ili kuleta mandhari nzuri na kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wakazi wa nyumba hizo. Kamati inashauri, ujenzi huo uzingatie matumizi bora ya ardhi na usiwe wa sura ya Vijiji au kambi. Aidha, nyumba hizo ziwe za gharama nafuu ili wafanyakazi wengi wamudu bei ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti wizi wa vifaa vya ujenzi katika maeneo mbalimbali, kwa mfano, katika barabara ya Songwe - Tunduma, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi na kuwashirikisha katika kulinda mali hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati inashauri kuwa, katika kivuko cha Kigongo na vinginevyo mizigo ya mafuta isichanganywe na abiria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujadili kwa kina bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Kamati yangu imeridhika na malengo, mipango na bajeti ya mwaka 2004/2005 na hatimaye Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili na likubali kupitisha kiasi kilichoombwa cha Sh. 287,237,763,100/= ambazo kati ya hizo, Sh. 214,142,400,000/= zikiwa ni mpango wa maendeleo na Sh. 73,095,363,100/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru pia Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu

Mkuu wa Ujenzi, Ndugu *Engineer* John Kijazi, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Ujenzi. Ushirikiano wao pia umeiwezesha Kamati kutembelea miradi ya ujenzi wa barabara za Dar es Salaam - Bagamoyo, Mwanza - Shinyanga - Shelui, Lindi na Mtwara. Ziara hizo zimeisaidia Kamati katika kupitia Bajeti ya Wizara ya mwaka 2004/2005 na kufanya zoezi la kuandaa taarifa hii kuwa rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Henry Dafa Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kwa ushauri na busara zake zilizoweza kunisaidia kuiongoza Kamati yangu. Naomba pia niwashukuru kwa namna ya pekee wanakamati wenzangu, kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa umakini mkubwa na uadilifu hivyo kufanya kazi yangu kama Mwenyekiti kuwa rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Msemembo Mussa, Katibu wa Kamati ya Miundombinu, Ndugu Justina Shauri na Wafanyakazi wengine wa Ofisi yako, kwa kuihudumia Kamati vizuri katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Wananchi wa Jimbo la Chonga, napenda kuwapa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, kutokana na msiba mkubwa uliowakumba kutokana na kifo cha Mheshimiwa huyo wiki iliyopita. Vilevile ninawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdalla Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao hivi karibuni. Aidha, ninawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao. Wafiwa wote hao Mungu awape subira na azilaze roho za marehemu mahali pema. *Amina.*

Ninawapa pole pia wale wote waliofikwa na masahibu mbalimbali kama vile ajali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Bohari Kuu ya Serikali Jijini Dar es salaam yamechakaa na kuchoka kwa kiwango kikubwa. Taasisi hiyo ambayo iko mbioni kufanywa Wakala wa Serikali ni nyeti katika kufanikisha huduma za Serikali, lakini kwa sababu zisizoeleweka, imeendelea kuachwa ikiwa na majengo yasiyofanyiwa ukarabati miaka na miaka. Hali ya uduni wa majengo ya taasisi hii pia inajionyesha Mikoani ikiwa

ni pamoja na Dodoma. Serikali ni lazima ichukue hatua za makusudi kuimarisha taasisi hii ambayo inalo jukumu la kutunza na kusambaza mali zenye thamani kubwa sana za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado lipo tatizo kubwa la alama za barabarani, hasa zile zilizotengenezwa kwa chuma, pamoja na vyuma na mabomba katika kingo za madaraja kuhujumiwa kwa kuibiwa au kuharibiwa kwa makusudi. Tatizo hili limekuwa likiongeza ajali za barabarani na kukatisha maisha ya Watanzania kadhaa. Tatizo hili lipo katika barabara zote nchini, Mijini na Vijijini. Ni muhimu sasa Wizara ibuni aina ya vibao vya alama za barabarani zisizohujumiwa kwa wepesi na ibuni namna mbadala za kulinda kingo za madaraja kwa kukwepa matumizi ya vyuma na mabomba. Wananchi katika maeneo mbalimbali yalipo madaraja washawishiwe kushiriki katika kulinda madaraja na alama nyingine muhimu za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vibanda maalum vya kupumzikia abiria katika maeneo mengi pembezoni mwa barabara ambavyo vilijengwa kwa fedha nyingi na hasahasa Jijini Dar es salaam, hasa katika barabara itokayo Morogoro kuingia Dar es salaam, tangu maeneo ya Kibaha hadi Magomeni, vinaendelea kuhujumiwa kwa kugongwa na madreva wazembe kila kukicha. Inaelekea madreva wanaofanya hayo yote hawapati adhabu yoyote ya maana kutokana na labda unyonge wa sheria zilizopo au pengine kutoa rushwa kwa mamlaka zinazotakiwa kusimamia katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taa za barabarani Mijini zilizo chini ya Mamlaka ya Wizara ya Ujenzi zimekuwa zikikosa maangalizi ya kutosha kwa siku nyingi sasa. Hazifanyiwi matengenezo pale inapohitajika. Zikiungua au kugongwa na madreva wazembe, huachwa zikining'inia hivyo hivyo na nyingine zimegeuka kuwa makazi na mazalia ya ndege. Jambo hilo sio tu huwa linaharibu haiba ya Miji yetu, lakini tatizo zaidi ni kule kuwa kichocheo cha ajali za barabarani na fursa nzuri sana kwa majambazi na vibaka, kitu kinachopelekea maisha ya watu kupotea na watu kuporwa mali zao.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa matatizo hayo, Kambi ya Upinzani inahimiza kuwa hali hiyo irekebishwe ili kurejesha haiba ya Miji yetu na kunusuru maisha ya watu wetu na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali *(TBA)* ni chombo chenye jukumu la msingi la kuhakikiksha Watumishi wa Umma wanapata nyumba bora za kuishi.

Hata hivyo, Wakala huu umekuwa ukijihusisha na zoezi la kujenga nyumba na kuziua. Nyumba zinazojengwa na *TBA* bado hazionekani kuwasaidia watumishi wa umma wa ngazi ya chini kutokana na ukweli kwamba, zina bei ya kutisha ambayo inaonekana pengine kuvifanyia dhahaka na kejeli vipato vya watumishi hao na hata wa kawaida. Mfanyakazi anayelipwa mshahara wa shilingi 70,000/= kwa mwezi kabla ya makato anao uwezo gani wa kuweza kununua nyumba ya shilingi milioni 27?

Hata kama angelipewa muda mrefu kiasi gani katika kulipa deni hilo taratibu, muda wake wa utumishi ungeisha bila ya kumaliza deni lake. Kambi ya Upinzani inalipongeza jambo la Serikali la kujenga nyumba ili kuwauzia wafanyakazi, lakini tunashauri pia ijenge nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wafanyakazi wa kipato cha chini. Kwa suala la ujenzi wa nyumba, Kambi ya Upinzani kwa manufaa ya wafanyakazi na wananchi wote kwa ujumla, inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

- Kujengwa kwa nyumba za bei nafuu zaidi ili watu zaidi wafaidike na nyumba hizo;
- Nyumba hizo zijengwe katika miji yote mikubwa ya nchi hii lakini kama kweli tumenuia kuifanya kuwa Dodoma Makao Makuu ya nchi yetu, basi mkazo zaidi uwekwe katika kujenga nyumba hizo hapa Dodoma;
- Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa nyumba hizo katika Miji Mikuu ya Mikoa, zoezi liendelee katika Miji Midogo Midogo au Miji ya Wilaya; na
- Kwa kuwa nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi na kwa kuwa makundi hayo yote yanachangia katika Pato la Taifa ni vyema Wizara ya Ujenzi hatimaye ikapanua wigo wa wateja mbali na wafanyakazi ili na wakulima wafaidike na huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema kupima uzito wa magari yanayotumia barabara zetu kuu, kwa usalama, ustawi na hifadhi ya barabara hizo, ambazo hujengwa kutokana na jasho la wananchi pamoja na misaada kutoka kwa wafadhili na wahisani wetu. Katika kufanya jambo hili, Serikali haina budi kuwa makini sana kwani kwa hulka ya binadamu ni dhahiri kuwa, wenye magari wangependa kukwepa kabisa vipimo hivyo kwa kuhofu kutoa malipo.

Lakini pia wakati mwingine zoezi hilo huleta usumbufu mkubwa kwa abiria kutokana na mlundikano wa magari katika vituo hivyo hususan katika mizani ya Kibaha, muda ni mali na ni fedha pia hivyo ni lazima utumike vizuri. Kama tatizo ni mitambo au mashine zenyewe, tunaihimiza Serikali izirekebishe ziweze kufanya kazi haraka au kama ni mabishano kati ya madrevu na maofisa wa vituo hivyo pia tungependa kuona kuwa hali hiyo inaisha mara moja ili wananchi waondokane na adha hii. Tunaipongeza pia Serikali kwa kuwachukulia hatua kali waliogunduliwa kutokuwa waaminifu katika vituo hivi lakini bidii zaidi ya kuwabana watu hao inahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kila sababu ya kubuni vyanzo vingine zaidi vya Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) kuliko kutegemea ushuru wa mafuta peke yake kwani hautoshi kuleta makusanyo bora zaidi. Kwa kuisaidia Serikali ili iweze kutunisha zaidi mfuko huo, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri kama ufuatao: Wawekezaji mbalimbali kwenye maeneo ambayo barabara hizo zinapita, kwa wachimbaji wakubwa wa madini, wamiliki wa mahoteli ya kitalii nje ya miji, wenye viwanda kando ya miji pia na hata wale wenye shule za Kimataifa katika maeneo hayo, wahamasishwe kama sio kulazimishwa,



kuchangia Mfuko huo kwa ama ujenzi au matengenezo ya barabara katika maeneo ambayo shughuli zao zipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikia kupitia vyombo mbalimbali vya habari kuwa zipo dalili za kuanza kuharibiwa taratibu lakini kwa uhakika kwa daraja muhimu kwa maendeleo ya eneo la Kusini mwa Tanzania Bara, yaani Daraja la Mkapu. Pamoja na ahadi za kuwekwa ulinzi imara katika daraja hilo kwa saa 24, upo wasiwasi kwamba, mali hiyo muhimu kwa uchumi wa Taifa haina ulinzi madhubuti. Pamoja na kukanushwa kwa vitendo hivyo vya kuharibu daraja hilo, ni muhimu Serikali ililinde kwa uhakika daraja hilo ambalo liko *quite strategic*, siyo tu kwa uchumi wa nchi, bali hata kwa mshikamano wa Kitaifa. Badala ya Askari wetu kufukuzana na wavuja jasho kama vile Wamachinga na wapiga debe katika miji mbalimbali, washike zamu za kulinda mali muhimu kama daraja hilo. Lakini zaidi ni kwamba, tunaomba Serikali kupitia Wizara husika, itupe kauli ya uhakika ili tuondokane na kuwa kwetu njia panda kuhusiana na ukweli wa jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanahitajika katika kila kona ya Tanzania, ni jambo la busara rasimali za kimiundombinu ya kiuchumi zikasambazwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kiuchumi na kijiografia, badala ya vigezo vya kisiasa na kiubinadamu peke yake. Hizi ni zama za kutanguliza mbele ufanisi (*efficiency*) wa kiuzalishaji na siyo kung'ang'ania kugawana (*equity/distribution*) ambacho hakipo au ambacho hakiwezi kuhalalishwa kwa sababu za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kuu na hata zile za vijijini uzingatie sana uchumi wa kijiografia kwa kuyafungua na kuyasisimua maeneo mbalimbali ya kibiashara na kiuchumi. Vilevile msambao na mwingiliano wa barabara uongozwe na *economic logic* badala ya sababu za kisiasa na kihistoria. Maeneo yasizawadiwe barabara eti tu kwa sababu eneo hilo anatoka fulani au atazikwa fulani. Barabara ziendeele kuunganisha nchi yetu na nchi jirani maeneo mbalimbali na mitandao mingine ya miundombinu ya kiuchumi na kibiashara kama bandari, reli, viwanda muhimu, viwanja vya ndege, migodi mikubwa, mashamba makubwa, mbuga za wanyama, mabohari makubwa, vitovu vya kibiashara kama miji mikubwa, vyanzo vya nishati, vyanzo vya maji, maeneo yenye taasisi za utafiti na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila mwenye akili timamu anaamini kuwa ufanisi wa kiuchumi wa nchi yoyote makini hutegemea sana kiwango cha uwekezaji katika miundombinu ya kiuchumi, hasa kuhakikisha nchi inao mtandao bora wa barabara na madaraja imara. Kwa nchi kama Tanzania ambayo bado uchumi wake umejikita katika kilimo cha wakulima wadogo wadogo, maendeleo ya kiuchumi na kijamii yatategemea sana uwekezaji katika ujenzi na matengenezo ya barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, barabara hutumika kumfikishia mkulima zana bora za kilimo pamoja na pembejeo. Barabara humsaidia mkulima kupata soko la mazao yake ama kwa kufuatwa yeye na wateja mahali alipo au kuchukua yeye mwenyewe bidhaa zake na kuzipeleka mahali ambapo watu wanazihitaji. Kwa mantiki hiyo, tunashauri bajeti ya

Wizara hii na hasa sehemu ya ujenzi wa barabara, iongezwe kutoka Serikali Kuu na hata katika Serikali za Mitaa na kwa kutoa umuhimu zaidi katika suala la barabara basi ni vyema pia Serikali ikaanza kufikiria kuziweka barabara zote kabisa chini ya Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka 2003 kuwa, bado watu wengi wanaliangalia suala la jinsi ujenzi wa majumba makubwa ya ghorofa Jijini Dar es Salaam na kwingineko kwa mashaka makubwa na kuwaza mambo mengi kwa mfano:-

(a) Wana waza na kufikiri hivi Serikali haina haja ya kuhifadhi historia au uasili wa Jiji la Dar es Salaam kama kumbukumbu muhimu ya utamaduni wa Taifa letu kwa kuzihifadhi nyumba zilizojengwa enzi na enzi kama wanavyofanya wenzetu katika Mataifa mengine likiwemo kama Taifa la Uingereza.

(b) Nyumba nyingine zinajengwa karibu karibu sana hata kasoro ya mita moja baina ya nyumba moja na nyingine, je, kuna usalama katika hilo kwa masuala ya moto na hata kwa matetemeko ya ardhi?

(c) Bodi ya Usajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi inafanye kazi yake sawasawa kuhakikisha viwango vya ubora wa majengo hayo vinafikiwa. Kwa manufaa, usalama na ustawi wa uhakika wa miji yetu, Serikali iwapatie wananchi majibu juu ya mashaka hayo yanayowaghasi na kuwanyima raha. Pia tunaiomba bodi hiyo kuwa iwe makini zaidi na zaidi katika kusimamia ujenzi wa nyumba hususan za ghorofa popote zinapojengwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuipatia Wizara ya Ujenzi nafasi kubwa zaidi ya kushughulikia ujenzi na matengenezo ya barabara kuu na za vijijini, Kambi ya Upinzani inashauri Chuo cha Ujenzi Morogoro kiingizwe katika Mtandao na mfumo wa Vyuo vinavyomilikiwa na *VETA*. Kituo cha Tanzania cha Uhamishaji Teknolojia pia kinaweza kuingizwa ndani ya *College of Engineering and Technology* chini ya mwamvuli wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama taasisi mojawapo ya kiutafiti na kukuza teknolojia. Tangu kituo hiki kianzishwe mwaka 1997 kimekuwa na ukaribu mkubwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hatua hizo zitaifanya Wizara ibakie na *core activities* badala ya kutawanya sana raslimali zake kwa kukumbatia shughuli zinazoweza kufanywa kiufanisi zaidi na taasisi nyingine za Serikali na Wizara ikapata kile inachohitaji kwa kuwasiliana na taasisi hizo bila ya kumiliki moja kwa moja taasisi yoyote ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya barabara zote za Tanzania kupitika kwa tekisi tangu Mtwara labda hadi Kagera kufikia mwaka 2005, sina uhakika kama pia inazihusu barabara muhimu za vijijini, waliko Watanzania zaidi ya asilimia 80. Kama hoja ni kusambaza barabara zinazopitika vizuri kwa magari yote mwaka mzima basi zisiwaziwe barabara kati ya mji na mji tu, ila pia kati ya kijiji na kijiji, ndani kabisa ya Tanzania, mbali kabisa na zinakopita barabara kuu. Suala si kuwepo kwa mipango mizuri, bali ni kujengwa na kutengenezwa barabara na madaraja vijijini waliko Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamalizia kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuliendesha Bunge letu hili kwa uadilifu mkubwa na umahiri wa kutosha. Aidha, ninampongeza sana rafiki yangu, Waziri wa Ujenzi, kwa kuchapa kazi bila kuchoka pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, *Engineer* Kijazi, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine. Ninawatakia kheri katika kazi yao hii muhimu. Ninawaambia kuwa ili na mimi nijichotee uzoefu wa kutosha katika mambo hayo, ushirikiano wao wa karibu nami unahitajika zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Kwanza kabisa, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mpwapwa, napenda niwape pole wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kifo cha Mbunge wao.

Pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena na Wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki, tunamkaribisha ajiunge nasi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa hotuba yake nzuri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na wataalam wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na barabara ni muhimu katika uchumi wa nchi yetu na kazi ambayo tumewakabidhi kwa kweli wenzetu wanajitahidi Wizara hii kutekeleza majukumu yao pamoja na ufinyu wa bajeti lakini wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na mchango wangu kwa kuzungumzia barabara Kuu. Barabara kuu nikianza na hii barabara ya kutoka Dodoma-Singida -Shinyanga - Mwanza, napenda niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ya uamuzi wa busara kuhakikisha kwamba, barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami. Mimi nakumbuka tangu nimeingia Bungeni mwaka 1990, tunazungumzia barabara hii sasa Serikali kwa kweli imetoa uamuzi wa busara na mimi nina hakika barabara hii itakamilika kwa muda uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na ujenzi wa barabara hii, tunaikumbusha Serikali ujenzi wa barabara ya Minjingu-Babati- Dodoma-Iringa. Hii barabara ni muhimu sana Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii, tusitegemee Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba ndiyo watengeneze barabara hii, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii. Barabara hii ni fupi Iringa-Dodoma-Arusha, hivi sasa magari yanayotoka Mbeya na Songea ni lazima yapite Morogoro kuja Dodoma na kwenda Babati. Kwa hiyo, tunaikumbusha na kuishauri Serikali kwamba, ni vizuri isikie kilio cha Waheshimiwa Wabunge na wananchi na itekeleze ushauri wa

Waheshimiwa Wabunge, hii barabara ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma una mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 1,256, barabara kuu ni kilomita 557. Sasa kwa barabara kuu nimeshazizungumzia lakini kuna kipande cha barabara kutoka Dodoma kwenda Morogoro, hii barabara imeharibika sana. Kwa hiyo, tunataka tujue mikakati ya Serikali kufanyia matengenezo makubwa hii barabara.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2003/2004, Mkoa wa Dodoma ulitengewa fedha shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mkoa. Jambo la kusikitisha ni kwamba, kati ya fedha hizo shilingi milioni 258 zimekatwa kwa ajili ya kodi ya VAT. Sasa Waheshimiwa Wabunge, tulikwisha ishauri Serikali kwamba, fedha za miradi yote ya maendeleo, VAT iondolewe. Fedha zinatoka Hazina halafu zinarudishwa tena Hazina maana yake nini? Hizo fedha shilingi milioni 258 zingeweza kutengeneza barabara nyingi katika Mkoa wa Dodoma. Barabara ya kutoka Mbande, Mpwapwa hadi Pandambili, matengenezo makubwa kabisa. Barabara ya Malolo, Kinusi-Malolo ambayo inahitaji matengenezo makubwa, barabara ya kutoka Gulwe-Berege- Mima hadi Fufu hizo fedha zingetumika kufanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba, ni vizuri izingatie ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu sisi Waheshimiwa Wabunge ni kuishauri Serikali, haiwezekani fedha za miradi ya maendeleo zinatozwa VAT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali hapa Bungeni na bahati nzuri nilijibiwa kwamba, fedha za miradi za Halmashauri kodi ya VAT ilikuwa imefutwa. Sasa Serikali Kuu kwa nini isifute kodi ya VAT katika fedha za miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni ujenzi wa Daraja la Godegode. Niliwahi kuuliza swali na Serikali ilinipa matumaini. Daraja la Godegode ni barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Mangangu, Kimagai, Godegode, Lumuma hadi Mbuga na nashukuru sana Serikali barabara ya kutoka Lumuma hadi Mbuga imetengenezwa, nashukuru sana hilo. Lakini daraja hili ni muhimu sana kwa sababu ndiyo kiungo kikubwa kati ya Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe na barabara hii inakwenda kwenye eneo la umwagiliaji la Lumumu na nilishawahi kulieleza Bunge hili kwamba, mwaka 2002, watu wawili walikufa walikuwa wanavuka kwa sababu maji huwa yanajaa watu wanashindwa kuvuka lile daraja. Serikali ilinipa matumaini kwamba, watajenga lile daraja. Sasa mpaka leo sijui Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, utanisaidiaje hili. Sitaki majibu kwamba hii barabara iko chini ya Halmashauri Serikali ni moja. Hakuna jibu la kusema hii barabara iko chini ya Halmashauri. Halmashauri fedha ambazo tunatengewa ni kidogo sana, shilingi milioni 20, shilingi milioni 30 tutajenga daraja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kusema kwamba hiyo barabara iko chini ya Halmashauri, hilo sitaki kulisikia kabisa, atoe ahadi ya kujenga daraja la Godegode. Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ni Serikali moja tu. Ninachotaka ni barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa juhudi zake za kutengeneza barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Gulwe, hiyo barabara imechongwa vizuri na tunaomba tu barabara ya kutoka Gulwe kama nilivyosema, Mima mpaka Fufu basi tupate fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Lakini kuna barabara ya Malolo ambayo kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, mwezi Aprili, 2004, alifika kule kutembelea wananchi na aliona barabara ile ni mbaya sana na itagharimu fedha nyingi sana kwa sababu kuna mlima na mawe mengi, kwa hiyo, tunaiomba Serikali itupatie fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ila namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Wizara yake inafanya kazi nzuri, hatuna ugomvi naye, ndiyo maana tunaiunga mkono. Lakini naomba Daraja la Godegode, lile jibu la kusema barabara ile ni ya Halmashauri hapana, nataka atupe ahadi kama ikiwezekana tuongozane na Mheshimiwa Waziri, siku ya Jumamosi twende akalione daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumzia Wizara hii. Nadhani ni vizuri niungane na wenzangu ambao wametoa salamu za rambirambi kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya, kwa kumpoteza Mbunge wao, ndugu yetu, rafiki yetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye alikuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Naomba pia nimpe pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, ambaye amefiwa na mtoto wake hivi karibuni. Kwa bahati nzuri wengine wote nilikwishawapa pongezi na kuwapa pole wakati nachangia Muswada wa *SUMATRA*.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu, kuzungumzia suala la Wizara ya Ujenzi. Wizara hii kwa bahati nzuri sana amepewa *comrade* mmoja, Mheshimiwa John Magufuli. Nimesema mara nyingi sana mtu anayeitwa *comrade* si mtu wa kawaida sana. Mtu yeyote ambaye ana matatizo anaitwa ndugu lakini *comrade* ni *comrade*. Mheshimiwa John Magufuli, ni *comrade* ni mwenzetu kabisa katika mapambano na mimi nasema kwa dhati kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Mahenge, naomba Mheshimiwa *Comrade* John Magufuli, pokea pongezi za Wananchi wa Mahenge.

Namshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, anamsaidia vizuri sana Waziri wake, nampongeza kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya chini ya Mheshimiwa *Comrade* John Magufuli. Wako wenzetu wanaomsaidia Ndugu John Kijazi na wenzake wote nawapa pongezi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo yangu mimi nimefarijika sana katika hali isiyo ya kawaida, Mheshimiwa Waziri amegawa hotuba yake mapema kabisa jana, hongera sana. Ni mara ya kwanza katika historia ya Bunge letu kupata hotuba ya Mheshimiwa Waziri siku moja kabla ya kuisoma. Haijapata kutokea! Hotuba ambayo ameunganisha pamoja na utekelezaji wa mipango yake miaka kadhaa inayokuja. Nasema

pengine ni vizuri wengine wangufuata mfano huo, si lazima kusema lakini inatupa nafasi ya kufanya uchambuzi wa ndani kabisa juu ya nini Wizara inafanya na juu ya nini Mbunge achangie. Tunatazamia kuanzia leo kuendelea mbele wengine wafuate mfano huo. Mheshimiwa *Sir* George Kahama lete hotuba mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kwa mipango yake ya baadaye anasema itakapofika mwaka 2012 kilomita zaidi 10,300 zitakuwa zimetiwa lami katika nchi yetu. Moja ya kitu ambacho kitatufanya tukimbie katika nchi hii, ni suala la miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu Mahenge mchele unauzwa kopo la kimbo senti 20/= ni kwa sababu hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, tukipata mawasiliano mazuri nina hakika suala zima la wananchi kuwa karibu na maendeleo yao na uchumi wao utakuwa ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa lipo jambo moja ambalo nataka niliseme nalo ni kwamba, Mheshimiwa Waziri ametaja maeneo fulani fulani, ametaja kiasi gani cha fedha zimetengwa kwa barabara ya Dodoma - Morogoro, barabara ya Mbwemkulu - Mingoyo, barabara ya Dodoma - Manyoni, barabara ya Shelui - Nzega, barabara ya Msimba - Ruaha - Mafinga, barabara ya Kidatu - Ifakara mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Spika, naanza kupata nini maana ya Askari wa Mwavuli alivyosema Mheshimiwa Rais wetu mwaka 2000, tunataka Askari wa Miavuli wanaoteremka kwenye miti na wengine bado wananing'inia kule juu. Askari wa Mwavuli ni yule ambaye anakwenda hewani na baadaye anateremka, habaki kule juu. Sasa mfano mzuri ni Mheshimiwa John Magufuli, ameteremka na sasa yuko anazungumza na Mabalizi wa nyumba kumi kumi kule chini. Hao ndiyo tunawahitaji, inatupa moyo sana sana. Mimi nasema kwa dhati kabisa nikitoka Morogoro kwenda Dar es Salaam nikiona barabara za lami zinapishana magari matatu haijapata!

Kwa hiyo, nasema kwa dhati kabisa kwamba, tunahitaji Askari wa Miavuli wanaoteremka siyo wanaoning'inia kule juu, waende kwa watu. Watu wanazungumza mambo ya elimu na maji kule vijijini. Sasa Askari wa Miavuli wateremke.

Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Ujenzi, tatizo langu ni moja tu katika Wilaya ya Ulanga. Wilaya ya Ulanga ni Wilaya nzuri sana, ina ardhi nzuri, ina mito mingi sana, tunavuna kule mavuno wakati wote kwa sababu yapo mabonde mazuri na kadhalika. Lipo tatizo ambalo si la kawaida, nafikiri tatizo hilo nimkabidhi Askari wa Mwavuli, ambaye yuko chini anapita kwa balizi, Mheshimiwa John Magufuli.

Liko tatizo la barabara inayotoka Ifakara-Lupiro- Kichanganyi-Mbindo-Chikuti mpaka Mahenge kilomita 74 tu. Wakati wote wa miezi ya Machi, Aprili na Mei, Watanzania wa Wilaya ya Ulanga hasa Mashariki na kule Magharibi, tunatumia magari aina ya malori na magari hayo yanatumia siku tatu kufika Ifakara kilomita 74.

Wapo akinamama, wapo wazee, wapo wagonjwa wanaokuja katika hospitali kubwa ya Ifakara wanalala njiani siku tatu. Sasa anafanyaje kushughulikia barabara

nzuri ashindwe kilomita 74. Sasa tatizo la Wilaya ya Ulanga ni hilo kwamba, barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mahenge ni tatizo kubwa sana. Bahati nzuri sana nashukuru kwamba, angalau sasa iko kwenye bajeti kuwa barabara ya kutoka Kidatu, Kiberege mpaka Ifakara itengenezwa kwa kiwango cha lami safi sana, hongera kabisa kabisa lakini baada ya pale sasa ndiyo unakwenda huko Mahenge.

Sasa kwa kumbukumbu ya tatizo la wananchi wa Wilaya ya Ulanga, ambao wanalala njiani siku tatu kutoka Mahenge kuja Ifakara, nimefanya uamuzi mbele yako kumletea kanda Mheshimiwa Waziri, inayoonyesha ubaya wa barabara hiyo. Kanda hii hapa nitampatia baadaye.

*(Hapa kanda husika ilioneshwa)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Ubaya wa barabara hiyo wapo akinamama wanaotembea kwa miguu, wapo vijana wanaotembea kwa miguu na malori yanakwama siku tatu, nne, sasa nadhani akiona ataelewa kwamba, kumbe kilomita 74 zinaweza zikashughulikiwa mara moja.

**SPIKA:** Hapana, hapana, hiyo si Shughuli ya Bunge, utampa *comrade* wako huko nje.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa mwongozo mzuri ambao unaendelea kuimarisha uzoefu wangu katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nasema nashukuru sana kwamba angalau umenipa mwongozo kwamba nitamkabidhi baadaye. *Comrade* wangu nitamkabidhi baadaye.

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya shukrani za wananchi wa Wilaya ya Ulanga. Tumepata pantoni mpya kabisa. Kwa muda mrefu sana tulikuwa na matatizo ya pantoni Waziri Magufuli na Serikali ya Chama cha Mapinduzi wameisimamia tumepata leo tuna pantoni ya kisasa. Tulikuwa tunavuka kwa muda wa dakika 45 sasa kwa pantoni mpya tunavuka kwa dakika 3. Kazi nzuri sana. Nafurahi sana kwamba katika Bajeti zimetengwa tena fedha kwa ajili ya kuimarisha pantoni hiyo. Nina hakika Mkurugenzi wa Umeme na Ufundi ambaye yuko karibu sana na masuala ya pantoni hasa ya Kilombero na nina hakika atafanya kazi zake vizuri sana.

Pili, nimefurahi sana kuona kwamba wametenga fedha kwa ajili ya kuweka lami mlima wa Ndololo. Kuna lami inaitwa *waterseal*. Lami hiyo imetiwa kilomita mbili na nusu safari hii wameongeza zaidi. Mlima ule ni mlima mkorofi sana kwa yeyote aliyefika Mahenge kabla hajafika atajiuliza pale Mahenge ni mlima mbaya sana. Lakini nashukuru kwamba katika Bajeti hii imewekwa pesa kwamba utashughulikiwa. Hayo ndiyo mambo ambayo nadhani yanahakikisha ushindi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kwamba nimejaribu kufuatilia jambo moja. Nimefarijika kwa kazi nzuri za Waziri huyu nikafuatilia na nikafanya pia *case study*.

Nikatembelea Wizara hii ya Ujenzi. Nimetembelea Ofisi ya Mkurugenzi wa Barabara (*Trunk Road*), nimetembelea Ofisi ya Mkurugenzi wa Barabara Vijijini, nimetembelea Ofisi ya Mkurugenzi wa Ufundi na Umeme kuona hivi hawa wakoje.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuambia kwamba lugha ya Waziri. Lugha yake ya kusimamia kazi, lugha yake ya kufanya *follow ups* ya kila kitu, ndio lugha ya Wakurugenzi hao. Lugha yao ni hiyo hiyo. Wanakusikiliza na wanatoa jibu. Kuna uhakika msingi wake ni kwamba huyu *comrade* ametengeneza *system* nzuri. Sasa hawa watu wanapewa Wizara sasa sijui watakapopewa nchi. Inatia moyo sana. Timu hii ni nzuri sana. Waziri huyu anatutia moyo sana. Kila Mkurugenzi ukizungumza nayo anakwambia jibu anasema hili linawezekana ramani ni hii hapa, barabara ni hii hapa, tunakwenda pale tunafika hapa unamwangukia kwa kweli hivi huyu amebadilika lini wanasema asili yake ni John Magufuli.

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza ni kwamba hivi Serikali kweli haiwezi ikawaonea huruma wananchi wa Wilaya ya Ulanga ambao tuna matatizo makubwa sana ya Mto Kilombero. Tumepata pantoni nzuri sana hivi haiwezekani Serikali hii ikatamka tu kwamba tatizo la Wilaya ya Ulanga kwa Mto Kilombero Serikali ina mpango, iseme tu ina mpango wa kujenga daraja. Itamke tu. Nani anajenga, tutajuana miaka kumi ijayo. Itamkwe tu kwamba hili tatizo baada ya Rufiji kuweka Daraja Mheshimiwa Spika, unajua kwamba athari ya Mto Rufiji ni Mto Kilombero. Ukiziba Kilombero Rufiji unavuka kwa mguu tu. Kule sio tatizo. Sasa kule kwetu sisi sasa iseme tu kwamba Mheshimiwa *Comrade* ebu kawaambie wananchi kwamba tumefikiria. Itamke tu kwamba daraja ipo siku litajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo narudia tena kusema kwamba ndugu yangu Magufuli wananchi wa Wilaya Ulanga wamenipigia simu jana wanasema tunakuomba katika kuzungumza Wizara hii umwombe Mheshimiwa Waziri kwamba tunamwalika kutembelea Wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Lakini kabla sijaanza kuchangia naomba na mimi niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa Wabunge ambao wamefiwa nao ni Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mzazi.

Aidha, napenda pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Hoogan kwa kufiwa na binti yake. Pia nitoe pole kwa ndugu na jamaa na wapiga kura wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Yete Mwalyego. Pia napenda nitoe pole kwa Dr. Gama ambaye amefiwa na mtoto wake. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote hao peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa rambirambi hizo naomba pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kutoa pongezi kwa Wabunge wote ambao



walichaguliwa kwenda kuungana na wenzao katika Bunge la Afrika nao ni Mheshimiwa Getrude Mongella, Dr. William Shija, Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Remidius Kisassi na Mheshimiwa Athumani Janguo. Pia nitumie nafasi hii kumpa pongezi za pekee Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira na Dr. Balozi Pius Ng'wandu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Tume ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia. Nimpongeze pia Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuchaguliwa kutuwakilisha katika Baraza la Wabunge wa *SADC*. Nimalizie pongezi zangu kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye amechaguliwa na wananchi wa Bariadi Mashariki kuwa Mbunge wao kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza sana na hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi sasa naomba mimi nichukue nafasi ya kuchangia maeneo machache ya hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Mimi nianze kwa kumpongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameiandika. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya hadi sasa. Katika barabara zile kuu kwa kweli wamejitahidi sana kutengeneza barabara hizo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika nchini kote. Aidha, kupitia Wizara ya Ujenzi na kupitia *TANROADS* wanajitahidi sana kutengeneza barabara za Mikoani na Vijijini napenda niwashukuru kwa kazi nzuri ambayo imefanyika na mimi nawapongeza sana kwa kazi hiyo na naomba waendeleo na jitihada hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitoe pia pongezi za pekee kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dodoma. Pamoja na fedha kidogo ambazo anapatiwa lakini anafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kazi nzuri ambaye ameifanya. Baada ya kuzungumzia na kutoa pongezi hizo sasa naomba nizungumzie eneo dogo tu ama sehemu ndogo tu ya barabara. Pamoja na pongezi zote hizi lakini mimi napenda nikumbushie Wizara ya Ujenzi kwamba mmejitahidi kufuatilia na kuainisha barabara muhimu za nchi hii na kuziwekea ama kuzitengeneza kwa kiwango cha lami. Lakini nashangaa kuona barabara moja mnaisahau.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje ameikumbushia hiyo barabara kwa jina maarufu inaitwa: *The Great North Road*, barabara ya kutoka Cape Town mpaka Cairo. Barabara hii haijashughulikiwa kwa muda mrefu sana. Sioni sababu gani barabara hii inatekelezwa. Tulikuwa tukizungumza kwa muda mrefu sana kuhusu ubovu wa barabara hii lakini hakuna hatua yoyote ya muhimu iliyochukuliwa katika maandalizi ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Nitawakumbusha labda kabla sijawakumbusha ahadi ambazo zilizotolewa na Wizara hii naomba kwanza niwakumbushe umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kiungo muhimu cha mawasiliano ya barabara Afrika nzima hasa tukijua kwamba inatoka Cape Town hadi Cairo. Ni barabara ambayo tunaweza kusema ni barabara ya Umoja wa Afrika ama Muungano wa Afrika. Lakini barabara hii sisi katika nchi yetu tumeitelekeza hasa kutoka Iringa, Dodoma, Babati,

Minjingu. Wenzetu kwa kutambua kwamba hii barabara ni muhimu nchi zote kutoka Afrika ya Kusini mpaka Kaskazini wameweka kwa kiwango cha lami isipokuwa ni sisi tu. Sasa mimi nafikiri kwamba tusiwe wazembe kiasi hicho tujitahidi kuiwekea mikakati sehemu hii ya barabara iwekwe kwa kiwango cha lami.

Pili, barabara hii tunao ushirikiano wa Afrika Mashariki, tuna Makao Makuu Dodoma. Sehemu ya barabara kutoka Minjingu mpaka Dodoma ni kiungo muhimu cha Mji Mkuu Dodoma na Mji Mkuu wa Afrika Mashariki ambao ni Arusha. Wenzetu wa Kenya na Uganda wamejitahidi kuunganisha Makao Makuu ya nchi zao kwa kiwango cha lami. Sisi tu ndio hatujaona umuhimu huo.

Mimi nashangaa sana sijui kama kuna Kitengo cha Mipango katika Wizara hii. Kama hakipo kiundwe kwa sababu sioni sababu hana macho anaweza kuona mbali huko Mtwara na kwingine lakini hapa Dodoma anashindwa kuona. Naomba kitengo hicho kiundwe ili kiweze kuona na kuweza kuweka mikakati ya kuweza kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona umuhimu wa kuzungumzia barabara hiyo kwa kifupi, sasa naomba nichambue kuona hivi Serikali imekuwa na juhudi gani za kutengeneza barabara hii kwa muda mrefu. Mimi nitaanzia katika Bajeti ya mwaka 1993 na nitajaribu kufuatilia niweze kuainisha kwamba tumeahidi nini na tumefanya nini mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 1993/1994 aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wakati ule alisema hivi naomba kwa ruhusa yako ninukuu: “Kuhusu sehemu ya Minjingu/Babati/Dodoma/Iringa upembuzi yakinifu umekamilika”. Kwa maana hiyo kama hatua hiyo ingekuwa imefuatwa sasa hivi barabara hii ingekwishajengwa kwa kiwango cha lami. Lakini tumefanya nini kuanzia pale. Hakuna tulichofanya. Upembuzi yakinifu umefanyika lakini vitabu vimewekwa kapuni mpaka leo. Ningeweza kuendelea kunukuu hotuba za Mawaziri mbalimbali waliokuwa wametoa wakati huo lakini itanipotezea muda. Lakini kuna maneno mengi yametolewa, ahadi nyingi zimetolewa mwaka 1994/1995, 1995/1996, 1997/1998 na kadhalika.

Lakini ilipofika mwaka 1997/1998 katika hotuba ya Waziri alisema kwamba na naomba ninukuu: “Kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu ya barabara ya Minjingu/Dodoma/Iringa uliofanyika miaka ya nyuma kwa madhumuni ya kurahisisha utafutaji wa wahisani”. Akamalizia hapo. Akaweka kitabu chake hakurudi tena kufanya shughuli hiyo.

Kwa hiyo kuanzia mwaka 1998/1999 mpaka leo hakuna kilichozungumzwa. Nashangaa hivi tunafanya mipango namna hiyo. Tunafanya kazi mpaka inafikia hatua ya kuanza ujenzi halafu tunaweka kapuni halafu tunaanza upya tena. Sasa kwa miaka 6 barabara hii haikuzungumziwa kabisa nasikitika sana. Sijui kwa nini? Mnafahamu mnatufikisha mahali tunasema labda watu wanapendeleana labda niseme neno hili. Mnatufikisha mahali mnasema kwamba hapo kuna upendeleo wa aina fulani kwa kupeleka fedha kwenye barabara fulani fulani. Mnatufikisha nyinyi sio sisi tunaofikiri.

Mimi mnanifikisha nifikirie hivyo. Naomba msitufikishe mahali pabaya namna hiyo. Kabisa naomba sana barabara hii ni muhimu tuiwekee kipaumbele ili iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa utani ulioanza tena mwaka huu. Katika hotuba ya mwaka huu nisingependa kunukuu sehemu ya hotuba isipokuwa napenda ninukuu sehemu ya fedha zilizotengwa. Barabara ya Babati/Dodoma yenye kilomita 261 imetengewa shilingi milioni 10. Shilingi milioni 10 narudia. Hivi shilingi milioni 10 hata huwezi kujenga choo. Unaniambia barabara ya kilomita 261 unatenga shilingi milioni 10. Nasema mmetufikisha mahali pabaya sana. Barabara ya kutoka Dodoma/Iringa imetengewa shilingi milioni 900 wala sijui itafanya kazi gani. Nimeambiwa katika hotuba ya Waziri nimeona katika jedwali kwamba kuna bilioni moja na nusu lakini msema kweli ni kitabu hiki. Hamna humu. Sasa hizo bilioni moja na nusu zitapitishwa kwenye kikao kipi cha Bajeti? Utaleta *Mini-Budget*. Mimi naomba kwa kweli mambo mengine tusifanywe kama watu wengine hawana akili. Naomba Wizara izingatie umuhimu wa barabara na itenge fedha za kutosha kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, athari ya kutokutengeneza barabara hii ni nini. Tunadumaza sana maendeleo ya wananchi wanaoishi katika maeneo ambako barabara hii inapitia. Ukitoka Iringa/Ismani/Mtera/Dodoma yenyewe Kondo, Babati tunadumaa kimaendeleo kwa sababu hatuna mawasiliano mazuri ya barabara. Tunakwamisha tena usafiri kati ya Makao Makuu ya nchi na Makao Makuu ya Afrika Mashariki tunabidi kuzunguka Chalinze, gharama inakuwa kubwa. Aidha, tunakwamisha maendeleo ama mawasiliano ya Afrika nzima kwa sababu barabara hii ndiyo inayotegemewa iweze kukata Afrika kutoka Kusini mpaka Kaskazini. Halafu barabara nyingine zina *branch* kwenda maeneo mbalimbali Mashariki na Magharibi. Lakini sisi tumekuwa watu wa kukwamisha kwa sababu hatujatengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu naomba tuzingatie umuhimu wa barabara hii na tutenge fedha na mimi nasisitiza fedha za ndani. Maana yake hapa kila siku wahisani, wahisani, fedha za ndani zipo tengeni. Mbona hii ya Dodoma/Manyoni mmetenga fedha za ndani. Naomba zitengwe hizo fedha. Pili, nashauri Serikali ihamie Dodoma ili miundombinu ifuate Serikali badala ya kukaa kule Dar es Salaam. Kuendelea kukaa Dar es Salaam Serikali ndiyo inayosababisha miundombinu yote ielekee Dar es Salaam. Tunajua Dar es Salaam ni mji mkubwa lakini ili miundombinu iweze kufuata Serikali tuhamie Dodoma ili miundombinu iweze kufuata pamoja na barabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kweli naona aibu sana kuunga mkono, lakini naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka huu wa fedha tulionao. Nianze kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Bunda kutoa pole kwa familia pamoja na wananchi wa jimbo la Mbeya Vijijini kwa kufiwa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Ujenzi kwa asilimia mia moja. Nitoe shukrani zangu na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya ambayo Watanzania wote wanaafiki kwamba Wizara hii inafanya kazi nzuri sana. Nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kukubali kilio chetu wananchi wa Bunda na kututengea fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ya kutoka Ikizu/Nyamuswa kwenda Bunda yenye urefu wa kilomita 25 katika Bajeti hii ya mwaka wa fedha tulionao. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna mambo mawili ambayo napenda nichangie katika hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi. Moja ni kuhusu maombi ya wananchi wa Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Mara kuhusu ujenzi wa barabara kutoka Kiabakari/Butiama kupitia Nyamuswa kwenda kwenye *Ikoma Gate* wakati unaelekea hifadhi ya Serengeti. Maombi haya yamekuja kupitia sehemu mbalimbali tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge. Jibu la Serikali limeonyesha ni la matumaini kwamba Serikali ina mpango wa kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa kuanza kwa mwaka huu wa fedha tayari barabara kutoka Makutano ya Kiabakari kwenda Butiama mkandarasi yuko kwenye barabara anatengeneza kwa kiwango cha lami. Lakini bado sehemu kubwa ndiyo haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwamba majibu ambayo mmekuwa mkiyatoa na hasa kupitia Bunge ni ya kutupa matumaini kwamba Serikali ina nia ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Lakini siku zote jibu ni kwamba Serikali inaangalia uwezekano wa kupata fedha. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake maana wahenga walisema kila mchonga mwiko hukimbiza mkono wake. Sasa naomba na mimi katika mipango yenu ya Wizara mnapokuwa mnatafuta wafadhili mbalimbali ebu naomba hii barabara ipewe kipaumbele cha hali ya juu kuhakikisha kwamba na yenyewe inawekwa katika mipango ya Taifa ya kuhakikisha kwamba inaombewa fedha ili iweze kutengenezwa ifanane na ile ambayo inatokea Makuyuni kwa upande wa Mkoa wa Manyara kuja katika *gate* la Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mnatafuta fedha za kujenga barabara hii nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu Serikali ina mpango wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami basi ni vizuri zingefanyika juhudi za makusudi kwamba zitafutwe fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Kwa sababu kama tunavyoelewa ujenzi wa barabara ya lami unahusisha bomoa bomoa ya nyumba ambazo zinakuwa karibu na barabara. Ili kama wananchi watakaokuwa wanahusika na zoezi la ubomoaji upembuzi yakinifu ukifanyika mapema wale wanaohusika watapata fursa ya kutambua kwamba ni miongoni mwa wale watakaokumbwa mapema ili waweze kujiandaa kujenga makazi mapya wasisubiri hapo zoezi litakapokuwa linaanza wakati wa kujenga barabara ile ya lami.

Kwa hiyo, naomba wakati mkisubiri kutafuta fedha za kujenga barabara hii basi zitafutwe fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili wananchi wale ambao wako karibu na barabara waweze kujua mapema na kujiandaa kujenga makazi mapya ili isije kuwa usumbufu itakapofika wakati muafaka wa kujenga barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili napenda Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Ujenzi, naomba hilo unisikilize vizuri. Kwamba Halmashauri yetu ya Wilaya ya Bunda tuliomba toka mwaka juzi kwamba barabara inayotoka Baridi pale karibu na Bunda Mjini kupitia Vijiji vya Kunzugu, Bukole, Nyamatoke, Mihale, Hunyari, Kihumbu, Maliwanda pamoja na Mngeta. Barabara hii inatoka kwenye barabara kuu inayotoka Musoma kwenda Mwanza inakwenda kuungana na barabara ya mkoa inayotoka Musoma kwenda Serengeti. Tungeomba barabara hii iondolewe miongoni mwa zile barabara za Halmashauri na iwe chini ya *TANROAD*.

Mimi niliuliza swali hili kwamba nakumbuka ilikuwa mwaka 2001/2002 na jibu la Wizara ilionekana kwamba imeteuliwa timu ya wataalamu ambayo inazunguka nchi nzima ili kufanya uhakiki wa barabara zipi ambazo ziko chini ya Wilaya zinazotakiwa sasa ziingizwe kuwa chini ya mkoa na mapendekezo hayo yaliporudishwa Wizarani. Barabara hii hakuweza kuingizwa kuwa chini ya barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu nyingi tulizokuwa tumezitoa kwamba tunaomba barabara hii iingizwe iwe chini ya mkoa na isiwe chini ya Wilaya kuonekana kwamba haziridhishi ukiongeza katika zile ambazo tuliongeza kwamba barabara hii inapita kando ya hifadhi ya Mbuga ya wanyama Serengeti. Hivyo watalii wengi wanapohitaji kwenda katika Mbuga ya *Serengeti Gurumeti Tented Camp* ile hoteli pamoja na Kilawira wengi wanapenda kupitia barabara hii kama njia ya mkato. Ni moja sababu tulisema wakati ule lakini Tume ile ambayo niliteua Kiwizara haikuridhika na sababu zile. Sasa kuna sababu nyingine ya msingi ambayo tunadhani Wizara ina kila sababu ya kuweza kusikiliza kilio cha wananchi wa Bunda kupitia Halmashauri yao. Hivi sasa kuna mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya Serengeti. Mradi huu ni mkubwa ambao utahusisha ubebaji wa magari mazito, mitambo mizito kama nguzo, waya na *transformer* na kadhalika.

Kwa maana kwamba pamoja na ujenzi utakapokamilika itahitaji magari makubwa ya *TANESCO* yaweze kuwa yanapita barabara hii mara kwa mara kwa ajili ya *service line*. Hivyo pamoja na shughuli nyingine zilizopo katika barabara hii za kibinadamu pamoja na maendeleo ya wananchi katika barabara hii. Ninaomba sasa kwa mara nyingine tena Wizara hii kupitia kwa Mheshimiwa Magufuli, kinara wa Wizara hii. Ninaomba sasa barabara hii isiwe chini ya Halmashauri tena sasa iwe chini ya mkoa ambayo ni *TANROAD* ndiyo iweze kusimamia matengenezo ya barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu fedha tunazozipata kwa ajili ya *Road fund* ule Mfuko wa Barabara ni kidogo sana na barabara tulizonazo katika Wilaya ni nyingi. Kwa hiyo, kwa kufanya hivi kama barabara hii itakuwa chini ya *TANROAD* itatusaidia kiasi kidogo kile tunachokipata kiweze kuelekezwa katika barabara nyingine za Vijijini ili kuweza kutatua tatizo la barabara mbovu kule Vijijini. Nadhani kwa

kufanya hivi Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imefanya kazi kubwa na wananchi wataendelea kuwa na imani nayo zaidi kwa kuonekana kwamba inasikia kilio chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi naamini Mheshimiwa Magufuli pamoja na timu yake ni wachapa kazi na ninavyoona Waziri anavyonitazama pale anaonyesha kwamba kuna namna ya jibu la matumaini. Ebu nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unafanya majumuisho ebu tupe na hili angalau wananchi wa Bunda waweze kufurahi wajue kwamba barabara hii itakuwa chini ya mkoa na tujue kwamba utakuwa umetukwama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nianze kwa shukrani kwako Spika kwa kuniona safari hii kunichagua kwa mara ya kwanza niweze kuzungumza kwa mara ya kwanza. Nashukuru sana.

Pili, nitoe pole zangu kwa Wabunge wenzetu wote wale waliopata mikasa ya namna moja au nyingine. Nawapa pole sana na Mwenyezi Mungu atawajalia watapona haraka wale walioumia na wale wengine waliokwisha basi Mwenyezi Mungu atawatuliza haraka. Lakini nitoe rambirambi za pekee kwa familia ya mwanamiundombinu mwenzangu Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego aliyefariki majuzi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi na awape subira wale wote waliopotelewa na ndugu yao huyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nianze kwa kusema naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Magufuli kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi ziende kwanza kwa Waziri mwenyewe kwa kubadili sura nzima ya Wizara ya Ujenzi. Watanzania sasa wanaona ni Wizara ambayo inaaminika kwani huko nyuma ukizungumza ujenzi, tulikuwa na hisia za kirushwa rushwa. Lakini tunashukuru hilo Mheshimiwa Magufuli umelifuta. Ahsante sana, tunakushukuru sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, pili, nitoe pongezi zangu za kazi nzuri uliyoifanya, kwa kweli wewe ni *front-liner* hasa kwa kuisaidia nchi ku-*improve transport accessibility* ukilinganisha na wenzetu wa Afrika Mashariki. Sasa hivi na sisi tunaweza kwenda vizuri katika muungano wetu wa Kenya na Uganda kwa kuwa angalau tume-*improve transport accessibility* vizuri na tunaweza kwa kweli tuka-*compete* vizuri katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Magufuli, lakini pia nikupongeze kwamba umesaidia sasa kuiweka nchi hii kupambana vizuri na athari za utandawazi. Sitakuwa na mengi, lakini nina sehemu tatu tu za kutaka kuzungumza. Ya kwanza niseme tu kwamba, nakushukuru sana kwa kuzingatia falsafa nzima ya uchumi wa jioografia katika kujenga barabara

zinazokwenda mahali na ku-avoid kujenga barabara zinazokwenda *to nowhere*. Angalau barabara sasa zinakwenda *to somewhere*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini tunaposema uchumi wetu wa jiografia tunasema nini? Tunajikita katika uwezo wetu sasa wa kujenga miundombinu ili kuweza kuhudumia soko la Kimataifa la shehena za mizigo. Sisi Tanzania tunaposema jiografia tuna maana ya pale tulipowekwa na Mwenyezi Mungu. Tuna *advantage* ya kuwa *Maritime Nation* na tuna *advantage* ya soko lenyewe, ni la Maziwa Makuu. Shehena ambayo tuna-*compete* na wenzetu wengi. Lakini huwezi kuzipata faida hizo mpaka umeubeba huo mzigo ukaufikisha kwenye bandari zetu. Lazima kuwe na *node* ambayo unapeleka, siyo upitishie tu upeleke *nowhere*, lakini unapitisha unapeleka kwenye bandari, ndiyo hapo uta-*realize benefits* za uchumi wa jiografia. Kwa maana hii, ni lazima ujenge barabara zinazolenga kuunga kwenda Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, basi mimi nitaanza na tafsiri sahihi tu ya *corridor* katika kusaidiana na ndugu yangu hapa, Askari wangu wa mstari wa mbele kabisa ambaye yeye ameshuka kwenye mti sasa yuko mstari wa mbele anapambana kuiokoa nchi kutoka kwenye athari za utandawazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kutoa tafsiri nzuri ningependa nichukue hiki kitabu ambacho kinasema: “Nyongeza ya Hotuba ya Waziri wa Ujenzi.” Nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu kichukue kile, *page* yako ya kwanza tu ile yenye ramani. Sasa tunaposema *corridor* tuna maana *corridor* inakwenda kwenye soko maalum. Kuna *cluster* ya soko pale ndiyo inakwenda *corridor*. Sasa tuanze chini kabisa, *Mtwara Corridor* ile iliyoonyeshwa pale. Itakuwa hakuna maana nzuri kama *Mtwara Corridor* itakwenda *Mbamba Bay* peke yake.

Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, wakati mwingine hata bila kujua umeshaitengeneza *corridor* inavyotakiwa iwe kwa kweli. Mimi nieleze tafsiri yake vizuri hapa. *Mtwara Corridor* maana yake ni lazima itoke Mtwara na lazima ipite Songea kwa sababu itaungana na Makambako ambayo itaunga na Mbeya inaunga na Tunduma na barabara yako ya kwenda Sumbawanga mpaka kwenda Kasanga. Karibu zote hizo umeshazijenga, sasa hivi unamalizia kile kipande cha Sumbawanga na ndiyo maana tumekuomba pale isiishie Sumbawanga Mjini itakuwa haijakamilika, iende kwenye bandari ya Kasanga. Tunataka kugawana na Afrika Kusini hili soko la Congo la mzigo *on transit*. (Makofi)

Kwa hiyo, *Mtwara Corridor* maana yake ni Kasanga, Tunduma, Makambako, Songea na Mtwara. Ndiyo *logic* inakamilika, mantiki nzima ya *corridor*. Kuna soko zima unali-*serve* na unapeleka kwenye *node* ya bandari maalum. Una-*realize* ile *value* utakayopata kwenye *transit* ya *haulage* na *node* maana yake bandari una-*realize* pia pale, unakuwa umekamilisha uchumi wa jiografia. (Makofi)

Sasa twende kwenye Kanda ya Kati (*Central corridor*). Ile tuliyoonyesha green pale ni sehemu ya *Central Corridor*, lakini siyo *Central Corridor* yenyewe ni *branch* ya

*Central Corridor.* *Central Corridor* ni Dar es Salaam, Dodoma, Manyoni, Itigi, Tabora na Kigoma. *Branch* zake ndiyo hiyo moja ya kutoka Manyoni inakwenda Singida inapita inakwenda mpaka Isaka na kuendela. *Branch* nyingine inatoka Tabora inapanda Mwanza mpaka kufika kwenye lake na *branch* yake nyingine inatoka Kaliua inakwenda Mpanda na ndiyo maana tumeomba barabara iongezwe sasa kutoka Mpanda mpaka Karema, unakuwa umekamilisha *corridor* na mantiki yake kamili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *Northern Corridor* ni Tanga, Arusha na Musoma. Ndiyo unakamilisha logic yenyewe. Nimezungumza definition hii kwa sababu gani? Nimezungumza tafsiri hii kwa sababu moja. Hizi *corridor* zinashindana, ukisema *Central Corridor* maana yake umekwenda Isaka, ukaenda Rwanda. Ile *corridor* inakwenda Rwanda bado haiendi Congo. Siku Rwanda akichachamaa huendi Congo, hupati mzigo wa Congo.

Barabara ile inayopita Manyovu inakwenda Burundi, siku Burundi tukim-*quarantine* kama tulivyofanya miaka michache iliyopita, maana yake mzigo wa Congo hupati. *Advantage* ya *corridor* hakuna. Ukienda Kigoma maana yake uko mpakani na Congo, ni *country to country*. Una uhuru kamili wa ku-*deal* na yule mmoja tu kwa hiyo mpaka wako ni mmoja. Ukitoka Kalemii unakuja Kigoma unakwenda mpaka mwisho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimezisema hizo kwa sababu sasa hivi kule Serenje, Mpulungu wenzetu wanajenga. Ukienda Malawi *definition* ya *Mtwara Corridor* ni lazima tuwe nayo nzuri. Huwezi kuwa na *definition* ya *Mtwara Corridor* inaingiza na Nakala, siyo kweli. Nakala wana *corridor* yao, Malawi ndiyo *priority* yao wanafanya kazi kule. Ningependa hilo lieleweke sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini la msingi zaidi na ambalo ni *urgent* na linafanya ninazisema hizo *corridor* namna hii ni kwamba, hizi ambazo zinatupa sisi *advantage* ya moja kwa moja ni *priority* sasa hivi. Pamoja na kwamba tuna *comparative advantage*, katika utandawazi wenzetu wanatengeneza wanatumia mazingira hasa wale wenye uwezo, *factors* nyingi tu kwenye kitu wanaita *physical distribution elements*. Vitu kama *adequate supply* ya *capacity security, safety* na vitu kama hivyo vyote vinakuwa ni gharama mojawapo, *total cost* ya *distribution*.

Kwa ku-*minimize* ile ukielewa kwamba adui mkubwa wa utandawazi ni *distance* ndiyo maana kuna *spatial gaps* na *spatial* nini hizo. Utandawazi kila siku una-*tend* ku-*minimize* na ku-*equate distance* kuwa zero. Sasa wanapoanza ku-*minimize total cost* namna hiyo wana-*shift comparative advantage* yako kwa kutumia *competitive advantage*. Kwa hiyo, ukichelewa kama hauna *priority* ya haraka wao wanatumia gharama ili kuwa na *competitive advantage* wanakunyang'anya *comparative advantage* uliyonayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mipango amesema kwamba, sasa tutakuwa tunakwenda kwa *priority* na mimi nasema kupanga ni kuchagua, ndiyo ku-set *priority* zenyewe. Unapokuwa na *scarce resources* kama kwenye nchi yetu, ni lazima uwe na



*priorities*. Naomba *priorities* zianze hapa sasa hivi, si vizuri kuonyesha kale ka-dot dot kanakwenda kule Kigoma. Si vizuri kuziacha hizi *corridors* zikakaa zina-*hang* hewani wakati ni faida kwa nchi ni kubwa leo na kesho. *Commander* wangu wa mstari wa mbele, basi ukumbuke kikamilifu. Naamini wewe tukikukabidhi kazi hii mapambano ya utandawazi tutakuwa tunayakamilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu tunachotaka ni kwamba tu-*realize* ile *efficiency* yenyewe ya sisi kuweza kushinda utandawazi, ndicho tunachosema hapa. *Construction* ya barabara ni *tool* moja muhimu sana ya kuiwezesha nchi kupambana na athari za utandawazi, lakini kwa mpangilio maalum kama huu tulionao. Nasema sasa kama tunafanya *priority, priorities* ndiyo hizo sasa, tusiache barabara zetu hizi zina-*hang* hewani, tu-*link* mpaka mwisho.

*Central Corridor i-link* mpaka mwisho, Mtwara *Corridor* iende mpaka mwisho na ile pale *Northern Corridor* iende mpaka Musoma tuisitesite. Cha msingi kabisa, *Great North Road* iko hapa. Ile inasaidia *spill over effect* ni *corridor* muhimu sana ile. Zote hizi zikija kuna mahali ambapo zinaangukia kwenye hii. *Spill over* zote hizi ili uwe sasa una uhakika kabisa wa kwamba hata barabara mojawapo katika hizi *corridor* itakapopata matatizo iko *North South Corridor* itakusaidia wewe ku-*link* kwenye *corridor* yoyote kati ya Kaskazini na Kusini. (Makofi)

Ndugu yangu Magufuli niliona niyaseme haya kwa sababu naamini kwa wewe tumefika na tunapoyasema yanakamilika. Kwanza tumeshaona barabara ukizisema zinaonekana, zikijengwa zinakuwepo, hatujasikia maajabu ajabu kwamba barabara hii imekwama katikati pale kwa sababu inaonekana watu wamekula, hapana. Sasa atakayekuonea wivu kwa uzalendo wako na uchapakazi wako shauri yake, *at Stake* hapa ni Wananchi na vizazi vijavyo vya Tanzania, ndivyo tunavyoangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga hoja mkono. (Makofi)

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kutoa Salam zangu za rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutengeneza barabara za nchi hii na kuiweka nchi yetu katika ramani ya ulimwengu. Vile vile, naomba nimpongeze Naibu Waziri; Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi kubwa waliyofanya ya kutayarisha Bajeti na kuiwasilisha hapa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ujenzi ni mchapakazi maarufu sana na hivyo anastahili pongezi zetu kubwa. Siyo mchapakazi tu, lakini nadhani ana kipaji cha pekee cha kuweza kuzifahamu barabara zote za nchi hii. Hakuna asiyejua kwamba ukimuuliza barabara fulani atakutajia mpaka Kitongoji inapopita barabara hiyo. Nampongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika barabara zote zilizotengenezwa ningomba kutoa ushauri ufuatao: Kwa barabara za Dar es Salaam, *drainage* katika barabara hizo ni mbovu sana, kuna madimbwi wakati wa mvua na mifereji haizibuliwi. Kwa hiyo, ninatoa ushauri kwamba barabara zinapojengwa ziwekewe mifereji na izibuliwe mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitembelea Temeke kuna mifereji iliyojengwa na *TASAF* Wananchi wanaichafua. Tunaomba Wananchi wa Temeke wajitahidi kadri iwezekanavyo kusafisha mifereji yao. Huo ni ushauri ambao ninatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ningetoa ushauri kwa barabara ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami. Nyingi hazina mifereji, lakini vile vile uchafuzi wa mazingira umekuwa ni mkubwa. Nashauri magari yote ya abiria yawekewe sehemu ya kuweka takataka wakati Wananchi wanaposafiri ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na Wananchi wapewe elimu ya kuhakikisha kwamba wanaweka barabara zetu katika hali ya usafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri kwa kuwahusisha wanawake katika ujenzi wa barabara. Sehemu ambazo tumepita kwa mfano Mafia, wanawake wamepewa ukandarasi wa barabara na wanaifanya kazi yao vizuri sana. Naomba Wilaya nyingine ziige mfano wa Mafia na sehemu nyingine ambapo wanawake wamehusishwa. Naziomba na Wilaya nyingine ziwahusishe wanawake katika ujenzi wa barabara maana wana uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende katika Mkoa wangu wa Kigoma. Naomba nimpongeze Waziri kwa kuweka fedha za kujenga barabara ya Mwandiga - Manyovu ambayo tulikuwa tukiipigia kelele sana kwa sababu Wananchi ni wakulima sana wa kahawa, migomba pamoja na mananasi. Nadhani barabara hii itakuwa ni ukombozi kwa Wananchi wa Kigoma. Vile vile, barabara hii itakuwa na manufaa sana kwa biashara ya mpakani, lakini naomba tuelezwe fedha hizi zilizotengwa kwa ajili ya barabara hii zinatoka wapi. Tunaomba tuelezwe ni watu gani wanaifadhili hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma ni Mkoa ambao ni *very highly productive*, umesaidia na utasaidia sana kama barabara zake zitajengwa vizuri kuondoa tatizo la njaa. Nimeishaisemea sana barabara ya Kigoma - Kalya. Barabara hii kwa kuangalia imetengewa Shilingi milioni 30, naona kama ni mzaha!

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Kalya ambayo iko mwambao wa Ziwa Tanganyika haina njia nyingine ya usafiri wa kusafirisha mazao yao mpaka Kigoma. Ni barabara hii ya Kalya - Kigoma ambayo inategemewa na bado iko katika hali ya ujenzi. Barabara hii inapita Mto Malagalasi. Niliishawahi kuuliza swali kama Mto Malagalasi pale inapopita upande wa Ilagala watajenga kivuko chenye uhakika. Kivuko kilichopo sasa hivi ni kile cha zamani ambacho kwa vyovyote vile tukiendelea na nacho kitahatarisha maisha ya binadamu. Je, kivuko hiki kwa nini hakikutengewa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunategemea kwamba mazao ya kutoka Kalya, Mgambo, Sunuka na Sigunga kwamba yaweze kusafirishwa kwenda Tabora na sehemu nyingine za Tanzania. Je, yatapita wapi ikiwa hakuna kivuko hapo na wala hakuna daraja? Kama kivuko kikitengenezwa kitasaida sana. Barabara ya Tabora - Kigoma mpaka sasa sijaona kama imetengewa fedha, fedha zilizotengwa ni kufika Mto Malagalasi sehemu ya pili. Watu wa Kigoma sehemu ya Mto Malagalasi hawahitaji chakula, wanacho chakula cha kutosha, tunahitaji tusafirishe mazao yafike Tabora mpaka Dar es Salaam. Tumeishasema kuwa reli ni mbovu, kwa hiyo hatuwezi kusafirisha mazao kwa kutegemea reli peke yake. Tukisema tupite barabara ambayo inatayarishwa, ambayo iko katika matayarisho ya Sumbawanga ni mbali sana. Kutoka Kigoma kupita Sumbawanga twende mpaka Mbeya ndiyo tuweze kufikisha mazao Dar es Salaam ni mbali sana, kwa nini barabara ya Tabora - Kigoma isijengwe?

Tuliweka daraja, lakini hilo daraja liko juu juu tu halipitiki. Daraja lipo, lakini hakuna barabara. Tunaomba Waziri atueleze kwa nini hii barabara ya Tabora - Kigoma isitengenezwe kusudi Wananchi wa Kigoma wakaweza kusafirisha mazao yao mpaka Dar es Salaam kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya barabara, namshukuru Waziri kwanza kwa kuweka alama katika hifadhi ya barabara na kuonyesha ni sehemu zipi ambazo zitaathirika na utengenezaji wa barabara. Lakini tunaomba elimu izidi kutolewa kwa Wananchi kwa sababu hizi barabara nyingine zilijengwa wakati wa babu zetu. Mwananchi hajui ikiwa nyumba yake au shamba lake liko katika hifadhi ya barabara au kama babu yake alilipwa au hakulipwa.

Kwa hiyo, Wananchi waelimishwe wajue ni akina nani watakaopata fidia na akina nani hawatapata fidia. Wale ambao hawatapata fidia basi watafutiwe sehemu au wapewe mashamba waweze kujitayarisha mapema pindi nyumba zao au mashamba yao yatakapokumbwa na ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, katika ujenzi wa barabara hizi au katika matayarisho au katika tahadhari ya kuwatahadharisha Wananchi kwamba barabara itapita pale, wameweka alama ya X katika majumba, katika vibanda na katika mabango.

Mheshimiwa Spika, nadhani kungehitaji marekebisho kidogo. Hayo mabango ambayo yanatoa mafunzo kwa Wananchi kwa mfano elimu, UKIMWI unaua, yasingewekewa alama ya X kwa sababu kwa kuyawekea alama ya X ni kumweleza mwananchi kwamba UKIMWI hauui. Wananchi wanahitaji elimu, unawaambia hawahitaji elimu. Kwa hiyo, mabango ya namna hiyo hizo alama za X zifutwe. Wenye mabango hao watakuwa wanafahamu, kwa sababu hayo mabango yanahitajika kwa kuelimisha mpaka hapo yatakapokuwa yamehamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Waziri kwa Ujenzi wa nyumba Dodoma na Dar es Salaam, lakini nashangaa kwa nini sasa nyumba ambazo zimeishawekwa tayari kwa kuuziwa Wananchi zinachukua hela nyingi za Serikali kwa ajili ya matengenezo!

Sioni kwa nini hizi nyumba zitengenezwe na baada ya siku mbili wauziwe Wananchi, inakuwa ni kupoteza hela za Serikali. Kama ni kuwauzia Wananchi, basi na hela za matengenezo ziwekwe katika gharama za ununuzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuongezea, naomba nijumuishe kwamba Mkoa wa Kigoma haukutengewa fedha yoyote kwa matengenezo ya barabara muhimu, tunaomba Waziri aikumbuke hiyo. Wanawake katika Wilaya zote wapewe ukandarasi wa barabara. Pia, mabango hayo ambayo yanaelimisha alama za X ziondolewe mara moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Naomba kuanza kwa kuipongeza Wizara, Waziri mwenyewe wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wengine wote kwa namna walivyoandaa Mpango wao wa Bajeti wa Mwaka 2004/2005. Nilichokiona katika Bajeti hii, wameonyesha *financial performance* na *physical performance* ya kipindi cha mwaka 2003/2004 na kwa hiyo kwa utaratibu huo wameweza kupata *variance* ambayo iliwasaidia kujenga Hoja ya Bajeti ya Mwaka 2004/2005. Kwa ajili hiyo, nawapongeza sana sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kusikiliza kilio cha Wananchi wa Jimbo langu la Kilosa maana kwa muda wa miaka karibuni miwili sasa nimekuwa nachangia katika hotuba zake kumwomba afikirie kutupatia barabara kutoka Korogwe, Handeni, Mziha, Turiani, Mkindo, Hembeti, Mvomelo, Mandela, Magole, Dumila, Madudu, Kitete, Msowelo, Mvumi, Rudewa, Kimamba, Chanjulu, Kilosa, Magomeni hadi Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana kwa kuweka barabara hii katika mpango wa *design* kwa mwaka huu wa 2004/2005. Naomba sana wataalam wako watakapofika pale Msowelo wamwone Mwenyekiti wa Kijiji cha Msowelo awaonyeshe mahali pazuri pa kujenga daraja maana lile daraja la sasa hivi halifai kwa magari makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hii unajengeka katika hoja kubwa mbili. Kwanza inapita katika bonde ambalo kiuchumi linastawi mazao karibuni yote yanayolimwa Tanzania. Barabara hii inapita katika bonde ambalo linalimwa miwa, mpunga, mahindi, pamba na pia kuna ufugaji wa mifugo ya ng'ombe. Kwa hiyo, kiuchumi barabara hii itainua sana ukanda huu ambapo barabara hii inapita. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Aidha, kama wote tunavyofahamu, barabara ya kutoka Morogoro kwenda Mikumi inapita katikati ya Mbuga ya Wanyama ya Mikumi na mara nyingi tumekuwa tunasikia wanyama jinsi wanayouawa kwa kukongwa na magari.

Kwa ajili hii, kwa kukubali sasa barabara hii kupitia Kilosa, namshauri Waziri afikirie hiyo *design* ianzie Magole kuelekea Mikumi kwa sababu kwa kufanya hivyo kutakuwa ni wepesi zaidi kwa magari kutumia njia hiyo badala ya kupitia Morogoro kwenda Mikumi, kule waende watalii tu. Barabara hii ikimalizika mapema itazuia sana vifo vya wanyamapori katika mbuga yetu ya Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kukubali ombi langu la kuchangia na *pressure* yangu umeipunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ahsante sana, naunga mkono hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili nichangie hoja hii muhimu iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza kabisa na mimi niungane na Wabunge wenzangu ili nitoe salama zangu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, pamoja na familia ya Marehemu Yete Mwalyego, Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amen. Vile vile naomba nichukue nafasi hii nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, kwa kufiwa na mwanee mpendwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii ya Bajeti kwa umahiri mkubwa sana. Hongera sana. Kama wenzangu walivyosema, mwenye macho anaona, asiye na macho basi hataki kuona. Kwa hiyo, mimi nasema wazi kwamba Wizara hii ni mfano wa kuigwa. Mimi nianze na kuchangia barabara za ulinzi. Barabara za ulinzi katika mipaka yetu zimesahauliwa sana. Tunafahamu mipaka yetu ni mipana na naamini kabisa kwamba tutahitaji fedha nyingi, lakini mimi ninashauri Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Wananchi, kishirikishwe katika kuziweka barabara za ulinzi katika hali ya kupitika wakati wote. Hii siyo tu tutapunguza gharama na hasa ikizingatiwa kwamba kwa kawaida gharama zao zinaweza kuwa ndogo kuliko za wakandarasi. Hili ni jambo muhimu sana na nasema hilo kutokana na uzoefu hasa barabara zilizokuwa za ulinzi kuanzia Chiwindi Wilaya ya Mbinga mpaka Lituhi zimefutika kabisa hazipitiki. Kadhalika barabara inayotoka Songea kwenda Mitomoni na kuvuka mto pamoja na daraja lake kwenye eneo la Mitomoni Mto Ruvuma, nayo imekufa kabisa. Kwa hiyo, ni muhimu suala hili la barabara ya ulinzi likaangaliwa ili kila wakati tuwe katika hali ya tahadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nafahamu Waingereza walikuwa wameleta kivuko kwenye Mto Ruvuma sehemu za Mitomoni, sasa daraja hilo liliamishwa kwenda sehemu nyingine kwa hiyo, ningependa Wizara iangalie namna gani tunaweza tukapata daraja lingine ili wananchi wa Mbinga na Ruvuma, waweze kupata nafasi ya kufanya biashara halali na jirani zao wa Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, ningependa sasa niseme kidogo kuhusu suala la barabara naiita barabara ya uchumi kutoka Songea hadi Mbinga. Miaka ya 1990 Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya, iliamua kutengeneza barabara kutoka Songea kwenda mpaka kiwanda cha kukoboa kahawa Mbinga. Kazi hii

ilifanyika, ilianza kufanyika na madaraja yote yalijengwa kwa umadhubuti mkubwa kabisa na lami ikaanza kuwekwa kilometa 20 kutoka Songea mpaka Likuyufusi. Lakini baada ya hapo kazi hii haikuendelea tena. Sasa kwa wale wanaolima kahawa wanafahamu kahawa ina tabia ya kunyonya kila kitu kinachozunguka eneo hilo likiwemo pamoja na vumbi. Wilaya ya Mbinga, ambayo inazalisha zaidi ya asilimia 20 ya kahawa ya nchi hii aina ya Maudi *arabica* kahawa yake inapungua ubora wake kutokana na vumbi ambalo linafanya kahawa hii ipate bei ndogo kuliko kahawa ya aina hiyo hiyo inayolimwa maeneo mengine kama vile Kilimanjaro, Arusha na Mbozi.

Sasa ikizingatiwa kwamba uchumi wa Wilaya hiyo hasa unategemea zao muhimu kama hilo nashauri na naomba kabisa kwamba Wizara iangalie na ijaribu kubadilisha vipaumbele vyake ili eneo hili la kilometa 76 liwekewe lami hasa ikizingatiwa kwamba kazi ya madaraja imekamilika. Vile vile tuta liliwekwa lakini pamoja na kwamba mvua za *El-nino* zilibomoa mimi naamini kabisa kwamba gharama yake itakuwa ni chini zaidi kuliko kuanza kujenga barabara mpya. Nasema hivi hili ni muhimu kwa sababu tutaweza kuongeza pato la taifa mara mbili au zaidi. Ni muhimu kwamba tuone uamuzi kama huo ni sawa sawa na kuanza sasa kutekeleza kwa vitendo utengenezaji wa barabara ya Mtwara, *Mbamba Bay* kwa awamu. Kwa hiyo, hili ni ombi na ni matumaini yangu kwamba kwa kuwa Serikali hii na hasa Mheshimiwa Magufuli ni watu wasikivu sana wataliona hilo na kulipa umuhimu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa niligusie ni suala la ujenzi wa nyumba za watumishi linalofanyika Dodoma. Mimi napongeza sana Serikali, naungana na wenzangu kupongeza uamuzi wa Serikali, kwa kweli mwaka jana sikupendezwa sana tulipoambiwa nyumba zinajengwa Dar es Salaam wakati Serikali inatakiwa iwe imehamia Dodoma. Kwa hiyo, mimi nadhani hiyo ni hatua nzuri sana. (*Makofi*)

Lakini ili tuweze kuharakisha azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma, Wizara muhimu kama vile Hazina ndiyo ingehamia kwanza, ikihamia Hazina hakuna mtu atabaki Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni vizuri sasa Wizara yako ikaangalia na kuandaa mipango ya kujenga jengo litakaloshughulikia masuala ya fedha. Yote haya ni mipangilio, najua kuna watu hawataki kutoka Dar es Salaam, lakini kama Wizara ya Fedha, itahamia hapa, nakuambia tutahamia hapa kwa muda wa miaka miwili tu. Kwa hiyo, naomba hilo nalo Mheshimiwa Waziri aliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ninalotaka nichangie ni suala la kuwashirikisha wananchi katika ujenzi na utunzaji wa barabara. Mimi nadhani umefika sasa wakati wa Wizara kuoanisha mambo sawasawa, shughuli zipi zifanywe na nani? Naelewa sina matatizo na shughuli zinazofanywa na *TANROADS*. Lakini ninapofika kwenye Wilaya, unakuta mkandarasi anapewa kazi ya kutengeneza barabara ya vumbi wakati kusema ukweli wana vijiji wenyewe wangeweza kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi na hasa ikizingatiwa hizi barabara za vumbi zinatengenezwa wakati wa kiangazi, wakati wa masika zinaharibika. Mimi nadhani hapo kuna tatizo kubwa sana.

Mimi nadhani mipango iwe wazi itakayosema mkandarasi katika ngazi ya barabara za vijiji anatakiwa ajenge nini. Mimi ningeshauri washirikishwe zaidi katika kujenga madaraja ya kudumu au kalvati za kudumu ili angalau pawe na *impact* kwa sababu haingii akilini unajenga kalvati ya muda wakati wa kiangazi wakati unajua kabisa wakati wa masika itaondolewa. Kwa hiyo, mimi nadhani hili liwe waziwazi kwamba sasa kazi ya wakandarasi iwe ni kujenga madaraja ya kudumu, kalvati na inapobidi barabara kwenye kiwango cha changarawe au lami. (*Makofi*)

Sisi tuna uzoefu wa kutosha kule kwetu kabla ya masuala haya ya wakala wa barabara wanavijiji wenyewe walikuwa wanawajibika moja kwa moja katika kutengeneza barabara. Sasa hali hii sasa imepotea kwa hiyo, mimi ningeshauri Wizara itupe huo mwongozo ili na sisi Wabunge, tuweze kuwa katika hali ya kuhamasisha wananchi wetu. Naamini kabisa kwamba kama wananchi watashirikishwa na patakuwa na utaratibu unaoeleweka hata ile tabia ya kuzuia mifereji ya kutolea maji na wengine kulima mpaka kwenye maeneo ya akiba nadhani itatoweka.

Mheshimiwa Spika, mwisho baada ya kusema hayo napenda tena nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wako wote kwa jinsi mliyoweza kuonyesha ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili nami nitoe mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi. Awali ya yote nami naomba nitoe pole zangu kwa msiba mkubwa uliotokea wa ndugu yetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpa salaam za pole ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama kwa kufiwa na mwanae. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningependa kutoa shukrani na pongezi kubwa kwa Wizara hii ya Ujenzi. Kama mtakumbuka mwaka 2000 mimi nilijaribu kuwaeleza vizuri zaidi maana ya askari wa miavuli. Nikaeleza wasiwasi kwamba katika *process* hii tunavyoendelea wengine wanaweza kukwama kwenye miti, nyaya, kwenye paa za nyumba. Lakini kwa Wizara ya Ujenzi imeonyesha wazi kwamba huyu ni askari wa mwavuli thabiti ambaye ametelemka ardhini na anapigana vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Wale ambao hawakutimiza azma hii ya uaskari wa miavuli nafikiri Wabunge wenzangu mmeanza kuwaona katika salaam zao za Bajeti, kuna wengine bado wananing'inia. Lakini tunashukuru kwamba huyu amekwishatelemka na anafanya kazi barabara. Katika miaka hii mitatu mambo mengi ameyafanya yamedhihirika kiuwazi kabisa. Kwa hiyo, timu hii ya Waziri Magufuli, Mheshimiwa Mwenegoha na *engineer* Kijazi inaonyesha kiuwazi kwamba wanaelewa majukumu waliyopewa na wanayatekeleza barabara, endeleeni kutekeleza hivyo hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu ningependa kumshukuru Mheshimiwa John Magufuli, kwamba ametuletea vitabu mapema kidogo na tumewahi kuviangalia kwa undani zaidi na kuona mambo mbalimbali yaliyomo katika hotuba yake. Nimeangalia katika ukurasa wa 100 nimekuta katika barabara hii itakayotoka Masasi Songea mpaka *Mbamba Bay*. Nimeona wametenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya upembezi yakinifu, *design* pamoja na *tendering*. Sasa ukiangalia kiasi hiki kwa mwaka mzima utaona kwamba ni kiasi kidogo. Sasa huwa najiuliza ni kweli kwamba mwaka mzima tutakuwa tunafanya kazi ya *design* tu bila kuanza kazi ya ujenzi katika barabara hii kubwa? Mimi naona kwamba ikiwa tutatumia muda mrefu kufanya hizi *design* basi kukamilika kwa barabara hii ambayo wananchi wa Malawi, Msumbiji, Zambia wanaisubiri tutakuwa tumechelewa sana. Nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, kwamba hapa wangeweza kufanya utaratibu kama wanavyofanya sehemu nyingine, mbona wana design halafu baada ya ku-*design* wanaanza kujenga na baada ya kujenga tunaona kwamba kazi imefanyika. Lakini sasa hii ikiwa ni kuandika tu na kadhalika, kwa kweli mimi naona kwa kutumia mwaka huu mzima kwa kazi hiyo, haitakuwa kwa manufaa makubwa ya eneo hili. (*Makofi*)

Halafu hapo hapo nilitaka kuunganisha suala la *design* au kazi watakyofanya mwaka huu na *concept* nzima ya *Mtwara Corridor*. Mwenzangu pale Mheshimiwa Karavina amelezea vizuri sana na mimi nilitaka kuzungumzia kwa masikitiko kwamba inaonekana sisi uongozi wa Tanzania, hatukazanii sana suala hili la ujenzi wa *Mtwara Corridor*. Tunafanya mambo ambayo yanaelekea kuwa ni nusu nusu na ambapo wenzetu wa Malawi, Msumbiji na Zambia wanasubiri kwa muda mrefu.

Kwa mfano sisi ndiyo Wenyekiti, lakini tulitakiwa kuitisha Mkutano wa Mawaziri wa nchi hizi. Mkutano huu mpaka leo kwa nini haujaitishwa na Mwenyekiti wetu ni huyu askari wa miavuli Mheshimiwa Magufuli. Sasa itisha bwana mkutano. Uitishie ili waone wenzetu kwamba sisi kweli tuna nia ya kuendeleza hiyo *Mtwara Corridor*. *Concept* ya *Mtwara Corridor* ni lazima isukumwe zaidi na sisi Tanzania kuliko sehemu nyingine yoyote na ndiyo maana hata sisi wengine tunasema ukitaka kuwa *effective* ni afadhari hata uwe na ofisi pale Mtwara ya kushughulikia mambo yote yatakayojadiliwa au yatakayofanywa katika *Mtwara Corridor* kama ilivyo Dodoma hivi leo, *CDA* iko hapa, Wizara ilikuwepo, sasa tunachoshindwa na sisi kuhamia Mtwara kutoka huko chini ni nini? (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, mimi naomba ebu jaribu kuwakusanya wale wenzako wanaoeleaelea. Maana *Mtwara Corridor* inahusu mambo mengi. Kuna mambo ya utalii, kuna mambo ya kilimo, wavute hawa na mimi naamini kwamba mkifanya kazi kutoka Mtwara kwa vyovyote vile maendeleo yake yatakuwa makubwa. Mkisema kwamba tutaendelea kuiendelea kuiendeleza *Mtwara Corridor* kutoka Dar es Salaam mimi naamini kwa miaka mitano ijayo, kumi ijayo, *Mtwara Corridor impact* yake haitakuwepo. Kwa hiyo, naomba sana kwa kuwa wewe ndiyo Mwenyekiti, naomba kazi hii ikamilike na *Mtwara Corridor* iwe na maana katika nchi yetu. Nimekwishaona kuanzia Mtwara mpaka Masasi katika ujenzi wa barabara hiyo ya Mtwara, Masasi, Songea Mpaka *Mbamba Bay* wameanza kuchora X katika nyumba za watu. Sasa hivi “X” zimeanza sijui toka mwaka 2002, “X” hizo zinawakera sana sana watu kwa sababu “X” zipo katika majumba yao



hawaoni ujenzi wowote wa Barabara. Sasa kwa nini hizi “X” zimekaa muda mrefu namna hii? Halafu nikueleze pia Mheshimiwa Magufuli barabara hii wakati inajengwa kwenye miaka ya 1970, nyumba zilizopo sehemu kubwa ya maeneo haya kati ya Mtwara na Masasi nyumba zilikuwepo, barabara imefika baadaye. Sasa hivi leo mnapiga nyumba “X” halafu mje muondoe zile nyumba bila kuwalipa fidia. Hiyo ni haki jamani? Ingawaje ni utaratibu wa kisheria na kadhalika, lakini ni lazima muangalie na ubinadamu kwa watu wamekaa katika maeneo yale kwa muda mrefu sana.

Mimi naamini wewe askari wa miavuli katika kutekeleza jambo hili bila shaka utahakikisha kwamba watu wa ardhi wanakagua maeneo haya, wale walio na hati waweze kulipwa fidia na hata wale wazee ambao hawakuwa na hati walijenga nyumba zaidi kwenye miaka ya 1970 kusema kweli walipwe. Bila kulipwa haitakuwa haki jamani. Mimi naamini kabisa kwamba juhudi mnazozifanya zitaweza kabisa kukamilika kufanya haki katika maeneo haya. (*Makofi*)

Mwisho nataka kuzungumzia kidogo juu ya Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara huu nimeuona kwamba unafanya kazi vizuri katika maeneo yale ambayo utendaji katika Halmashauri zetu ni mzuri. Mimi nina mfano pale Masasi, katika mwezi wa Septemba, mpaka Desemba, fedha tulizotengewa na *TANROAD* hazijatumika mpaka leo, hazijatumika si kwa sababu watu wa Masasi hawana shida, hazijatumika kwa sababu utendaji katika Halmashauri yangu siyo mzuri.

Sasa kwa Mfuko wa Barabara kuchukua hatua ya kutoa fedha zile ili zisiweze kutumika, mimi naona hatua za namna hiyo zitaumiza sana wananchi wa Halmashauri ile. Badala yake tuwe na utaratibu mzuri, mnapoona kwamba mambo hayaendi vizuri muwahusishe Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo ili wafahamu kwamba kuna matatizo hapo waweze kusukuma na fedha hizo ziweze kutumika. Fedha za *road fund* tunazihitaji sana lakini mara nyingi Wabunge, hawahusishwi katika kuhakikisha kwamba zinatumika vizuri na kuona kwamba kazi zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara hizo, unafanyika.

Kwa hiyo, naomba sana hapa wananchi wa Masasi wasipate adhabu hiyo, bali mturudishie fedha hizi tutazitumia kwa sababu tuna barabara nyingi sana vijijini za kutengeneza ambazo tunahitaji fedha hizo. (*Makofi*)

Mwisho, ulikuwa umezungumza na nimeona katika kitabu hiki kwamba sehemu ile mbovu ya Chipite itatengenezwa mwaka huu, lakini kwa upande wa mbele sehemu ya Nangoo, hivi karibuni kumekuwa na ajali moja mbaya sana ambapo basi lilitumbukia na kuua watu 12, kwa sababu Daraja la Nangoo toka wakati wa mafuriko mpaka hivi leo halijatengenezwa. Katika mpango huu sikuona kitu chochote. Labda baadaye wakati unatujibu utatueleza ni lini kazi hii itafanyika. Ni muhimu sana kwa Daraja la Nangoo kutengenezwa ili tuelekane na hizi ajali zisizo na sababu na siyo hivyo tu lakini katika ujenzi wa barabara kutoka Mtwara mpaka Tunduru mpaka *Mbamba Bay* ni muhimu sana eneo hili lijengewe hilo daraja Lake. Baada ya kuzungumza hayo napenda kurudia tena kutoa pongezi kwa Wizara ya Ujenzi na kuwahakikishieni kwamba mimi naiunga mkono hoja yenu hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Lakini ningependa kueleza kwa nini vitabu vya Wizara ya Ujenzi viligawiwa jana, kwa sababu Mheshimiwa Kasapira alisema haijapata kutokea, ni kwa sababu utaratibu wetu ni kwamba nyaraka zote zinazogawiwa kwa Wabunge lazima ziwasilishwe mezani kwanza halafu ndiyo zinakuwa *public*, Waheshimiwa Wabunge watu wengine wote wanaotaka wanapewa. (*Kicheko*)

Sasa ratiba iliyoitishwa na Kamati ya Uongozi ya Mkutano, huu inaonyesha kwamba jana tarehe 30 Juni, 004 ndiyo ingekuwa siku ya Waziri wa Ujenzi, kuwasilisha hoja yake Bungeni. Lakini kwa uamuzi wa juzi wa Bunge hili, siku ya jana ikaondolewa kwenye shughuli za Bajeti. Lakini kwa kuwa ilikuwa ni siku yake basi tukamshauri kwamba awasilishe hati zake mezani, halafu zitajadiliwa siku inayofuata. Msingi ni kwamba lazima hati ziwasilishwe mezani kwanza ndiyo zigawiwe.

Kwa hiyo, Mawaziri wengine waliotangulia na watakaofuata kwa kuwa wanawasilisha nyaraka zao siku ile ile waliyopangiwa basi hawataweza kuzigawa kabla ya hapo. Hayo ndiyo maelezo yake. Sasa ratiba ya leo ni kwamba tutaendelea na mjadala wa jumla mpaka saa 12.00 na msemaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hassan Kigwalilo kwa kipindi cha mchana. Ikishafika saa 12.00 atakayekuwa kwenye kiti, atafunga mjadala ili wenye Wizara yao waanza kujibu hoja na baadaye tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi kama kawaida. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli.

Kabla ya yote ningependa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kilichotokea hivi karibuni hapa Dodoma. Kwa hilo nimefadhaika kwa kuona kwamba hatukuweza hata kidogo kushusha angalau Bendera yetu ya Bunge kwa ajili ya kukiheshimu kifo cha mwenzetu ambaye tulikuwa naye katika kuchangia Bunge hili linaloendelea.

Vile vile ningependa kutoa pole kwa mzee wangu Mheshimiwa Lawrence Gama, ambaye amefiwa na mtoto wake hivi karibuni. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu

pamoja na wataalam wake kwa hotuba hii nzuri ambayo leo hii naiunga mkono mia kwa mia. Kazi ambayo imefanyika kusema kweli Wizara hii isingestahili kuwekwa kiti moto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuweza kuweka mikakati mizuri na mipango mizuri ambayo itaimarisha barabara kuu pamoja na barabara za Mikoani.

Kabla ya hapo ningependa kupata maelezo zaidi kutokana na jarida hili la nyongeza ya hotuba ya Waziri. Kwenye hii ramani, *key* ambayo imeoneshwa kwa mfano *key* Na.5 ambayo ni *Lake Circuit Corridor*, ukija kwenye ramani yenyewe inaonekana *T4*, sielewi kama rangi zinanibabaisha au kuna hitilafu ya aina fulani, ningependa baadaye Mheshimiwa Waziri mhusika aweze kufafanua hali hiyo.

Hata hivyo bado naendelea kuipongeza Wizara kwa mikakati na mipango mizuri ya kuboresha barabara zetu. Wasiwasi mkubwa nilionao katika Bajeti hii ni kwamba kupitisha peke yake haitatusaidia kitu. Lakini kinachotakiwa baada ya kupitisha, Wizara hii ambayo ina mikakati mizuri ya kutengeneza barabara iweze kupata pesa hizo mara moja ili iweze kufanya kazi hii kabla ya masika kuanza. Kwa hilo, naomba Serikali ifuatilie kwa karibu zaidi ili imwezeshe Waziri huyu pamoja na wataalam wake kufanya kazi yao kama walivyotarajia katika mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara ya Kibiti kwenda Lindi. Kwa bahati mbaya au nzuri barabara hii pamoja na kwamba inaendelea vizuri, lakini namtaka Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa karibu zaidi shughuli za makandarasi waliopewa maeneo hayo, kwa mfano, Karafi pamoja na wale Wachina kusema kweli *speed* ya utendaji kazi imepungua. Mwezi Mei kwenye tarehe 12 na 13 tulikuwa na kikao cha Mkoa cha *Road Board* Mkoa wa Lindi - Kilwa. Tulipata fursa ya kutembelea mradi huo. Tulichokiona ni kwamba kazi nyingi hazijakamilika wala hazijafikia sehemu ambayo tunaweza kupata matumaini kwamba kweli barabara hii itakamilika katika awamu hii ya tatu tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karafi baada ya kuuliza wataalam wake wakatueleza kwamba atakachoweza kufanya ili kazi hii iende haraka ni *ku-subcontract* eneo lake ili kazi hii iweze kwenda vizuri. Sina uhakika kama hivyo ndivyo inavyofanyika hivi sasa au la.

Barabara ni nzuri kidogo kwa maeneo mengine, kwa mfano daraja la Matandu nimeridhika kwamba ni zuri na kwamba tunapita bila wasiwasi wowote. Sehemu ambayo ni kikwazo kikubwa kwa sasa hivi ni kutoka Somanga kwenda Nyamwage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili kusema kweli kwa kuwa labda kandarasi au mipango ya kupata mtu wa kujenga haijakamilika au iko mbioni, ina matatizo sana. Matatizo yaliyoko maeneo hayo hasa kwenye mwezi Aprili na Mei, huenda mwanzoni mwa mwezi Juni, palikuwa na mashimo makubwa sana kiasi kwamba malori na magari yalikuwa yanalazimika kwenda mwendo mdogo. Hiyo ilikuwa inahatarisha kwa kuwa

majambazi walikuwa wanajificha na kuleta bughudha katika maeneo hayo. Baadhi ya wananchi wamejeruhiwa na baadhi yao wameuawa na majambazi kutokana na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni kwamba, Waziri wa Ujenzi kwa kutumia nguvu zake za *TANROAD* aweze kwa kipindi hiki ambacho tunajaribu kusubiri mradi kamambe wa ujenzi wa eneo hilo, basi angalau afanye ukarabati wa hapa na pale ili mradi watu waweze kupita kwa usalama katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii nimefurahia sana kuona pia Wizara imepanga kuboresha sehemu korofi kwa kujenga na kuendeleza kujenga hasa kwa barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale na pia kutoka Liwale kwenda Nachingwea. Naipongeza sana Wizara kwa kutusaidia hivyo hasa ukitilia maanani kwamba Wilaya ya Liwale iko kando sana na tuna matatizo ya mawasiliano, haifikiki kirahisi.

Aidha, kutoka Nachingwea au kutoka Nangurukuru, hata mawasiliano ya simu sasa hivi ndio huenda yakaanza kutengemaa, lakini sina uhakika kama kweli yatafika karibuni au vipi lakini nimeshaahidiwa hivyo. Kwa hiyo, Wilaya ya Liwale tuko katika hali ngumu sana. Kwa hiyo, katika kuendeleza kujenga barabara zetu Mheshimiwa Waziri anatusaidia vizuri mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka mwaka 1999 Mheshimiwa Rais alilazimika kupanda helikopta kutoka Kilwa kwenda Liwale kutokana na barabara kuwa mbaya na msafara wake ulikwenda kwa kutumia barabara kwa shida sana. Alipofika Liwale Mheshimiwa Rais aliongea na wananchi na aliwaahidi kwamba atafanya kila atakaloliweza ili barabara hii kutoka Nangurukuru kwenda Liwale na sio Liwale tu hadi Masasi iweze kupitika wakati wa kipindi chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwa Bajeti hii huu mwanzo ni mzuri. Naomba kabisa kwa heshima na taadhima kauli hii ambayo aliitoa Rais mwaka 1999, leo hii namkabidhi Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, ili aifanyie kazi haraka iwezekanavyo tuweze kupata manufaa ya barabara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Liwale kwenda Nachingwea kuna kilometa 30 za mchanga sana. Eneo hilo ni gumu sana. Kuna magari yanakwama, magari mengine yanaleta *diesel* pale kwa ajili ya mitambo ya *TANESCO* lakini inashindikana, inaweza kukaa pale siku tatu au nne. Kuna magari ya wafanyabiashara yanakwama katika eneo hilo.

Tunashukuru kwamba kuna mradi kamambe utakaofuatia baada ya mwezi Julai ya kukarabati eneo hilo. Lakini ningepanga kwa wakati huu aruhusiwe Meneja wa *TANROAD* ambaye anafanya kazi yake vizuri sana, Ndugu Mwita Chacha au Chacha Mwita, apewe nyenzo za kuweza kukarabati eneo lile na ile barabara kutoka Nangurukuru kwenda Liwale kama hivi anavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilizungumza naye kwa simu kama sio jana na akanihakikishia kwamba kazi zilizokuwa kiporo mwaka 2003 sasa hivi zinaendelea vizuri. Naomba sana Mheshimiwa Waziri amuunge mkono huyo *Engineer* Chacha Mwita kusudi aweze kutusaidia kikamilifu wakati tunangojea mipango mingine kabambe katika barabara ya Liwale - Nachingwea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa sababu wanaliwale tumekwama kutokana na barabara hiyo. Kuhusu makandarasi ya akinamama, Liwale kwa bahati mbaya tumekuwa na uzoefu mbaya. Tuliletewa akinamama kutengeneza sehemu korofi, kwa bahati mbaya sielewi hawakupewa nyenzo nzuri, sehemu hiyo ikazidi kuwa korofi baada ya wao kukamilisha kazi hiyo.

Sasa naomba hili liangaliwe au lifuatiliwe. Sikujua kama hawa walikuwa wataalam kweli au waliwekwa barabara ya mafichoni ili isieleweke nini kinafanyika huko. Lakini naomba kwa utaalumu wako ujaribu kufuatilia hilo ili kusudi tatizo la aina hiyo lisitokee tena. Hatuna *alternative* ya barabara, kwa hiyo, naomba watu wa aina hiyo wapewe Mijini ambako *alternative roads* ziko nyingi tu za kufika wanakotaka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi kwa zoezi la kuuza nyumba kwa watumishi. Lakini mimi naamini zoezi hilo halikukamilika kwa kuwa kuna ma-DC, kuna ma-*Regional Commissioner* ambao wanye wadhifa ambao wanasaidia tu katika nchi hii. Lakini hawa majumba yao inaelezwa kwamba ni Ikulu ndogo, hadi sasa hivi hawana mpangilio wowote wa kujua watafaidika vipi na zoezi hili. Sio hivyo tu, hata baadhi ya sisi Wabunge tulipokuwa tunafanya kazi Serikalini, hatukukaa majumba ya Serikali lakini pia tulikaa majumba ya Msajili kwa hiari yetu na kwamba tumekaa katika majumba haya kwa muda ya miaka 30 na nadhani tuna haki ya kupata fursa ya kununua. Hebu Mheshimiwa Waziri aliangalie na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabango wanayowekwa pembeni ya barabara, kweli naafiki pamoja na Wabunge wengine kwamba yaondolewe haraka iwezekanavyo. Kinachojitokeza hasa nyakati za usiku, kwamba *reflection* inayotokana na alama X nyekundu na *reflection* ya lile bango ambalo tangazo limewekwa pale inasababisha mtu afikirie kwamba anacho-*overtake* ni gari na sio bango. Sasa hali hii inatia wasiwasi. Naweza kutoa mfano, juzi jumamosi tulitoka hapa saa 2.30, ilikuwa bahati mbaya mke wangu nilikuwa namtegemea kufika na basi la Shabiby, likaharibikia Kibaigwa.

Mimi na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan ikabidi tutoke hapa saa 2.30 usiku. Tumekwenda na hali hiyo ilitubabaisha sana humo njiani na kwa bahati Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan ni dreva mzuri kuliko mimi. Kuna eneo ambalo mimi niliona kibao nikadhania ni gari tunataka ku-*overtake*, mbele yake kuna daraja. Kusema kweli kama ningekuwa mimi, ninge-*overtake* daraja. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri ang'oe vibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. OMAR MOHAMED MWENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye dira ya maendeleo. Pia nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya kwa kutujengea daraja. Kwa kweli daraja lile ni ukombozi mkubwa. Kabla ya kujengewa daraja tulikuwa tunadhalilika watu wa Kusini wote. Ndugu zetu wa Rufiji walikuwa wanafanya mipango ya makusudi kuiharibu ile *boat*, lakini wakati huo walikuwa wamekwishawatanguliza wake zetu, wamewapeleka ng'ambo sisi wenyewe wanatuacha huku. Kwa hiyo, hivi sasa mpango huo haupo tena, tunashukuru. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona ameelezea kilometa 60 zilizobaki kuanzia Ndundu hadi Somanga kwamba mkataba utafanywa mwezi huu Julai na utakamilika mwezi Machi, 2005. Hili limenipa mashaka kidogo kwa sababu muda huu wote imeonekana kipande hiki sisi dhahiri hatutakipata kwa wakati huu. Nadhani labda itakuwa mwaka 2010. Sasa pamoja na uzuri huu wa daraja, lakini ili ulifikie daraja hili lazima barabara zake zote ziwe safi. Sasa tunalifikiaje daraja hili kama kilometa 60 hizi bado hazijatengenezwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja ni kama chupi, huwezi kujisifu una chupi nzuri ukatoka nje kama hujavaa suruali au shuka. Sasa sisi tunajisikiaje na daraja hili? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Naomba utumie lugha ya Kibunge. Endelea lakini tumia lugha ya Kibunge, futa hilo neno.

**MHE. OMAR MOHAMMED MWENDA:** Ahsante. Nafuta suala la chupi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie eneo la barabara kutoka Somanga hadi Nangurukuru na kutoka Nangurukuru hadi Mbwenkuru na kutoka Mbwenkuru mpaka Mingoyo, hii tunaishukuru Serikali. Lakini kuna tatizo moja lililojitokeza na hilo ndilo walilonituma hasa wananchi na ningewaomba watu wa redio wanukuu sehemu hiyo. Wananchi wamenituma kama wakandarasi wale hasa kutoka Nangurukuru mpaka Mbwenkuru hakuna kazi wanayoifanya. Kwa muda sasa wa mwaka mmoja na nusu hata kilometa 30 bado. Wana mashaka makubwa kwamba hawa hawatamaliza hii barabara na pale imekuwa kama wamewekwa kanyaboya kwa sababu hawafanyi ile kazi hasa inayotakiwa. Sasa sijui hilo kama Waziri analijua na kama analijua analichukulia hatua gani. (*Makofi*)

Lakini lingine, wananchi wanaomba sana zile alama za X basi ziwekwe ili muda huu wa kiangazi wapate kuvunja majumba yao na kujenga majumba mengine kwa sababu kwa sasa hivi hawana kazi ya kilimo. Lakini X zikijakuwekwa wakati wa kifuku

watashindwa kujenga majumba kwa sababu wana shughuli za kilimo. Hili wanaliomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la bomoa bomoa. Tunajua sheria ya *Road Reserve* ilikuwepo toka mwaka 1935, lakini sheria hii wananchi hawakujua, ilibaki ndani ya makabrasha. Sasa kama wananchi hawakujua na leo wanakuja kuambiwa mvunje majumba yenu bila malipo, hivi hatuoni kama tunawaonea? Maana sheria haki yake waijue, lakini Wakoloni walikuwa hawaitangazi sheria na hakuna asiyejua. Sio sasa hivi Serikali iko wazi, tunaitangaza sheria. Sisi Wabunge tunapotunga sheria hapa, tunaporudi kwa wananchi wetu tunawaeleza. Lakini zamani haikuwepo hivyo. Sasa tunafanyaje?

Lingine, kuna maeneo barabara imewakuta wananchi, kama pale Mandawa. Barabara hiyo imewakuta wananchi kwa sababu wananchi wenyewe ndio waliotoboa ile barabara. Sasa hawa tunawaambiaje?

Kwa hiyo, ningepomba hawa watu walipwe, tena maskini ya Mungu vibanda vyenye wala havina thamani kubwa. Hakuna nyumba inayoweza ikafika milioni tano, sita, hakuna! Ni vijumba vya kawaida tu. Sasa kwa nini tusiwalipe ili tusipambane nao hawa wananchi bila sababu? Namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kuwa sheria ndio imesema hivyo, lakini izingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la mizani. Mizani imekuwa tatizo kubwa sana katika barabara zetu na hasa ukiangalia hapa karibu na Mkuranga, tunayo pale mizani tena tunasema ya kisasa. Lakini mizani hiyo mimi naishangaa sana. Tumewahi kuja na basi na basi hilo abiria hatukutimia 65. Basi hilo linaitwa Nuzurani, mimi nilikuwepo ndani ya basi hilo na halina mzigo wowote. Lakini bado waliambiwa wamezidisha tani na wakatozwa faini. Sasa sijui hii mizani mbovu au utaratibu tu wanaofanya hawa kwa makusudi! Sasa ningepona hili liangaliwe, ushahidi huu upo.

Lakini kitu kingine, kunakuwa na magari yana uzito mdogo tunafahamu. Gari la tani nne, tano, lakini hilo nalo bado linakuwa tatizo, inaonekana limezidi uzito. Kwa hiyo, ningepomba suala hili la mizani liangaliwe, magari pale yanakaa foleni na yanawekwa foleni kwa mpango mzima tu. Si hapo tu, hata Kibaha utayakuta yamekaa foleni. Lakini pia ile faini nayo ni kubwa, Wafanyabiashara wanashindwa. Faini hiyo iangaliwe. Hatukatai kama wale wanaozidisha uzito wasipigwe faini, wapigwe faini, lakini iangaliwe faini hii ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuta gari la Mbunge mmoja sitaki nimtaje, yeye mwenyewe anajijua, kapigwa faini laki moja na nusu. Amehangaika maskini, dreva hakupata, abiria wameshindwa kusafiri, nikapita mimi akaniazima. Sasa hili ni tatizo kubwa, iangaliwe hii faini. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja ya Waziri wa Ujenzi. Kwa kuwa

nilikwishatoa rambirambi, nitaendelea kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu yote ya Maafisa katika Wizara hii kwa kuandaa hotuba ambayo ni ya kina na imegusa maeneo yote ambayo yalihatijika yaguswe katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipitia hotuba ya Waziri, nimeridhika sana alivyonukuu dhamira ya Serikali katika utendaji, kwa sababu kama alivyoeleza Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsishaji, kwamba ni dhamira ya Serikali kuimarisha miundombinu ambayo itawezesha kufungua maeneo mbalimbali yatakayochangia katika uzalishaji katika kilimo na uchukuzi. Dhamira hii inatokana pia na maamuzi au maazimio ya viongozi wa nchi za Afrika, ukanda wa Afrika Mashariki na Serikali zao na kuimarisha kanda mbalimbali katika nchi hizi katika masuala ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana hotuba ya Waziri kwa sababu nikiangalia ukanda wa Magharibi, hotuba inaonyesha mipango ambayo inaziunga nchi za Uganda na Zambia na hii itawezeshwa na barabara ya Nyakanazi kupitia Kasulu, Sumbawanga na Tunduma. Barabara hii ni barabara nzuri itakayofungua ukanda huu wa Magharibi. Lakini kama walivyosema Kamati ya Miundombinu ili barabara ya namna hii iweze kuwa na ufanisi katika matarajio yake ni lazima iungwe na njia nyingine za uchukuzi.

Kamati hii ikaainisha kwamba barabara hii ambayo nimeitaja ikiungwa na barabara za kufika hadi Ziwa Tanganyika itakuwa imeunganisha na uchukuzi kwa njia maji na wakataja bandari ambayo inaweza kunufaika, bandari kama ya Kasanga. Mheshimiwa Waziri naomba nimwongeze kipande kingine cha barabara katika ukanda huo ambacho kikiunganishwa na barabara hii kitakuwa kimefungua eneo ambalo lina umaarufu mkubwa kutokana na raslimali zilizopo katika eneo hilo. Hiyo ni barabara ya Mpanda kwenda Mwese hadi Rukoma kwenye Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu itakuwa imeunganisha mbuga mbili za Taifa za Hifadhi, Mbuga ya Mahale na Mbuga ya Katavi, maarufu kwa utalii. Kwa sababu ipo barabara kutoka Mpanda mpaka Mwese na kutoka Mwese hadi Rukoma hakuna barabara isipokuwa *feasibility study* au uchambuzi ulikwishafanyika pamoja na usanifu bado gharama za ujenzi. Sasa wito wangu kwa Waziri katika hili ni kuangalia uwezekano wa Serikali kujenga kipande hiki cha barabara Mwese hadi Rukoma kwenye Ziwa Tanganyika na kutoka hapo unaweza kwenda hadi Buhingu na Buhingu ni Kituo kilicho karibu na Mahale kama mbuga ya wanyama na ambayo natarajia hata Waziri wa Mawasiliano atakapokuwa anawasilisha hotuba yake, natarajia azungumzie suala la gati kwenye kituo hiki, kwa sababu watalii wanaokwenda kwenye mbuga ya wanyama ya Mahale wanapata taabu sana katika kituo hiki cha meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili kama nilivyosema lina fursa za kilimo, uvuvi ambapo wa daga na samaki wengi, lakini kuna fursa pia ya Utalii na Madini.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wengi watakuwa waliona tangazo au taarifa katika gazeti moja la Mwananchi, ninalo hapa ambalo linasema: “Madini Mapya Yafoka Kigoma.”

Haya ni madini ambayo yako katika eneo hilo ambako Kampuni ya *Anglo American* wamefanya jitihada kubwa katika kuyatafiti madini hayo na madini mengine. Si ajabu kwa eneo hilo likawa na madini kwa sababu Mpanda kwa asili tunajua kuna dhahabu na kwa hiyo eneo linalopakana na Mpanda lazima litakuwa na uwezekano wa madini ya dhahabu au hata mengine kama haya ambayo yamezungumzwa na uchunguzi wa hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikiacha eneo hilo, ipo barabara ambayo imeoneshwa kwenye hotuba ya Waziri ambayo nitamwomba sana Waziri anisikilize katika hili ninalolisema, ni barabara ya Mwandiga hadi Manyovu mpakani mwa Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha kwamba itawekwa lami, lakini amesema ni *otta seal*.

Mimi naomba aiangalie tena hii kwa sababu ni barabara muhimu sana, ni barabara itakayokuwa inaunganisha nchi mbili katika kufanya biashara na nchi ya tatu ni Kongo ambayo kwa maana hiyo kama barabara unaiweka lami ya *otta seal* maana yake ni lami nyepesinyepesi. Biashara tunayoitazamia kupitia kwenye barabara hii ni kubwa na nzito itakayohitaji lami ambayo ni imara zaidi kuliko hiyo nyepesi nyepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo pia barabara hii ya Kigoma-Uvinza-Kaliua hadi Tabora. Nimeangalia kwenye kitambatisho namba tano, nimeitafuta siioni kabisa. Kwa hiyo, natazamia Mheshimiwa Waziri wakati wa mafungu anithibitishie kwamba hiyo barabara imo, kabla sijasema hilo fungu lake aende nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara nyingine katika ukanda huu. Nauzungumzia ukanda huu kwa sababu tunataka ukanda huu ufunguliwe. Ipo barabara ambayo niliwahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, ofisini kwake na bahati nzuri akamwita na Mtendaji wake Mkuu, Katibu Mkuu, ni barabara ya Ilagala kwenda Kalya. Hii barabara ina urefu wa kimlometra zipatazo 130 na ni barabara ya Mkoa. Lakini hadi sasa barabara hii haijawekwa kwenye programu yoyote. Mwanzoni waliombwa *OPEC* lakini haikufanyika na haina fungu lolote. Kwa hiyo, ili barabara hii ya Mkoa iweze kufanya kazi na iunganishe maeneo yote ya Sigunga, Herembe, Kaparamsenga, Mgambazi hadi Rukoma kutoka Ilagala ikaungane na ile ya Mpanda-Mwese-Rukoma tutakuwa tumeunganisha na Mkoa wa Tabora kwa kupitia Mpanda kwa sababu Mpanda umeunganishwa na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mkakati huo ambao naamini kabisa Mheshimiwa Waziri na timu yake wanaweza kufanyia kazi, tutafika mahali tunalifungua hili eneo na nasisitiza zaidi kwamba barabara hii si ya kiuchumi peke yake ni barabara ya ulinzi pia. Maeneo haya tumekuwa tukisumbuliwa sana na watu kutoka nchi za jirani, wakimbizi na

kadhalika. Sasa tunahitaji barabara ambayo itatufungulia njia hii na kuwafanya wananchi waweze kufanyakazi za maendeleo ya uchumi. Kwenye barabara hii nilikwishamweleza Mheshimiwa Waziri wakati tunazungumza ofisini kwake na nikamwandikia barua mwezi wa pili ambayo bahati mbaya hajanjibu. Sasa nadhani atanjibu baada ya mazungumzo haya.

Kuna tatizo la kivuko, amelizungumzia Mheshimiwa Bernadine Ndaboine. Mimi nitaongeza zaidi, kivuko hiki ni kidogo, ni kikuukuu nadhani kilijengwa kwa ajili ya kuvusha watu pamoja na kwamba sasa hivi wanajaribu hata kuvusha saruji kwenda kujenga shule ng'ambo ya Mto kwa njia za lori la tani tano. Sasa wazo alilokuwa amenieleza Mheshimiwa Waziri kwamba kifanyiwe ukarabati. Nadhani si vema kufanya ukarabati kwa kitu ambcho ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachozungumza kwenye hii barabara kivuko hiki kwa kweli kinahitaji kubadilishwa ili kipatikane kipya chenye uwezo wa kuvusha mitambo ya kwenda kushindilia barabara ng'ambo ya pili. Kwa sababu kivuko cha tani tano kitavushaje mitambo ya tani 20 au tani 30, haiwezekani. Kwa sababu tunahitaji kuendeleza barabara hii na wananchi kutoka Kalya, Mgambo, Sigunga, Sunuka hadi Ilagala, wote wamehamasika na wako tayari kusaidia katika kazi. Serikali tutaiomba ishughulikie madaraja na makalvati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri aje Kigoma na nina uhakika atakapokuja tutakwenda wote mpaka Ilagala tuvuke Mto kwa kutumia kile kivuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Waheshimiwa Wabunge waliokuja Kigoma wakati wa Maadhimisho ya Sherehe ya mwaka wa Familia Duniani, walifika pale na Mheshimiwa Margareth Mkanga ni mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walishangaa, wakatuhurumia, kivuko bado kinavushwa kwa kukanyaga kwa miguu na kamba. Si kivuko cha karne ya 21! Kwa hiyo, ni rai yangu kabisa na kwa sababu jana kwenye hotuba ya Rais amesema alishiriki sana katika kuandaa Bajeti hii na amefuatilia na aliruhusu iletwe Bungeni na akasema michango ya Waheshimiwa Wabunge itazingatiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikiliza kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri na timu yake watazingatia haya tunayoyasisitiza ili Sekta hii iweze kushamiri kama inavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOB:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Lakini kabla ya yote ningechukua nafasi hii kuipa pole familia ya marehemu Yete Mwalyego, aliyefariki hivi karibuni na kumwomba Mungu kwamba awape nguvu, waweze kuhimili hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Wizara hii kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa vitengo mbalimbali vya ujenzi kwa kazi zao kubwa wanazozifanya katika kuendeleza gurudumu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyemfahamu Mheshimiwa John Magufuli, kwa kazi anazofanya na hakuna atakayepinga hilo. Mheshimiwa John Magufuli amekuwa anajituma na ndiyo maana hata watendaji wake wanafanyakazi kwa bidii kutokana na jinsi mwenyewe anavyojituma katika kazi zake. Kwa hiyo, lazima tumpongeze katika hilo kwa kuonyesha mfano huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze kwamba katika kuwasilisha kwake amesema kwamba daraja langu la Kigamboni litajengwa hivi karibuni na kwamba hivi sasa unafanywa utafanywa utaratibu wa *feasibility study* ili kuhakikisha kwamba daraja linajengwa mapema. Pia amezungumzia barabara ya *Kilwa Road* ambayo ni kero kubwa nadhani Mheshimiwa Waziri hata mwaka 2003 niliwahi kukuomba kwamba ungetembelea Mbagala ungejionea tunavyopata tabu asubuhi tunapokwenda kazini. Nadhani hilo Mheshimiwa Waziri ungelichukulia uzito unaostahili na kwa sababu umetaja kwenye Bajeti yako naamini kwamba sasa kazi hii itafanyika mapema.

Lakini nilikuwa naomba kwamba wakati huo tunasubiri utaratibu ukamilike ningekushauri kwamba hiyo barabara ingepanuliwa kwa kawaida tu wakati tunasubiri lami ili watu, madreva na magari yaweze kupita pembezoni kwa urahisi. Kwa sababu hali imekuwa mbaya sana Mheshimiwa Waziri, watu wengi sasa hivi wamehamia Kigamboni na watu wengi wanataka kujenga kule lakini hali ya barabara ni mbaya na ni finyu mno na ajali zimekuwa nyingi kwa sababu barabara hiyo imekuwa ni finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba wananchi wangu hawatalipwa kwa sababu mlisahasema kwamba tulikiuka misingi ya sheria na kwamba watu walijenga katika maeneo ya *road reserve* lakini nasema wazi kwamba hawa watu hawakujenga kwa makusudi na pia niombe Serikali kwamba kutokana kwamba kulikuwa na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Madiwani kipindi hicho na Wajumbe wa Nyumba kumi, kumi. Mimi nadhani kungekuwa na sababu ya kuwachukulia hatua kwa sababu wao ndiyo waliwa-*mislead* wananchi wangu kujenga katika maeneo ambayo ni ya akiba ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani mtu akajenga bila sababu. Watu walikuwa wamejenga kwa sababu walikuwa wameshapewa maeneo na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Madiwani walishiriki moja kwa moja kuwapa vibali vya kujenga wananchi hawa. Leo hii wananchi hawa wamebomolewa nyumba tena kwa hiari yao baada ya kuwashawishi kwamba wakubali kubomoa kwa sababu Serikali inataka kuleta maendeleo katika maeneo yetu. Lakini ikategemewa kwamba wangelipwa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila kwa sababu Serikali ilisema tunavunja sheria, lakini nasema Serikali siyo kwamba tumevunja sheria sisi, isipokuwa viongozi ambao waliteuliwa na Serikali ndio wamevunja Sheria kwa kuwa-*mislead* wananchi wangu

kujenga katika maeneo ya barabara. Kwa hiyo, naomba wananchi hao au viongozi hao wachukuliwe hatua na ikiwezekana walipe fidia wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba kama Mheshimiwa Waziri atanielewa katika hilo nitamshukuru zaidi kwa sababu *Kilwa Road* kwa kweli inatia aibu. Siyo kutia aibu tu lakini inawafanya watu wanaokwenda kazini wachelewe kwenda kazini kuzalisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara inayokwenda Charambe, hii barabara iko chini ya Serikali Kuu. Barabara hii imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu na wananchi. Kwanza kuna ajali nyingi, pili kuna mifereji ambayo imeelekezwa kwa wananchi. Mifereji hiyo, iko katika eneo lote la Charambe ambayo inakusanya maji kutoka Chamazi na Charambe yenyewe inaingia kwenye nyumba za wananchi. Wananchi wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu karibu sasa hivi mwaka wa pili na tumejaribu kuleta maombi kwa Mkurugenzi wa *TANROAD* ili alione hilo, akasema tutashughulikia, tutashughulikia, lakini naona sasa hivi mwaka wa pili unakwenda hilo suala halishughuliwi mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, wewe mwenyewe kwa makusudi yako kama kutokana na jinsi unavyotenda kazi zako naomba utembelee eneo hilo ujione na nyumba zilizobomolewa na wananchi kutokana na mvua kubwa inavyonyesha wananchi sasa wamehama maeneo hayo hawakai tena kwenye nyumba zile. Kwa sababu mvua inaponyesha mfereji ule unachukua maji mengi na kupeleka kwenye nyumba za wananchi, kiasi kwamba nyumba zimebomoka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamelalamika kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri, naomba sana hilo ulitatie, inawezekana kwamba hawa watu tunawafuatilia labda wana majukumu mengi, labda kwa kukuona utafuatilia mwenyewe watatoa kipaumbele kuhakikisha kwamba ile mifereji inabadilishwa inakwenda katika sehemu ambayo haihusiani na nyumba za watu na wananchi wangu wako tayari kusaidiana na Serikali kuhakikisha ile mifereji hata kwa kuchimba, wako tayari kuchimba kuelekeza kwenye Mto Kizinga ambao ndiyo sehemu ambayo ilitakiwa ipeleke hayo maji.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri ulizingatie hilo kwa sababu wananchi wamenituma na licha ya kunituma wamelalamika, wamekwenda mpaka Ofisi ya *TANROAD* kule Ubungo kuelezea kilio chao, lakini ukweli mpaka sasa hivi hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa licha ya ajali ambazo zinatokea. Lakini ukweli ni kwamba bado hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba tunazuia ajali na pia wananchi wangu wanapata faraja kuishi kwenye nyumba zao ambazo wamejenga kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije kwenye barabara inayokwenda Mji Mwema. Barabara hiyo inatoka Mji Mwema kwenda Kimbiji, barabara ya lami imeishia Mji Mwema. Barabara hiyo ni barabara ambayo kwa sasa hivi kama tukiweza kuijenga itaweza kuinua uchumi mkubwa katika nchi yetu. Kwa sababu sasa hivi inabeba watalii

wengi, kwa sasa hivi Jimbo la Kigamboni linabeba watalii wengi siku za *weekend* kwa sababu bahari ile inapendwa kuliko sehemu nyingine yoyote sasa hivi.

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba ili kuimarisha uchumi tungewajengea barabara ambayo itakwenda mpaka Kimbiji-Yaleyai-puna-Pemba Mnazi ndipo ambapo utakuta week end huwezi ukakuta nafasi hata moja ukienda kupumzika kule. Kwa sababu watu wengi wanatoka sehemu nyingi kwenda kupumzika kule. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni eneo la uchumi kama kweli tutaiboresha hiyo barabara, hata kama sasa hivi hatuwezi kuweka lami, lakini kiwekwe kwa kiwango cha kokoto lakini ipitike kwa uzuri. Hivi karibuni walifanya ukarabati lakini ukarabati ulikuwa hauna uzito mkubwa kiasi kwamba mvua ikinyesha kidogo inarudia hali ile ile ya zamani na usafiri wananchi wangu wanashindwa kupata usafiri kwa sababu hakuna gari zinazokwenda kutokana na hali ya barabara ilivyo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie kwa hilo, siyo kunisaidia tu lakini pia atakuwa amesaidia kuinua uchumi wa Pato la Taifa letu kwa kuingiza hela za kigeni kwa kutumia wageni wanaokuja kutembelea bahari pale Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije kwenye suala la magari ya Serikali, hili kila siku nitakuwa nagombana na Serikali kwa sababu ni lazima niseme hali halisi ilivyo. Hapa juzi wakati nachangia kwenye Wizara ya TAMISEMI nilisema kwamba kumekuwa na mtindo sasa Wakuu wa Idara au viongozi wa Wizara kutoa magari Mikoani kuyapeleka Dar es Salaam kwenye matengenezo.

Mimi naona kama ni kufuja fedha za Serikali. Leo hii unaitembeza gari kilometa 500 kwenda kutengeneza Dar es Salaam na kurudi kilometa 500, kilometa 1,000 hazijafanya kazi kwenye shughuli za Serikali na ukiangalia gharama za kutengeneza magari ya Dar es Salaam kwa *dealers*, ukichukua mahesabu, ukichukua miezi sita unaweza kukuta unaweza kununua gari mpya, *why?* Hii ni fedha ya wavuja jasho, kwa nini tusi-*economize* fedha? Tunakubali kwamba magari ambayo yako kwenye mkataba wa *dealers*, yaende kwa *dealers* kweli.

Hapa Dodoma kuna kitengo cha Ujenzi, kwa nini kisiimarishwe ili magari ya Serikali yakatengenezwa pale. Kuna sababu gani? Kitengo hicho kiimarishwe, kipewe hela, kitengeneze magari na kwa sababu sasa hivi viongozi wengi, *I mean* Wizara nyingi wanashindwa kupeleka magari pale kwa sababu wanahisi kwamba hakuna mafundi wa kuaminika pale, kitu ambacho si kweli, naamini tu kwamba kitengo hicho hakijaimarishwa na kina mafundi wazuri ambao wanaweza wakafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunasema kwamba hakiwezi kutengeneza magari ya Serikali basi kifungwe, tuelewe kwamba hakuna *garge* inayoweza kutengeneza magari hayo katika maeneo yetu. Haiwezekani gari utoe Mbeya upeleke Dar es Salaam kwa matengenezo. Gharama inakuwa ni kubwa, kwa nini unampa fedha dreva, bei ya mafuta kwenda na kurudi pia muda wa kusubiri gari Dar es Salaam kwa nini? Kwa nini tusione kwamba ni tatizo hilo?

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa John Magufuli uliangalie suala hilo katika kitengo chako hicho. Hiyo ni Wizara yako inahusika. Naomba uliangalie hilo na ulitupie macho.

Aidha, kwa sababu Serikali imejitoa kwenye mambo ya biashara nasema Kitengo cha Ujenzi kinataka kufanya biashara, basi mjiondoe kwenye suala la kusimamia magari, ili kitengo cha Ujenzi kijitegemee kama kitengo cha biashara ya kutengeneza magari. Lakini mkiimarisha, kwa sababu kina mafundi wazuri, *m-control* kusimamia shughuli hizi kuliko ilivyo sasa kwamba mnatengeneza magari ya Serikali huku mmesimamia gereji za watu binafsi. Mtashindwa kueleweka.

Kwa mfano, mmetoa kibali, hivi karibuni mmetoa *tender*, *let say* mmetoa *tender* ya kutengeneza magari hayo. Sasa *tender* gani, gari bado inakwenda Ujenzi kukaguliwa tena. Sasa huo ni usumbufu ambao unakuwa hauna ulazima. Nilikuwa nadhani kwamba ukishampa mtu kibali, basi gari iende moja kwa moja kutengeneza gari, kuliko tena gari irudi Ujenzi, irudi tena kule inakuwa vigumu kuelewa ni nini tunafanya.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri hilo pia aliangalie. Nadhani Mkurugenzi wa Ufundi na Mitambo Bwana Ndunguru atanielewa katika hilo kwa sababu mara nyingi nadhani yeye ni msimamizi wa hizi shughuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimpongeze Mkurugenzi wa Ufundi na Mitambo kwamba kivuko changu cha Kigamboni kinafanya kazi yake vizuri sana na pale kinapoharibika kinachukuliwa hatua za haraka sana kuhakikisha kwamba kivuko kinafanya kazi wakati unaotakiwa. Kwa kweli lazima nimpongeze kwa sababu ni adha ambazo ameziondoa kuliko wakati wa nyuma alikuwa anapata tabu sana kivuko kinakaa wiki nzima hakifanyi kazi. Kwa hiyo, nampongeza kwa usimamizi mzuri. (*Makofi*)

Lakini nimesema sifa hizo wewe ndiyo umesababisha zipatikane kwa sababu unasimamia kazi yako vizuri na kwamba mara nyingi umekuwa ukifuatilia mwenyewe kwa karibu. Kwa hiyo, naomba nimpongeze Mkurugenzi wa Ufundi na Mitambo Bwana Ndunguru, kwa usimamizi wake mzuri. Lakini pia ningepomba kwamba afuatilie suala la ratiba, bado kuna tatizo la ratiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ratiba nilikuwa nimemwomba kwamba kipindi cha wakati wa asubuhi sana kuna wananchi wangu wanaochukua mazao kutoka maeneo ya Pemba Mnazi, Kimbiji na Yalelepuna. Wanapofika pale wanachelewa kuuza mazao yao ambayo wanatakiwa wayapeleke Kariakoo. Ikifika saa moja yale mazao yanakuwa hayawezi kununuliwa kwa sababu tayari biashara inafanyika asubuhi sana.

Sasa kivuko kinapokwenda saa moja wanakuwa wameshachelewa na wananchi wanalala Kivukoni pale, nimeshasema mara nyingi kwamba kuna wake wa wananchi wangu wengi wameachika kwa sababu sasa hawaelewi kwamba wanaume zao wanalala wapi! Mtu anakuja na mazao pale Kivukoni saa 9 alfajiri, analala pale mpaka asubuhi saa moja anakuwa hajarudi. Sasa mtu anakuwa na wasiwasi na hilo kwamba aah, hivi ni kweli biashara au kuna kitu kingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba ili kutokuvunja ndoa za wananchi wangu, naomba utaratibu huo ubadilishwe na ratiba ipangwe upya ili wananchi wangu wafaidike na hilo na wauze mazao yao kwa muda unaotakiwa ili waweze kupata pato lao ambalo wanatoa jasho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namshukuru Mheshimiwa John Magufuli kama kweli amenisikia na kama atatekeleza haya, lakini nisisitize kwamba *Kilwa Road* naomba ikiwezekana sasa ianze kupanuliwa hata kwa kiwango cha kokoto wakati tunasubiri masuala ya lami ili wananchi wasipate taabu na tusiweze kuchelewa katika kuzalisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nitumie dakika chache kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Kwanza kabisa nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu Waziri pamoja na Wataalam wake wanaofanya kazi kwa bidii sana nchi nzima, kila mahala unapokwenda unakuta *foundation stone* imewekwa ya barabara. Kwa hiyo na mimi nitaomba kuwa akae mpaka mwaka 2012 aone kuwa amemaliza zile kilometa 10,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuchangia kwa upande wangu mimi nilikuwa na machache tu kama mawili, matatu, hivi. Ya kwanza kabisa ningependa kujua uhusiano wa *TANROADS* na sehemu nyingine za Serikali. Kwa kuwa *TANROADS* wana *Managing Director* kule juu na watu wake wapo mpaka Mkoani tu, Wilayani hawana *TANROADS Manager* wanae kwenye Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *TANROADS* wanahusiana vipi na Wizara yenyewe, halafu *TANROADS* na Mkoa ni *TANROAD* na *District*, sijui kama wana uhusiano wa namna gani? Halafu kazi kubwa ya *TANROADS* je, kazi yao ni kujenga barabara au ni kusimamia kazi wanazofanya ma-*contractor*? Kwa hiyo, ningependa na mimi nieleweshwe zaidi kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninalotaka kuongelea kidogo ni kuhusu miradi ya Kanda. Ameeleza kidogo ukurasa wa 7 mpaka wa 10 kwenye kitabu chake cha hotuba, lakini kwa sisi hapa Tanzania nadhani tunazo nyingi tu hizi *corridor* kama alivyoweka yeye mwenyewe pale. Lakini kwa sasa hivi tunashughulika nazo kwa dhati mbili, ile *Mtwara Development Corridor* pamoja *Central Development Corridor*. (*Makofi*)

Sasa Mtwara iko na vipande mbalimbali ndani ya *corridor* hizo kuna miradi maalum ambayo inaendelezwa na hiyo inaenda vizuri, hata *Mtwara Development Corridor* na yenyewe inaenda vizuri. Isipokuwa mahala padogo ni kuwa vikao maana

waliweka vikao vya wataalam, vikao vya Makatibu Wakuu, vikao vya Mawaziri ndani ya kila nchi halafu kuna vikao vya Mawaziri wa hizi nchi tatu za *Mtwara Corridor*, *Zambia-Malawi-Mozambique* na sisi Tanzania na sisi ndiyo waratibu wa *Mtwara Development Corridor*, sisi maana yake Tanzania, sisi ndiyo waratibu. Lakini naona kwa muda mrefu kidogo hawajaitisha kikao cha Mawaziri kuongelea habari ya hiyo.

Sasa kwa hofu hiyo, mimi nahofu kuwa wale wengine wameanza kusukuma miradi ya *Nakala Development Corridor*, yaani wanaenda Kusini zaidi. Kwa hiyo, nao wanakwenda Zambia, wanaenda lakini nia yao kule hasa wenzetu wale wa *South Africa* ni kuitengeneza tena *corridor* na kuvutia biashara toka *DRC*, Rwanda, Burundi iende Kusini na sisi hapa tukichelewa zaidi tutakosa hiyo *Mtwara Development Corridor* yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa na nguvu sana. Pili, ni kwamba wale waasisi wa hiyo *Mtwara Development Corridor* naona kama wamefikia muda wa kung'atuka hivi. Bwana Bakili Muluzi kule Malawi amesha ng'atuka na Bwana Joachim Chisano nadhani mwaka huu naye anang'atuka na Mzee wetu Bwana Benjamin William Mkapa nadhani mwakani anang'atuka. Sasa tutakuwa na watu wapya, labda hawatakuwa na moyo ule ule wa kusukuma hilo *Mtwara Development Corridor*.

Kwa hiyo, ningependa kwamba tufanye juhudi za vikao hivyo haraka vya wale Mawaziri ili kusudi hao Marais ambao wameingia karibuni wawe *involved* tangu wanapoanza kazi zao katika wakati huo. Kwa hiyo, ilikuwa Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho kabisa niongelee habari ya Jimbo la Peramiho au Songea Vijijini. Nako pia nina maombi makubwa mawili. Tuliandikiana na Mheshimiwa Waziri na yeye aliniandikia, nashukuru sana. Lakini naona kuwa niyachukue hayo kama maombi.

Moja, ni barabara inayotoka Songea kwenda Mitomoni pamoja na Daraja la Ruvuma ili tuweze kwenda Mozambique na kwa kweli hiyo tukiweza kuimarisha inaweza kuwa pia *corridor* nyingine ya kutoka Nairobi kwenda Kusini kupitia Songea kwa kutoka hiyo ya *Cape Town to Cairo* kuanzia Makambako inaweza kuwa Makambako-Njombe-Songea-Lichinga unaweza kufika Lichinga kuna *infrastructure* zinaunganisha na Maputo pamoja na Kusini kote, Malawi kwa kupitia *East Malawi*, *East* ya *Lake Nyasa* pamoja kufika Zimbabwe pamoja na Afrika Kusini.

Kwa hiyo, nilidhani kuwa ni muhimu, naomba pia Mheshimiwa Waziri aiweke kwenye ramani zake ili iweze kujenga barabara. Kwa sasa hivi naomba tu ile ya kwenda Songea mpaka Mitomoni na daraja lake ya kwenda Lichinga. Siyo zaidi ya hapo. Hiyo natoa tu mawazo kuwa baadaye inaweza ikawa hivyo.

Halafu ya pili, nayo ni ya muda mrefu ni kutoka Wino kwenda Ifinga. Hiyo barabara ipo na ilikuwepo lakini kwa nusu ya barabara inapita kwenye *swamps* kwenye Mito. Sasa iliamuliwa kuwa tuweze kupitisha mwaka mzima tupite milimani ambako inakuwa *divide* ya Mito, inakoanzia ile Mito ndiyo tupite huko.



Kwa hiyo, tulifanya, nashukuru sana kwani Wizara yako ilitusaidia sana na tukafanya hiyo kazi, ikatoboa Wino ikafika mpaka Ifinga. Sasa kabla ya kutengeneza ile *final finishing* zile kukata ile milima kwa *gradient* fulani kuweka kalvati pamoja na kujengea kingo za maji pembeni, ikawa katapila waliloliazima likajakuchukuliwa na ile imebaki bila kitu tena cha kuendelea.

Kwa hiyo, barabara imesimama na kule kwenye vikao vyetu vya *Road Board* tunapigiana mpira kuwa hii barabara si ya *TANROAD* ni ya *District Engineer* na ukimtazama *District Engineer* hana nafasi yoyote ile hata ya kujenga kilomita moja ya barabara hiyo.

Kwa kuwa ni milima tupu pale na yeye hana pesa ya kufanya kitu chochote. Ukimpa *TANROAD* na yeye anasema bwana uta-*bust budget* yangu. Mimi Bajeti yangu haipo hiyo njia ya Wino kwenda Ifinga.

Kwa hiyo, naishtaki hiyo barabara kwa Mheshimiwa Waziri kule Wizarani ndiyo mwenyewe. Basi yeye ataamua afanyeje ili tupate hiyo njia tuweze kufika huko Ifinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilitaka kutoa hayo machache. Kwa hayo, machache pia naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kuwa Serikali ilitoa tamko rasmi kuhusu bomoa bomoa ya nyumba na majengo mengine yaliyo katika hifadhi za barabara kuwa zoezi hilo litakuwa likifanywa unapowadia wakati wa ujenzi wa barabara za maeneo husika. Naipongeza sana Serikali kwa kuamua na kutamka hivyo. Naishauri Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa tamko hilo uwe wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema uwe wa kudumu kwa sababu kuna hisia kuwa uamuzi huo wa Serikali umekuja wakati huu ambao ni nyeti sana kisiasa, kwa vile Uchaguzi Mkuu unawadia na bomoa bomoa ya ovyo ovyo imewaathiri na kuwaudhi sana wananchi na hata baadhi ya viongozi imewagusa wakiwemo hata Waheshimiwa Wabunge na hata watu tu waliowaonea huruma waguswa hao. Hofu yetu ni kuwa uamuzi huu ni wa kuifagilia CCM kwa angalau kurejesha imani za wananchi kwa Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo ningependa kuishauri *seriously* Serikali ifanye upembuzi yakinifu katika kuandaa Mipango Miji yenye kuzingatia mitandao ya barabara na maeneo ya hifadhi zao ili huko tunakokwenda kadhia hiyo ya bomoa bomoa isizidi au kuendelea kuleta mtafaruku kwa Wananchi hususan katika maeneo ya makazi mapya yanayochipuka nchini. Barabara ya Dar es Salaam – Bagamoyo ni kigezo kizuri cha kufuatwa na kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa kupata nafasi ya kuchangia mbele yako hotuba ya Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, kuhusu Wizara hii nyeti ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu, Wahandisi wote wa Wizarani, vile vile Wahandisi wa *TANROAD* Mikoani na hasa Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wangu wa Rukwa, ndugu James Nyabakari, kwa kazi nzuri anazofanya katika Mkoa wetu.

Awali ya yote napenda kutoa shukrani kubwa kwako Mheshimiwa Waziri juu ya kuweza kutukumbuka kwa barabara ya Kagwila – Karema na kutupatia kiasi cha shilingi milioni 140. Nashukuru sana. Palipo na dogo kubwa linakuja. Si sawa na shilingi milioni 18 katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri kuwa fedha hizo ni ndogo kulingana na mahitaji ya fedha yaliyooombwa na pia hali ya barabara ilivyo. Ombi letu lilikuwa shilingi 767,952,000/=. Kwa muda wote tangu Uhuru wa nchi yetu barabara ilikuwa haipitiki hadi Makao ya Wilaya umbali wa kilometa 110. Hivyo, tunazidi kumwomba Mheshimiwa Waziri kuona umuhimu wa barabara yetu hiyo kwa vile eneo lote la Karema kwanza ni mpakani ambapo majambazi wengi wanatumia usafiri wa Ziwa Tanganyika kwa kuiba na kuvamia mali za watu. Kwa hiyo, njia pekee ya ulinzi na usalama ni barabara hiyo.

Vile vile, eneo hilo lina umuhimu sana wa kilimo cha mpunga, mahindi na uvuvi, kadhalika ni eneo la ufugaji. Kwa yote hayo, kuimarishwa kwa barabara hiyo ni njia kuu ya kuondoa umaskini kwa watu wa Tarafa ya Karema. Pia, kutokana na uvuvi, Wananchi wa Mjini Mpanda watapata lishe bora kutokana na samaki. Vile vile, ni sehemu ya biashara kati yetu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia. Mnamo mwaka 1994 alipotembelea Karema Mzee wetu Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, alitangaza sehemu hiyo iwe soko huria baina yetu na nchi zilizotajwa. Barabara iwe ya kudumu na kwa ajili hiyo gati lijengwe pia ulinzi uimarishwe. Naomba tamko hilo liendelezwe kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, katika Jimbo langu kuna tatizo la barabara iendayo Tarafa ya Mwese. Barabara hiyo ina ubovu mkubwa toka Kibo – Kapanga mpaka Mwese. Katika Bajeti hii 2004/2005 haikupewa fedha licha ya barabara hiyo kuwa ina umuhimu sana kwa zao la kahawa, zao la mpunga na zao la mahindi. Kutoka Kata ya Katuma na Mwese yenyewe pia ni eneo la ufugaji. Zao la ndizi ni kubwa huko Mwese na Katuma. Walaji walioko Mpanda Mjini wanategemea sana zao hilo kutoka Mwese. Kuimarika kwa barabara hiyo kutarahisisha upatikanaji wa chakula Mjini Mpanda na kuwapunguzia umaskini wakulima. Namwomba Mheshimiwa Waziri azidi kutufikiria juu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 108 ili aweze kutupa fungu la matengenezo kutoka mfuko wa dharura ulio chini ya Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumpongeza zaidi Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya kuhusu barabara yetu ya Tunduma – Sumbawanga hadi Kasulu, kwa mwanzo mzuri wa kukamilisha madaraja ambayo yatazinduliwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, ndani ya mwezi huu. Barabara hii ikikamilika ni ushindi kwa Wanarukwa, Nyanda za Juu Kusini na Tanzania kwa ujumla. Itasaidia kuongeza tija ya chakula kwa wakazi wa Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi kwa bei nafuu. Kadhalika itaongeza nguvu za wawekezaji katika kilimo kwa vile ardhi ni yenye rutuba na mvua za uhakika. Pia, tuna maeneo tele yenye madini na hivyo uhakika wa biashara mbalimbali utakuwepo. Hiyo itatia changamoto kwa watu wa Mkoa mzima wa Rukwa na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii pendwa mia kwa mia.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Wizara hii kwa sasa ndiyo kioo cha Serikali cha kujidai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi mimi na Kamati yangu ya Miundombinu tulikwenda kutembelea Kisiwa cha Mafia, mengi tuliyaona, lakini moja naomba nitumie nafasi hii kumweleza Waziri ili alifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia ni kisiwa ambacho kiko nyuma sana kimaendeleo hasa kwa upande wa barabara, hakuna barabara hata moja ambayo ni ya kiwango cha lami au angalau changarawe, barabara zote ni vumbi tupu na udongo. Hali hii ni mbaya na ya kusikitisha sana. Baada ya kupata maelezo tuligundua kwamba kumbe jitihada za Serikali zimepelekwa, lakini hazikuzaa matunda. Fedha zaidi ya milioni 80 zimeyeyuka mikononi mwa wajanja bila hatua yoyote kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mkandarasi mmoja ambaye alichukua fedha ili kutengeneza barabara kutoka Mjini Mafia hadi kwenye Hoteli ya Kitalii. Mkandarasi huyo alivuruga barabara yote kwa kuweka tuta ambalo hakulishindilia hata kidogo. Mvua iliponyesha tuta lilibomoka na ikawa ni afadhali bora ingebaki kama ilivyokuwa. Magari sasa yanapita pembeni mwa barabara kwenye mikoroshu badala ya kupita barabarani. Mkandarasi huyo alichukua fedha zote na kazi haikufika hata robo, kama huu si wizi ni nini? Na ni nani alimpa fedha bila ya kumaliza kazi, kama si rushwa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri ikiwa barabara hii ni ya Mkoa, Wilaya au vyovyote vile viwavyo, ilimradi fedha hizi za Serikali na ubadhilifu unaonekana dhahiri, atume ujumbe wake kwenda kuangalia jinsi juhudi zake vinavyotumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkumbusha Waziri kwamba angefanya juhudi zote kuona maendeleo ya ujenzi wa barabara anafanya bila upendeleo. Mfano, Wabunge wengi wanalalamika kwa barabara ambazo wakati wa masika ni lazima

zijifunge zenyewe. Lakini Waziri ni kigezo gani ametumia kuacha kutengeneza barabara hizo na Wizara yake ikaongeza mabega kwa barabara itokayo Chalinze kwenda Tanga? Barabara hii ni nzuri sana au ni barabara ya kwao nani mpaka akaamua kuongeza mabega badala ya nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zote zimfikie Waziri kwa mpango wake wa kusema kabla ya 2005 barabara kutoka Mwanza hadi Mtwara itakuwa ni ya kiwango cha lami. Jambo hili nilidhani ni dogo, lakini namshukuru Waziri kwa kutupa uwezo wa Kamati yangu ya Miundombinu kuweza kuziona hatua zote za ujenzi. Ni kweli inawezekana kuipata barabara hii kwa muda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikosa uamuzi Wapinzani wakati wa kupiga kura kupitisha Bajeti ya Serikali kwa kusema *abstain*. Maana yetu ni kwamba, katika Bajeti mambo mengine yananuka uvundo na mengine ni mazuri kwa mfano yafanywayo ya Wizara hii, kwa jinsi Wizara hii inavyofanya kazi vizuri bila kushawishiwa. Nashawishika kuunga mkono kwa asilimia moja na namwomba aongeze juhudi Askari huyu wa mwavuli, Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa hii ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Pili, pongezi zangu za dhati pia kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kwa kazi nzuri kabisa anayoifanya na kutoa msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Waziri. Nawapongeza pia Katibu Mkuu, Ndugu Kijazi na wasaidizi wake wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri pia ya kuimarisha miundombinu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha hotuba nimekisoma, lakini kutokana na mahesabu haikuonyesha kabisa Mafia kutengewa pesa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Mkoa ya kutoka Utende hadi Rasi Mkumbi yeye urefu wa kilometa 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi pia kushukuru Wizara (Serikali) kwa kutupatia pesa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mkoa, Wilaya na za Vijiji. Lakini kikubwa tunachokiomba, kwa heshima zote tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupe upendeleo maalum wa kupatiwa vifaa vya ujenzi wa barabara viwepo Mafia kama tulivyoomba katika barua yetu tuliyompelekea pamoja na Mheshimiwa Mama Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe. Naamini ombi letu hili atalipa upendeleo wa kutufanikishia.

Baada ya hayo machache, narudia tena kukuombeeni dua na kheri kweli na mwisho naunga mkono hoja hii mia kwa mia na Mwenyezi Mungu akupeni baraka zote.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai na afya ya kuungana na wenzangu humu Bungeni kuchangia hotuba hii nzuri sana ambayo ni miongoni mwa Wizara yangu kwa Kamati ya Miundombinu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mungu, naomba nichukue fursa hii maalum kabisa ya kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa John Magufuli pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kwa kuiongoza Wizara hii katika ufanisi huu akiwa anasaidiana na Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na wasaidizi wao kwani siku zote moto unazaa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ambazo wengi wa Wabunge wa Bunge hili pamoja na wananchi wema wanaojua maana ya utendaji uliotukuka wanasema wanayoyaona kutokana na ujasiri wa Waziri huyu na wasaidizi wake na hata Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa anatuambia hilo. Kabla sijaenda ndani zaidi, nina wajibu mkubwa wa kuendeleza dua za kumuomba afya njema na kupona haraka Mheshimiwa Rais wetu na *inshallah* uzima huu uje kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ambayo imeandikwa kwa ufundi mkubwa, imeandikwa kwa kujiamini na bila ya hofu yoyote kwani imeelezea ukweli mtupu, unaoonekana usiku na mchana. Yote yameelezwa, maandalizi yake na vipi yanafanywa, vipi yamefanywa, nani amefanikisha na lini yamefanywa, wapi yanafanywa ni jambo ambalo ninalipongeza sana. Huyu Waziri ni muungwana, mwenye maadili mazuri ya CCM ambayo yana tabia au hulka ya ukweli. Mheshimiwa John Magufuli, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maumbile ya Wizara hii hayaonyeshi kuwa si ya Muungano kwani namna ambavyo Waziri huyu ameonyesha mapenzi yake kwa Zanzibar. Nimekuwa nikisema bila ya uficho wala upendeleo kitendo cha kuisaidia Zanzibar kwa kutafuta na kupeleka misaada kule Zanzibar yaani Unguja na Pemba imeonyesha namna ambayo Wizara hii inavyoongozwa na mtu anayeitakia kheri na mema Zanzibar kwa faida ya kuimarisha Muungano. Tunajua wapo wasioupenda wala kuutakia mema Muungano wetu, kwa hakika wanezibwa vidomodomo. Kuisaidia Zanzibar kupata miradi ya ujenzi (Dola za Kimarekani milioni 23.376) ni ushahidi tosha kuwa maendeleo ya Zanzibar ni maendeleo ya Tanzania Bara. Hakika ni kweli kuwa katika miradi ambayo imenipa furaha na faraja ni ule mradi wa ujenzi wa barabara za kati Unguja ambayo inapita Kitope, Kidimni na Machui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia kwako naomba kuleta ombi kwa kirefu, mimi binafsi kama Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge kwa niaba ya wapigakura wa Kitope, naomba kwake Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa ujasiri kabisa na upenzi wake kwa wananchi wa Kilombero – (Shehia), Pageni (Shehia) hadi Upinja

uwasaidie kuwapatia wataalam wako wa barabara waje kututembelea na kuiona barabara yetu ya kilometa 5 Upinja – Kilombero na hatimaye aangalie uwezekano wa kupata mhisani wa kusaidia barabara hii kuweza kupitika vizuri. Mheshimiwa Waziri atapata wasaa wa kuiona hiyo hali na nina uhakika kabisa kuwa kwa tabia yake na wasaidizi wake watakuja na jawabu linalofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na watu wangu wote wa Kitope kwa furaha tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na ninawaomba Wabunge wenzangu wote tumpe pesa akafanye kazi. Shukrani.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa masikitiko makubwa kutoa salaam za rambirambi zangu kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge mwenzetu kwa kifo cha ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii zinazojidhihirisha wazi maana zinaonekana kwa macho. Lakini pia Mheshimiwa Waziri amezeleza kwa kina katika hotuba yake na kwa vielelezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango mizuri ya utekelezaji unaoridhisha, nashauri barabara ya Kyaka – Kayanga – Kasulu nayo ifikiriwe kujengwa kwa kiwango cha lami ili iwe kiungo muhimu kati ya Rwanda, Burundi na Tanzania (Bukoba) kupitia Karagwe, lakini pia kwenye barabara ya *Central Corridor*, bila kusahau kuwa hii ni barabara ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuwapongeza na kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu, Ndugu J. Kijazi na watendaji wote pamoja na Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya na ushirikiano mkubwa walionao katika kuhakikisha kuwa mawasiliano ya barabara yanagawanywa sawasawa mpaka kuwafikia Wananchi wa vijijini na kutatua tatizo la makazi (nyumba) kwa wafanyakazi wetu. Kwa kweli nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuzungumzia barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga. Tunashukuru kwa jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara hii mpaka kukamilisha upembuzi yakinifu kama ilivyopangwa.

Sasa naomba kujua nini kinachofuata kwa mwaka 2004/2005 kwani nimepitia kitabu cha Hotuba ya Bajeti bado sijaona fedha iliyotengwa kwa barabara hii kuonyesha kwamba kazi itaanza mara moja isipokuwa katika ukurasa wa 103 wa kitabu cha hotuba nimeona shilingi milioni 700 tu kwa ajili ya kuendeleza ukarabati uliokuwa unafanywa

wa sehemu korofi. Mheshimiwa Waziri, kama kazi itachelewa kuanza naomba fedha ya ukarabati iongezwe ili kusudi barabara hii iweze kupitika wakati wa mvua mwaka huu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa upande wa usajili wa makandarasi wa nje wanaokuja kufanya kazi nchini. Kumekuwa na makandarasi wanaofanya kazi bila kujisajili kama sheria inavyosema. Ningependekeza kuwa pamoja na mkandarasi kuchukuliwa hatua, Taasisi au Shirika lolote litakaloonekana linaajiri au kuingia mkataba na makandarasi wa aina hiyo nao wawajibishwe mara moja ili kuwapa nafasi Makandarasi wa Kitanzania kuweza kupewa kufanya kazi wanazoweza kwani sheria hii isipofuatwa kikamilifu itaruhusu makandarasi wa aina mbalimbali kuingia na kufanya kazi kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la makandarasi wa barabara wenye uwezo na wenye vifaa vya ujenzi wa barabara ni kubwa sana katika baadhi ya Mkoa kitu ambacho kimechangia sana ucheleweshaji wa kutengeneza barabara zilizopo chini ya Mkoa hata kama pesa zikifika kwa wakati. Je, Wizara ina mpango gani wa kutatua tatizo hili la makandarasi hawa wasiwe sehemu moja tu ya maeneo.

Je, ule mpango wa majaribio ya makandarasi wadogo wadogo wa barabara uliofanywa mwaka 2002/2003 uliishia wapi kama ulivyofanywa Mkoani Mbeya? Kiasi cha pesa kilitolewa na kuwapa kazi ili kuona uwezo wa utendaji wao wa kazi, nafikiri mpango huu ungeendelezwa ungesaidia kuwapata Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi za matengenezo ya barabara kila Mkoa na kufanya kazi ziende haraka na tenda kufanywa kwa haraka kwa sababu uwezo wao unakuwa unafahamika tatizo liwe bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa John Magufuli, Mbunge wa Biharamulo Mashariki na Waziri wa Ujenzi, kwa hotuba yake ambayo imetoa matumaini makubwa ya nchi yetu siyo tu kukimbia bali kuruka kimaendeleo. Nampongeza pia Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kwa kazi kubwa anayofanya. Nawapongeza watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mhandisi Kijazi, kwa kazi nzuri wanayoifaya kusimamia Sekta muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROADS* ina wakala nyingine kama vile ile ya nyumba za Serikali, ameonyesha mfano mzuri wa utendaji Serikalini. Wananchi wa Wilaya ya Rungwe hususan wale wa Rungwe Mashariki wamenituma nieleze yafuatayo:

Kwanza, barabara ya Katumba – Tukuyu ambayo inapita Suma, Mpombo, Isange, Lwangwa, Mbambo mpaka Tukuyu ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya, Mkoa wa mbeya na Tanzania. Inapita eneo kubwa la kilimo cha chai na vyakula mbalimbali na ni barabara ya Mkoa. Wakati wa mvua kubwa hasa mwezi wa tatu na wa nne haipitiki. Kila mwaka inabidi chai imwagwe njiani baada ya kuharibika. Mwaka huu tatizo lilikuwa kubwa. Sikumbuki ni lini ilikarabatiwa ili ipitike vizuri mwaka mzima. Lakini wakati sasa umefika kutafuta fedha ili barabara hii ijenge kwa kiwango cha lami. Wazo

hili linatokana na umuhimu wa barabara hii kiuchumi. Kabla ya hapo basi itengewe fedha za kutosha ili ifanyiwe matengenezo. Wakati mwingine barabara za Wilaya zinapitika kuliko za Mkoa. Labda tungefikiria Halmashauri za Wilaya ziwe na wakala wa *TANROADS* katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna daraja kubwa lililo kwenye Mto Lufilyo, Rungwe Mashariki. Hili daraja linajulikana kama daraja la Tapio. Liliujengwa na Mjerumani baadaye na Mwingereza na hatimaye Serikali Kuu. Ni pana na Mto Lufilyo ni mkubwa. Daraja hili liliharika wakati wa mvua za *El-Nino*. Limesahaulika na kufanya mawasiliano kutokuwepo kati ya Rungwe Mashariki na Kyela na baina ya Kata za Rungwe Mashariki. Hakika daraja kubwa kama hili si la Halmashauri. Nimemwandikia Katibu Mkuu kuhusu hili na naamini litapewa umuhimu unaopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Ndugu Kijazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake. Kama kawaida yake atafanya vizuri sana. Ni matumaini yetu kwamba barabara ya Katumba - Isange - Mbambo, Tukuyu au Katumba - Tukuyu itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, salaam na pongezi kwa hotuba ya Waziri. Ninayo mengi ya kumpongeza, ushahidi ni pongezi nyingi walizozitoa Wabunge wengi kwake na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu nashauri kila jitihada zifanywe ili barabara ya Tunduma – Sumbawanga hadi Ziwa Tanganyika ijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara hii itahakiki uchumi wetu kupitia *TAZARA* kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya *DRC*. Pia, barabara hii ni ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Wizara ya kutolewa mfano kwa kazi nzuri wanayofanya. Naomba sana Mwenyezi Mungu azidi kuwatia nguvu waendeleo kuchapa kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu napenda kuuelekeza katika mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wote wa Wilaya ya Korogwe, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri inayofanyika Mjini Korogwe kwa kuweka lami kipande cha kilometa 1½ toka njia panda ya *Korogwe Girls* hadi *Old*



*Korogwe*. Kipande hicho kilikuwa kero kubwa sana, lakini leo hii Wananchi wote wamefarijika na sasa Mji wa amani wa *Old Korogwe* utafufuka. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo kero sugu ya barabara muhimu sana ya kutoka Korogwe Mjini hadi Magoma, Mashewa, Maramba, Mabokweni – Tanga Mjini. Hii barabara ndiyo uhai wa Jimbo la Korogwe Mashariki na Jimbo la Mkinga hadi Tanga. Pia, ndiyo njia pekee ikitokea tatizo la njia ya Segera inayoweza kufikisha mtu Tanga. Vile vile, ni barabara muhimu kwa ulinzi. Ninaomba barabara hii ipatiwe kipaumbele kwani Kata takriban 10 zinategemea barabara hii kwa usafiri na kusafirisha mazao. Ninaomba sana barabara hii ipewe uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zoezi la bomoa bomoa, lipo tatizo nyeti la kisheria ambalo naomba Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Hifadhi ya Barabara na Sheria ya Ujenzi Mipango Miji, inatokeaje mtu apewe kibali cha kujenga (hati) na Mipango Miji halafu ujenzi wanakuja kuweka X ili nyumba ibomolewe? Mfano Korogwe lipo tatizo hilo kwa nyumba zifuatazo, *Motel Travellers*, *Sabrina Hotel*, Shosi, Magereza na kadhalika. Kwa nini Serikali isikae kwa pamoja suala hili likarekebishwa? Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya kutoka Kweronge – Kizara – Amani – Muheza. Barabara hii ni muhimu kwa utalii *East Usambara*. Tumeomba iwe ya Mkoa, lakini jibu hadi leo bado, hivi ni kwa nini?

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii. Kwa kweli imeandaliwa kwa umahiri mkubwa na yenye lengo la kuimarisha barabara zetu kwa nchi nzima. Mungu awape nguvu, uwezo na mshikamano katika kutekeleza yote waliyoyaandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, kwani amekuwa makini sana katika kuandaa na kufuatilia utekelezaji kwa karibu na kila anapobaini mapungufu hufanyia kazi yeye mwenyewe. Wizara hii imejengea heshima Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia mia moja. Hivyo basi, naiunga mkono asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Meneja wa *TANROADS* na timu nzima ya Ofisi ya *TANROADS* ya Mkoa wa Singida, Ndugu Lyakurwa, kwa kazi nzuri wanayofanya katika ujenzi wa barabara za Mkoa wa Singida kwa Wilaya zote kwa kiwango kinachotakiwa. Sifa hizi nilizitamka pia kwenye kikao cha *RCC* na Wajumbe wote waliniunga mkono. Naiomba Serikali pia imtambue kwa juhudi hizi. Vile vile, nampongeza kwa utoaji tenda, ni mzuri sana unajali uwezo, vifaa na gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nichukue nafasi hii kutoa ushauri na maombi kwa baadhi ya maeneo. Mji wa Singida ndiyo Makao Makuu ya Mkoa, lakini Mji huu hauna hadhi kama Miji mingine iliyoko Makao Makuu kwa Mikoa mingi.

Natambua wazi kuwa ipo chini ya mgao unaotolewa na *TANROADS Board Fund* yaani asilimia 30 kwenda TAMISEMI. Kwa kuwa Mji wa Singida una barabara fupi fupi, tatu tu zenye kiwango cha lami, naiomba Serikali itoe huduma ya pekee ili Mji huu uweze kutengeneza barabara zake kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu Mheshimiwa John Magufuli akilisema hili katika majumuisho yake, wananchi wa Mkoa wa Singida pamoja na wawakilishi watafurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kumpongeza Waziri kwani katika juhudi zake za kuangalia barabara zake Singida, pia amefika hadi Iramba. Huko Iramba aliiiona barabara ya Misigiri hadi Kiomboi na alitoa ahadi ambayo hadi leo haijawa rasmi kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Sasa kupitia Bunge hili Tukufu, ninamwomba ahitimishe kauli yake ili Wananchi wa Iramba wapate faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa nyumba mpya na za kisasa kwa ajili ya watendaji wa Serikali. Kwa kuwa bado chache, ni matumaini yangu *speed* hii bado inaendelea ili Mkoa uweze kujitoshleza kwani wapo watumishi wanaokataa kukaa Singida sababu ya kukosa nyumba. Vile vile, nategemea ujenzi huu utafika na Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya barabara Mkoani Singida inatia moyo sana. Sasa naiomba Serikali kuwahimiza wazabuni wetu wa barabara za Dodoma hadi Manyoni, Manyoni hadi Singida, Singida hadi Shelui na Shelui hadi Nzega ili zimalizike kwa muda muafaka. Kwa ujumla wananchi wa Mkoa wa Singida wanaipongeza sana Serikali ya CCM bila kumsahau Mheshimiwa Benjamin William Mkapu, Rais wa Serikali ya CCM kwa juhudi zake kubwa kwa Serikali hii ambayo imekuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirudie tena kutamka kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja, Bajeti ambayo ilisomwa kwa ufasaha wa hali ya juu na kwa muda mfupi yaani nusu saa, haijapata kutokea. Adumu Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Ahsante sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nitumie fursa hii ili nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Mameneja wa *TANROADS* hususan Ndugu Koroso na Meneja wa *TANROADS* Mkoani Mwanza.

Pili, natoa pongezi kwa Bajeti nzuri na kwa kazi nzuri na umahiri wao wa kazi ambao wanaendelea kuonyesha katika Wizara hii. Kama yapo malalamiko basi yatatokana zaidi na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali yetu na katu si kutokana na

utendaji mbaya wa watendaji katika Wizara. Hii imetokana na Wizara yenyewe kujisafisha na kukemea ubovu kila mara ulipokuwa ukijitokeza na pia kwa kusafisha makandarasi ambao mara kwa mara walikuwa wakiharibu jina zuri la Wizara. Haikuwa kazi rahisi, lakini ujasiri wa Mheshimiwa Waziri umesaidia sana. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa jinsi Wizara kwa kipindi chote cha miaka iliyopita ilivyokuwa ikishughulikia barabara katika Jimbo langu Wilayani Kwimba. Barabara ya Mabuki – Jojiro – Malampaka inakuwa ikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na kuruhusu magari kupita japo kwa kipindi kirefu cha mwaka.

Barabara ya Magu – Ngudu - Jojiro nayo imekuwa ikipangiwa fedha. Japokuwa mwaka 2003 haikupata, nashukuru mwaka 2004 imepangiwa japo kiasi kidogo. Lakini naamini kutayawezesha Makao Makuu ya Wilaya kufikika

Barabara ya Ng'warhaya – Ilongo – Itale, kwa bahati mbaya mwaka huu barabara hii haikutengewa kitu. Ni matumaini yangu kuwa pamoja na kutokutengewa kitu, fursa ikijitokeza nayo itakuwa ikifanyiwa ukarabati wa hapa na pale ili iruhusu Wananchi kusafiri kwa ajili ya kukidhi mahitaji na maendeleo

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa ombi kuwa kwa vile fedha kwa ajili ya barabara ya Mabuki – Jojiro – Malampaka imekuwa ikitolewa kidogo kidogo. Ni vyema fursa itakaporuhusu pesa za kutosha zitolewe na matengenezo makubwa yafanywe ili barabara hii iwe imara kwa muda mrefu zaidi na Serikali kupitia Wizara hii ipumzike na kuweza kushughulikia barabara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Magu – Ngudu – Jojiro, barabara hii ndiyo pekee inayofungua Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba na ulimwengu wa nje. Nashauri barabara hii nayo ifanyiwe matengenezo makubwa na kwa kuzingatia kuwa barabara hii inapitiwa na magari makubwa yanayozidi hata uwezo wa barabara hii, magari yatokayo Shinyanga – Mara (*and vice versa*). Pia nashauri ulinzi wa barabara hiyo ungeimarishwa ikiwezekana mizani iwekwe kwa kuzuia magari makubwa zaidi ya uwezo wa barabara yasiwe yanapitia. Ni kutokana na suala hili ndiyo maana nilishauri Mkoa uchukue barabara itokayo Ngudu kupitia Nyamilama kwenda Hungumalwa, ushauri ambao naona bado haujazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi na kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BALOZI GEORGE C. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hongera sana kwa maelezo mazuri sana kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini zaidi kwa bidii yake na moyo wake na juhudi zake za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wilaya ya Karagwe ifikiriwe kipekee katika mipango ya ujenzi ya baadaye kuanzia 2005/2006. Katika Mkoa wa Kagera, Wilaya inayozalisha mazao ya kilimo na mifugo ni Karagwe. Karagwe ndiyo imeongeza mazao ya kahawa. Karagwe ndiyo inalisha migodi ya Geita na Kahama kwa maharage na ndizi.

Hivyo, iko haja ya kujenga barabara ya lami kutoka Kyaka - Bugane - Nyaishozi mpaka Benako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi na naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ielekeze na kuunganisha Tanzania na nchi za Rwanda, Burundi, Kongo, Zambia na Malawi kwa barabara za lami moja kwa moja na kwa haraka ili Tanzania isiuawe kiuchumi na nchi nyingine (Afrika ya Kusini). Nchi ya Kongo ni mgodi usioondosheka, tujenge barabara za Tabora – Kigoma, Kasanga – Tunduma haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali Mheshimiwa Waziri aunganishe Njombe na Kilombero kwa barabara ya *TANROAD (Regional Road)* kama sisi Wabunge wawili tulivyoomba. Ni eneo dogo tu limebaki.

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru mtoa hoja kwa umakini na uchapakazi wake yeye na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu, Wataalam na Watendaji wa Wizara, nami nimehamasika nichangie machache ndani ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka katika Kitabu cha Nyongeza ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 14, ibara ya 2.2.39 – Miradi ya Ujenzi Zanzibar. Kwa sababu Tanzania ni nchi moja yenye Serikali mbili ile ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Zanzibar, hivyo tatizo la upande mmoja wa Jamhuri litafsirike kwa vitendo kwamba ni tatizo la upande mwingine.

Kwa *spirit* hiyo basi, jitihada ambayo inafanyika ya ukarabati wa baadhi ya barabara muhimu za Zanzibar kama zilivyoainishwa Mkoani hadi Mtuhaliwa, Mtuhaliwa hadi Chake, barabara kuelekea Uwanja wa Ndege Pemba, barabara za Unguja kilometa 30 na ukarabati wa dharura wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri nia hii safi iendelezwe kwani maeneo ambayo yana matatizo ya barabara mbovu ni mengi mno Zanzibar hasa Kisiwani Pemba ingawa maeneo yake ni madogo mno, kwa barabara kuu na zile za vijijini hasa ukizingatia kwamba barabara za vijijini ndiyo uti wa mgongo wa maisha ya wakazi wengi wa huko ambao hutegemea bidhaa za kilimo za chakula na za biashara katika kusafirishia bidhaa zao kwenda sokoni. Mfano mkubwa ni barabara ya Jimbo langu la Mtambwe ambazo hazipitiki kwa muda wa mvua hata zile ndogo. Hivyo, naishauri Wizara kupitia Waziri ashirikiane na Serikali ya Zanzibar kuona tatizo hili liweze kutatuliwa kwa haraka.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri inayozingatia umuhimu wa barabara

kama nyenzo muhimu katika kuzalisha ajira hasa kwa vijana na wanawake na kwa hiyo kulifanya zoezi la kupambana na umaskini kuwa la kutekelezeka.

Kwa niaba ya wananchi wa Urambo, naomba nimshukuru Waziri na Wizara yake kwa kuendelea kuzitengea fedha barabara zetu za Tabora - Ulyanhulu na Urambo- Kaliua - Malagarasi. Kwetu sisi huu ni ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya wananchi wa Urambo naomba kukumbusha ahadi yake ya kutupatia fedha kati ya shilingi milioni 30 hadi 50 kwa utengenezaji wa barabara ya Kaliua - Uyowa ambayo ni sehemu ya barabara inayounganisha Urambo na Kahama. Pia tunaomba barabara ya Tabora - Ulyanhulu, msaada wake usiishie hapo tu. Tunaomba iendelee Tabora - Ulyanhulu - Kashishi - Kahema ili kufungua eneo hili. Ikiachiwa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo peke yake haitoweza kwa sababu kati ya Kashishi na Kahama panahitajika daraja kubwa na pia barabara yenyewe inahitaji fedha nyingi kinyume na fedha kidogo ambazo huwa tunatengewa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye Kikao hiki cha Bajeti kwenye Sekta ya Wizara hii ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

Nampongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu wa Wizara, Watendaji Waku wote wa Wizara yake na Idara zake zote kwa kazi nzuri wanayofanyia nchi hii hususani kwenye ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa barabara zetu.

Shukrani za pekee zinatoka kwa raia wote wa Jimbo la Uchaguzi la Kilombero kwa kuwawezesha baada ya miaka kadhaa kutengeneza barabara ya Mlimba - Utengule, *periodic maintenance* ya barabara ya Kidatu - Ifakara, Ifakara - Mlimba na awali ya yote hivi sasa kuanza kujenga barabara ya Kidatu - Ifakara, kwa kiwango cha lami, changarawe na utengenezaji wa madaraja.

Kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo langu naunga mkono hoja asilimia mia moja na kuombea kila la kheri Wizara ya Fedha iongeze gawio kwenye Wizara hii siku za baadaye. Ni dhahiri kwa mafanikio ya Wizara hii chini ya Mheshimiwa John Mafuguli, Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na watendaji wake wote kwa pamoja na wanazingatia sera ya nchi ya Utawala Bora.

Baada ya kusema haya, ningeomba Wizara yake iendelee kuboresha barabara za Jimbo la Kilombero ili ituunge mkono kwenye jukumu la Jimbo letu la kuinua na kuboresha Sekta ya Kilimo kupitia Vituo vya Kilimo tulivyoanzisha. Ombi langu ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuendeleza matengenezo ya barabara ya lami Kidatu - Ifakara, kutoka kilometa kumi angalau kufikia kilometa 80 (*TANROAD*).

(b) Kuimarisha barabara ya Ifakara - Mlimba kiwango cha changarawe ili ipitike mwaka mzima (*TANROAD*).

(c) Kuendeleza barabara ya Mpanga - Taweta (*TANROAD*).

(d) Kuwezesha kupitia Mfuko wa Barabara ya Mlimba - Uchindile kukarabatia hususani daraja moja na matengenezo kiwango cha udongo au changarawe.

Hivi sasa kuna wawekezaji kutoka nje wakishirikiana na Kanisa Katoliki Jimbo la Iringa ambao wameanza kuhudumia barabara hii. Ni matumaini yangu kuwa iwapo Halmashauri itawezeshwa zaidi pamoja na michango ya wafadhili hawa kero niliyokuwa nikisema Bungeni kila wakati itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Ahsante.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara nchini. Pia naipongeza Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Picha ya Ndege - *TAMCO*, Wilayani Kibaha. Hata hivyo, kuchelewa kuanza kwa Mradi huu kumezua taarifa zisizo sahihi kuwa labda ujenzi wa barabara hiyo hautafanyika.

Nitashukuru kama Mheshimiwa Waziri ataweza kuthibitishia wananchi wa Kibaha na Watanzania kwa jumla kuwa barabara hiyo ya Picha ya Ndege, Tumbi, *TAMCO* itaanza kujengwa hivi karibuni.

Napenda kupongeza pia juhudi za Serikali kupata msaada wa kutengeneza bara ara ya Mkoa ya Chalinze - Magindu inayounganisha Wilaya za Bagamoyo (Jimbo la Chalinze) na Wilaya ya Kibaha. Napenda kupongeza kazi ninayofanywa na *TANROAD* Mkoa wa Pwani katika Wilaya ya Kibaha.

Naomba Wizara ifikirie kuweka lami barabara inayotoka barabara kuu ya Morogoro kwenda Mkoani. Wilaya haina uwezo wa kujenga barabara hiyo ya kilometa tatu kwa kiwango cha lami. Hapo ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na ya uwazi baada ya kuifikiria kwa makini pamoja na nyongeza yake.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunifikiria kwa fedha za barabara ya Mlowo - Kamsamba ya kilometa 129 na ile ya Igamba - Msangano ya kilometa 58. Sina maneno mazito ya kumshukuru zaidi ya kusema ahsante sana, Mungu aibariki kazi yake na wasaidizi wake. Mara kwa mara wachapakazi hawapendwi na wavivu, yeye asijali hilo, achape kazi lakini amtangulize Mungu mbele yake, atashinda.

Mwisho, namtakia kila la kheri Waziri wa Ujenzi katika *presentation* ya hotuba yake na majibu mema kwenye kupitisha vifungu.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Nimeshindwa kukaa kimya, nimeona angalau niandike kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa ujumla chini ya uongozi wa Mheshimiwa John Magufuli, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru sana na kumpongeza sana yeye binafsi na Naibu Waziri wake na timu yake kwa jinsi anavyoendelea kufanya juhudi za kuendeleza kutengeneza barabara za nchi nzima. Mungu ampe nguvu, ujasiri na uzalendo huu alionano aendelee nao ili kutuondoa katika hali tuliyonayo hivi sasa na kutusogeza mbele zaidi. Kwa sababu sio siri Mheshimiwa huyu amekuwa mstari wa mbele kukemea rushwa ambayo ilikuwa imekithiri katika Wizara hiyo hapo nyuma. Fedha zilizokuwa zikitolewa na kupelekwa Mikoani, zisifanye kazi na kurejeshwa tena Makao Makuu kwa ajili ya mgao, hali hii ilikuwepo, lakini sasa inatia imani. Haijawahi kutokea!

Napenda tena kukumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, kwa dhati kabisa, kwa kazi nzuri unayoifanya. *Keep it up!* Mungu akubariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri yuko imara, nasi pia tuko imara naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimtafuta sana ofisini hadi nyumbani lakini nilishindwa kumpata. Nafurahi kumwona yupo na ana afya nzuri. Namtakia kila la kheri.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kufahamu shilingi milioni 108 zilizotengwa kwa barabara ya Ushirombo - Buselesele kama ni pamoja na ujenzi wa Darala la Mto Nyikonga.

Tatizo kubwa hapa ni huu mto ambao unakata mawasiliano ya wananchi wa pande hizi mbili. Tathmini iliyofanywa na Halmashauri ya Wilaya za Geita na Bukombe 2001/2002 ilionesha daraja hilo linahitaji shilingi milioni 120 fedha ambazo hawakuwanazo. Hivyo walishindwa kujenga daraja hilo. Je, mpango huu uliowasilisha utekelezaji utakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba maelekezo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, *mwangaluka imwashi!* Leo *nitakuhilija* na kukupeleka Gambushi ya Bariadi. Mtani, nakutakia kila la kheri. *So nene.*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba nzuri inayojieleza yenyewe kwa pamoja na nyongeza ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nakiri mapema kuwa usimamizi mzuri, uwajibikaji na nidhamu ya kazi ndiyo siri kubwa ya mafanikio katika Wizara ya Ujenzi. Hivyo nawapongeza wafanyakazi wote kwa ushirikiano wanaouonyesha wa kumsaidia Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri anayofanya ya kuliletea Taifa letu heshima katika Sekta ya Miundombinu upande wa barabara, naomba nilete ombi langu ili ikiwezekana kufuatana na uwezo wa Serikali itenge kiasi cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Maligisu. Daraja hilo Mheshimiwa John Magufuli analifahamu kutokana na ahadi iliyotolewa. Pia katika mpango endelevu na Wizara yake aangalie uwezekano wa kuweka lami barabara ya Magu - Bukwimba - Ngudu - Jojiro - Mabuki au Hungumalwa. Barabara hiyo ikiwekewa lami itapunguza msongamano wa magari kupita Mwanza yakitokea Musoma au yakitokea Shinyanga kwenda Musoma.

Lakini Daraja la Mto Simiyu (Maligisu) ni muhimu sana kutokana na ukubwa wa mto, wakati wa masika huleta usumbufu kwa wananchi wanaokaa ng'ambo nyingine. Wakati Serikali ikijiandaa kuiwekea lami barabara ya Magu - Bukwimba - Ngudu - Jojiro na Mwabuki au Hungumalwa ninaomba Serikali iwe na utaratibu wa kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara barabara zake ili kuendelea kubaki imara muda wote kuliko hivi sasa ambapo barabara zinatengenezwa na kuachwa muda mrefu hadi kupelekea kutumia pesa nyingi zinapofanyiwa matengenezo.

Ushauri huu naomba Wizara iuchukue kwa barabara zote kama inavyofanya hivi sasa kwa barabara za lami kama vile Chalinze - Morogoro na kadhalika.

Pia naomba hasa ikizingatiwa kuwa barabara toka Shinyanga - *Mwanza Border* inatengenezwa kwa kiwango cha lami, lakini kuanzia ilipoishia lami hadi ilipoanzia Mwanza hadi barabara hiyo siyo ya kuridhisha, yapo maeneo inaonekana yameshindikana kwani kila wanapotengeneza baada ya siku mbili tatu panafumka.

Hivyo ingekuwa vizuri barabara hiyo inayojulikana kama Mwanza - Ilula kilometa 101 ikatengewa fedha za ukarabati mkubwa siyo kama inavyofanyika hivi sasa, huko ni kupoteza fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Wizara ya Ujenzi imekidhi matarajio ya wengi, naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja. *Aluta Continua!*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote wakiwemo wa *TANROADS* Makao Makuu na *Regional Manager Tanroads*, Singida kwa kazi nzuri sana wanazofanya. Wananchi wa Iramba Mashariki kwa umoja wao wamenituma niwapongeze sana.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na wananchi wangu tunampongeza Waziri na Watendaji wake kwa sababu barabara zetu zote zinatengenezwa kama ifuatavyo:-

Ilongero - Gumanga inatengenezwa na Wachina, Iguguno - Nduguti kazi inaendelea na kwa kweli Kampuni ya Kichina inafanya kazi nzuri sana. Nkungi - Kidarafa - Tenda imeshatangazwa, kwa hiyo kazi itaanza mapema sana. Ulemo - Msingi - Gumanga - Mkalama - Chemchem, tenda imeshatangazwa ikiwa ni pamoja na kukarabati daraja la Mto Ndurumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri la kuomba atutafutie fedha toka Serikalini au kwa wafadhili za kujenga Daraja la Mto Sibiti na pia kutengeneza kilometa 12 upande wa Iramba Mashariki ili kufungua mawasiliano kati ya Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Kagera, Rwanda, Rurundi, Uganda na kadhalika na Mikoa ya Singida (Iramba Mashariki) Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Kenya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu wa kiangazi magari ya aina zote madogo na makubwa yanapitia hapo kwa sababu njia ni nzuri na ya mkato toka pande zote na inapitia kwenye maeneo ya wakulima, wafugaji wachimba madini, wavuvi, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, tumekuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri, sasa asaidie juu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuomba ufadhili wa Daraja la Mto Sibiti na kilometa 12 zinazojaa mafuriko.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, *muli mhola nkoyi!*

Kwanza nakushukuru sana kwa shilingi milioni 100 kwa barabara ya Chambo-Kahama.

Pili, ulikuwa mtaalam kutathmini barabara ya Kahama - Ulowa (ulipopita Kahama mwaka huu), je, nini matokeo mazuri ya barabara hii? Kwani ndio nguzo ya uchumi wa Wilaya (tumbaku, pamba, mahindi, mazao ya misitu).

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi yeye binafsi kwa umakini na umahiri wake katika kuiongoza Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upeo wake pamoja na ari ya dhati ndiyo chimbuko kubwa sana la ufanisi wa Wizara hii ambayo ni mfano wa kuigwa siyo tu hapa nchini bali hata nchi jirani. Pia, napenda niwapongeze kwa dhati pia Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kumsaidia Waziri katika kutekeleza majukumu yake.

Mwisho katika pongezi hii nawapongeza pia Watendaji wote wa Wizara kwa ngazi zote na kwa Taasisi zote pia. Naomba waendeleze jitihada na mshikamano katika kulijenga Taifa letu.

Pili, pamoja na pongezi hizi, napenda tu kutoa changamoto zifuatazo:-

Barabara ya Mkoa ya Lamadi - Mkula - Sapiwi ya Kilometa 16 haikuwekwa katika bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni. Naamini imesahaulika tu kimakosa kwa vile ni moja ya barabara muhimu sana ikiwa kiungo cha barabara itokayo Shinyanga - Maswa - Bariadi hadi Lamadi (Magu) na kuunganisha na Mwanza au Musoma - Nairobi.

Barabara hii haijafanyiwa matengenezo ya kulingana na matumizi yake na hasa ukizingatia huwa barabara ya Bariadi imetengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha tofauti na kwangu na pia barabara hii inapitisha magari makubwa ya mizigo na abiria yenye uzito mpaka tani 50 kinyume na maelekezo ya uzito usio zaidi ya tani 10. Hii imepelekea barabara hii kuharibika sana mara kwa mara na hata madaraja na makalvati yake ku-fail kuhimili uzito.

Nashauri sana Wizara itenge fedha za kutosha kutoka kwenye mfuko wa jumla ili barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha kutosha. Ikumbukwe barabara hii hivi sasa ni mbovu na huwa inajifunga wakati wa masika. Kwa uzito wa hoja hii, natarajia Mheshimiwa Waziri ataipatia uzito stahili kwa manufaa ya wananchi wa Mikoa hii mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara jana ilijibu swali langu Na.154 kuhusu ajali na uharibifu wa barabara ya Nyagunge - Musoma. Licha ya majibu ya Serikali bado natoa wito wa haraka kwa Serikali kuhakikisha kuwa matengenezo yanayofanyika katika barabara hiyo na hasa ya kuziba viraka yanayofanyika kwa kiwango cha kuridhisha kwa kuwa ni fedha nyingi inatumika, lakini kiwango cha ubora wa viraka hivyo ni chini sana kwani hubanduka hata kabla ya kukaa kwa siku mbili. Hivyo kupelekea zoezi zima kuwa kama ni mzaha tu na matumizi mabaya ya fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kandarasi anayepewa kazi hiyo awe na ujuzi na vifaa vya kutosha na kukidhi matakwa ya kazi. Mara kadhaa nimewasilisha maoni yangu ya kutoridhishwa na kiwango hicho kwa Meneja wa Mkoa (*TANROADS*).

Pia ni vyema suala la kuweka vizuizi barabarani (*Road Humps*) na alama za barabarani vikatekelezwa ili kuokoa maisha na mali za watu ambazo zinasababishwa na ajali mbaya za magari. Tafadhali suala hili lichukuliwe kama dharura na sio utani au mzaha. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri wa Ujenzi kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni kazi kubwa zinazofanywa katika maeneo yote yaliyo chini ya majukumu ya Wizara hii.

Kabla sijaendelea mbele, naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego. Ameacha pengo kubwa la uwakilishi kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Mchango wangu nitauielekeza zaidi katika ujenzi wa barabara kwa kuelewa kwamba barabara hususan Vijijini ni moja ya mambo yaliyopewa kipaumbele katika ujenzi wa uchumi na kupunguza umasikini. Ujenzi wa uchumi wa kisasa lazima uambatane na ujenzi wa miundombinu ya kisasa zikiwemo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika ujenzi wa barabara kuu nchini ikiwa ni pamoja na kukamilika na kufunguliwa kwa Daraja la Mkapa - Mto Rufiji ni mambo ya Kujivunia. Lakini mafanikio sawia hayajapatikana kwa barabara Vijijini. Hivyo iko haja kwa Wizara ya Ujenzi kufuatilia kwa karibu changamoto kubwa ya ujenzi wa barabara Vijijini. Nitatoa kielelezo cha changamoto hiyo kwa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilosa ina jumla za barabara zenye urefu wa kilometa 1,415. Barabara za Wilaya zenye urefu wa kilometa 446, barabara za Vijijini zenye urefu wa kilometa 470, barabara za Mkoa zenye urefu wa kilometa 209, barabara kuu zenye urefu wa kilometa 290.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2003/2004 Wilaya ilipatiwa shilingi 148,429,290.70 fedha za mfuko wa barabara. Mchango wa Halmashauri za nguvu za wananchi ulikuwa ni shilingi 8,550,000.00 na zilitumika kuchangia barabara zenye urefu wa kilometa 42.75 tu katika miezi sita ya Januari hadi Juni, 2004 na fedha za Mfuko wa Barabara zilitosheleza kwa matengenezo ya kawaida kama 32.5, matengenezo ya dharura (*spot improvement*) kilometa 44.6 na matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) kilometa 47 tu. Hii inaonesha uwezo mdogo sana wa Wilaya.

Takwimu hizo zinaonyesha jinsi hali ya utengenezaji wa barabara Wilayani Kilosa ilivyo ya kukatisha tamaa. Ukweli wa mambo ni kwamba kuna baadhi ya barabara Vijijini Wilayani Kilosa ambazo kwa miaka nenda miaka rudi hazijaguswa.

Moja ya barabara hizo ni ya Gairo hadi Nongwe yenye urefu wa kilometa 56. Katika Jimbo langu la Uchaguzi la Gairo. Mwaka 2001/2002 na mwaka 2002/2003 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipatiwa msaada wa Serikali ya Uswiss ya takriban shilingi milioni 144 akapewa mkandarasi *Chrome Ltd (Massawe and Co.)* wa Morogoro kutengeneza kiasi cha kilometa 24 za barabara. Mkandarasi huyo hakutengeneza barabara bali aliiharibu barabara hiyo. Wahisani wakaamua kutoendelea kumlipa mkandarasi huyo na kuitaka Halmashauri isitishe mkataba. Matokeo yake *Chrome Ltd* ameifikisha Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa Mahakamani kuidai fidia ya shilingi milioni 100 kwa kuvunja mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kuna uwezekano wowote, Wizara kwa kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi ambayo moja ya majukumu yake ni kuratibu mwenendo wa makandarasi na Bodi ya Usajili ya Wahandisi yenye jukumu la kuratibu mienendo ya shughuli za kihandisi za Wahandisi, itusaidie kuikwamua Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kuwezesha kazi ya kutengeneza barabara ya Gairo hadi Nongwe iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi duni wa mkandarasi *Chrome Ltd* wa Morogoro uko wazi na madai yake kwa Halmashauri yanastahili kubatilishwa tuweze kupata mkandarasi mwingine afanye kazi hiyo kwa kutumia fedha za Wahisani hao hao ambao naambiwa wako tayari kuendelea kuufadhili mradi huo kwa kutumia mkandarasi mwingine. Maendeleo na maisha mazuri ya wananchi wa Tarafa nzima ya Nongwe inategema barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Halmashauri za Wilaya kumudu ujenzi wa barabara bila msaada wa Wahisani na Serikali Kuu ni mdogo sana. Wilaya ya Kilosa tumeathirika sana kutokana na kuvunjika kwa mahusiano mazuri na Serikali ya Ireland iliyotufanyia kazi nzuri ya kututengenezea barabara zetu katika Wilaya ya Kilosa. Sasa Wilaya haina Mhisani mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi katika ujenzi na matengenezo ya barabara ndio utakuwa ukombozi wa kuimarisha na kuendeleza ujenzi wa barabara Vijijini. Hivyo naiunga mkono kwa dhati Wizara ya Ujenzi kwa azima yake ya kutoa umuhimu wa matumizi ya teknolojia hii kwa kushirikiana na TAMISEMI. Halmashauri za Wilaya zipatiwe mwongozo unaokusudiwa mapema iwezekanavyo.

Vile vile iko haja ya kujenga utamaduni wa utunzaji barabara. Utamaduni huu haujajengeka vya kutosha. Barabara mpya huachwa ibomoke na kuharibika yote kisha tunarudi kwa Wahisani kuwaomba watujengee upya, hiyo ni aibu. Lazima tuchukue juhudi za kuwahamasisha wananchi ili wakati wote wawe tayari kuzitunza barabara zao na kuzifanyia matengenezo madogo madogo kule zinapoharibika badala ya kuziacha ziharibike kabisa na kujengwa upya. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa rambirambi kwa familia ya wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kifo cha ghafla cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama kwa kufiwa na mwanawe. Naomba Mwenyezi Mungu awape nguvu za kuhimili msiba huu mkubwa.

Pia, nawapongeza Mheshimiwa Waziri John Magufuli na Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye maelezo ya kina na kwamba kila kitu kiko wazi. Hata hivyo kuna maeneo machache ambayo nitayazungumzia. Ukurasa wa 25 wa hotuba umeleza suala la upungufu wa mitambo unaosababisha makandarasi wazalendo kutomudu vizuri utekelezaji wa kazi za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wakati umefika sasa Serikali iweke taratibu za upendeleo wa makusudi ili kuwawezesha wataalam hawa kupata mitambo hiyo ndiyo maana ni muhimu kwa Benki zetu kutoa mikopo na kadhalika. Nimefurahishwa na mpango wa kutoa elimu kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari kuhusu usalama wa barabarani. Lakini nashauri kuwa tathmini isichukue muda mrefu kwa Shule chache, mitaala iandaliwe na somo, hatimaye lifundishwe katika Shule zote nchini kwani ajali nyingine zinatokana na wananchi kutofahamu matumizi salama ya barabara achilia mbali uzembe wa madreva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 imeelezwa kwamba moja ya malengo ya Idara ya Ufundi na Umeme kwa mwaka 2004/2005 ni kubadili mfumo wa uendeshaji vivuko kutoka uvutaji wa kamba unaofanywa na watu kwenda kwenye matumizi ya winch katika Kituo cha Mto Ruhuhu. Hii ni hatua nzuri sana ya kupongezwa kwa vile kweli ni hali ya kusikitisha kuona jinsi nguvu kazi kuwa inayotumika katika shughuli hii katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Hata hivyo Serikali ina mpango gani *either* wa kufanya marekebisho haya katika kivuko cha Mto Malagarasi huko Kigoma ambacho kiko katika Kijiji cha Ilagala? Au napenda kufahamu ni lini Serikali itanunua kivuko katika mto huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa kwenye ziara mwezi Mei, 2004 uongozi wa Mkoa uliona ni vyema kwenda kunionesha hali halisi ilivyo na ndipo nilipoona hali hiyo. Hivyo naomba kwa dhati kabisa kupata majibu ya kueleweka.

Katika ukursa wa 67 wa hotuba inafafanua kuwa Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiraji Majengo imekamilisha matayarisho ya Rasimu ya Sheria ya Taifa ya Majengo na kuwakilisha mapendekezo yake kwenye vyombo vya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iharakishe kukamilisha taratibu za rasimu hiyo kuwa sheria kwa vile nina matumaini makubwa kuwa sasa mazingira ya majengo mbalimbali hapa nchini yatazingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu, wazee na kadhalika (*accessibility*) jambo ambalo linalalamikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 91 katika jedwali hili imeonyeshwa kuwa ukusanyaji wa vifaa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Mogorogoro - Dodoma ungekamilika Juni, 2004 lakini hali halisi ni kwamba hatua hiyo bado haijafanyika au hiyo ndiyo ile hali ya wapimaji wachache kuanza upimaji? Yafaa sababu za ucheleweshwaji huo zifafanuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa mipango ya Wizara ya kuendeleza barabara kwa kuunganisha barabara hizo kikanda ili kufungua maeneo mbalimbali ya nchi yetu kiuchumi, kijamii na kadhalika. Kwa mfano ufufuaji wa barabara ya Iringa - Dodoma - Babati ikiwa ni sehemu ya *The Great North Road* uwekaji lami barabara ya Masasi - Songea, *Mbambabay*, utarahisisha usafiri wa usafirishaji wa abiria na bidhaa mbalimbali na kuendeleza Miji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Kamati kuwa ujenzi wa nyumba za Serikali usiwe katika mtindo wa Vijiji au Kambi, kwa sababu hali ya namna hiyo italeta sura ya *squatters* kwa nyumba kubanana bila kuacha eneo la kutosha kwa kupanda maua na kupendezesha mandhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi kwa asilimia mia moja.

Awali ya yote nashukuru mno kwa Wizara kujenga barabara ya Mkoa wa Mtwara - Pachani hadi Likusenguse. Maelezo ya ukurasa wa 117 ni ukombozi mkuu kwa wananchi wanaoishi eneo hili la mbali la Kijiji cha Likusenguse ambao tangu Uhuru mwaka 1961 barabara hii haijajengwa, imekuwa ikiliwa na mvua za masika. Shukurani nyingi sana kwa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraja ya barabara hii nayo yatajengwa? Nilipoleta ombi langu hili nilijumuisha pia madaraja yake matatu, yaani daraja la Msanjesi I, daraja la Ngaheghela na daraja la Msanjesi II.

Aidha, Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Songea ina mpango wa kutoboa barabara ya urefu wa kilometa 120 kwa lengo la kuziunganisha barabara za Mikoa ya Morogoro yaani Ifakara - Lupilo - Kilosa kwa Mpepo hadi Mto Londo na Wilaya ya Songea yaani Songea - Kitanda hadi Mto Londo. Songea - Kitanda ni barabara ya Mkoa pia Lupilo - Kilosa kwa Mpepo nayo ni barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kuunganisha barabara hizi za Lupilo - Kilosa kwa Mpepo (Morogoro) na pili, Songea - Kitanda (Ruvuma) ni kuwa barabara hizi zitanufaisha wakazi wa Songea na Ulanga kwa kufupisha usafiri kati ya Mikumi na Songea bila kupitia Iringa na Njombe, kurahisisha usafiri wa watalii watokeao *Mikumi National Park* kuja kutembelea *Selous Game Reserve* bila ya kupitia kwanza Iringa, Njombe na Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuchangamsha kilimo cha mpunga katika mabonde ya Mito ya Kitanda, Londo na kuyafikisha mazao hayo Dar es Salaam bila ya kuyazungusha nyuma kwanza hadi Songea. Narudia tena kutamka kuwa naiunga mkono hoja ya Waziri mia kwa mia.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii na mimi kuichangia hotuba hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Hotuba ni nzuri sana na ninaipongeza na kuiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na watendaji wahusika wa Wizara hii ameonsha uwezo wake mkubwa wa kiutendaji, kiusimamizi na kiufahamu kwa kiwango cha juu sana kitu ambacho hujui uanzie wapi na aseme lipi. Jambo linalobakia linakulazimu kumuunga mkono na kumwomba dua kwa

Mwenyezi Mungu ambariki zaidi katika majukumu haya makubwa ya nchi yetu hii kubwa ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa pili unaoelezea dira ya Wizara, inasema kuwa: “Dira ya Wizara ya Ujenzi ni kuendeleza Sekta ya Ujenzi ili iwe endelevu yenye ufanisi na inayotoa huduma bora na nafuu katika mazingira ya ushindani ili kuchochea na kuleta ufanisi katika maendeleo ya jamii na kiuchumi na hivyo kuchangia kikamilifu uchumi wa nchi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya ya Dira ya Wizara ni ushahidi wa kutosha unaothibitisha uwezo mkubwa wa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawatakia mafanikio katika majukumu haya makubwa ya Taifa na ya Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niligusie ni suala la rushwa ambalo liko katika ukurasa wa 79. Ninanukuu; “Vita Dhidi ya Rushwa. Mikakati ya kupiga vita rushwa katika Sekta ya Ujenzi ambayo Wizara yangu inaendelea kuitekeleza ni pamoja na kuendelea kutekeleza kikamilifu sheria Na.3 ya mwaka 2001 (*Public Procurment Act No.3*) ambayo inapunguza sana mianya ya rushwa katika utoaji zabuni za ujenzi, ushauri na ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wenzake pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kuiona sheria hii umuhimu wake na kuisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri aliyofanya na anayoendelea kuifanya Mheshimiwa Waziri inahitaji kuwa na kitu muhimu na kizuri ambacho kinaweza kulinda heshima yake na utu wake na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imeshasababisha Waziri na Katibu Mkuu waliopoita kufikishwa Mahakamani na Katibu Mkuu kufungwa jela. Kwa hiyo, nawaombea dua kwa Mungu Mheshimiwa Waziri na wenzake awanusuru na balaa la aina hiyo, kashfa, maradhi na uadui na awape maisha mazuri ya amani na salama na waendeleo kusimamia majukumu hayo makubwa waliyopewa kwa faida na maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha nyongeza ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ukurasa wa 14 ninanukuu 2.2.39 inaelezea miradi ya ujenzi Zanzibar (US\$ 23.376 milioni). Miradi ya ujenzi inayoendelea kwa upande wa Zanzibar ni kama ifuatavyo:-

- Ukarabati wa barabara ya Mkoani hadi Mtuhaliwa yenye urefu wa kilometa 5.5.

- Ukarabati wa barabara ya Mtuhaliwa hadi Chake yenye urefu wa kilometa 23.

- Barabara ya kiungo kuelekea uwanja wa ndege wa Pemba yenye kilometa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge kutoka Pemba, ninakiri kuwa ni kweli barabara hizi zipo Pemba na pia haya yaliyoelezwa ni kweli kuwa barabara hizi zinajengwa. Naipongeza sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa barabara hizi za Pemba.

Mwisho, narudia kumwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kunijengea barabara zangu za Vitongoji zenye urefu kilometa 24. Barabara ya Vitongoji - Vikutani/Uwandani/Ole Kianga, Mzambaru Mboko/Wawi Matreta/*Vikunguni Road* na Uwanja wa Mpira Gombani/ Ng'ambwa/ Ole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hongera nyingi zinazotolewa kwa Wizara hii ya Ujenzi, maswali mengi yamefutwa. Hongera! Hii inatokana na uongozi makini wa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wetu wote Wizarani. Hongera sana.

Katika barabara za Mkoa wa Morogoro, kuna baadhi ya barabara Jimboni ni mbaya sana kama vile Mdaula - Kidugallo, Ubena - Ngerengere - Kiganila, Ngerengere - Kidunda, Kwaba - Usungura.

Madaraja ya Ubena, ukiunga na Ruvu, Mbegowasimba - Ngerengere, Madamu - Tegetero, Msomvizi - Lubungo, Kwaba - Usungura - Kisalawe, Chalinze - Magindu - Selegete B. Daraja la Mto Ruvu kwenda Mvuha. Hizi barabara ni muhimu sana. Naomba kipindi hiki zipatiwe fedha. Naunga mkono hoja.

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kujenga barabara kwa viwango vyote.

Katika ukurasa wa 14 wa nyongeza, naipongeza Serikali ya Muungano kwa kusaidia ujenzi wa barabara za Pemba na Unguja kwa mikopo ya *OPEC*, Benki ya Dunia na kadhalika.

Je, nani atalipa deni hilo? Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua barabara za kati Unguja ni zipi? Zina urefu gani? Pia zina gharama kiasi gani? Naunga mkono hoja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pole nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na pole nyingi kwa familia ya Mheshimiwa Yete Mwalyego aliyefariki mwezi Juni. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*



Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza Wizara ya Ujenzi, Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti Wizara hii imefanya kazi kubwa na nzuri katika nchi hii. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kilolo ningeshauri Wabunge wote waiunge mkono hoja hii haraka ili tuwaache wataalam waendeleo kuchapa kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba nitoe ushauri katika sehemu kuu tatu:-

Kwanza, Wizara hii isimamie na kuwa makini katika utoaji wa *tender* za barabara ili kupata wakandarasi wenye uwezo na kutekeleza kikamilifu sheria Na.3 ya mwaka 2001 (*Public Procurement Act No.3*) hii itatusaidia sana kupunguza mianya ya rushwa.

Pili, kwa kuwa *TANROAD* imefanya vizuri katika Sekta hii na kwa kuwa Halmashauri nyingi za Wilaya zinashindwa kusimamia vizuri ujenzi wa barabara, nawaomba sana watoe mafunzo zaidi ya kuwapa uwezo zaidi ili nao pia wafanye kazi hii vizuri kwani bila barabara maendeleo hakuna.

Tatu, napenda kutoa pongezi katika udhibiti mzuri wa rushwa kwenye Vituo vya Mizani, ningepomba muendeleo na uzi huo huo. Pia wafanyakazi wasikae muda mrefu katika kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nitoe shukrani nyingi kwa ujenzi mzuri wa barabara ya Dar es Salaam - Zambia sehemu ya Iringa Kitonga barabara imejengwa kwa utaalamu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba kwa kuwa aina ya ujenzi uliojengwa pale ni tofauti ni *Cement* tupu, hivyo ni vyema utaalamu huo uendelezwe katika sehemu nyingi za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi na kwa kuwa nchi hii inategemea kilimo, ni vyema Wizara hii akashirikiana na Wizara ya kilimo ili kujua baadhi ya Wilaya zinazozalisha chakula vizuri, ziweze kuimarisha barabarara ili tusiendeleo kutia aibu ya kuomba chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano barabara ya Iringa - Dabaga - Idete, hii ni barabara ya Mkoa na ipo chini ya *TANROAD*. Ningepomba tupate nyongeza kidogo yaani Idete - Itonga - Muhanga. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi na kilimo kwani ikitengenezwa itaungana na reli ya Tazara sehemu ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hii tulileta kwako ombi la kuipasisha barabara yetu mpya ya Mkoa ambayo tayari Wizara yako imeshafunga utafiti na vipimo kwako ambayo inaanzia Ilula - Mlafu - Watalisoli - Mkalanga - Ipalamwa - Kisinga -

Lulanzi - Kilolo. Barabara hii kwa kiasi kikubwa kazi imeshafanyika kwa msaada wa *TANAPA* imetoka Ilula na kuishia Watalisoli. Hivyo kilometa zilizobaki ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuwa alitoa ahadi ya kutembelea barabara yetu ya Iringa - Idete, wananchi wanampenda na wanategemea Waziri atatimiza ahadi hiyo ya kutembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa pongezi nyingi kwa Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu Bwana Kijazi na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi yao nzuri ya kuboresha sekta ya ujenzi nchini. Yapo mafanikio dhahiri ya mtandao wa barabara kila pembe ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Wizara na *TANROADS* kwa kutoa fedha ambazo zimetumika katika kutengeneza baadhi ya barabara na baadhi ya madaraja ya kudumu ndani ya Wilaya yetu ya Ileje. Ili Wilaya yetu ambayo iko pembezoni, iweze kufikika wakati wote, tunaomba barabara za Mkoa zinazotunganisha na Wilaya jirani za Mbozi, Mbeya Vijijini, Rungwe na Kyela ziendeleo kufanyiwa matengenezo ya *TANROADS* ipasavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maombi maalum mawili. Kwanza naishukuru sana Wizara kwa kutenga fedha za matengenezo kwa barabara ya Mpemba - Isoko kilometa 102. Barabara hii ndiyo uti wa mgongo wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Wilaya yetu. Tunashukuru kwa tengeo la shilingi milioni 100. Tunaomba huu uwe mwanzo wa kuelekea hatua ya kuipandisha hadhi barabara hii kuwa ya kiwango cha lami, kupitia Itumba makao makuu ya Wilaya. Wilaya nzima haina hata mita moja ya lami. Wizara ingeweza kufikiria kwanza na barabara za makao makuu ya Wilaya pale Itumba.

Pili, miaka michache iliyopita, tulishirikiana na Wizara pamoja na wenzetu wa Malawi kujenga daraja pale Isongole. Daraja hilo linahitaji kuimarishwa ili liweze kuhimili uzito wa magari makubwa yanayovuka kutoka na kwenda kwenye nchi zetu mbili. Kwa mipango ya baadaye, tunaomba eneo hili la daraja liendelezwe kama ilivyo kwa eneo la Kasumulu kule Kyela mpakani na Malawi.

Mwisho napenda kuangalia kwamba Wilaya yetu iko pembezoni na mpakani na Malawi. Ni Wilaya changa ambayo uchumi wake bado ni duni, inahitaji kusaidiwa kwa mipango maalum ya barabara na madaraja. Nawataki mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yenu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii. Pamoja na kazi nzuri ya Wizara hii, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatenga fedha nyingi kwa ajili ya *feeder roads* ambazo zinajengwa kwa udongo. Kazi inayofanyika haionekani kwa sababu mvua ikinyesha ndogo wote hutoka. Hali hii inafanya barabara za Vijijini kubaki katika hali mbaya kwa muda wote nashauri *feeder roads* muhimu kama zile za Ngongo - Mandawa, Nanganga - Mandawa na Nachingwea - Liwale - Nangulukulu, zijengwe kwa kiwango cha lami ili tuhakikishe kuwa tuna barabara za uhakika na za kudumu. Ni heri kujenga eneo dogo kwa awamu badala ya kutaka kuhudumia eneo kubwa kwa kazi inayotakiwa kurudiwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mtwara - Mingoyo - Masasi - Songea - *Mbamba Bay* imefanyiwa upembuzi yakinifu, naipongeza Serikali. Lakini eneo la kutoka Nyangao hadi Masasi barabara inapita kwenye eneo ambalo ni la mafanikio. Ujenzi wa barabara katika bonde hili utakuwa aghali sana. Nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kutumia tuta la zamani la reli toka pale Nyangao hadi Masasi. Barabara ikipita kwenye tuta itakuwa imara na itaepa kabisa mafuriko. Mipango yetu izingatie kuwa nchi yetu ni maskini na uwezo wa kiuchumi ni mdogo.

Barabara ya Kilwa ni mpango utakaosaidia kupungua eneo la kuelekea Kusini. Lakini wananchi wamebomolewa majumba na hakuna dalili ya shughuli yeyote kuanza. Nashauri Serikali ianze angalau kazi ionekane ili wananchi wasione kuwa wameonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza uamuzi wa Serikali kwa kubomoa nyumba kwenye *road reserve*, pale tu ujenzi utakapokuwa tayari kuanza. Pamoja na pongezi, nashauri kiongozi wa maeneo yatakayobomolewa wajulishwe mapema ili kuwaandaa wananchi kabla ya kuwekewa alama ya X na kuanza bomoabomoa. Alama za eneo la za barabara ziwekwe wazi ili wanaokiuka watambuliwe haraka. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwa maandishi kwa lengo la kuunga mkono na kushauri maeneo machache lakini muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, ikiongozwa na Mheshimiwa John Magufuli, imekuwa ikifanya kazi nzuri. Barabara kuu na zile zinazounganisha Mkoa na Mkoa na nchi na nchi zimejengwa na zinatiletea nchi heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwamba kwa kuwa kazi kubwa ya barabara kuu kuwekwa lami sasa kunapunguza urefu wa barabara za vumbi zilizokuwa zinahudumiwa na *TANROAD*, nashauri zile zilizobaki chini ya *TANROAD*, mfano ile ya kutoka Muhutwe - Kamachumu - Nshamba - Muleba iangaliwe kwa karibu. Barabara hii sasa hivi ina mashimo mengi sana haina mtaa wa kupitisha maji kwani eneo hili ni lenye mvua nyingi. Barabara pia haina *road reserve* wala haifyekwi kando kando. Barabara haina mabega hivyo kusababisha kuonekana nyembamba na kusababisha usufumbufu kwa waenda kwa miguu na wapanda baiskeli. Nashauri barabara hii na nyingine za aina hii nchini kote sasa zikarabatiwe mara kwa mara. Ikiwezekana ziwekwe katika orodha ya kuwekewa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalotokana na hilo pia ni la ushauri. Kwa kuwa *TANROAD* sasa inazidi kuwa na barabara chache basi Serikali ione uwezekano wa kuongeza fedha katika matengenezo ya barabara za Halmashauri na upasuaji wa barabara mpya ili kuongeza mawasiliano ya watu ambao ni raslimali ya maendeleo ya uchumi wetu. Ikizingatiwa kwamba asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania wanakaa vijijini (*Rural Areas*) wakiboreshewa njia za mawasiliano itaharakisha *modernisation* na hivyo kuboresha kilimo, elimu, afya, ulinzi na usalama na mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara sasa baada ya kufanikisha kazi kubwa ya barabara nchini, liwepo fungu la ukarabati wa barabara zote za lami, badala ya kusubiri ziharibike kwanza. Matengenezo ya haraka yawe ni kazi ya kila siku. Tabia ya kuchimba mashimo barabarani ama kupitisha mabomba ya maji au kwa kutaka kuyaziba isiachwe kuendelea. Shimo linapobaki wazi muda mrefu linazidisha ubovu wa barabara na kusababisha usumbufu kwa watumia barabara, mfano ni eneo la *Bahi Road* hapa Dodoma - karibu na makaburi mkajionee leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nashauri Serikali iangalie upya na itafakari suala zima la ukarabati wa barabara. Badala ya kusubiri kutoa *tender* wakati barabara imekwishaharibika, Serikali ifikirie kuwekeana mkataba wa walau miaka miwili (miezi 24) na irekebishwe mara kwa mara, jinsi itakavyoonekana inafaa. Ushauri huu unazingatia ukweli kwamba yule msaini mkataba atawasilisha makadirio ya matengenezo ukarabati kwenye mamlaka inayohusika kwa lengo kwamba ataikarabati barabara ile kwa kipindi chote alichokubaliwa. Hataruhusiwa kuiacha barabara iwe mbovu hata mara moja. Serikali itakuwa ikikagua tu barabara kuona kazi inayotekelezwa. Nina amini ikieleweka na kufikiriwa ipasavyo inaweza kuondoa tatizo tunaloliona barabarani la kubaki mashimo muda mrefu huku Serikali ikisubiri kuomba pesa na kuteua mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nawapongeza watendaji wa Wizara husika.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa natoa hongera kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi. Nimesoma nyaraka ulizotupatia, mbona sikuona kiasi cha fedha kilichotengwa kutengeneza au kukarabati barabara ya Mkoa inayoanzia Omurushaka - Nkwenda - Kaisho Rwabununka - hadi Murongo kwa mwaka huu? Au kuna mahali inaonyesha kwenye hotuba yako?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kufiwa na Mwakilishi wao Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mungu alitoa na Mungu ametwaa neno lake litimizwe. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali kuamua kutenga fedha za ndani ili zijenge barabara zetu, naipongeze sana Serikali kwa uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na timu yake wamekuwa wakombozi kwa barabara ya Dodoma - Mwanza, wananchi wa mikoja inapopita barabara hii wamefurahi sana pamoja na fedha za wafadhili zimetumika lakini usimamizi mzuri wake Waziri ukombozi huu wananchi hatutamsahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameonyesha uwezo wa kuimudu Wizara kwa kuona kazi za matengenezo ya barabara, unaonekana hakuna ubabaishaji. Watanzania watakombolewa kama mawasiliano ya barabara utaboreshwa wataendesha biashara zao za uhakika, unafuu wa gharama za mabasi zitapungua, samaki mbichi zitasafirishwa toka Mwanza hadi Dar es Salaam bila kuharibika. Hongera sana Waziri.

Naomba Makandarasi waliojenga barabara ya kutoka Butimba hadi Ilula katika Jimbo la Kwimba wachukuliwe hatua maana wamelipwa kwa kazi mbaya, barabara hiyo iliwekwa mchanga mtupu sasa hivi ina mashimo sana. Hafai kabisa asipewe kazi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru *TANROAD* wameanza kuziba, lakini hata hivyo nao hawatengenezi vizuri. Nazidi kuipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri inayoonekana wazi hapa hatuna mabishano katika ukweli Mungu awape nguvu zaidi ili mkamilishe ujenzi wa barabara Dodoma hadi Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia na wapewe fedha zote na waongezewe zingine.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mimi nilisoma ripoti ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, naomba sasa nichangie kama Mbunge wa Tabora Mjini.

Nampongeza Waziri, wasaidizi wake kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kushughulikia mtandao wa barabara nchini. Nampongeza pia kwa kusikia kilio cha wana Tabora kupitia kwa Wabunge wake, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo na Mheshimiwa Dr. James Msekela kuhusu suala la bomoa bomoa. Naomba sasa elimu kwa wananchi kuhusu suala hili iendelee kutolewa. Lakini vile vile wahusika wahakikishe kuwa wananchi hawaendelei kujenga katika hifadhi za barabara na watakaoshindwa kusimamia zoezi hili wawajibishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Tabora tuko katika harakati za kuufungua Mkoa wetu na tunaomba Serikali iunge mkono juhudi zetu kwa kutenga fedha za kutosha ili barabara zifuatazo zijengwe kwa kiwango cha lami.

- (a) Manyoni - Itigi - Kigura - Tabora - Urambo - Kigoma.
- (b) Nzega - Tabora - Sikonge - Rungwa - Mbeya.
- (c) Tabora - Ibiri- Ulyankulu - Ushetu - Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi chache zilizofanywa katika kutengeneza barabara ya Tabora - Kigwe - Itigi, hivi sasa kila siku kuna mabasi yanayotoka Tabora kwenda Dar es Salaam na Dar es Salaam kwenda Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ya kuwaondolea kero wananchi wa Mkoa wa Tabora. Wana Tabora wanatumaini kuwa punde si punde barabara hii itakuwa ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wizara inapojenga nyumba za wafanyakazi wa Serikali izingatie ushauri wa kamati yangu hususan kujenga uzio wa nyumba ili kuwe na usalama wa wakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa maamuzi ya kutengeneza barabara zetu kwa kiwango cha kuwezesha kupitika kwa muda wote na hivyo kuiunganisha Mikoa na Wilaya. Nimepata fursa ya kutembelea maeneo ya mipaka yetu karibu yote inafurahisha kuwa karibu barabara zote kuu zinazounganisha na nchi jirani zimejengwa kwa kiwango cha lami, hususan Tanga - Mombasa - Mbeya - Zambia, Mara - Sirari - Kenya, Arusha - Namanga - Kenya hususan Tanga - Mombasa - Mbeya, Zambia, Mara - Sirani - Kenya, Arusha Namanga - Kenya, Bukoba - Mutukula - Uganda - Biharamulo Rusumo - Rwanda, Ngara - Bujumbura. Nashauri sehemu zilizobaki zipewe vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada na dhamira yake ya kujenga barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay* kwa kiwango cha lami. Lakini ni dhahiri kuwa kazi hiyo ni ya muda mrefu. Natoa ombi maalum kuhusu umuhimu wa barabara ya Songea - Mbinga kupewa kipaumbele ili barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa umuhimu wa eneo hili kiuchumi. Pamoja na kazi ya ujenzi wa madaraja yote ambayo yamekamilika. Ujenzi wa barabara hiyo utaongeza mapato ya eneo hilo pamoja na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kahawa ya Mbinga ambayo ni asilimia 20 ya kahawa yote ya Tanzania inazalishwa katika eneo hili na kukobolewa kiwandani Mbinga. Ubora wa zao hili unaathiriwa sana barabara ya vumbi yenye urefu wa kilometa 76 kutoka, Likuyufusi hadi Mbinga. Naomba sana Wizara itizame upya vipaumbele vyake na ikibidi mkopo au fedha za ndani zielekezwe katika ujenzi wa barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay* kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kushukuru tena kwa hatua za Serikali kujenga barabara ya lami kilometa 4 Mijini Mbinga, hali hii itakuwa imebadiri kwa

kiwango kikubwa sura ya Mji wa Mbinga. Kadhalika nimefurahishwa na kazi nzuri ya iliyofanyika katika kupanua barabara za Nyoni- Mkoha hasa kwenye mlima Mawono, ambao umekuwa ni kikwazo kikubwa cha usafiri wa Bonde la Hagati ambalo ni eneo linalozalisha zaidi ya nusu ya kahawa inayozalishwa Wilayani Mbinga. Naunga mkono hoja hii na kuihakikishia Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wake kuwa nitashirikiana nao kwa kila hali.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Natoa pongezi kwa Wizara hii kwa kupitia *TANROADS*, Iringa kwa kushughulikia barabara sugu ambayo ilitelezwa kwa miaka mingi Ludewa - Manda (*Kandamija Road*) sasa inatengenezwa. Naunga mkono hoja hii, hata hivyo naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Kwanza juu ya barabara ya Mkoa ya Mkiwu - Madaba katika eneo la Mundindi - Maranga kwenye mlima wa Ganga la Nzuki haliwezi kupitisha magari yenye uzito unaozidi gari la tani tano na kuwa sehemu hiyo pametokea shimo kubwa linalotishia kufunga barabara hiyo na kuwa shimo hilo halizibiki sasa nashauri Serikali ikubali barabara hiyo ichepushwe kama wananchi wa Ludewa walivyoomba tangu mwaka 2001 kwa kupitia Wabunge wao.

Pili, naitaka Serikali kuheshimu ahadi ya Rais aliyotoa Ludewa aliyotembelea mwaka 1996 kuwa barabara ya Lusala - Makete ipewe hadhi ya barabara ya Mkoa suala hili liliulizwa Bungeni na Wizara iliahidi kufanya uchunguzi wa ahadi hiyo. Mwisho nawapongeza kwa kazi nzuri.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka uliopita wa 2003/2004. Aidha, napenda kuunga mkono hoja hii ingawa ninayo machache yafuatayo:-

Kwanza, miradi ya barabara iliyopo kwenye maandalizi. Miradi kadhaa ambayo iko kwenye maandalizi na ambayo itatekelezwa katika mwaka huu 2004/2005. Kwa mfano upembuzi yakinifu wa barabara ya Sumbawanga - Kigoma - Nyakamazi, utafanyika mwaka huu lakini haukutengewa fedha. Aidha barabara ya Tabora - Kaliwa - Malagarasi - Uvinza - Kigoma imefungiwa kufanyiwa usanifu na uandaaji wa tenda katika mwaka 2004/2005. Lakini kwa kiasi gani bajeti ya Wizara hii haionyeshi.

Vile vile barabara ya Mwandiga hadi Manyovu, itajengwa kwa kiwango cha lami (*otta seal*) lakini Bajeti haisemi vile viwango vya matumizi havikuonyeshwa Serikali itatumia fedha ipi kuendeleza miradi hii au ni kiini macho tu?

Pili, barabara za kufadhiliwa na *NEPAD* au Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nashauri Serikali kuendelea kutenga fedha yake yenyewe kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara mbalimbali hapa nchini bila kuweka mategemeo yake kwenye taasisi kama

*NEPAD* na Jumuiya ya Afirka Mashariki kwani taasisi kama *NEPAD* haionyeshi matumaini yoyote kwani tangu ianze siyo chini ya miaka mitatu hakuna ilichofanya hapa nchini.

Tatu barabara za mipakani. Wizara ya Ujenzi izingatie umuhimu wa kuimarisha au kujenga kwa kiwango cha lami barabara za mpakani hasa ile ya Sumbawanga - Kigoma - Kasulu - Kibondo hadi Nyakamazi ili kukabiliana na hatua za kiusalama na kuwezesha maeneo ya mipakani kuibua mipango ya kiuchumi na hasa ku- take advantage ya *geographical position* ya nchi yetu *vis a - vis* nchi za Kongo, Burundi, Rwanda, Malawi na Zambia ambazo zinapitisha mizigo yao nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi kwa hotuba yake nzuri sana, ambayo ina maelezo ya kina na takwimu muhimu. Hongera sana.

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, *Engineer* John Kijazi, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo na Mashirika na Taasisi za Ujenzi kwa kumpatia Waziri wao msaada muhimu ya kitaalam na kuwezesha kusoma Bajeti yake kwa ufanisi mkubwa na kwa kujiamini na kutufanya na sisi tuamini. Naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Kwa upande mwingine napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri atutolee sisi watu wa Jimbo la Bumbuli shukrani zetu nyingi kwa *Engineer* Ako, Meneja wa Mkoa wa Tanga wa *TANROADS* kwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa akishirikiana na wataalam wengine anaowaongoza Mkoani - Tanga. Waendeleo hivyo hivyo na tutaendelea kushirikiana nao vizuri.

Mwisho naomba Waziri asisahau kutoa uamuzi wa kupandisha daraja (*up grading*) barabara ya uchumi ya Mbelei - Baga - Ngwashimayo - Bumbuli kuwa ya Mkoa. Maombi yametolewa na Bodi ya Barabara Mkoani.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa kazi nzuri zenye kuridhisha zinazofanywa na Wizara hii chini ya uongozi wa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli. Kazi zote nzuri zinaonekana, kwani barabara nyingi zimejengwa na zile mbovu zimekarabatiwa. Hongera sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono makadirio ya Bajeti hii. Napenda kuchangia yafuatayo:-

(a) Kuhusu alama za barabara, katika ujenzi wa barabara mfano ukiwa barabara ya Dar es Salaam - Morogoro. Kuna baadhi ya alama mbalimbali zilikuwa zinatumiwa kama ishara mbalimbali wakati wa ujenzi ikiwemo ya tahadhari ya tuta au kupunguza mwendo kufikia kilometa 30 alama hizi baadhi bado zimo barabarani ingawa ujenzi



umeisha. Je, bado zina kazi gani? Ntoa ushauri ziondolewe kwani zinaleta usumbufu kwa waendesha magari kwa kuwa hazina maana na zinaweza kusababisha ajali.

(b) Madreva wanaposababisha ajali na kuleta uharibifu wa barabara na kingo za madaraja. Mifano ikiwa kwenye madaraja na kona mbalimbali zilizopo kwenye barabara kuanzia Dumila hadi Gairo. Je, ni kazi ya nani kutengeneza au kufanya *reapair* ya uharibifu na hawa madreva wanalipia uharibifu huo na kama ni hivyo basi kwa nini repea hazifanywi za kingo ya madaraja haya?

(c) Napongeza kwa kuanzisha masomo ya usalama barabarani mashuleni. Ntoa ushauri ya kwamba ili watoto wetu wawe na uelewa mzuri na iwe ni tabia iliyojengeka ya usalama, basi mafunzo yale yote yanayohusu alama za barabarani na zile wanazofundishwa madreva wanafunzi zingefundishwa. Hii pia itarahisisha hata madreva wa baadaye kufahamu kanuni zote mapema badala ya kutegemea tu ile ya kujifunza tu ili apate leseni.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa hakika kazi yao ni ya mfano pia kwa Wizara zingine, hasa kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makabrasha yaliyotolewa na Wizara yakiambatana na Bajeti hii, *Central Corridor* inaonyesha katika ramani ya *trunk roads map 1*. Napenda kukiri bayana kwamba *traditional understanding of the central corridor has been defined*. Hakika utofauti huu wa *definition* ya *central corridor* unatakiwa kutolewa maelezo na Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia *Map 1*, naomba Mheshimiwa Waziri aeleze nafasi ya barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora - Urambo - Kigoma katika uchumi wa nchi hii na athari za kuendelea kutokujenga kwa kiwango cha lami, kitu kitakachotoa njia fupi zaidi kwa mizigo mingi isiyo kifani kutoka *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi, kupitia wakala wake wa majengo (*TBA*) kwa kazi nzuri wanaopendelea kuifanya katika kuongeza kujenga makazi mapya kwa watumishi hapa nchini.

Hivi sasa kunajengwa nyumba 300 katika eneo la kisasa Mjini Dodoma. Ukifika katika eneo hilo pamoja na kufurahishwa na juhudi hizo, pia utasikitishwa na huko kuzagaa kwa majengo hayo katika eneo kubwa la Mjini. Nadhani hii si falsafa nzuri ya ujenzi wa makazi Mijini na hasa katika Mji Mkuu. Hakika, haya si matumizi mazuri ya ardhi na pia wakazi wa nyumba hizo watakuwa mbali hawataweza kutembea kwa miguu kufikia huduma za shule, zahanati, Kanisa, Misikiti na kadhalika. Hii itaongeza gharama za kuishi katika nyumba katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti kama wangejenga *flats* hakika gharama nyingi zingepungua na hata wakazi wa eneo hilo wangesaidiwa kuokoa gharama ambazo

hawatazikiwepa. Gharama za upelekaji wa *utilities* pia zingepungua katika kuzifikia nyumba hizo kwa pamoja. Lakini pia niseme ujenzi wa aina hiyo unapunguza radha ya Mji na individualism kwa wakazi watarajiwa.

Kwa maeneo hayo napenda kwa mara nyingine tena, bila kuchoka, kuitazama upya falsafa ya ujenzi wa aina hii na hasa katika Miji mikubwa kama Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zilizo chini ya Wizara hii zimekuwa zikiendelea kufanya kazi nzuri sana. Hata hivyo kazi kubwa bado zinahitaji kufanywa na taasisi hizo zenye jukumu la kusimamiwa na kuendeleza taaluma na kampuni za kitaaluma kwa maeneo yote ya kihandisi au kiteknolojia. Naipongeza Wizara kwa kutoa ushirikiano mkubwa kupitia programu nyingi ikiwemo ile ya kusaidia wahandisi wahitimu kusaidiwa katika kupata uzoefu wa kazi zao kama wahandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Wizara zingine na makampuni binafsi zinazonufaika na huduma za wahandisi pia wachangie katika kuwapatia uzoefu hawa wahandisi wahitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na bodi kama *ERB, CRB, AQSRB* na *BMM* ni nzuri lakini matatizo wanayoyakuta site katika kusimamia sheria zao ni kikwazo kikubwa, kunahitajika mila ya kuheshimu taaluma hapa nchini. Mila hiyo itakuzwa kwa msaada wa Serikali yenyewe kwa mstari wa mbele kwani wao ndiyo wanunuzi wakubwa wa huduma za kihandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia kutukua utamaduni huu, basi walau iondoe vyeo na majina ya wahandisi kwa baadhi ya waajiriwa yaani watumishi wake wenye majina hayo kinyume cha sifa zao kitaaluma. Pia, Serikali sasa ikubali kutumia wahandisi katika miradi yake kama vile *MMEM* na *MMES* inayoandaliwa. Bila kufanya hivyo na kwa kweli Serikali ikidharu ushauri huu itamaanisha wao pia wanakikuka taratibu na sheria zilizowekwa. Itakuwa ajabu sana Serikali itegemeo watu binafsi kuheshimu sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haja kubwa na ya msingi ya kupunguza kuokoa gharama bado nafasi ipo kabisa ya kuheshimu sheria na taratibu kwa kuhusisha Wahandisi, Wasanifu, Wakandarasi na kadhalika wenye sifa zinazotambuliwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu pia kwamba Wizara itatoa ushirikiano mkubwa na haraka katika kurejea sheria na kupitisha kanuni za bodi zake ili kuziwezesha kuwa na ufanisi zaidi katika kazi zake. Napenda tena kuipongeza Wizara iliyoongozwa na Waziri Mheshimiwa John Magufuli, kwa kazi ya manufaa makubwa wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu kuchangia Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara hii kwa mapinduzi ya kihistoria yaliyofanywa kuunganisha mikoa ya nchi hasa Tanzania Bara na pia baadhi ya Wilaya kwa kukarabati na kujenga barabara nyingi na kwa ufanisi mkubwa. Kwa maana hii naunga mkono hoja hii asilimia kwa mia na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote hata hao wa Upinzani waunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa awamu ya tatu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuondoa umaskini na kuendeleza uinujaji wa uchumi na kwa kuwa haya hayawezekani bila wananchi huko vijijini kufikiwa kumbe sheria za madaraja ya barabara nchini ni zile na kurithi toka kwa wakoloni, basi naishauri Serikali ifanye mabadiliko katika sheria hizo kama ifuatavyo kwa Wilaya ya Ngara na kwingineko kuliko na tatizo la namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya za Mipakani hususan Ngara, inapakana na nchi zenye matatizo ya vita vya kikabila kwa miongo mingi. Nchi hizo za Rwanda, Burundi na Demokrasia ya Kongo zimekuwa zikiingiza wakimbizi Ngara tangu mwaka 1948. Maisha ya watu na mali zao yamepotea wakati wote na kikomo ilikuwa ni vita ya 1993 nchini Burundi na 1994 Nchini Rwanda. Vyombo vya dola hapa nchini kwa kiasi fulani vilifika mipakani ama kwa kuchelewa au kwa shida kwa sababu ya barabara za Mkoa kuwa mbaya zisizopitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema barabara hii kuanzia Kijijini *Rusumo Border*, Nyabiziba, Ntobeye, Chiozi, Kirushya, Murutabo, Kasange, Mubayange, Mukikomero, Murunyagira, Mabawe, Ngundusi, Kabanga, Murukukumbo, Ibuga, Djuraligwa, Kigarama, Murulama, Mubwirinde, Kihinga, Nyarulama, Bugarama, Muganza, Rwimbogo, Murusagamba, hadi Nyakahula Mzani (barabara ya lami) toka Isaka hadi Rusumo sasa ichukuliwe na Wizara kusudi kuingia Wilaya ya Ngara maafa ya mpakani kwa kuimarisha ulinzi. Hii ni barabara moja inyozunguka Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara inayo madini ya *Nickel* yanayopatikana *Kabanga Nickel Mines*, Kijijini Busarama, Kata ya Bugarama. Pia yapo madini ya *Cobalt*, Ulanga, beti na kadhalika tafara hiyo ya Kulenge.

Kwa miaka 43 sasa badala ya *Nickel* kugunduliwa ambayo ina soko na bei kubwa duniani kwa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wana Ngara, yameshindikana kuchimba kwa sababu tahadhari ikiwa ni pamoja ukosefu barabara nzuri kuyasafirisha. Nilishamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Jibu lake ni zuri na sahihi kulingana na sheria zilizopo. Lakini haukidhi msimamo wa maendeleo leo. Kwa kuwa barabara ya Nyakahula, Rulange hadi Murugarama kuvuka daraja Mumwendo linahitajiwa kutengenezwa, basi nashauri Wizara itengeneze kipande cha barabara ya Rulenge, Bukiriro hadi *Kabanga Nickel Mines*, kilometa 22 ili iwawezeshe wawekezaji kuvutwa kuwekeza katika machimbo hayo kwa faida ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa hii ni barabara ya Wilaya pamoja na mimi, uongozi wa Ngara unaona kwamba kuna umuhimu wa pekee na wa kwanza kwa maendeleo ya nchi kiulinzi na kuchumi, Serikali iweke katika mamlaka ya *TANROAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena na naunga mkono hoja hii, tena.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lalamiko langu kubwa liko kwenye utekelezaji wa *road board* ya Mkoa wa Mbeya kuhusu barabara za Ruanda, Iyuka hadi Nyimbili. Barabara hii haifanyiwi ukarabati wowote zaidi ya maika 6 sasa. Kila tunapoeleza jibu ni kwamba *contractor* ametafutwa na huanza kuchimba changarawe na hakuna kazi inayofanyika. Isansa - Magamba hadi Itaka. Pamoja na kwamba ramani inaonyesha barabara hii imejengwa, si kweli. Hakuna njia yoyote iliyoandaliwa wala kulimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mlowo - Msangano na Mlowo - Kamsamba, barabara hizi zimepita katika maeneo yenye mvua nyingi sana. Miaka yote barabara hizi hugrediwa tu bila kushindiliwa vifusi. Matokeo yake ni kwamba barabara ziko chini sana na kuwezesha kusaidia zaidi maji kuzifanya barabara hizi kugeuka mito na kushindwa kupitika kabisa wakati wa masika. Ipo haja ya kufanya rehabilitation kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ya Songwe - Tunduma - Kandarasi ni Mchina. Wachina ni hodari kwa kazi lakini hawa wanakarabati barabara hii hawaeleweki wala hawaaminiki. Tatizo ni kwamba wanaishi Mbeya na kuja site kufanya kazi. Kwa hali hii kazi haziendi kama inavyotarajiwa. Naomba ufuatiliaji uwe wa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbozi tulipewa mradi wa *VTTP* kwa maendeleo ya barabara vijijini wa kuwezesha usafirishaji vijiji kuwa wa mafanikio. Wilaya ya Mbozi imefanikiwa sana maana wananchi hulima barabara kwa mikono yao. Naomba mradi huu uendelezwe zaidi hasa kupata vifaa vya ujenzi kama sululu, sepetu na karai pamoja na ujenzi wa madaraja, makalvati. Kazi hii imedhihirisha kwamba kwa nchi maskini kama yetu, tukitegemea magreda hatutafika mbali. Naiomba Wizara ipate nafasi kutembelea maeneo ya mradi huu ambao kwa hakika ndio ukombozi wa usafirishaji vijijini.

Pia ujenzi wa nyumba kwa watumishi nashauri isiwe Dodoma na Dar Es Salaam tu. Wilaya hazina nyumba za watumishi wa Serikali. Ipo haja kuwa na mpango wa kujenga nyumba kwa watumishi wa Serikali, vinginevyo utendaji kazi Ofisi za Serikali utakuwa mbaya sana.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa huduma nzuri ya usimamizi mzuri wa ujenzi wa barabara na madaraja na nyumba na kazi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Jimbo langu la Mikumi na wananchi wa jimbo la Mikumi tunaishukuru sana Serikali kwa kusikiliza kilio chetu cha kuokoa vifo vya wanyama katika *Mikumi National Park* kwa kutenga fedha usanifu

Korogwe - Handeni - Kilosa - Mikumi barabara hii itaibua uchumi ambao upo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu yapo tayari Wizarani nilipeleka barua ya kuomba matengenezo ya daraja Zombo ambalo tumelizungumzia hata Mkoa. Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu nategemea nitakumbukwa katika fedha za *road board* hasa kuongeza usalama kwa wanyama wetu Mikumi pamoja na watu kwani inapotokea ajari ya gari na mnyama hutokea vifo hata kwa watu. Hasa kubwa kutokana na ongezeko la kipato kikubwa kwa utalii katika Mbunga ya Mikumi kwani barabara ile ilikuwa watu wanaona bure mara barabara itakupoisha itakusanya mapato vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri John Magufuli, Mheshimiwa Naibu Waziri Hamza Mwenegoha, Ndugu Katibu Mkuu wa Wizara na watalaam wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Nawatakia kazi njema na nawangojeni Mikumi karibuni.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuiwezesha kufanya kazi nzuri katika Wizara hii. Naunga mkono hoja na kuwapongeza wafanyakazi wote wa ngazi zote kwenye Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri, itazameni kwa jicho la huruma barabara ya Manyoni - Itigi hadi Tabora. Pamoja na msaada uliotolewa kufanikisha kuanza ujenzi wa barabara hii, angalau kwa mchanga, kifusi, mmefungua mlango wa magari makubwa yenye *trailers*, yenye uzito usiopungua tani 80 yakipita kwa msululu usio chini ya malori 10 kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uzuri wa malori hayo yakipita na kutokana na tairi kuwa nyingi zilizofungwa, basi kila tairi likipita linabeba lile vumbi na kusambaza kifusi chote na kuacha mahandaki. Nina wasiwasi, wakimaliza kifusi hicho, watagonga vidaraja vilivyopo ambavyo ninaamini vinahimili vigari vyetu vidogo vidogo tunavyotumia kwenye kampeni au tukienda mnadani. Sasa haja ya kufungua Mji wa Tabora kwa kutumia barabara hii itakufa, kwani kwa mtindo huo, barabara itapotea na kubaki mapanda ya ng'ombe na sisi watafuta wapigakura tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha angalizo hilo na ikiwezekana lifanyiwe kazi ili wapiga kura wa Jimbo la Manyoni Magharibi, Igalula na Tabora Manispaa, waweze kuwasiliana kwa urahisi na kwa wakati, ili pia uchumi ukue katika eneo hili, uonekane kwa faida ya wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuunga mkono ili wananchi wajikwamue kiuchumi na kimawasiliano.

**MHE. ROBERT K. MASHALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa mipango mizuri iliyomo kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ikiongozwa na Mheshimiwa John Magufuli, kwa kuhakikisha kuwa kila Mkoa na Wilaya, zinakuwa angalau na barabara moja ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukombe, namshukuru sana kipekee Mheshimiwa John Magufuli baada ya kutembelea Wilaya ya Bukombe, alijionea yeye mwenyewe tatizo la wananchi wa Bukombe kutokuwa na barabara inayohudumiwa na Serikali Kuu na baya zaidi, hakuna mawasiliano ya wananchi wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Kagera kwa Wilaya za Geita, Biharamulo na Bukombe hali ambayo inaathiri sana hali ya wananchi hawa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kujenga barabara ya Ushirombo - Buselesele ni ukombozi kwa wananchi wa Mikoa na Wilaya husika. Ombi maalum ni kuwa kwa kuwa ujenzi wa Barabara ya Ushirombo - Buselesele lazima uhusishe ujenzi wa daraja la Mto Nyikonga, mto ambao umetengenisha mikoa mitatu niliyoitaja na Wilaya zake, naomba fungu la Ujenzi wa Barabara hii liongezwe, kwani shilingi milioni 108 zilizotengwa kwa ujenzi wa barabara hii hazitoshi, kwa vile gharama ya ujenzi wa daraja pekee ni shilingi milioni 120. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika mwaka 2001/2002 na Halmashauri za Wilaya za Bukombe na Geita na *DRDP* na kujenga barabara bila daraja, tatizo litabaki pale pale, kwa vile wananchi hawatavuka kwenda ng'ambo ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa jinsi wanavyoshirikiana kutenda kazi ambazo Taifa hili na Kimataifa zinaonekana na kuwezesha barabara za lami kuunganisha Makao Makuu ya mikoa na baadhi ya Wilaya, na hata barabara za changarawe kupitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza yeye binafsi kwa kusimamia Wizara hii na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Naomba nishauri yafuatayo:-

Kwanza, ni barabara ya Babati - Dodoma - Iringa, itengenezwe kwa muda uliopangwa.

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu wa kujenga barabara, zijengwe kufuata umbali unaotakiwa na siyo kuelekeza kijimbo kama ilivyofanyika huko Moshi, kwani kufanya hivyo ni kujijengea Serikali uadui na baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi na namtakia kila la kheri ashinde kwenye uchaguzi ujao na aje apate nafasi kubwa ili aje asaidie kukamilisha na kusimamia mpango huu na ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nimehudhuria sherehe za kuweka msingi barabara ya Nzega - Shelui na ile ya Tinde - Isaka. Nilifurahishwa sana na uwazi wa Mheshimiwa Waziri mbele ya Rais kwa makandarasi wa barabara hizi. Pongezi sana kwa uwazi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu muhimu ninachomwomba Mheshimiwa Waziri ni kuwaamsha *TANROADS* washughulikie vizuri barabara zinazobaki kama vile barabara ya Nzega - Kagongwa, barabara ya Tabora - Mambali - Bukene - Itobo - Mwangoye hadi Chamachankola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ningezungumzia Bohari Kuu baada ya sheria mpya ya manunuzi. Inaonekana shughuli hapo zimepungua mno kama si sana. Je, Mheshimiwa Waziri, nini hatma ya maghala haya? Naomba maelezo. Ningependekeza maghala haya yatolewe kwa Bohari ya Madawa. Nahofia sana yasije yakabinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia katika hoja ya Wizara ya Ujenzi, niruhusu nichukue fursa fupi ya kutoa salaam za rambirambi kwa familia za wananchi wote wa Mbeya Vijijini kwa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza Menegoha, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanaoyifanya. Jambo moja la kujifunza hapa ni kwamba upo ushirikiano wa hali ya juu kati ya wanasisia wa Wizara hiyo na watendaji wao, ndiyo bila shaka siri ya mafanikio haya makubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu daraja la Mkundi. Mwaka jana, Waziri wa Wizara hii alitupatia shilingi 140,000,000/= kwa ajili ya Darala la Mkundi na barabara ya Mkomazi - Mnazi hadi Uмба. Kiasi cha shilingi 100,000,000/= kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mkundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana makadirio yalipofanywa upya, ilionekana daraja kwa sasa lingegharimu shilingi 300,000,000/=. Ingawa Meneja wa Barabara wa Mkoa wa Tanga alinihakikishia kuleta maombi Wizarani ya kuongezwa pesa katika bajeti hii, nimeona nyongeza ya shilingi 50,000,000/= tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara hii umekuwa ni kero kubwa kwa muda mrefu. Maana hasa ya hali hii ni kwamba daraja hili sasa halijengwi kabisa. Naomba sana sana zitafutwe pesa mwaka huu huu wa fedha ili daraja hili lijengwe. Serikali yetu na Chama chetu, kamwe hazitaeleweka kwa wananchi wa Tarafa ya Umba na Jimbo la Mlalo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Lushoto - Mlalo. Hali ya barabara hii siyo nzuri kabisa. Huko nyuma, barabara hii ya changarawe ilikuwa nambari moja. Baada ya misukosuko mingi ya mafuriko na maporomoko ya mwaka 1993 na baada ya hapo, mvua za *El-Nino* zilichafua sana. Sehemu kubwa ya changarawe iliondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona barabara hii kwa mwaka huu imetengewa shilingi 48,000,000/= kwa matengenezo ya kawaida. Nasema fedha hizi hazitoshi. Matengenezo ya kawaida yamefanyika mara kwa mara, lakini bado barabara hii haijatengamaa. Barabara hii ndiyo uti wa mgongo wa uchumi na maendeleo kwa ujumla ya Jimbo la Mlalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Malindi - Nkelei - Lukozi - Manolo - Mtae. Barabara hii pia ni ya mkoa na iko ndani ya Jimbo la Mlalo, nayo inahi ni ya mkoa na iko ndani ya Jimbo la Mlalo, nayo inahitaji matengenezo kamilifu. Matatizo yaliyoikumba barabara ya Lushoto hadi Mlalo ndiyo yale yala yaliyosababisha hadi leo matatizo ya barabara hii. Hivi sasa sehemu ya barabara hii imepigwa *grader* na kwa kuwa ni kiangazi, eneo zima ni vumbi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba barabara hii isirudie tena kuwa vumbi badala ya barabara ya changarawe kama ilivyokusudiwa mapema. Barabara hii ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mbao, magogo, matunda, mboga mboga, viazi mviringo na mazao mengine. Naomba ipangiwe fedha na itengenezwe kwa kukrudishia changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Mkomazi - Mnazi - Umba. Barabara hii ni ya mkoa. Kwa bahati mbaya tangu barabara ipandishwe daraja, ni kazi chache mno zimefanyika ili kuifanya itipitike. Barabara hii ndiyo yenye daraja la Mkundi na mara nyingi wakati wa mvua za vuli na masika, haipitiki. Naomba iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HARITH B. MWAPACHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Katibu Mkuu, Ndugu John Kijazi na Wataalam wake, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara katika kubuni na kuandaa dira yenye nia ya kuleta maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mbunge wa Wilaya Tanga, napenda kutoa shukrani zangu na wananchi wa Tanga, kwa Wizara ya Ujenzi kufikiria na kuendeleza barabara ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya Tanga. Barabara ambazo ni muhimu kwa sasa ni kama zifuatazo:-



Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tanga - Horohoro ni muhimu sana kwa maendeleo ya Tanga. Tunashukuru kwanza kuwa ukarabati wa *Port Access* kukamilika. Aidha, tunashukuru kwamba madaraja yaliyokuwa yakijengwa na *Konoike* kutoka Tanga kuelekea Horohoro, yamekamilika. Tunasubiri uzinduzi wa madaraja hayo. Niongezee tu kwamba *Konoike* imefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosubiri sasa ni ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Azma hii ikikamilika, barabara hii itakuwa kiungo kizuri na Mombasa na Kenya kwa ujumla katika kukuza utalii, biashara na matumizi ya Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba lami iwekwe haraka iwezekanavyo. Hivyo, *feasibility study* ya barabara hii (ukurasa wa 96) ni ya nini tena? Hivi *feasibility study* haikufanyika wakati wa kujenga madaraja yenye gharama kubwa kama yale. Kwa kifupi, tunachooomba ni kunguza mlolongo wa *studies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili ni ya Bagamoyo - Pangani - Tanga. Barabara hiyo italeta maendeleo makubwa katika sekta ya utalii, uvuvi, kilimo, biashara na viwanda. Tupo tayari kushirikiana na Wizara ya Ujenzi katika kutekeleza *concept* hiyo ya *BoT*. Lakini wapo wawekezaji ambao wameanza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya tatu ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Tanga na hasa ujenzi wa Bandari mpya ya Mwambani, ni barabara ya Magore - Mziha - Handeni - Tanga. Barabara hii ita-*open up* maeneo yote hayo kimaendeleo. Lakini kubwa zaidi, barabara hii itakuwa *viable* kwa sababu itatumiwa na wazalishaji na wasafirishaji wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida na Morogoro. Bandari hii pia itakuwa *import/export conduit* kwa mikoa hiyo. Lakini zaidi ya hapo, Rwanda na Burundi. Hivyo Bandari ya Mwambani itaweza kujengwa na ku-*operate viably*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba katika kukamilisha na kujumuisha hotuba hii, ayagusie masuala hayo matatu niliyoyafikisha kwake. Nashukuru.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja hii. Napenda pia kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa katika ujenzi wa barabara za lami hapa nchini. Pamoja na pongezi hizi, napenda kutoa ushauri na maombi machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa barabara ya Dodoma - Manyoni. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, umeanza na tunaishukuru sana Serikali kwa hatua hii. Kwa kuwa ujenzi unafanywa kwa *design and build* kwa maeneo ambayo ujenzi haujafika, wananchi hawana uhakika wa *alignment* mpya ya barabara. Itafaa *alignment* hiyo ijulikane mapema ili wananchi waelewe vizuri na waanze kufanya maandalizi ama ya kuhamisha shughuli zao au kutafuta viwanja jirani na *alignment* mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mjini Manyoni, barabara mpya ya lami, sasa inafahamika kuwa itapita pembeni. Hivyo, tunaomba Wizara itenge fedha za kuweka lami katika *alignment* ya sasa ambayo haitaguswa na mkandarasi. *Alignment* ya sasa bado itaendelea kutumiwa na magari yanayoingia Mjini Manyoni, hivyo bado ina umuhimu. Kipande hicho kinatazamiwa kuwa cha kilometa 2 - 3 tu, kitaanzia pale barabara ya lami inapocheputa hadi kuunganisha tena barabara hiyo pale inapokutana na ile iendayo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara za Mkoa (*TANROADS*). Ofisi ya Meneja wa Mkoa *TANROADS*, Singida, inafanya kazi yake vizuri. Barabara nyingi zinatengenezwa Mkoani Singida. Tunapongeza kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha za msaada na mkopo toka *ADB* kwa barabara zilizoathirika na *El-Nino* kwa Mkoa wa Singida zimeelekezwa kwa barabara za Wilaya za Iramba na Singida Vijijini pekee, barabara za Wilaya ya Manyoni hazimo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbusha ombi letu la mwaka jana kuwa fedha za ndani (*road fund*), sehemu kubwa zielekezwe katika *Regional Roads* za Wilaya ya Manyoni ili kufidia fedha *ADB* ambazo Wilaya hii imezikosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kupongeza kazi nzuri ya Wizara hii na naunga mkono Bajeti yenu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri John Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi wanayoifanya ya maendeleo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuja kutembelea barabara zetu za Milima ya Same. Namshukuru pia kuwa katika kipindi cha miaka miwili tangu 2002, amejitahidi sana kutenga pesa kidogo kudumisha barabara za udongo (*unpaved roads*) Same. Barabara zote kule ni za udongo (vumbi), hakuna hata moja ya changarawe. Kwa hiyo, matengenezo haya yanawezesha barabara hizi kupitika wakati wa kiangazi tu. Mvua zikishanyesha, hatuna hata barabara mkoa inayopitika, na matengenezo yote yaliyofanyika husombwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu, sasa nina hoja au kero zifuatazo ninazomwomba Mheshimiwa Waziri azifanyie kazi na kuzijibu: -

Kwa nini barabara tu za Wilaya ya Same katika Mkoa wa Kilimanjaro, ndizo zinazoongoza kwa ubovu, hali mafungu makubwa yakipelekwa Wilaya zingine Mkoani Kilimanjaro? Nimesema Wilaya ya Same haina hata barabara moja ya changarawe. Ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba barabara ya Mwembe-Mamba - Ndungu, iingizwe katika Bajeti ya 2004/2005, kwa kiwango cha changarawe kwa kipande kidogo kuanzia Mwambe hadi Mbagga. Sasa sikuiona katika Bajeti na haijatengewa Bajeti kwa kiwango hicho. Ni kwa sababu gani, wakati Waziri alinishauri nimwandikia na kumwomba ili aingize katika Bajeti yake ya 2004/2005? Nikawaambie nini wananchi wa Same?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo ni za udongo, Wizara ihifadhi barabara hizo kwa kuziwekea *drainage system*. Vinginevyo, kuendelea kutumia fedha za wananchi kuzikarabati bila *drainage system* ni kuharibu fedha zao. Wizara inatakiwa iwajibike kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. lakini nitamwunga mkono akinipatia ufafanuzi na majibu ya uwiano mzuri wa matengenezo ya barabara katika Wilaya ya Same.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii kwa kuandaa na kutekeleza vizuri mkakati wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizotolewa katika Bunge hili, zinaonyesha uwezo, ubunifu na usimamizi mzuri sana wa Viongozi na Watendaji wa Wizara hii. Kwa mafanikio yaliyoainishwa katika vitabu vya bajeti ya Wizara, ushindi kwa CCM mwaka 2005 ni dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Iringa - Dodoma - Babati - Minjingu, imenipa faraja kubwa. Kuanzia sasa nitakwenda kuhamasisha wananchi ili wajue na wajiandae ili wasiendeele kujenga katika hifadhi ya barabara pindi upembuzi utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuona juhudi zimewekwa za kuendelea kukarabati barabara za Iringa - Pawaga, Iringa - Msembe (*National Park*) na Iringa - Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ipo siku, uwezo ukiruhusu, barabaraza Iringa - Pwaga na Iringa - Msembe, zitakuja kuwekwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuchapa kazi ya kuigwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ujenzi au Wizara imepambanua wazi kabisa nini Wizara ilitekeleza, nini sasa inatekeleza na ni miradi gani wanakusudia kuitekeleza.

Hii ni Wizara moja kati ya zote ya kuigiwa mfano hapa Tanzania kama si Afrika. Hongera sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Lakini, Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vile vile kwa aina yake kwa angalau kuitaja Zanzibar (Unguja na Pemba). Nampongeza kwa hilo. Tumelewa ufafanuzi wa barabara karibu zote za Pemba na kwa Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu hoja atufafanulie barabara hizo ni zipi na atupe maelezo ya wapi pamefikiwa ujenzi wa barabara itokayo Chwaka - Uvuwa - Pongwe - Kiwengwa - Pwani Mchangani - Matemwe, barabara ambayo alieleza maendeleo yake katika bajeti iliyopita ambayo kwa safari hii amekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile azingatie wakati wanapopanga mipango ya ujenzi wa barabara kwa Afrika ya Mashariki (Viongozi wa juu wa Afrika ya Mashariki) wanapokutana, wajue kuwa Tanzania ni pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika Mwenyekiti, ukurasa wa 8 - 9, ibara ya 7 ya hotuba ya bajeti, wamesema kwamba, mkakati mpya wa kuondoa umaskini (*NEPAD*), ni pamoja na ujenzi wa barabara Zanzibar, nayo ifikiriwe kuingizwa kwenye mipango hiyo, kwa njia moja ama nyingine. Kwa hiyo, ama Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, wasiachane na majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 20, ibara ya 3, Mheshimiwa Rais ameomba Japan nao wasaidie ujenzi wa daraja kubwa tu umoja, hakuna alichokiona kwa Zanzibar. Naomba Mheshimiwa Magufuli, awe anamshauri vyema Mheshimiwa Rais kama kawaida yake. Awe anamkumbusha hali ya Zanzibar, kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Asante.

**MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa John P. Magufuli, Waziri wa Ujenzi, kwa kutoa hotuba yake nzuri yenye mpangilio mzuri sana. Hotuba hii inayo mipango inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote, Mheshimiwa Mwenegoha, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wake, Bwana Kijazi. Ninampongeza pia Mhandisi Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Bwana Kahapale, ni mbunifu na msikivu na pia ni mchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Viongozi wa Kigoma wamekuwa wakizungumzia juu ya *Gateway* la Kigoma. Kigoma ni mkoa ambao una uwezo wa kuzalisha mazao mengi ya chakula na mengine yangeweza kuanzishwa kama mkoa utafunguliwa kwa mikoa mingine ya nje. Hivi sasa mkoa umefungwa kwa sababu ya ukosefu wa barabara, tatizo ambalo linazuia kwa masoko hata yale ya mikoa ya jirani kama vile Tabora, Rukwa, Kagera na Shinyanga. Ili kutatua matatizo haya, naomba

barabara ya Tabora - Kigoma ni muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya mikoa hii miwili. Ninatambua kwamba, daraja la Mto Malagarasi ni gharama kubwa. Ninachoomba, Serikali ijipange vizuri itujengee barabara hiyo kama Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alivyoahidi mwaka 1995. Naomba Serikali ifanye *commitment* ya sawasawa ya lini shughuli ya kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Mwandiga - Manyovu, tumelezwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, itajengwa kwenye kiwango cha lami mwaka huu. Kwa fedha zipi? Tafadhali sana naomba ufafanuzi. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa mikoa ya Magharibi. Ni kwa nini barabara hii haitengenezwi na kuwekewa lami kama ambavyo tumekuwa tukiomba kwa takriban miaka 15 iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatudhalilisha kama Taifa. Barabara ya Bujumbura mpaka mpakani mwa Tanzania - Manyovu, kuna barabara ya lami ya Burundi. Serikali ya Burundi kwa muda mrefu iko tayari kuitumia na ikiwezekana kuweka *dry port* katika Tarafa ya Manyovu. Kwa kuwa sasa itajengwa kwa lami kama ulivyotamka, basi wananchi wa mkoa ule wataimwagia sifa Serikali yao, maana biashara nyingi zitafunguliwa kwenda Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Kigoma - Nyakanazi, ili kuukomboa mkoa huu, ni vyema barabara hii nayo ikajengwa kwa kiwango cha lami. Tulitumia karibu Sh. 6bn./= kujenga barabara. Tunashukuru kwamba, Serikali ilikubali kutumia fedha hizo. Baada ya miezi sita mvua zilinyesha, barabara hiyo ikaharibika sana na ikalazimu Serikali kuendelea kuifanyia ukarabati mkubwa sana. Lakini katika dhana nzima za kuufungua mkoa kwa mikoa mingine, lazima barabara hii iwekwe lami itoe *confidence* kwa wafanyabiashara kuwekeza katika mkoa ule na ijenge matumaini ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma, Kagera na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka Mheshimiwa Waziri, atayafanyia kazi haya na atapanga safari ya kuja Mkoa wa Kigoma na Makamu wa Rais hivi karibuni aliahidi kukueleza ufike, ukae na viongozi wa Mkoa wa Kigoma.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuipata nafasi hii ili nami niungane na wenzangu katika kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Muu na Wataalam wote, walioshirikiana katika kuiandaa taarifa nzuri. Hongera sana. Ila nashauri mipango yote iliyowekwa, hakikisha mnafuatilia na usimamizi wa karibu ili kuona ufanisi zaidi unatekelezeka sawa na malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda na dada yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kifo cha marehemu Baba yao. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole vile vile kwa familia za marehemu 12 waliofariki kwa ajali ya gari katika Daraja la Nangowo, Mkoa wa Mtwara. Namwomba Mwenyezi Mungu, awape moyo wa faraja katika kipindi kigumu. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwa jinsi Wizara ya Ujenzi inavyotambua wanawake kwa kuwashirikisha katika ujenzi wa barabara na ajira za wanawake. Nashauri kitengo hiki kipewe kila msaada kushirikisha wanawake. Nchi yoyote yenye maendeleo, wanawake hawakuachwa nyuma. Ongeza idadi ya wanawake wawe wengi ili wazidi kuimarisha maendeleo ya familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa jitihada zinazofanywa za ujenzi wa barabara kupitia uongozi wa Mheshimiwa John Magufuli, Mungu ambariki sana ili aendelee na afya njema na aendelee na kazi sawa na malengo. Daraja la Rufiji limekamilika na sasa linaitwa Daraja la Mkapa. Naendelea kupongeza kwa kazi nzuri. Nashauri ulinzi uwekwe na kuwashirikisha wananchi waishio pale na raia wema watawafichua wabaya na watatoa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Dar es Salaam - Mingoyo, utekelezaji unarithishwa kwa vipande vya Mnazi Mmoja - Lindi, Kibiti - Dar es Salaam na Mateja - Daraja la Mkapa, kazi haipendezi, sijui tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengenezaji wa barabara hii siyo mzuri. Hata wakati wa masika, baadhi ya wasafiri walipata tabu. Magari yao kuharibika au kunasa kwenye matope kutokana na ubovu. Mheshimiwa Waziri afuatilie haraka iwezekanavyo ili hadhi ya Daraja la Mkapa iende sambamba na malengo yake. Kama makandarasi walipewa kipande hiki hawawezi, ni bora kuwatoa mara moja na kuwaweka wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya mpakani mwa Mtwara na Msumbiji, utekelezaji wa ujenzi unakwenda pole pole sana. Nashauri sana ipewe kipaumbele katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Mtwara Corridor*, shughuli zimeanza na naipongeza Serikali kwa mipango mizuri kwa kujitahidi kupeleka maendeleo kwa wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inapita pembezoni mwa Mkoa wa Mtwara, atakachofaidika mwananchi wa Mtwara ni kwamba inanzia Bandarini katika faida yake au sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambayo ndiyo tegemeo la uchumi, usafirishaji wa watu na mali zao ni ya kutoka Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi, nayo inapita Makao Makuu ya kila Wilaya. Hii ndiyo tegemeo la mkoa, lakini inatisha kuwa Serikali yetu haijasikia kilio cha viongozi na wananchi wa Mtwara. Barabara ina vumbi na haina hadhi ya kuitwa ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ina vilima na makorongo na kadhalika. Tunasema Waziri wa Ujenzi wewe ni msikivu, lakini mbona kilio cha Mtwara, barabara hii hutamki kuweka lami? Kila mara majibu ni kwamba, itafanyiwa matengenezo. Tunasema weka lami ili kuwaokoa wana-Mtwara, magari yanakwama wakati wa masika. Yanaporomoka kwenye makorongo. Angalia bajeti yako, tumia ujasiri wa kuthubutu ili barabara hii iwekwe lami haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Newala - Kitangali - Mtama, nilishasema huko nyuma kuwa imekufa. Naishukuru Serikali kwamba, dalili zipo za kutengeneza, ila ni mbovu na baadhi ya maeneo hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Waziri mia kwa mia. Ipite ili Waziri aijenge barabara hii ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi na kadhalika.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Katibu Mkuu, *Engineer* Kijazi na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Wizara hii imekuwa ya mfano wa kuigwa katika nchi yetu na kufanya msemu wa “inawezekana, timiza wajibu wako”, uwe wa ukweli kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yaliyofanywa na Wizara hii chini ya uongozi wa Waziri wa Ujenzi, ni mengi na mazuri yanayoonyesha kiasi gani anao uzalendo, upendo kwa nchi yake na watu wake, uadilifu, kujituma na weledi. Namtia moyo adumu katika mwenendo huu na hakika historia haiwezi kumsahau na kufutika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa barabara. Nashukuru na kuupongeza uamuzi wa kuipa barabara ya *Old Shinyanga* - Salawe - Kakola fedha za matengenezo kwenye maeneo korofi, lakini napenda kueleza kuwa barabara hii inahitaji kujengwa yote kwa kiwango cha changarawe, kiasi cha km. 85. Aidha, ningeshauri iingizwe katika mpango wa barabara za kujengwa kwa teknolojia ya *otta seal*, ili iweze kudumu. Kwani inakwenda eneo la mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Victoria kwenda Kahama Mjini na baadaye Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itarahisisha kazi za upelekaji vifaa vya kazi hiyo pamoja na usombaji wa mazao mengi ya chakula na biashara, kwani sehemu yote ipitayo barabara hii ni ya uzalishaji mkubwa wa mazao. Aidha, huunganisha Wilaya ya Geita, Misungwi na Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia baada ya JWTZ kufanya kazi nzuri katika ujenzi wa nyumba za watumishi wa Serikali. Ni vyema sasa Wizara ione

umuhimu wa kuwatumia sasa kwenye ujenzi wa barabara nchini. Hii itafaa hasa kwa fedha zetu nchini na kuwaongezea uzoefu na vifaa vya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kutumia *otta seal* utumike kwa miradi yote ya barabara za mijini na za mkoa, kwani gharama zake ni nafuu na ni imara sana kama inavyoonyesha maeneo mbalimbali yaliyojengwa kwa teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii, *TANROAD*, *CRDB* na kadhalika, yajengwe Dodoma badala ya kuendelea kuwa Dar es Salaam. Hii itaonyesha mpango wa kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma unaungwa mkono na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri katika kufanikisha kazi zote za mwaka huu wa 2004/2005. Tutashirikiana wote.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa naanza na pongezi za dhati kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu, akishirikiana na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa barabara ya Singida hadi Shelui, nimefurahi kuona kwamba, katika hotuba ya Waziri, ameeleza hatua zilizofikiwa katika kusudio la kujenga. Nasisitiza suala hili lisichukue muda mrefu, ili sehemu nyingine inayounganisha hapo iende pamoja. Maana kama kipande hicho kitabaki bila lami, pekee kitatia dosari barabara nzima ya Dodoma hadi Mwanza, maana ndiyo kipande kisichokuwa na mjenzi anayeendelea. Aidha, barabara ya Nzega - Mbeya - Ipole hadi Mpanda, ni vyema iwekwe katika mpango wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kufanyiwa matengenezo ya barabara ya lami kati ya Ilula kwenda Ng'wanangwa, eneo lililojengwa na Mkandarasi wa *SIETCO* kwa kiwango cha lami, maeneo mengi yameharibika. Ni lini itatengenezwa upya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza ujenzi/ukarabati wa barabara ya Dodoma - Morogoro, uanze mapema ili isiharibike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kazi njema zenye ufanisi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Watendaji wake Wakuu, kwa kazi nzuri wanayofanya, ambapo vielelezo vyake vinaonekana katika utekelezaji unaoendelea hivi sasa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekeza ushauri wangu na kutaka kujua hali ilivyo katika maeneo yafuatayo: Sehemu za barabara kuu au barabara za mikoa zinazovuka reli. Japokuwa pendekezo la kujenga matuta kuwezesha magari kupita kwa usalama katika



sehemu za vivuko vya reli, niliwahi kulitoa mwaka 2001/2002, lakini bado halijapewa uzito na hakuna mpango wa kuyajenga matuta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya barabara kuu ya kutoka Tanga kwenda Moshi/Arusha, kwa eneo la kati ya Korogwe na Mombo peke yake, zipo sehemu nne ambapo barabara inavuka reli. Maeneo hayo yamesababisha ajali nyingi na wananchi kupoteza maisha. Tutaendelea hivyo mpaka lini? Nashauri tena kwamba tuwe na mpango wa muda mrefu wa kujenga matuta ili magari yapite juu na kuiacha reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisheria reli ndiyo yenye haki ya kwanza katika barabara na hivyo barabara kuu au za mikoa zinachukua nafasi ya uvamizi kwa kuvuka reli. Siku wananchi watakapotambua jambo hili, basi watumia haki yao kuibana na kuidai fidia Serikali wakati ajali na vifo vinapotokea kutokana na barabara kuu za Serikali kuvamia reli na kusababisha ajali na vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za lami zilizoharibika ndani ya Miji Midogo au Halmashauri za Wilaya. Hoja ya kuitaka Serikali kusaidia Halmashauri kuziweka lami upya barabara za Miji Midogo na hata Manispaa zilizowahi kuwa na lami, ilitolewa hapa Bungeni na kuonekana ina uzito mkubwa. Hali ya barabara hizo ni mbaya sana, lami imebomoka, kokoto na mawe yako nje na kuwa kero kubwa kwa watumiaji wake wa miguu, baskeli na hata magari. Je, katika hoja hiyo ambayo inakubalika kwamba Halmashauri husika hazina mapato wala uwezo wa kuzijenga, mpango wake Kitaifa uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji Mdogo wa Muheza, zipo barabara tano za aina hiyo. Licha ya kuwa fupi, zinapita maeneo nyeti ya mji, ikiwepo eneo la soko kuu. Napendekeza Serikali itengeneze mpango maalum ili hatua kwa hatua barabara hizo zitengenezwe. Sina uhakika kama mpango huu ndio uliotumika kuandaa ukarabati wa kilomita moja na nusu za barabara ya Mkoa - Muheza - Amani, ambapo naipongeza Wizara kwa kuitengea fedha na kutafuta mkandarasi mwaka huu wa 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nguzo za umeme zilizopo ndani ya hifadhi ya barabara. Katika maeneo mengi, nguzo za umeme zipo ndani ya maeneo ya hifadhi za barabara. Je, Wizara ya Ujenzi inasema nini kuhusu hali hiyo katika kuziwekea X nguzo za umeme? Ni dhahiri lazima Serikali ifahamu kwamba, kama itasisitiza kutekeleza amri ya kuziondoa nyumba na hata alama nyingine kama mabango na hata nguzo za umeme, basi ifahamu kwamba, inahitajika kuwa na mpango maalum wa kuiwezesha *TANESCO* kutekeleza kazi hiyo. Hii ni kazi ya gharama kubwa na kwa vyovyote vile itatumia fedha za wananchi badala ya kuzielekeza zaidi katika shughuli za kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Muheza - Amani, hapa Bungeni mara kadhaa na hata mwaka 2003/2004, Serikali ilitamka nia ya kuiwekea lami barabara hiyo ya Muheza - Amani. Kwa mpango uliopo wa Wizara ya Ujenzi, sijaona mpango wa utekelezaji wa tamko hilo la Serikali. Kimsingi umuhimu wa barabara hii umeendelea kuongezeka kila mwaka, ikiwa na kuongezeka kwa Mashamba na Kiwanda cha Chai cha *East Usambara Tea Company (EUTCO)*, vivutio na vituo vya utalii, Vivutio vya Hifadhi

ya Misitu na Maeneo ya Utafiti, Zahanati na Kituo cha Afya, Shule za Sekondari, Kituo cha Utafiti cha Afrika Mashariki cha Malaria, Uvumbuzi wa Madini (Dhahabu) na Utafiti unaoendelea wa madini hayo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wananchi wa Wilaya ya Muheza wana imani kubwa kwamba, Serikali itaiwekea mkakati thabiti na kutekeleza ahadi ya kuiwekea lami barabara hii ya Muheza - Amani na kudhihirisha kuwepo kwa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii Wizara ya Ujenzi kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri na mtani wetu wa jadi, kwa kazi nzuri ya ushirikiano wa hali ya juu walio nao na kuonyesha katika utendaji wao wa kazi kila siku. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba sasa barabara ya Dodoma-Mwanza imeanza kujengwa na kazi yake inaonekana. Ila naomba na kusisitiza isiishie hapo, ili ikamilike upesi iwezekanavyo, kwani barabara hii, yaani Dodoma - Mwanza kupitia Singida-Shelui-Nzega-Tinde-Mwanza. Barabara imezungumzwa kwa miaka mingi sana, tangu enzi za wazazi wetu wakiwa Wabunge wa Bunge hili lako Tukufu *in vain* yaani bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunazungumza, siyo maneno matamu kama ilivyokuwa zamani, sasa ni vitendo. Waswahili husema, Ukimsifia Mgema, Tembo hulitia Maji, kwa misingi hiyo, naamini kwamba barabara hii itakamilika bila wasiwasi. Nasisitiza barabara hii, naomba ikamilike, isiachiwe njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri ilivyo sasa, kuna barabara ya Dodoma - Itigi - Tabora na kuna barabara niliyoitaja hapa inapitia Nzega, Mkoa wa Tabora na nataka kuzungumzia barabara ya Nzega - Tabora, ambayo inasahaulika au imesahaulika. Barabara hii ni kiungo kikubwa sana na barabara ya Dodoma - Nzega - Mwanza na pia barabara ya Mwanza -Nzega - Tabora - Kigoma. Ni kiungo kikubwa kwa nchi za jirani yaani Burundi, Rwanda na Kongo kupitia Tabora. Kwa misingi hiyo, naomba barabara hii iwekwe pia katika utengenezaji wa barabara kwa kiwango cha lami.

Wananchi wa sehemu hii yaani Nzega, Tabora kupitia Puga-Nkineziwa, ni wakulima wa tumbaku, vitunguu, mpunga na kadhalika. Barabara hii ikitengenezwa kwa kiwango cha lami, wakulima wa mpunga na vitunguu wataenda Tabora na Nzega hadi Burundi kuuza bidhaa zao kwa urahisi zaidi na pengine wataweza kwenda na kurudi kwa siku moja au mbili tu. Naomba Serikali ifikirie kipande hiki kidogo sana ili kuunga mikoa hii miwili yaani Tabora na Kigoma kupitia Malagarasi na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie barabara nyingine ambayo naamini ikitengenezwa kwa kiwango cha lami, tutakuwa hatuna njaa nchi hii na tutajikwamua kiuchumi haswa haswa. Umaskini nchi hii utakuwa *bye bye*. Barabara hii ni ile ya kutoka Kidatu - Ifakara - Mahenge - Mtimbila - Sofi na kadhalika Mkoani Morogoro. Kusema kweli kama barabara hii ikiwekewa mikakati ya hali ya juu, mimi naamini kabisa kuwa hatuna sababu ya kukosa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni nzuri mno, ina rutuba, we acha. Mpunga unakubali, mahindi na ufuta, kwa kifupi kila kitu na watu au sehemu hii inapata mvua mwaka wote, ila mazao yanabaki kule kule. Hayafiki Dar es Salaam au Mikoa mingine isiyo na rutuba kama huu. Barabara hii ifikiriwe ili tupate chakula nchi nzima, njaa *out* na wakulima waseme umaskini *bye bye*, wajae mapesa kibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale penye njia ya kuwatajirisha wananchi na uwezo upo, basi tufanye hivyo. Siyo tuache watu waendeleo kuwa maskini. Naomba kuwasilisha.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanazofanya katika kuboresha miundombinu ya barabara, madaraja na kadhalika ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa maoni yangu juu ya msukumo unaotolewa na Serikali katika ujenzi wa barabara nchini, hususan suala zima la namna ya kuzigawia fedha barabara za Kitaifa na za Kimkoa kwa upande mmoja na barabara za vijijini kwa upande mwingine.

Kama tujuavyo, barabara za Kitaifa na za Kimkoa ndizo zimekuwa zikipatiwa fedha nyingi zaidi kupitia *Road Fund* takriban asilimia 70, wakati barabara za vijijini ambazo zina kilometa nyingi zaidi nchini, hupatiwa chini ya asilimia 30 ya fedha kupitia mfuko wa *Road Toll*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuelewa umuhimu wa ujenzi wa barabara za Kitaifa na za Kimkoa, lakini napata taabu sana kuona barabara za vijijini zinaendelea kuwa duni, barabara ambazo ni nyingi zaidi na ndiyo ziko kwa wananchi wengi ambao ndio wazalishaji wa mali za Taifa hili na ndiyo walengwa wa maendeleo. Barabara za vijijini katika Wilaya zetu, zimeendelea kuwa mbovu kwa sababu hazitengewi fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa barabara za Wilaya ya Kahama. Zipo barabara tatu tu za Kitaifa na Kimkoa. Ukiacha barabara ya lami kati ya Isaka na Lusahunga, iko barabara ya Kitaifa kipande kati ya Kagongwa na mpaka wa Nzega na barabara za Kimkoa za Kahama - Kakola, iliyokarabatiwa na kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na Kampuni ya kuchimba dhahabu ya Kahama (*KMCL*) na barabara ya Kahama - Butibu. Kwa ujumla, barabara hizi hupatiwa fedha za kuridhisha kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tofauti kabisa na barabara zilizosalia na ambazo husimamiwa na Halmashauri ya Wilaya. Ni nyingi zaidi na jumla ya urefu wa kilometa 1,600. Barabara hizi zimekuwa zikitengewa si zaidi ya shilingi milioni 140 kwa mwaka kwa kipindi kirefu. Kwa mfano, mwaka 2002/2003 - TAMISEMI iliipa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama *ceiling* ya shilingi milioni 140 za *Road Toll*, ambapo mahitaji yalikuwa zaidi ya shilingi bilioni 1.0b. Kilichopatikana ni shilingi 136,474,726/50 ambazo zilitolewa katika mikupuo 12. Matokeo yake, barabara hizi hazipati matengenezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kahama, zipo barabara za namna hii tatu. Nyandekwa - Ulowa kilometa 76, Kahama - Chambo kilometa 65 na Nyandekwa - Bulungwa kilometa 41. Kwa ujumla wake, barabara hizi hutengewa si zaidi ya shilingi milioni 40 kwa mwaka, japo ndizo vitovu vya uzalishaji wa mazao ya mahindi, pamba na tumbaku na mazao ya misitu Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nieleweke kila mara ninapotetea hoja kwamba barabara hizi ni muhimu sana, zinastahili kupandishwa hadhi kuwa za Kimkoa, zinapita maeneo ambayo huko nyuma, yalikuwa mapori. Lakini sasa yamefumuka na kuwa na wananchi wengi sana, hasa sehemu ya Lulungwa (Kata kubwa kuliko zote Wilayani) na ina wakazi wanaofikia 50,000, Ulowa na Chambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo ya uhakika ya barabara hizi zitaokoa mazao hayo niliyotaja na kunufaisha au kufaidi kiuchumi na kijamii wananchi wapatao 300,000. Nyandekwa - Ulowa (watu 110,000), Kahama - Chambo (watu 83,000) na Nyandekwa - Bulungwa (watu 100,000). Hivyo, napendekeza vigezo vya kupandisha hadhi barabara kubwa za vijiji kuwa za Mkoa, zirejewe kwa kuzingatia zaidi maeneo ambayo wananchi wengi waliko. Aidha, zoezi la kupandisha hadhi barabara likamilike mapema.

Mwisho ni faraja iliyoje kwamba Mheshimiwa John Magufuli amekubali barabara ya Kahama - Chambo kuwa muhimu na kuitengea shilingi milioni 100 kwa mwaka 2004/2005. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kahama, napenda kutoa shukrani za dhata kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kiutekelezaji kipande hiki cha barabara ya Tabora - Bukumbi - Shitage - Chambo - Kahama (yaani kipande cha Chambo - Kahama), kionyeshwe chini ya Mkoa wa Shinyanga. Ndiyo kusema katika Kiambatisho Na. 6 cha hotuba ya Waziri, kipande cha Chambo - Kahama kionyeshwe chini ya *S/N. 1 Shinyanga Region* badala ya *S/N. 19 Tabora Region*. Hii itasaidia usimizi na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mapendekezo ya Waziri John Magufuli kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2004/2005.

**MHE. MUSA A.LUPATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhata Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli na Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza

Mwenegoha pamoja na timu makini ya Wataalam inayoongozwa na Katibu Mkuu *Engineer* John Kijazi na pia Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa Wizara hii wanasikiliza sana maoni, ushauri na maombi ya Waheshimiwa Wabunge na wanatekeleza mengi ya maombi yetu kwa kadri ya uwezo wa Serikali. Napenda kuwashukuru sana kwa kuzitengea fedha barabara za Jimbo langu, ambazo zimekuwa kero ya usafiri na uchukuzi wa mazao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Chai, Kahawa, Hiliki, Mboga na Matunda na kadhalika. Barabara hizo ni Korogwe - Dindira, Kwameta - Dindira, Msambazi - Lutindi - Kwabuluu na barabara kuu ya Segera - Mkomazi. Matengenezo ya barabara hizi yataibua uchumi uliolala katika maeneo ya Jimbo la Korogwe Magharibi, Wilaya na Mkoa wa Tanga kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba Mheshimiwa Waziri asichoke kwa maombi yetu ya mara kwa mara na pindi ifikapo Bajeti ya 2005/2006 pia aendelee kutusaidia katika barabara hizi zifikie kiwango cha changarawe zote na ile ya lami iendelee kuimarishwa. Naomba nichukue nafasi hii pia kuishukuru Wizara kwa kutupatia majengo ya *JBG* Mombo kwa ajili ya Shule ya Sekondari .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe msisitizo kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza juu ya umuhimu wa barabara za kanda kutoka na kuishia kwenye maeneo ya soko lengwa, pamoja na kupunguza umbali chini ya mfumo huu wa utandawazi. Pia nishauri juuya ujenzi wa nyumba za Serikali hapa Dodoma na maeneo mengine vyema kuwa na mpangilio na mtazamo wa muda mrefu juu ya matumizi bora ya maeneo kwa kuwa na mchanganyiko wa aina ya nyumba zinazojengwa. Mfano, *bungalows* na ghorofa na vile vile kutenga *business centers*, sehemu za burudani, shule, ibada na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa na mimi ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuzungumza ukiachilia mbali kujibu maswali. Naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Morogoro Kusini, niwape pole wale Wabunge wote ambao wamepata maafa mbalimbali na hasa kwa familia na wananchi wa Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Baada ya pole hizo, nataka niwape hongera wenzetu wote waliopata nyadhifa mbalimbali na hasa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella ambaye amekuwa Rais wa Bunge la Afrika na Ndugu Mchumo ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa *Common Fund for Commodities (CFU)* ya *World Trade Organization*. Hicho ni cheo kipya kimeongezeka katika Tanzania. Nawapa pongezi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bila ya Waheshimiwa Wabunge nadhani Wizara yetu ingeyumba sana. Ni ninyi mnaotusaidia, ni ninyi mnaotuweka sawa. Kwa hiyo, tunaweza na sisi huku

tukaongozwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri kwamba twende hivi, tufanye hivi. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini niwashukuru Watendaji wa Wizara ya Ujenzi, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara wote na wengine wote na mno mno nimshukuru Mheshimiwa John Magufuli. Yeye ndiye mwenye kutuweka sawa pale Wizarani. Lakini kazi yake anafanya kwa ushirikiano sana. Nadhani asingeshirikiana hivyo labda tungeyumba yumba sana. *(Makofi)*

Baada ya hapo mimi nitamsaidia Mheshimiwa Waziri kwa kujibu hoja za watu waliochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Zilizobakia zote atajibu Mheshimiwa Waziri na nitachangia vitu vingine ambavyo nimeona ni muhimu.

Mheshimiwa Benedict Losurutia, yeye kabla hajaondoka alisema anaunga mkono, aliniaga na akasema suala la barabara nyumba yake kuwekewa X afanyeje, amekubali kama Mbunge. Kwa hiyo, tuendeleo isipokuwa anaomba kabisa barabara isipindishwe pale ambapo imenyooshwa ipite tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Faustine Rwilomba, yeye alizungumzia juu ya barabara ya Chipingo-Butundwe haijakamilika. Ni sehemu ya barabara ya Mkoa inayoanzia Chibingo kwenda Bukondwe yenye jumla ya kilometa 39.

Barabara hii imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi pamoja na ukarabati kuanzia mwaka 2002/2003 na mwaka 2003/2004 ambapo jumla ya kilometa 15 kutoka Chibingo - Nyasembe - Chigunga zimeshatengenezwa kwa gharama ya shilingi milioni 120 na itaendelea kufanyiwa matengenezo mwaka huu tumeipangia shilingi milioni 50 bila shaka Mheshimiwa Mbunge ameiona.

Mheshimiwa Maria Watondoha, yeye alikuwa anazungumzia daraja la Nyangao anasema daraja hilo lijengwe. Daraja la Nyangao ni la muda, daraja hili lilifungwa mwezi Mei, 2004 baada ya kuharibiwa na gari. Hata hivyo, daraja hili lilifunguliwa baada ya muda mfupi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, uimarishaji wa kingo za daraja hili unakusudiwa kufanywa kwa hiyo, litakuwa daraja kamili kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Chipite lililopo kwenye barabara kuu ya Mtwara - Masasi liliathirika kwa mafuriko ya mwaka 1990. Katika mwaka huu wa 2004/2005, makalvati makubwa sita yatajengwa kwenye eneo hili ikiwa ni pamoja na kuinua tuta na kutengeneza kipande cha barabara kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja lililopo kwenye mchepuo wa barabara sehemu ya Nangoo ni daraja la muda na linapitika vizuri. Serikali bado haijapata fedha za kujenga daraja la kudumu eneo lililobomolewa na mafuriko ya mwaka 1990 yaliyoikumba eneo hilo. Hata hivyo, ili kuimarisha usalama wa eneo hilo pamoja na kuwepo alama za kuongoza magari, hatua zaidi zitachukuliwa na kuwekwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yote yaliyotajwa hapo juu ikiwa ni pamoja na daraja la Nyangao yamezingatiwa wakati wa upembuzi yakinifu uliokamilika Januari, 2004 ya barabara ya Mtwara - *Mambabay*. (Makofi)

Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, yeye amezungumzia suala ambalo tayari limeshajibiwa sana la *STABEX*. Nadhani sasa suala la *STABEX* kwa Waheshimiwa Wabunge limekaa sawa.

Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, alizungumzia barabara ya Kibororoni iwekewe matuta. Sehemu ya Kibororoni uelekeo wa Mjini Moshi una matuta matano na eneo linalozungumziwa na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo ni lile la uelekeo wa kwenda Himo. Eneo hili liliwekewa jumla ya alama sita za kupunguza mwendo wa magari kufikia kilometa 50 kwa saa lakini alama hizo zote zimeibiwa na kubaki mbili tu. Kwa vile uwekaji matuta zaidi utafanya barabara hii kukosa sifa za kusudio la kuitwa barabara kuu, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara itazijenga tena alama zilizoibiwa.

Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, alitaka daraja la Mto Sibiti lijengwe, barabara ya Makuyuni-Odioni-Lalago imeahidiwa kujengwa katika Ilani ya Uchaguzi na ameshukuru Makuyuni na Ngorongoro imejengwa. Uchunguzi wa awali uliofanyika umebaini kuwa bonde la Mto Sibiti lina upana wa zaidi ya kilometa tano ambazo zitahitaji kujengwa tuta na madaraja mengi makubwa. Kutokana na daraja kubwa ya ujenzi wa tatu hilo na madaraja husika, itakuwa vigumu kutekeleza mradi huo hivi karibuni kutokana na uwezo wa Serikali uliopo. Serikali itaendelea na juhudi zake za kutafuta wafadhili wakati matengenezo ya kawaida na maalum yanaendelea kwenye barabara zilizopo kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Lekule Laizer, yeye amesema barabara ya Rombo - Kamangwa izunguke hadi Olmoluk - Ngaranairobi. Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaoendelea sasa unaanzia Kamangwa unakwenda Tarekea hadi Marangu. Kwa sasa hivi hakuna mpango wa kuendelea kujenga barabara hiyo hadi Sanya Juu kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme, yeye alisema miradi mingi iliyopangwa kutekelezwa katika mpango wa *Mtwara Development Corridor* haitekelezwi mfano barabara ya Mtwara - Masasi - *Mamba Bay* hatuelewi imefika wapi, vile vile ujenzi wa *unit bridge* hatujui umefikia wapi. Bahati nzuri kwenye hotuba ya Waziri, maelezo haya yako wazi kabisa, nadhani Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme, ameyaona.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, yeye alikuwa anazungumzia barabara ya Dodoma - Itigi - Tabora itengewe fedha. Sehemu ya barabara iliyotajwa kati ya Dodoma na Manyoni imeshatengewa fedha na imejengwa kwa kiwango cha lami chini ya mpango maalum wa barabara kuu unaotekelezwa kwa kutumia fedha za ndani. Sehemu ya Manyoni - Itigi - Tabora imefanyiwa usanifu wa kina mwaka 1998 kwa lengo la kujengwa kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo ya kutenga fedha za ndani ili sehemu hii iliyobaki iweze kujengwa.

Mheshimiwa Anne Makinda, yeye alikuwa anazungumzia alama za X, Njombe. Naomba suala la X kwa Njombe naomba litazamwe kwani nyumba zile zimejengwa kabla mimi sijazaliwa yaani yeye. Wakoloni walithamini mwaka 1947 nyumba zikasogezwa pembeni mwaka 1956 ikaja tena Serikali hiyo hiyo ya Wakoloni wakatoa ramani ndio hizo nyumba ambazo sasa zimewekewa X.

Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 imetaja barabara inayopita mjini Njombe kuelekea Songea kuwa na upana wa hifadhi ya barabara ya mita 45. Mawasiliano yanaendelea kati ya Wizara ya Ujenzi, *TANROADS* Ruvuma na Iringa pamoja na uongozi wa Mkoa wa Iringa kubainisha upana wa barabara utakaokubalika kwa kuzingatia kuwa sheria ya barabara inaheshimu pia michoro au ramani za miji.

Mheshimiwa Robert Mashalla, wakati anachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye alizungumzia barabara ya Ushirombo - Bulembela iharakishwe. Wizara ya Ujenzi itatenga fedha kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 ambayo ameiona kwa ajili ya kufanyia matengenezo sehemu korofi barabara ya Bukombe - Ipalamasa hadi Busereresere. Barabara hiyo inaunganisha Wilaya ya Bukombe na Geita. Katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu itatenga shilingi milioni 108, naamini Mheshimiwa Mbunge ameiona. Hili ni moja nilitaka kulizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kusisitiza juu ya alama za X ambazo Wizara ya Ujenzi inaamini sasa Waheshimiwa Wabunge wameelewa vizuri na wananchi wameelewa vizuri. Niliona katika *television* wananchi wa Dar es Salaam wakilalamika kwa kutokuelewa tangazo tulilolitoa kwamba tumetoa tangazo na tumesema kwa ubinadamu sasa tunasimama, hapana. Hatukutoa tangazo, hivyo tulichokisema ni kwamba kwa sababu ya ubinadamu na kwa kuelewa Chama cha Mapinduzi kinajali watu wake na Serikali yake inasikiliza maoni ya wawakilishi wake tunatia alama za X nchi nzima lakini hatutabomoa nyumba ama vibanda pale ambapo hatuna pesa za kutimiza mradi huo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni vizuri likaeleweka vizuri lakini pale ambapo tunazo pesa za kutekeleza mradi huo, tunawaomba wananchi wabomoe na wananchi wa barabara ya Mandela pesa zipo tunataka kutekeleza mradi huo kwa hiyo tunawaomba wananchi wale wabomoe nyumba zao na vibanda vyao sisi tuko tayari kutekeleza mradi ule. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ambalo Wabunge wengi wamekuja kufuatilia ni kuhoji ni kwa nini Makandarasi wa Tanzania hawapati kazi tunawapa wa nje. Kweli kabisa Makandarasi wa Tanzania ni wengi sana kulikoni wa nje lakini wa Tanzania ni wadhaifu katika mambo yafuatayo, hawana mitambo ya kutosha ya kufanyia kazi, pia hawana pesa za kutosha za kufanyia kazi.

Tunawaomba na mimi hapa rasmi kabisa ninawaomba Makandarasi wa Tanzania waungane, wakitaka tuwape kazi hata kwa upandeleo waungane. Hii kuungana kwa Makandarasi watatu, wanne, watano kutafupisha rushwa katika biashara ya ujenzi wa



barabara kwa sababu Wakandarasi watatu, wanne, watano, walioungana sio rahisi kutoa rushwa kwa ma-*engineer*, lakini Makandarasi wetu hawataki kuungana, kwa misingi hiyo wanakosa kazi muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la muhimu kabisa ni juu ya mafunzo ya Makandarasi. Wabunge wengi wameuliza hizi pesa nyingi mnaotoa mafunzo kwa Wakandarasi pesa zitakwenda wapi? Mafunzo ya Makandarasi sio kwamba tuna chuo cha kuwafundisha Makandarasi, hapana. Fedha hizi zinatumiwa kwa mafunzo kwa vitendo kwa Makandarasi waliokuwa wameteuliwa na *Tanzania Civil Engineering Contractors Association (TACECA)* wao kwa kushirikiana na *National Construction Council* wanateua Makandarasi na kuwapa uwezo wa kuwafundisha hao Makandarasi wapya.

Kwa hiyo, hatuna chuo, tunatenga pesa kujaribu kufanya *capacity building* kwa Makandarasi wetu nchini wapate mafunzo ya uhakika hatutumii hizi kwa chuo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema hapa kwamba Mheshimiwa Waziri yeye ndiye atakuja kujibu hoja hapa na hoja ni nyingi mno mliochangia mko sitini na bado kuna muda wangu?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Dakika ngapi?

**MBUNGE FULANI:** Tano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Tatu?

**MWENYEKITI:** Naomba ufuate maelekezo ya Mwenyekiti.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Naam, Mwenyekiti bado nina muda?

**MWENYEKITI:** Usiongee na mtu mwingine endelea, bado una dakika kama tano hivi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Huku nina mashabiki huko Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dakika zilizobakia naomba nizungumzie ramani iliyokuwepo kwenye kitabu chetu cha nyongeza, *corridors*. *Corridors* hizi tumezipanga kwa madhumuni makusudi kabisa kwamba wenzetu Afrika ya Kusini wanakuja mbio tayari wameshaunda chombo kupitia *National Development Bank of South Africa* ambayo ndio inayoendesha *Maputo Corridor*, *Angola Corridor*, *Mtwara Corridor* wanataka kusikia yote lakini biashara kubwa wote tunayogombea ni biashara ya Kongo. Wao wanataka kuja kuchukua biashara zote kutoka Kaskazini ndio maana na sisi

tumetengeneza hii kuhakikisha tunafungua *Western Tanzania* na sisi tuingie huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hii wao wamekwishajitayarisha kule wakati sisi tunalilia kufungua ofisi hapa ya Mtwara wao tayari wana Mratibu wa *Mtwara Corridor in South Africa*. Wanachoogopa kuja huku kuchukua hiyo *Mtwara Office* ni kwamba *Mtwara Corridor* iko ndani ya Serikali, ama sivyo tayari wangeshakuja kuchukua hiyo.

Mwaka huu wao wana-*finance* mkutano Tanzania, watalipia kila kitu wa kuzungumzia *corridor* na huu ni utandawazi, huwezi kuepuka ukitaka kuepuka njia ni hii lazima tupange pesa za kufungua barabara zetu. Hii ndio njia pekee ya kushindana nao huwezi vinginevyo huwezi kushinda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wana *National Bank* tangu mwaka 1978 inafanya kazi hiyo, sisi hatuna hata kama tunayo ni changa. Hii jitihada ambayo Serikali inafanya ni jitihada ya hakika kabisa ya kukabili utandawazi na Waheshimiwa Wabunge jambo hili naomba kabisa mlizingatie, huyu sungura mdogo lazima atusaidie kufungua barabara katika Tanzania kwa *corridor* hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanajua *corridor* tatu tu huku. Wanajua *Mtwara Corridor*, *Central Corridor* na wanayo *TAZARA Corridor* katika mipango yao kwa kutumia reli ya *TAZARA*. Sasa sisi tumeendeleza kuweka *corridors* tisa Tanzania hii inaweza kufunguka kwa barabara na tunapofika mwaka 2012 tuna uhakika kama Tanzania itaendelea katika muundo huu barabara zote za Mikoza zitakuwa zinapitika kwa kiwango cha lami. Kwa kufanya hivyo, utapunguza umaskini kwa kiwango kikubwa sana. Chakula kitatembea kila mahali hakutakuwa na sababu ya kuwa na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyoona hoja ni nyingi sana ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na inawezekana ikawa vigumu sana kuzijibu hoja zote kwa dakika 45 nilizopewa ambazo nataka niyaeleze haya yote.

Hata hivyo, nitazungumza kwa jumla yale nitayayoyagusia yatakuwa pia yamegusa kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini napenda kuahidi kwamba zile hoja zao zote ambazo zimetolewa hapa kwa kuzungumza, kwa maandishi zote tutazijibu na baadaye tutazileta kwenye *pamphlet* na kuwagawia Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Wizara ya Ujenzi imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu walichangia Wabunge 11,

kupitia Ofisi ya Mipango na Ubinafisishaji walichangia Wabunge 15, TAMISEMI walichangia Wabunge 3 kwa sababu hawa wameshatajwa, nisingependa kuwataja majina yao.

Waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 67 na waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge 17. Labda nianze kwa kuwatambua hawa waliochangia kwa maandishi haraka haraka. Nao ni Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Cheyo, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura.

Wengine ni Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Dr. Alex Msekela, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Ameir na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Lucasa Seleli, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Juma Khatib Mohamed, Mheshimiwa Said Athumani, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Geogre Kahama, Mheshimiwa Jackson Makwetta na wa mwisho alikuwa Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza hapa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Alhaj Abdallah Shawaji, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Oscar

Mloka, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru wote kama nilivyosema kwamba nitajitahidi kuzungumza kwa ujumla lakini ninajua yale yote ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni ya msingi na tumeyazingatia katika kuhakikisha kwamba tunaendeleza mtandao wa barabara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyotoa taarifa zetu nia kubwa ya Wizara ya Ujenzi na Serikali kwa ujumla ni kuhakikisha kwamba barabara zote katika nchi hii ifikapo mwaka 2012 zinatengenezwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mwaka 2012 kwa kuzingatia hali halisi ya sasa hivi inavyoendelea kwa sababu tumeeleza hali ya barabara zilivyokuwa kwenye mwaka 1961 kwamba tulikuwa na kilometa 1300 sasa hivi tuna jumla ya kilometa 4800. Kwa hiyo, tunategemea katika *rate* hii na hasa baada ya kutenga fedha zetu wenyewe katika kuhakikisha kwamba tunatengeneza barabara ambazo kwa kweli hata wafadhili wameanza kutuheshimu na kujua kwamba kweli Tanzania tunaweza kufanya hivi. Kwa sababu hata barabara hii ya *Central Corridor* siku nyingi tumekuwa tukiomba wafadhili wametunyima lakini tulipoamua kujenga wenyewe sasa hivi na fedha zao zimeanza kupatikana kwa urahisi na huo ndio ukweli. Ninaamini hatua ambazo tumeanza kuzichukua katika kuhakikisha kwamba tunatengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami zitatusaidia katika kufungua *corridor* tisa ambazo tunaamini zitaongeza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba utengenezaji wa barabara una gharama kubwa. Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilometa moja ina-*cost* kati ya shilingi milioni 200-300 inategemea na barabara yenye iko mahali gani. Lakini tumegundua tunapojenga barabara kwa *design and build* yaani wakati huo unafanya *design* na wakati huo huo unajenga ile kwanza inakuwa na gharama kidogo lakini pia inapunguza muda wa kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara mfano ya kutoka Singida - Shelui yenye urefu wa kilometa 110 tumeisubiri tangu mwaka 1987 wakati *feasibility study* ilipofanywa na *World Bank* lakini mpaka leo hakuna kandarasi lakini kwenye barabara ya kutoka Singida - Manyoni - Dodoma ambapo tumeamua kutumia fedha zetu katika miaka miwili iliyopita sasa kuna Makandarasi na kazi zitakamilika katika kipindi cha miaka miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha ni kwa namna gani tunatakiwa kuwa na fedha zetu badala ya kila siku kusubiri mfadhili, wafadhili ni wazuri lakini sio kila siku tuwategeme wao ni lazima na sisi tuwaonyeshe ni namna gani tunaweza kutumia *resources* zetu katika kutengeneza barabara zetu na ndio maana Mheshimiwa Benjamin Mkapa kila siku amekuwa akikazania mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akiingia madarakani mapato kwa mwezi yalikuwa shilingi bilioni 25, kwa miezi miwili iliyopita mapato yalikuwa bilioni 136 kwa mwezi. Mapato hayo ndio yaliyotuwzesha kuwa zinatengwa fedha za barabara. Katika Bajeti ya mwaka 2000/2001 zilitengwa bilioni 11, katika Bajeti iliyofuata ya mwaka 2002/2003 zilitengwa bilioni 22, katika mwaka uliofuata 2003/2004 zilitengwa bilioni 32 mwaka huu zimetengwa bilioni 49.95 kwa ajili ya ujenzi wetu pamoja na kutegemea wafadhili pamoja na miradi mingine.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nia iko pale kwamba tuna uhakika kama mambo yataenda vizuri, kama mapato yataendelea hivi, kama *commitment* ya ninyi Waheshimiwa Wabunge mlionayo sasa itaendelea hivi hivi na bahati nzuri mkarudi hawa hawa, nina uhakika barabara nyingi zitakamilika zikitengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa *suggestion* na mapendekezo, nia ya kuhakikisha kwamba tunafungua *corridor* zote zikiendana na uchumi wa kijiografia tumezingatia sana. Kwa mfano, tumezingatia kwamba kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba barabara ya kutoka Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Biharamulo - Mtukura - Kampala inatengenezwa kwa kiwango cha lami na ndio maana mtaona madaraja yote 11 ya kutoka Tunduma - Sumbawanga yamekamilika na yanategemewa kufunguliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Julai, 2004, yale ni mafanikio. Katika Bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kufanya *design* pamoja na *feasibility study* katika barabara yote hadi Nyakanazi ambayo ndio ilikuwa imebakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeamua kuzingatia umuhimu wa *corridor* moja ambayo ilikuwa imesahaulikasahaulika hivi ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi hii nayo ni ya kutoka Dodoma - Itigi - Igalula kwa Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Tabora - Kaliua - Malagarasi - Kigoma. Ile barabara nayo ni muhimu na kwa sasa hivi kuna kandarasi ambaye anatengeneza tuta ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.5 zinatumiwa kutokana na Bajeti ya mwaka 2003/2004. Lakini katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 tumetenga fedha, barabara hiyo yote inafanyiwa *design* ili kusudi nayo itengenezwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Lakini tumeamua pia ile sehemu ya kutoka Arusha - Minjingu - Babati - Singida na ile ya kutoka Babati - Dodoma - Iringa ile nayo tumepata fedha za kuanza *design* pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami. Ni kweli kabisa barabara hii hatukuweza kuishughulikia na Mheshimiwa Pascal Degera, amezungumza kwamba mwaka 1993 ilifanyiwa *feasibility study* sasa mwaka 1993 ni barabara nyingi tu zilikuwa hazijatengenezwa hata Daraja la Mkapa halikuwepo, mimi nilikuwa bado shuleni Chuo Kikuu mwaka 1993, barabara za kwenda Mtwara hazikuwepo wala zilikuwa hazijengwi, barabara ya Dodoma - Manyoni - Singida hazikuwepo. Kwa hiyo, tusizungumzie ya mwaka 1993 tuzungumzie 2004. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 tumetenga shilingi milioni 1,500 kwa ajili ya kuanza kufanya *design* na mimi namhakikishia

Mheshimiwa Pascal Degera mwaka 1993 zilitengwa kwa ajili ya *feasibility study*, *feasibility study* ni ku-*prove* kama *economically* ni *viable* au sio *viable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 1.5 na fedha hizi zipo na tenda zitatangazwa ili wakishamaliza kufanya *design* ujenzi uanze. Ndio maana katika taarifa yangu ambayo nimeisaini na nitakuwa radhi kushtakiwa na Mheshimiwa Pascal Degera kama haitatekelezwa tumesema barabara ya kutoka Minjingu - Dodoma - Iringa itakamilika katika kipindi cha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pascal Degera, mimi huwa sina tabia ya kudanganya hasa kudanganya wazee kama wewe mwenye mvi, nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Pascal Degera barabara hii itatengenezwa. Ndio maana tunajenga nyumba 300, ndio maana tunajenga barabara ya kutoka Dodoma - Manyoni tumetumia zaidi ya shilingi bilioni 65 na ndio maana tunaunganisha kutoka Manyoni hadi Singida zaidi ya shilingi bilioni 40 zinatumiwa na ndio maana tumetangaza hata *tender* na kandarasi sasa yuko kwenye *site* kwa ajili ya *re-ceiling* nyingine ya kutoka Dodoma - Morogoro kuna zaidi ya shilingi bilioni 27 zinatumiwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nataka kuhakikishia Mheshimiwa Pascal Degera, barabara ya kutoka Minjingu - Babati - Farkwa ambapo ni sehemu za kijijini kwako kule kwenye matetemeko mengi kupitia Dodoma kuna shilingi bilioni 1.5 ambazo zimetengwa wataanza kufanya *design* na *design* ikashamaliza ujenzi utanza. Fedha zile zipo zimetolewa na Benki ya Dunia katika mkataba ambao umesainiwa na Benki ya Dunia zaidi ya shilingi bilioni 123 zimepitishwa mwezi Mei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumetenga zaidi ya shilingi milioni 900 kuanza kufanya *design* kutoka Dodoma - Iringa kupitia Mtera kwa hiyo, hizo fedha nazo zipo na *tender* zitatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumetenga shilingi milioni 740 za kuunganisha ile sehemu ya Singida ambayo inatengenezwa kwa kiwango cha lami kuja huku iunganishe na Hanang kwenye Babati. *Feasibility study* imekamilika mwaka 2003 na kwa sasa hivi zimetangazwa *tender* kwa ajili ya kufanya *design*. Nataka kuthibitisha kwamba hiyo sehemu itatengenezwa kwa kiwango cha lami na natumaini yetu hiyo sehemu itakamilika kama tulivyopanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia sehemu nyingi kwa hiyo, napenda niseme hata ile *lake circuit* ya kutoka Usagara - Sengerema - Geita - Biharamulo na Geita - Bwanga - Kyamolo ile sehemu nayo itatengenezwa kwa kiwango cha lami kwa *design and build*. *Tender* zimeshatangazwa na tuna uhakika kuanzia mwaka huu Makandarasi wataanza kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunajitahidi katika kila sehemu iweze kuunganika kwa lami. Mambo ya kukaa tunazungumza changarawe, changarawe, yamepitwa na wakati sasa tubadilike tuanze kuzungumzia lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Serikali yetu uwezo tunao na ndio maana tumeweza kutoa *summaries* ya barabara ambazo zimetengenezwa katika Awamu ya Tatu zenye jumla ya shilingi bilioni 227 lakini zile zinazoendelea ni shilingi bilioni 998 ndizo bado zinaendelea kujengwa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba ile miradi yote ambayo tumeitaja na bahati nzuri imefafanuliwa vizuri katika vitabu vyetu itaendelea kutengenezwa ikiwa ni pamoja na barabara nyingine za kwenda mpaka Mahenge.

Katika *plan* zetu tunataka Mahenge isikae tu ime-*hang* pale, Mahenge ni lazima iendelee kutokana na *suggestion* ambazo mara nyingi zimetolewa na Mheshimiwa Jackson Makwetta, ziunganishe, aidha, Tunduru au Songea. Hapo ndipo utakuwa unazungumzia juu ya *communication* na kuhakikisha kwamba *transport corridors* zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda unakwenda haraka, lakini labda nianze tu kujibu kwa haraka haraka. Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu alitoa ushauri, tunashukuru ushauri wao tutauzingatia na tutaufanyia kazi. Mara nyingi wamekuwa wakitoa ushauri mzuri sana na mimi napenda niahidi ushauri huu tunauzingatia na umekuwa na faida sana kwetu sisi Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa mara ya kwanza, leo nashukuru kwamba amepongeza. Hii inaonyesha ni kwa namna gani ameweza kujifunza haraka. Kwa hiyo, tuna mategemeo kwa kadri anavyojifunza hivi ataanza kujifunza sera za CCM ili kusudi miaka inayokuja aweze kujiunga nasi. Lakini amezungumza kitu kimoja kwamba amefurahishwa sana na kitendo cha kujenga nyumba na hasa katika kujenga nyumba hapa Dodoma zile mia tatu na angeshauri kwamba ziendeleo kujengwa hapa Dodoma kwa sababu ni Makao Makuu ya Serikali na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ombi kwa Waziri Kivuli kwa sababu bahati nzuri Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali lakini ni Makao Makuu pia ya Chama cha Mapinduzi, basi ni washauri na wenzetu wa Upinzani *CUF*, *NCCR* na kadhalika kwa vile wanakumbuka kwamba Dodoma ni Makao Makuu na wao ofisi zao wazihamishie hapa Makao Makuu Dodoma badala ya kuwa wanazungumza tu wakati wao ofisi zao zipo miembeni na kwingineko.

Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mwakilishi wa Upinzani na nina hakika atamshauri Mwenyekiti wake afungue ofisi yake hapa ili kusudi tuweze kupambana pamoja katika kuendeleza Makao Makuu Dodoma, badala ya wao kuwa wa kwanza kuilaumu Serikali haijahamia Dodoma wakati na wao hawajahamia Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa pia amezungumzia kuhusu uzito wa magari na kadhalika. Ushauri wake kwa ujumla wote ni mzuri na tunauzingatia. Ametoa *challenge* ya kwamba haitawezekana barabara ya kutengenezwa kufika mwaka 2005/2006 kutoka Kagera au Mwanza hadi Mtwara. Mimi nataka nimhakikishie tu na nimtoe wasiwasi kwamba hiyo sehemu katika kufika mwaka 2005/2006 itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami. Labda nimhakikishie kwa hili, kutoka Mtukula hadi

Kagoma kilometa 112 ujenzi utakamilika mwezi Julai hadi Agosti, 2004 na kutoka Kagoma hadi Muhutwe umeshakamilika. Kutoka Kagoma kuja Muleba kwa Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwenda Biharamulo kwa Mheshimiwa Anatory Choya hadi Nyakahura, Mkandarasi anateuliwa mwezi huu. Kwa hiyo, kuna zaidi ya shilingi bilioni 73. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishatoka Lusahunga kuja Isaka ni lami. Nataka nimpe jiografia ya Tanzania kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka pale Isaka kwenda Tinde hadi Nzega kuna Mkandarasi, kuna zaidi ya shilingi bilioni 59, zimetolewa na *European Union*, kuna kampuni inafanya kazi na Mheshimiwa Rais miezi miwili iliyopita alikwenda kuweka jiwe la msingi. Kutoka Nzega hadi Shelui kilometa 108, kuna kampuni ya Kichina ambayo inategemewa kumaliza kazi hiyo mwezi Desemba kwa kujenga kwa kiwango cha lami na kuna shilingi bilioni 21 zimetolewa. Kutoka Shelui hadi Singida kuna fedha zimetolewa na *World Bank* shilingi bilioni 50 na sasa hivi tumeshateua Mkandarasi na tumeigawanya hiyo sehemu katika sehemu tatu. Kutoka Singida hadi Manyoni kilometa 119, Mheshimiwa Rais miezi miwili iliyopita aliweka jiwe la msingi. Kuna shilingi bilioni 40 zinatumiwa, fedha hizi zimetolewa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Manyoni hadi Dodoma kuna Kampuni ya *KONOIKE* inafanya kazi unaweza ukaenda ukaiona kuna shilingi bilioni 67 zinatumiwa. Kutoka Dodoma hadi Morogoro kuna shilingi bilioni 27 na Mkandarasi yupo na michoro unaiona ukitoka Dar es Salaam. Kutoka Morogoro hadi Chalinze kuna Kampuni ya *NCC* shilingi bilioni 37 zinatumiwa kutoka Denmark. Dar es Salaam hadi Mlandizi imeshakamilika. Kutoka Dar es Salaam kwenda Kitonga kuna Mkandarasi. Kutoka pale Kitonga hadi Ndundu kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni 20 zimetengwa na Mkandarasi yupo kule. Daraja la Mkapa limekamilika na shilingi bilioni 35 zimetumiwa. Kutoka pale kwenye Daraja la Mkapa ambalo lina urefu wa kilometa 13.9 kuanzia Ndundu pale hadi Somanga kilometa 60, kuna fedha zimetolewa shilingi bilioni 11.5 na *design* zimeshaanza kwa ajili ya ujenzi wa lami.

Kutoka Somanga hadi Matandu kuna shilingi bilioni 13.5, zimetolewa na Serikali na Mkandarasi yupo. Kutoka Nangurukuru hadi Mbwemkuru kuna kampuni ya China inafanya kazi pale, kuna shilingi bilioni 39. Kutoka Mbwemkuru hadi Lindi - Mingoyo kilometa 95 kuna kampuni ya *MA CARAS* inafanya kazi. Kutoka pale Mingoyo hadi Mtwara kuna lami. Sasa hujaamini kwamba mwaka 2005 itakuwa imekamilika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushauri Mheshimiwa Waziri Kivuli ukawaeleze viongozi wako wa Vyama vya Upinzani kwamba hii sio *agenda* kwa sababu hii *agenda* imeshakamilika, watafute *agenda* nyingine kwa sababu barabara itakamilika na mimi nakuomba mashaka yale yaondoke kabisa Mheshimiwa rafiki yangu, barabara ile itakamilika. Hii ikikamilika itaongeza kilometa 6,500 na zingine zikishakamilika zitaongeza kilometa 8,500 na mwaka 2012, kilometa zote 10,300 zitakuwa zimekamilika



kwa lami na wewe utapita kwenye barabara ya lami kwenda kwenye nchi yoyote Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje wa Mpwapwa ametoa pongezi nyingi, amezungumzia kuhusu barabara yake ya kutoka Minjingu kuja Babati hadi Dodoma. Kama nilivyozungumza kuna shilingi bilioni 1.5 tumezitenga kwenye Bajeti hii. Ni kwa bahati mbaya sana kwenye kitabu chetu cha Hazina waliandika milioni kumi tu, hawakuandika ile shilingi bilioni 1.5. Kwa hiyo, wakati wa Kamati tutarekebisha lile na bahati nzuri watu wa Wizara ya Fedha wanafahamu. Kutoka Dodoma hadi Iringa kuna shilingi milioni 900 kama nilivyozungumza na hizi fedha ndiyo zinajumlisha Bajeti yote ya Wizara ya Ujenzi ya *287 billion point something*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lile daraja ambalo amelizungumza kwamba ni lazima tulitengeneze. Mheshimiwa George Lubeleje, ndugu yangu, ningependa tu nikushauri kwa sababu katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 Tawala za Mikoa watapata shilingi bilioni 21 zinazotokana na *Road Fund* unaweza kupeleka maombi maalum kwenye hilo daraja ulilolitaja ambalo lipo chini ya Halmashauri ya Wilaya liweze kutengenezwa na nina uhakika wenzetu wa Tawala za Mikoa watalizingatia hili ili kusudi daraja lile liweze kutengenezwa.

Sisi Wizara ya Ujenzi mtuache tung'ang'anie ile barabara ya kutoka Babati kuja Dodoma. Sasa hako kadaraja kadogo tuwaachie Tawala za Mikoa nao washughulike nacho kwa sababu kila kitu huwa kina mgawanyo wake. Kwa hiyo, hilo tu ningeweza kusema hivyo pamoja na kwamba ulisema nisizungumze chochote. Kwa bahati mbaya hilo lipo chini ya Wizara nyingine, hata ukiitoa shilingi utakuwa umenionea, kwa sababu halihusiki kabisa na mimi. Kwa hiyo, hilo daraja la Godegode nina uhakika kwa sababu Serikali ni moja, wenzetu wa Tawala za Mikoa watakuwa wamelizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *Captain* Theodos Kasapira, amezungumzia kwamba Bajeti ni nzuri na amefurahi tumewapa mapema na sisi tunawashukuru. Amezungumzia juu ya barabara zake, ni kweli kuna sehemu ya barabara ambayo tumeitengea fedha kwa ajili ya kutengeneza kwa kiwango cha lami pamoja na pale kwenye milima ambapo kumekuwa na matatizo makubwa sana, napo tumetenga fedha ili patengenezwe kwa kiwango cha lami.

Kama nilivyosema kwa kweli nia yetu kwa siku zijazo na nafikiri mwaka huu tukiweza kupata fedha kiasi kidogo tutawatuma wataalam wetu wakaanze kufanya sasa utafiti wa kuunganisha Mahenge na Mkoa wa Ruvuma kwa sababu ukiangalia kwenye ramani zetu pale pame-*hang* tu huwezi kutengeneza barabara ya Mkoa au ya Kitaifa halafu ikabaki barabarani tu, ni lazima sasa tubadilishe mwelekeo kama ulikuwa ni mwelekeo wa kikoloni basi tubadilishe tuweke mwelekeo wa Kitanzania, wa ki-CCM, CCM katika kuhakikisha kwamba nchi yote inaunganika. Kwa hiyo, hili tutalizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumzia pia kwamba angalau nitamke tu siku zijazo patatengenezwa daraja la Kilombero. Kwa sababu ni kutamka nina uhakika hata

kwenye daraja la Mkapa walitamka tangu mwaka 1961, sasa kama unataka nitamke tu mimi nina uhakika siku moja pale Kilombero patakuja kutokea daraja kutokana na hali halisi ya fedha zitakavyopatikana. Lakini kwa sasa hivi kuna kivuko ambacho tumekinunua chenye thamani ya shilingi bilioni 1 na kinafanya kazi nzuri na siku ya uzinduzi Mheshimiwa *Captain* Theodos Kasapira, yeye mwenyewe alikuwepo na wale wazee Machifu na wakasema ajali haitatokea na kweli tangu siku hiyo ajali haijatokea. Kwa hiyo, tunaamini hiki kivuko kitatumika vizuri wakati Serikali ikiangalia uwezekano wa kupata fedha huko baadaye za kuweza kutengeneza daraja. Siwezi kuahidi lakini uwezekano huo upo na hasa baada ya kufungua barabara ya kutoka Mahenge kwenda Tunduru au kwenda Songea au kwenda mahali pengine popote. Kwa hiyo, uwezekano huo upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paschal Degera kama nilivyozungumza kwamba kuna shilingi bilioni 1.5, nisingeweza kuzungumza uongo hapa mbele ya bosi wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye yupo hapa kwa sababu nitaweza kufukuzwa kazi.

Kwa hiyo, nakuhakikishia kuna shilingi bilioni 1.5 mwaka huu, kwenye kitabu mle tutarekebisha. Kwa hiyo, usitoe hata shilingi lakini kwenye mwaka 1993 bahati nzuri sikutegemea hata kugombea Ubunge, nimesema nilikuwa bado nipo shuleni, kwa hiyo, kama kuna makosa yalifanyika mwaka 1993, tuwasamehe walioyafanya. Lakini nia kwa sababu ule upembuzi yakinifu uliofanywa ndio umeleta hii kupata fedha za kufanya *design* mimi nafikiri ni katika *continuity* ya kazi zinafanywa na Serikali ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, amezungumzia kuhusu barabara yake ya Ikizu-Nyamswa imetengewa fedha anashukuru na kadhalika. Amezungumzia pia juu ya barabara ya Kyabari-Nyamswa pamoja na *Fort Ikoma*. Ni kweli kabisa kwamba barabara hii ni muhimu kama zilivyo barabara nyingine kama alivyosema. Katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 kwanza kwenye barabara ya kutoka pale Makutano kwenda Butiama yenye jumla ya kilometa 12 tumetoa fedha zetu za Serikali shilingi bilioni 2.4 na Mkandarasi yupo kule kwa kutengeneza kwa kiwango cha lami aina ya *ottar seal*.

Tunategemea mwaka 2005 Mkandarasi yule ataweza kukamilisha ile kazi. Lakini kutoka Musoma Mjini kwenda *Fort Ikoma* ambapo kuna jumla ya kilometa 140, mwaka 2004 tumeweka fedha kwa kuanza kufanya *design*. Ni kama tulivyotengeneza barabara ya kutoka Makunyuni kwenda *Ngorongoro Gate* kilometa 77, hivyo hivyo tutatengeneza barabara ya lami kwa kutoka Musoma kwenda *Fort Ikoma* ili kusudi tu-*promote* utalii katika maeneo haya.

Kwa hiyo, ombi lako la kwamba tuanze kuweka X mapema ili wananchi wajue tutaendelea kufanya hivyo, lakini hatutawabomolea kwa sasa hivi kwa sababu ujengi hauanzi mwaka huu. Katika Bajeti ya mwaka kesho nina uhakika kama *design* itamalizika tunaweza kuweka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara yake ambayo Mheshimiwa Tembe Nyaburi, alitaka ipandishwe hadhi iwe ya Mkoa badala ya kuendelea kuwa ya Wilayani, kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri Serikali imejipangia mipango yake, kuna barabara zinazohudumiwa na Wilaya na kuna barabara zinazohudumiwa na Mkoa. Lakini kwa kutambua maendeleo mbalimbali ambayo yamekuwa yakipatikana kutokana na barabara mbalimbali za Wilaya na za Mikoa aliteuliwa *Consultant* ambaye amefanya kazi katika Mikoa yote ili kusudi zile barabara zitakazokidhi haja ya kupewa kuwa barabara za Mikoa zitapandishwa na zile barabara ambazo zitateremka hadhi kwa mfano ilikuwa ya Mkoa iteremke zitashushwa ziwe za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na Sheria ya *Highway Ordinance* ya mwaka 1969, inayosema hakuna mtu yeyote mwenye mamlaka ya kubadilisha hadhi ya barabara isipokuwa Bunge. Kwa hiyo, ile sheria ina mambo mengi pamoja na hizo *classification* za barabara, tutaileta Bungeni ili kusudi Waheshimiwa Wabunge muweze kuchangia. Kwa hiyo, kama hii barabara itatakiwa kupandishwa itapandishwa. Kama itatakiwa kuteremshwa hata iwe *feeder road* badala ya kuwa *district road* napo itakwenda hivyo. Kwa hiyo, tutegemee mabadiliko ya barabara lakini *otherwise* tutaendelea kuhakikisha barabara zilizo chini ya Mkoa zinatengenezwa kwa kutumia fedha tunazozitenga kwa kupita *Road Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Karavina ameunga mkono na amezungumzia kuhusu suala la hali halisi ya *Transport Corridors*. Tunakubaliana naye na tunakubaliana na mapendekezo hayo yote aliyoyatoa. Ni kweli kabisa kwa siku za nyuma ile *corridor* ya Tabora na Kigoma ilikuwa imesahaulika kidogo, lakini tumeiingiza katika *corridor* zote kuhakikisha kwamba lile eneo lote linaunganishwa tena katika barabara kubwa ambazo zitatengenezwa kwa lami na ndio maana mtaona katika Bajeti hii Mkoa wa Kigoma unaunganishwa na barabara karibu tatu. Kuna ile barabara ya kutoka Tunduma kwenda Kigoma, barabara ya kutoka Itigi-Tabora-Malagarasi kwenda Kigoma. Hizi zote na *trunk roads* ambazo lengo lake ni kuhakikisha zinatengenezwa katika kiwango cha lami ili ziweze kuunganisha sehemu hii.

Kwa hiyo, tutaendelea kutenga fedha, tutaendelea kukaribisha *BOT*, tutaendelea kutumia *resources* zote ambazo zitatuwezesha kuhakikisha kwamba Mikoa hii nayo inaunganishwa kwa kiwango cha lami ili iweze ku-*promote* uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kabisa kwamba tukifungua vizuri bandari ya Kigoma ile mizigo mingi ambayo inatoka kwenye nchi ya *DRC* ambayo kwa kawaida kwa mwaka mzima wao wapo, watu wanaoweza kutoa tani zaidi ya milioni 12 zitaweza kupitia kwenye barabara zetu badala ya kutegemea tu reli ambayo *capacity* yake ni karibu mizigo tani milioni mbili kwa mwaka, kitu kama hicho, sina uhakika zaidi, lakini ni ndogo ukilinganisha na mizigo inayoweza kupatikana kule.

Kwa hiyo, tutazingatia uchumi wa kijiografia na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya hapa anasema ni uzito zaidi kwa hiyo, atafafanua vizuri. Lakini lengo letu ni katika kuhakikisha kwamba wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na sisi Wizara ya Ujenzi tunashirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba mizigo ambayo

inatakiwa kusafirishwa kupitia Tanzania *whether* inapitia kwenye barabara au kwenye reli inapita kwa mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na ile bandari ya Kasanga kufungua ile kwenda mpaka *Kasanga Port* na kadhalika. Hili ndilo lengo kubwa la kuhakikisha kwamba mawasiliano yanaimarika na hivyo kujenga uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, tunakubaliana na ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, ametoa ushauri wa *drainage* na amesema katika barabara mifereji haizibuliwi. Pia ametoa pongezi kwa kuweka fedha za Mwandinga-Manyovu kwa kujenga kwa kiwango cha lami, amezungumzia kuhusu barabara ya Kigoma-Kalya. Katika barabara hii tumetenga kutoka Ilagara hadi Kalya road. Ukiangalia katika kiambatanisho namba 7(H), kuna shilingi milioni thelathini zimetengwa, lakini pia ukiangalia katika *page 106* kiambatanisho namba 6, kuna shilingi milioni 38.5.

Kwa hiyo, kuna jumla ya shilingi milioni 68 ambazo zitatumika katika kutengeneza hii barabara. Lakini kwa ujumla tunakubaliana na ushauri wake ikiwa ni pamoja na hiki kivuko cha Ilagala. Kivuko cha Ilagala ni cha kuvuta kamba na katika Bajeti yetu tumepanga kwamba katika mwaka huu angalau tukifanyie matengenezo kisiwe cha kuvuta kamba angalau kijiendeshe kwa mashine. Kwa hiyo, haya yote tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia kuhusu hifadhi ya barabara, anashauri elimu itolewe kwa baadhi ya nyumba zilizojengwa na hili nakubaliana naye. Amesema mabango kama vile UKIMWI unaua yasiwekewe X. Ukiona bango limewekwa X, lipo barabarani, kwa sababu tatizo la kuwekewa X mabango haya sio kwamba mabango hatuyahitaji, mabango tunayahitaji ila yawekwe kwa utaratibu mzuri.

Mabango yasiwe chanzo cha ajali, kwa sababu kuna mabango mengine yanawekwa kwenye kona. Kwa hiyo, dreva anapokuja anaona bango badala ya kuona barabara. Kwa hiyo, badala ya kutoa elimu ya kuzuia UKIMWI, yanaua watu ambao hawana UKIMWI. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vitu vyote hivi ni lazima tuvizingatie. Elimu tunaihitaji, lakini hatuhitaji pia watu wengine ambao hawana hatia wafe kwa sababu ya mabango yale na ndio maana kwa sababu yale mabango yamevunja Sheria Na. 167 ndio maana tumeyawekea X. Kuyawekea X maana yake wayatoe ili yawekwe mahali pazuri, yasiwe chanzo cha vifo. Kwa bahati nzuri ukienda kwa mfano sasa hivi kwa Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha mabango sasa yanawekwa kwenye utaratibu mzuri. Mabango yanahitajika lakini yawekwe kwa utaratibu mzuri, kwa hiyo ndio maana tutaendelea kuyawekea X.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umemsikia Mheshimiwa amezungumza hapa kwamba, wakati wakija alishindwa kuelewa kama hili ni bango au ni daraja, kidogo apate ajali. Kwa hiyo, vitu hivi vyote vinategemeana. Kwa hiyo, njia iliyopo mabango yawepo lakini yawekwe kwa utaratibu mzuri na Wahandisi wangu wa Mikoa tumeshawapa maelekezo ni namna gani bango linatakiwa kuwekwa badala ya kila bango kuwekwa

mahali popote, *Guest House*, zuia Ukimwi, halafu mtu anakuja analigonga anapata ajali. Wakati mwingine mabango yale yanawekwa karibu na alama za barabarani, kwa hiyo zinazuia lile bango. Mbele kuna alama inayosema kona kali, linakuja bango linasema zuia UKIMWI. Kwa hiyo, mtu ataliangalia lile bango la zuia UKIMWI, lakini bango la kona kali hataliona, anakwenda kufa. Sasa ni kipi kizuri umezuia au umeua? Ndiyo maana tunataka yawekwe kwa utaratibu mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah ametoa pongezi kuhusu barabara yake ya kutoka Korogwe kwenda Kilosa na ametoa mapendekezo namna ya kuanza kufanya *design*. Tutayazingatia hayo mapendekezo, lakini nia ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *alternative routes* nyingi na kurahisisha maendeleo ya maeneo ambayo yanazalisha kiuchumi na yanaendelea vizuri katika masuala ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura amepongeza Wizara na pia amezungumzia juu ya kivuko cha Mitomoni kwamba daraja hilo lilihamishwa likapelekwa mahali pengine. Amezungumzia vile vile juu ya barabara ya Songea hadi Mbinga, ametoa mifano ya madaraja ambayo yalijengwa zamani na kwa nini sasa tusiyaendeleze katika kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Amezungumzia Hazina ianze kuhamia Dodoma na kadhalika. Tumezingatia ushauri wake, yale ambayo tutayaweza yatakayokuwa chini ya Wizara tutayashughulikia na yale ambayo hayatawezekana tutaweza kumjulisha kama tulivyosema tutazingatia haya yote. Lakini kuhusu suala la daraja la Mitomoni halikuwa lipelekwe pale Beira kuunganisha Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kwa upande wa Msumbiji pakawa hakuna *activities* zozote kwa zaidi ya kilomita mia mbili na hawakulitaka sana lile daraja kwa sababu walifikiria labda hapakuwa na sababu ya kuwepo pale daraja lakini pia kwa kuzingatia *political background* za Msumbiji kwa sababu upande wa *Northern Part* ya Msumbiji ndipo walipokuwa wanatawala *RENAMO*, *RENAMO* ndio walishindwa sana zaidi. Kwa hiyo, lile daraja likawa lina ubishi mwingi na sisi hatukuona sababu ya kuendelea kubishana mahali pa kuweka daraja na ndio maana lile daraja tukalitoa tukalipeleka kwenye daraja la Malagarasi ambako watu walikuwa wanalihitaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni fundisho pia kubishana bishana kunachelewesha mambo, tuwe kama kitu kinakuja ni kama sasa hivi siku za nyuma watu walikuwa wanabishana barabara ya kutoka Mtwara kwenda *Mbambabay* ipitie Newala au ipitie Masasi kwa Mheshimiwa Raynald Mrope.

Sasa mabishano yale saa nyingine huwa yanachelewesha maendeleo. Wenzetu akina Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na hawa ndio walipata hayo mabisho ya lile *Beira Bridge*, tukalihamisha lakini tulihamisha kwa manufaa mazuri lakini hata hivyo kwa sasa hivi tuna hatua mbalimbali tunazozichukua kwa sababu ukizingatia katika Bajeti ya mwaka huu tumetenga daraja la Liwana *along Songea* - Mitomoni kuna shilingi milioni 30 na kuna daraja la Wino, *Isinga road* kuna shilingi milioni 70. Zote hizi tumezipeleka huko kwa ajili ya kuhakikisha kwamba *communication* katika maeneo haya

inapatikana. Kwa hiyo, tutakuwa tunazingatia haya yote kwa pamoja na kuendelea na ushauri huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Raynald Mrope wa Masasi amepongeza. Pia amezungumzia juu ya kupatikana kwa shilingi milioni 50. Anasema hizi shilingi 50 zinaweza zisitoshe katika kuendeleza ile sehemu. Ni kweli kabisa ukiziona katika Bajeti zinaweza kuonekana kama ni ndogo, lakini ukweli ni kwamba katika Bajeti tuliyoitenga mwaka jana ilikuwa ya bilioni moja kufanya *feasibility study* kutoka Mtwara hadi *Mbambabay* jumla ya kilometa 837.

Sasa baada ya kutangaza *tender tuli-save* fedha ambazo zilibaki katika Bajeti ile na zile fedha ndio tumezitumia mwaka huu kuanza kufanya design pamoja na hizi shilingi milioni 50 tukaziongezea. Kwa hiyo, fedha zinatoshwa kabisa kufanya *design* na tunapanga ile *design* ikishamalizika tutakaribisha wawekezaji mbalimbali hata wale wa *BOT* kama wataweza kuja kule kujenga hata kwa kutumia fedha zetu.

Kwa hiyo, lengo kubwa ni kuhakikisha sasa tukishajua hii *design*, madaraja yatapita wapi na sehemu gani ili tuweze kuhakikisha kwamba hili eneo linaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yamezungumzwa lakini najua muda wangu umeanza kupungua. Lakini Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, ameunga mkono na amezungumzia kuhusu barabara ya Kibiti - Lindi na maombi ya barabara yake ya kutoka Nangurukuru-Liwale kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 tumelizingatia na Mkandarasi kwa bahati nzuri yupo kwenye sehemu ya kazi ili kuhakikisha kwamba sehemu hiyo inatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward Ndeka kule Kigoma nimezungumza kama nilivyomweleza Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, tunahakikisha kwamba tutazishughulikia zile sehemu ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Frank Maghoba, amezungumzia kuhusu barabara ya Kilwa. Kwa mwaka huu tutaanza ujenzi na itakuwa *dual courage ways*. Amezungumzia Kigamboni anasema daraja lile la Kigamboni ni lake. Hapana, lile daraja ni la Serikali ya CCM. Vile vile amezungumzia juu ya utengenezaji wa magari, ni kweli kuna kitengo cha kutengeneza magari kilicho chini ya Wizara ya Ujenzi katika kila Mkoa, lakini pia lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba magari yanatengenezwa katika standard nzuri. Ninafahamu Mheshimiwa Frank Maghoba, nimeshasikia sikia kwamba na wewe una gereji yako huko, lakini nisingetaka magari ya Serikali yaende kutengenezwa kwenye gereji ya Mheshimiwa Frank Maghoba, kwa hiyo, tutaendelea kuzingatia taratibu za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi yale aliyoyazungumza ni kama nilivyosema. Lakini amezungumzia pia juu ya *Mtwara Development Corridor TANROADS*. *TANROAD* huwa ipo chini ya Wizara ya Ujenzi, imeanzishwa chini ya *Amendment Act, No. 2* ya Mwaka 1998 ambayo imepitishwa hapa hapa Bungeni.

Ilianzishwa pia kwa kupitia Sheria Na. 30 ya Mwaka 1997 iliyoanzisha *Executive Agency*. Wao wapo *answerable* kwa Wizara ya Ujenzi na wanafanya kazi kwa *performance agreement* inayotolewa na Mfuko wa *Road Fund*. *TANROAD* hawana ofisi Wilayani kwa sababu Wilayani barabara zote za Wilayani zipo chini ya Tawala za Mikoa. Kwa hiyo, hayo ndio mahusiano, lakini kupitia Bodi za Mikoa *TANROAD* huwa wanawajibika katika kutoa taarifa katika Mikoa ya hali zote za barabara zikiwemo za Halmashauri zinavyoendelea. Kwa ufupi naweza nikajibu haya ambayo mengine naweza kuyajibu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawe umezungumza, angalau sasa nielezee kuhusu barabara zako kwa sababu umeshindwa kuuliza swali hapa kwa sababu wewe ni Mwenyekiti. Lakini kwa heshima yako pia tumetenga zaidi ya shilingi milioni 145 kwa barabara ya Mlool-Kamsamba ambayo kwa bahati mbaya siku nyingi imekuwa ni mbaya na huu ni umuhimu katika kuhakikisha kwamba barabara nyingi zinatengenezwa pamoja na ya Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha pamoja na kwamba ameshika shavu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi ambazo zimetengenezwa katika Mkoa tumeziambatanisha katika kiambatanisho hiki. Mkicheki vizuri Waheshimiwa Wabunge mtaona karibu kila barabara ambazo zipo chini ya Wizara ya Ujenzi ziwe barabara kuu au barabara za Mikoa zimetengewa fedha ili kusudi barabara hizi ziweze kutoa mchango mzuri katika uchumi wa nchi yetu. Katika Bajeti yetu ya mwaka huu pia tume-include barabara za Zanzibar ili kusudi Wabunge wanaotoka Zanzibar wajue ni kiasi gani cha fedha ambazo zimepitia huku ambazo zimekwenda kule. Kwa sababu mtaona katika kitabu hiki zaidi ya shilingi bilioni 9.08 zitatumika katika kufanyia ukarabati wa kiwanja cha Zanzibar cha Ndege pamoja na barabara zingine kama nilivyozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimeshagongewa kengele nisingependa kugongewa nyingine. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 47 - Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... .. shilingi 975,666,200/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati akimalizia hotuba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amesema kwamba barabara zote, barabara kuu na zile za Mikoa zimetengewa fedha. Lakini nakumbuka kwamba nimemtumia ujumbe asubuhi kwamba zile barabara zinazopita kwenye Jimbo langu kwenda Kaisho, Mrongo, sikuona humu kwenye makabrasha yake. Sasa sijui ananijibu

namna gani maana mimi niko kwenye kifungu 1001 kwenye mshahara wake. Nataka tu majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nimesema barabara zote zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi zimetengewa fedha. Nisingeweza kuandika orodha ya barabara zote zenye urefu wa kilometa 35,000 kwenye kitabu hiki. Lakini Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kama anaweza akafungua ukurasa 112 kwa kitabu changu hiki cha Bajeti kuna Mkoa wa Kagera, *Unpaved Regional Road* akiangalia katika Mkoa wa Kagera kuna kilometa 655 zitakazofanyiwa matengenezo na kuna milioni shilingi 491.2 zimetengwa. Kwa hiyo, hizo barabara zake zitahusika katika matengenezo hayo. Kwa hiyo, humo kuna *package* ya barabara nyingi ambapo orodha ya barabara zenye anaweza akazipata kutoka kwa Mhandisi wa Mkoa wa Kagera.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub- Vote 1001* mshahara wa Waziri. Imetamkwa katika kitabu chake cha nyongeza ya hotuba yake kwamba barabara ya Mkuranga hadi Kibiti imetengewa shilingi bilioni 10.5 kama mradi ambao unaendelea. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, atakumbuka kwamba mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ya barabara ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2003. Lakini nakumbuka kwa kadri karibu mwaka mmoja ujenzi haukuwa unafanyika na hata ujenzi unaofanywa sasa hivi unasuasua. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kusuasua huko ni kwa nini? Lakini la msingi vile vile ni kwamba hizo shilingi bilioni 10.5 ambazo amezitamka kwenye hotuba yake hazionekani popote katika vitabu hivi viwili na hasa kile kitabu cha maendeleo, sasa fedha hizo zitatoka wapi kwa sababu sasa hivi hapa sisi tunaaidhinisha matumizi, lakini utaidhinishaje matumizi ambayo hayapo kwenye vitabu hivi vya matumizi? Naomba anisaidie.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mkataba wa Ujenzi wa barabara hii ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2003 na Kandarasi ambaye anashughulikia kazi hii ni Kikosi cha *TANROAD* chini ya *Consultant* ambaye ni *GAP Consultant* kutoka Ujerumani. Tusingeweza kusaini mkataba kama tusingekuwa na fedha wala huo ujenzi unaosuasua usingekuwa unaendelea kama usingekuwa unatolewa fedha. Lakini ukweli kwamba fedha zinazotumika hapa ni kutoka mkopo wa *Kuwait Fund* pamoja na fedha za Serikali. Mwaka 2003 tulipata matatizo ya fedha zilizokuwa zimetolewa na mfadhili zikawa zimechelewa. Lakini kwa sasa hivi zimekwishapatikana, kwa hiyo, mwaka 2003 ujenzi ulikuwa unaenda polepole kwa sababu tulikuwa tunatumia fedha zetu tu ambazo zilikuwa zinatolewa kutoka *Road Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia kwamba fedha hizi zitaendelea kutumika na kazi zitaendelea. Ni kwa bahati mbaya yapo baadhi ya makosa ambayo yamefanyika katika kitabu cha nne ambapo tutakapokifikia nitayataja ili kutoa hizo dosari ikiwa ni pamoja na barabara ya Mheshimiwa Paschal Degera.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... .. 204, 670,800/=



*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... .. 246,555,800/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi langu ni dogo tu ninataka kupata ufafanuzi. Kwanza, nilikwishampongeza Askari wa Mwavuli ndiyo huyu na amefanya kazi kubwa nzuri. Kwa hiyo, ninachotaka ni kupata ufafanuzi katika jambo moja dogo tu. Ni kwamba ametaja kuhusu hii bomoa bomoa kando kando ya barabara. Kwa wale waliovamia mimi ninakubaliana naye kwamba kweli wamepata *grace period* ya kusubiri kwa wale waliovamia. Lakini kuna maeneo ambayo barabara ilipita kutokana na *design* ikawakuta watu na ni pamoja na sheria ya sogeza sogeza ya mwaka 1978 ya vijiji. Sasa hiyo barabara iliyokuta watu na wale watu wa pembeni bahati mbaya hawakufidiwa kwa wakati huo. Mheshimiwa Waziri hakuzugnumzia hilo. Nataka kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili suala la bomoa bomoa linaendana na sheria na bahati nzuri Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, yuko hapa kwa sababu aliapa sheria ikiwa ni pamoja na hiyo sheria namba 167 ya mwaka 1967 ilikuwa *Gazetted* tarehe 5 Mei, 1967. Wizara inachofanya na matangazo yetu tulivyoyotoa tumeeleza kwa miradi ambayo imekwishakamilika kwa mfano, kama Mradi wa Dar es Salaam-Bagamoyo, barabara ya Himo-Arusha, zile zimekamilika na barabara nyingine. Mtu anaenda kujenga kwenye *Road Reserve* lazima nyumba yake ibomolowe. Lakini tumeeleza pia kwenye miradi ambayo inaendelea kwa sasa hivi ambayo fedha zake zipo ikiwa ni pamoja na barabara ya *Port Access*, barabara ya kutoka Mwanza-Geita-Sengerema-Biharamulo- hadi Kyamiorwa kupita Bwanga na zingine nyingi ambazo kwa bahati nzuri nimezitaja katika orodha yangu watu ambao wako ndani ya *Road Reserve* mle ni lazima waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ile sheria inazungumza wazi kama barabara imemfuata mhusika huwa wanalipwa *compensation*, lakini kama mhusika ameifuata barabara anabomolehwa nyumba na anailipa *compensation* barabara na ndiyo maana katika taarifa yangu nimeeleza mpaka sasa hivi tumekwishalipa bilioni 6.8. Wale waliolipwa bilioni 6.8 ni wale ambao wako nje ya *Road Reserve* na katika barabara yoyote kabla haijajengwa huwa kuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipa *compensation* kwa watu ambao hawavunji sheria au fidia. Kwa mfano, kwenye barabara ya Nangurukuru kwenda Lindi kuna zaidi ya bilioni moja ambazo zimetengwa kwa ajili ya kulipa *compensation* kwa wale ambao watakuwa nje ya *Road Reserve*. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo yangu ambayo naweza kuyatoa kwa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Electrical and Mechanical* ... .. 3,215,275,900/=

Kifungu 3001 - *Supplies and Services* ... .. 1,022,553,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Buildings* ... .. 465,135,200/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu hiki anieleze hawa Maafisa wa *TBA* Kimkoa wanawajibika wapi, kama wakifanya makosa wanawajibika kwake moja kwa moja Wizarani au wanawajibika kwa *RC* ili nijue niende wapi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBA* ni kitengo ambacho kinaitwa *Tanzania Building Agency* ambacho kimeanzishwa chini ya Sheria namba 30 ya mwaka 1997. Hii ni *Agency* ambayo inatakiwa ifanye kazi kwa kujiendesha na kwa kujitegemea ni kama ilivyo *TANROAD*, kwa hiyo iko chini ya *Chief Executive* wa *TBA* lakini kwa maana hiyo wako chini ya Wizara. Lakini kwa mtu anapofanya kosa mahali popote alipo anaweza akashikwa na Polisi hawatasubiri mpaka apelekewe Waziri au nani, kwa sababu kosa ni kosa. Kwa hiyo, kama kuna mtu anafanya kosa lina-*depend* ni kosa la namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ni kosa la kisheria, sheria siku zote huwa inachukua mkondo wake. Kama ameiba huwa anashikwa anapelekwa Polisi anawekwa ndani anafunguliwa kesi halafu anajulishwa Katibu Mkuu wa Wizara kwamba mtu wako wa *TBA* amefungwa au hata kama ni wa *TANROAD* au hata kama ni nani, hata kama angekuwa ni Mbunge. Kwa hiyo sheria kama mtu amefanya makosa sheria itachukua mkondo wake. Lakini kama ni masuala ya maelekezo ambaye anawajibika kutoa maelezo na kuelekeza matatizo kama yapo basi ni *Chief Executive* wa *TBA*, lakini kwa yeye Mbunge bado anaweza akaandika kwangu moja kwa moja au akanijulisha na nikalishughulikia hilo tatizo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 - *Trunk Roads* ... .. 54,964,803,800/=

Kifungu 7001 - *Rural Roads* ... .. 1,004,907,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Kifungu 2001 - *Electrical and Mechanical* ... .. 4, 120,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Buildings* ... .. 1,335,000,000/=

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kifungu hicho 5001 *Buildings*, kifungu kidogo 4134, pale ukienda mwisho baada ya mahesabu pana herufi “L” badala ya “O” na halafu kwenye *EU* isomeke *IDA*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 - *Trunk Roads* ... .. 154,583,598,600/=

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuulizia mambo machache tu. Kwanza wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaeleza barabara ya kutoka Babati - Kondoa - Dodoma alitaja kijiji cha Farukwa. Sasa inaonekana kwamba barabara hizi hazielewi vizuri. Kwa hiyo, naomba kijiji cha Farukwa hakipo katika barabara hiyo, kijiji cha Farukwa kipo katika barabara ya kutoka Singida - Kwamtoro - Farukwa - Mayamaya - Dodoma.

Sasa kama anataka kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami nitashukuru sana. Lakini pia atengeneza barabara ya kutoka Babati-Kondoa na Dodoma. Sasa kwa maneno hayo ninataka nimwalike aje atembelee hizo barabara ili aweze kuzitofautisha ziko wapi.

Jambo la pili, kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri alisema kwamba kuna shilingi 1,500,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya barabara ya kutoka Babati hadi Dodoma. Sasa tunataka kupitisha kifungu hiki, nilikwishahoji kwamba humu kwenye kitabu cha nne kiwango hicho hakipo sasa tunapitisha vipi? Hapa alisema kwamba atafanya marekebicho, naomba afanye marekebicho kwanza halafu ndiyo tupitische. Naomba sana. Hilo la pili.

La tatu, nimeangalia Bajeti iliyopitishwa na Kamati ya Miundombinu ni tofauti na hii Bajeti ambayo tunataka kupitisha hapa. Bajeti ambayo ameisoma Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ni tofauti na hii ya Hazina sasa tunapitisha ipi? Kwa sababu Kamati ya Miundombinu imepitisha Bajeti yake na hapa kuna kitabu cha Hazina labda nimpe *figures* ili aweze kuona.

Kamati imepitisha Bajeti ya Mipango ya Maendeleo tu 214,142,400,000/= hiyo ndiyo Bajeti iliyopitishwa na Kamati, lakini Hazina hapa ukiangalia katika ukurasa huo utaona kwamba ni 184,249,658,600/= sasa tunapitisha ipi? Mbaya zaidi hotuba ya Mheshimiwa Waziri anataka kupitisha bilioni 225,138,194,000/= sasa mimi nashangaa tunapitisha ipi ya Mheshimiwa Waziri, ya Kamati ama ya Hazina? Mimi nafikiri tuahirishe waende wakarekebishe haya mahesabu ndiyo tuje tupitische.

**MWENYEKITI:** Kabla Mheshimiwa Waziri hajajibu yale mawili ya kwanza, kinachopitishwa hapa ni kitu kilicholetwa na Serikali hapa na hakuna Kamati

inayopitisha ndiyo maana tunapitisha sasa hapa. Kamati inatoa mapendekezo na maoni. Lakini hatupitishi Bajeti kwenye Kamati na ndiyo maana tuko hapa kupitisha Bajeti hii ambayo iko hapa ya Serikali kama ilivyo Muswada. Sasa Mheshimiwa Waziri utoe tu maelezo kwa yale mengine mawili, mengine ni maombi tu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikitoa maelezo kuhusu barabara ya Minjingu-Babati hadi Dodoma ni kweli natambua kwamba kuna mji wa Farukwa ambao unaenda mpaka Singida. Lakini hii barabara ya kutoka Farukwa kwenda Singida nayo inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi chini ya *TANROAD*. Lakini majina ya huko saa nyingine ni magumu magumu tofauti na ya Kisukuma. Lakini hata hivyo, barabara niliyokuwa ninamaanisha hapa ni barabara ya kutoka Minjingu - Babati kuja Dodoma ambayo imetengewa shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika maelezo yangu nilisema yapo makosa mbalimbali ambayo yamefanywa na vitabu hivi vilivyotoka Hazina. Katika kifungu hiki kuna makosa mengi ambayo kwa ruhusa yako ningeomba niyasahihishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo *Sub vote 6001 ya Trunk Roads* kipengele kidogo cha 2371 kuna barabara ya *Mwanza Urban Road actually pale Roads*, kujumlisha barabara ya *Airport Road* unajumlisha na barabara ya *Mwanza - Nyanguge Road*. Lakini katika kifungu kidogo cha 4102 pale wametaja Ilula-Tinde - Isaka lakini ukweli ni kwamba ni Ilula-Tinde-Isaka hadi Nzega. Wakandarasi wako kule na kuna zaidi ya shilingi bilioni 59 zimetengwa katika mradi wote. Sasa hizi ni *omitted* ambazo zimefanyika kule wanapokuwa wanachapisha vitabu.

Lakini pia katika 4110 wameandika Usagara-Bwanga pale ni Usagara-Bwanga-Kyamiorwa/Biharamulo. Hiyo 4112 kuna Uvinza-Malagarasi pale pia kuna Kigoma-Uvinza-Kaliua-Tabora. Ukurasa unaofuata wa 50, 4177 pale kuna Mkuranga kwenye *black Kitonga - Kibiti*. 4181 pale Kagoma Lusahunga pale baada ya fedha zile bilioni 6 kuna herufi "G", hiyo herufi inatakiwa isomeke L ni *Loan* siyo *Grant*, ni mkopo kutoka *Africa Development Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 4183 kuna Minjingu-Babati-Singida pale zimewekwa milioni 2,000 ukweli kwamba ni milioni 740, halafu kinachofuata kuna L, halafu kuna D, halafu *IDA* na *total* itakuwa ni milioni 740. Kwenye 4186 pale pameandikwa Msimba-Ruaha pale kuna kitu kingine kinaitwa Mbuyuni/ Ikokoto halafu badala ya G pawe na L. 4187 pale tuanze na neno Same halafu Mkumbara halafu Korogwe kwa hiyo mradi wote ni kutoka Same-Mkumbara-Korogwe siyo Mkumbara-Same. 4191 ile Kidatu-Ifakara pale kuna neno Sweden lakini *SDC*. 4193 kwenye *Road Safety Study* kuna neno G lile lifutwe liwe L.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 4195 ile imeandikwa Dodoma-Iringa wameandika *IDA* hapo pabadilishwe pawe *ADB* na zandikwe milioni 900. Inayofuata ni 4196 ni Dodoma-Babati huku wameandika milioni 10 halafu zile zingine hazikuwekwa, kwa hiyo kwenye *Forex* zandikwe milioni 1500 halafu iandikwe L maana yake ni Loan,

halafu D, halafu iandikwe *IDA*. Halafu kwenye *total* waandike 15 unaiunganisha na ile 10 ambayo ndiyo ilisahaulika hapo. Lakini pia kuna miradi mingine ambayo imekuwa *omitted* kabisa, hakuandikwa hapa ni Tanga - Horohoro ambayo ina milioni 560 kwa *forex* nazo ni *Loan*, halafu kuna D, halafu kuna *IDA*, kwa hiyo, *total* huku ni milioni 560. Lakini kuna nyingine ambayo inaitwa *Construction* za *TANROADS* zimeandikwa *Headquarter* na *Regional Offices* ambazo nazo kuna milioni 634 nazo ni *Loan* halafu kuna D zimetolewa na *IDA* nazo *total* yake ni milioni 634. Haya ndiyo marekebisha ambayo tumefanya na vitabu hivi vilivyotoka Hazina tuliwaandikia kuwaeleza kwamba kuna miradi ambayo imekuwa *omitted* imekosewa na wamekubali na hata mwaka 2003 walifanya hivyo hivyo, kwa hiyo, ni makosa ya uchapishaji inawezekana wanaochapa siyo ma-engineer.

Lakini pia katika swali lake la pili hakuna tofauti ya fedha zilizotolewa na Wizara ya Ujenzi hapa tulizozisoma na zile zilitolewa na Kamati ya Miundombinu. Kwa bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaweza akazungumza.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, jumla itabadilika Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *total* inakuwa kama ile tuliyoi-present kwenye kitabu changu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu *Hansard* itaonyesha marekebisha ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaeleza hapa. Sasa Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo siwezi kukupa nafasi kwa sababu nilishatoa nafasi kwa mtu mmoja aliyekuwa amesimama kwa mara ya kwanza wewe umechelewa. Lakini kwanza Mheshimiwa Paschal Degera.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kukamilisha hoja yangu. Nashukuru sana kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa lakini hii ndiyo tahadhari kwamba mara nyingi haya mambo yanaletwa bila kukamilika kwa hiyo tunayapitisha bila kuyasoma.

Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa marekebisha aliyofanya na zaidi napenda kushukuru kwamba ameingiza na fedha ambazo mimi nilikuwa nazifuatilia za kutoka Babati mpaka Dodoma. Kwa hiyo, namshukuru sana. Lakini pia naendelea kusema tu kwamba kama ulivyohoji wewe mwenyewe Mwenyekiti kwamba sasa *total* si inabadilika sasa tunafanyaje na tunapitisha ipi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameishajibu. Kwa utaratibu wetu Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo huwa wanasimama mara ya kwanza tunawaweka kwenye orodha, halafu ndiyo tunaendelea ndiyo utaratibu, tusianze kuvunja kanuni ambazo tumejiwekea. Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, hucusimama mwanzoni.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7001 - *Regional Roads* ... .. 24,211,060,000/=

**MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niko kwenye hiki kifungu cha 7001 *Regional Roads*. Kabla sijazungumzia hili niseme tu kwamba hakika ninampongeza sana Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, kwa kazi yake nzuri anayoifanya inayokwenda sambamba na wale wataalam walioko kule wote ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kifungu hiki cha *Regional Roads*, tuangalie sasa kitabu cha hotuba yake, wakati nazungumza kumpa pongezi kuna mingurumo huku ya kwamba mtu akifanya kazi nzuri apongezwe na akifanya vibaya asahihishwe. Sasa kifungu hiki tuangalie ukurasa 115, amesema *Unpaved Regional Roads Periodic Maintenance*. Katika hii pale chini ya namba 83 ameandika Mkoa wa Kilimanjaro. Katika Mkoa wa Kilimanjaro ameonyesha ambao wametengewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo za changarawe. Lakini tukiangalia katika Jimbo zima la Vunjo barabara hizo ambazo ni *Regional Roads* ukiangalia hapa baadaye atanielimisha mahali pa kupata fedha nyingine. Kwa sababu ukiangalia hizi barabara ambazo *Regional Roads*. Kwa mfano, ambazo ziko Kirua, Kirema, Marangu, Mwamba, Mwika, Rombo ni mwinuko na zinatengenezwa na *Regional Roads*. Sasa kama hapa hazipo ni wapi tena tunaweza kupata kama hazijatengewa kwa kutumia nafasi hii ili nao waweze kufanikiwa japo kutengeneza ile mifereji na mitaro ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hapa ni suala la kuelewa tu. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amezungumzia ukurasa wa 115 ambapo ameona *Unpaved Regional Roads*. Lakini mahali ambapo tumezungumzia juu ya *Regional Roads* sio ukurasa wa 115 tu, ningeomba nianze kumfunulia kila ukurasa atakapokuwa ataangalia kwenye *Regional*, ananikataza kwa sababu ataonekana hajasoma. Lakini mimi nataka nimsomee hapa.

Kwa ruhusa yako ukifunua Kiambatanisho Na. 6 utaona kuna Mikoa iliyotajwa. Kwanza ukianzia ukurasa wa 111 ukienda ukurasa wa 112 utakuta kuna *Paved Regional Roads*. Ukiangalia lile neno Kilimanjaro kuna kilometa 57, kuna shilingi milioni 18.12. Ukiingia cha pili *Unpaved Regional Roads*, Kilimanjaro tena kuna kilometa 110 na kuna fedha zimetengwa kule. Ukiendelea tena kwenye ukurasa wa 114 kuna Kilimanjaro kuna fedha zilizotengwa. Ukiendelea.

**MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sio kwamba nilikuwa sikusoma, sijasoma kitabu hiki, nilisoma vizuri sana. Ninachotaka ni kwamba katika kifungu hiki au katika ukurasa huu hii ipo, Vunjo ipo, basi. Habari za Vunjo zipo. Jibu lake? Alivyojibu amejibu kwa sababu huku kwingine kote nilikuwa nimeshasoma vizuri. Lakini kipengele hicho nilichouliza angeniambia hapana kiko hivi. Lakini kwamba kwa kusoma Mheshimiwa Mwenyekiti,

nimesoma na kazi yake ni nzuri. Namshukuru kwa kazi nzuri na kilometa za Mkoa Kilimanjaro nashukuru amezi-*cover* vizuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa taarifa tu Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, vijiji vyote katika Wilaya zetu wote havijatajwa kwamba na Mbozi, Karatu na kadhalika. Kwa hiyo, nafikiri itakuweco humu ndani na ameelewa na ameshukuru. Baada ya maelezo haya jamani. *Ooh, sorry*, kuna Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu hicho hicho cha *Regional Roads, Sub Vote 7100* nilikuwa tu nipate ufahamu kwa sababu katika ukurasa 112 nakiri na mimi kuwemo pengine na sio pengine katika Mkoa wa Pwani katika hizi *Unpaved Regional Roads*. Lakini tatizo linakuja kwamba vile vile hata kama nikiwemo kwa bahati mbaya hawa wakandarasi wanaokuja kule huwa wanachelewa kufika, utengezaji wao unachukua muda mrefu, vyombo vinavyokuja vinakuwa si vizuri, wanakuwa wanabambika bambika tu. Sasa kuna maombi ambayo tulioyaleta kwa Mheshimiwa Waziri atudokezee tu kidogo ili na sisi tuweze kufarijika wananchi wa Wilaya ya Mafia ni nini kile ambacho maombi yetu ambayo tumempa pamoja na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe ili tuweze kufahamu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, walileta maombi kuhusu hizi fedha zinazotolewa za kutengeneza barabara za mikoa katika Wilaya ambazo ni visiwa kama vile Kisiwa cha Mafia pamoja na Kisiwa cha Ukerewe. Kwamba saa nyingine huwa ni vigumu sana kupata Makandarasi kule na ukweli kwamba gharama huwa zinakuwa kubwa kwa mkandarasi kutoka Dar es Salaam au kwenda Mwanza akaanza kuvusha mitambo yake na kwenda kutengeneza kazi ya shilingi milioni kumi au milioni ishirini.

Ombi lao waliliandika Wizarani wiki iliyopita na sisi Wizara tulikuwa tunalifanyia kazi ili kusudi tuone ni kwa namna gani tunaweza tukasaidia hii Wilaya au visiwa hivi viwili vya Mafia pamoja na Ukerewe ambavyo kwa kweli vina suala ni *special* ambalo linahitaji *consideration* tofauti na Wilaya zingine. Kwa hiyo, hili tunalifanyia kazi na bahati nzuri wataalamu wangu nimeshawapa. Kwa hiyo, majibu yake nisingeweza kuyafanya hapa kwa sababu mambo mengine ni ya utendaji, mambo mengine ni ya kubadilisha. Kwa mfano, katika Sheria ya *Road Fund* inasema fedha zitatumika kutengeneza barabara tu kwa mkandarasi. Sasa tunajaribu tutazungumza sisi Serikalini tuone ni kwa namna gani tatizo hili tunaweza tukalitua. Lakini ukweli tatizo lao ni la msingi na sisi tunalikubali kwa kweli. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2004/2005 yalipitishwa na  
Bunge)*

*(Saa 01.37 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa  
tarehe 2 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*